

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 4 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo.

**Ukosefu wa Waganga na Watumishi  
wa Afya - Same Magharibi**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. DKT. DAVID  
M. DAVID)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka waganga, watumishi wa afya pamoja na vitendea kazi katika zahanati za Same Magharibi zilizojengwa kwa ushirikiano wa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt.David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika Jimbo la Same Magharibi, ambapo mahitaji ni watumishi 867 lakini waliopo ni 287, upungufu ni watumishi 585.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imepeleka watumishi wapya 10 wa sekta ya afya katika jimbo hilo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Same imeomba kibali cha kuajiri watumishi wapya 104 wa sekta ya afya ambao watapangwa katika vituo vyenye upungufu mkubwa wa watumishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Kakunda, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, atakuwa tayari kufika katika Wilaya ya Same ili kwenda kuona hali ambayo ipo sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Kilolo inajenga hospitali kubwa na nzuri, je, ni kiasi gani cha wahudumu au Madaktari wanaweza kuwatengea kwa msimu huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Dkt. Mathayo huko aliko kwamba nitafika Same baada tu ya Bunge la bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwamoto kwa kufanya ufuatiliaji wa kina na wa karibu, katika kipindi cha miezi minne au mitano ameweza kufanikiwa na Serikali imepeleka pale zaidi ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kujenga hiyo hospitali ya wilaya na Mheshimiwa Rais juzi ameweka jiwe la msingi. Nimhakikishie tu kwamba tutashirikiana na wenzetu wa utumishi kuhakikisha hospitali ile inapata watumishi wa afya kwa mujibu wa kitange na uwezo wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa majibu mafupi ya Serikali pamoja na maswali mafupi ya ziada, hongereni sana. Tunataka Bunge liende hivi, maswali mafupi na majibu mafupi. Mheshimiwa Mama Kilango na Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii. Kwa kweli wananchi wa Wilaya ya Same kwa ujumla wao wanajitahidi sana kujenga zahanati. Ningewomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa Serikali kwenda kuona jitihada zile, naomba atuambie hapa ndani atakwenda lini na atatoa msaada gani kwa sababu hali ya wananchi hasa wa milimani upande wa afya ni mbaya sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini tu utakwenda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na wananchi wote wa Wilaya ya Same kwamba nitakapokwenda katika Wilaya ya Same sitaishia katika Jimbo la Same Magharibi peke yake bali nitapita mpaka kwenye Jimbo la Same Msahariki. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, imeshatosha Mheshimiwa Naibu Waziri unakwenda tu basi, Mheshimiwa Mbatia. (*Kicheko*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nini utaratibu wa Serikali katika kuhakikisha wananchi au mashirika mbalimbali wakishajenga zahanati hizi kwa mfano Jimbo la Vunjo Zahanati ya Kochakindo ina zaidi ya miaka mitano ilijengwa na *TASAF* haina watumishi wala vifaa kwa ajili ya kutoa tiba. Utaratibu wa Serikali ni upi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwamba swali la Mheshimiwa James Mbatia linaonekana ni maalum kwa eneo maalum. Kwa hiyo, namwomba sana baada ya kikao hiki leo hii tuweze kuonana ili anipe *details*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu.

Na. 178

**Mishahara kwa Wenyeviti wa Vitongoji, Mitaa na Vijiji**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Serikali inaanza katika ngazi ya kitongoji, mtaa na kijiji:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Je, ni lini viongozi na Wenyeviti wa Vitongoji, Mtaa na Kijiji watalipwa mishahara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa sifa zinazomwezesha Mtanzania kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji, Kitongoji au Mtaa ni pamoja na kuwa na shughuli halali inayomwingizia kipato. Kwa muktadha huo, utaratibu wa viongozi kwa ngazi hiyo kulipwa mishahara kama ilivyoulizwa katika swali la msingi haujawahi kuwekwa kwenye sheria yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hata sisi viongozi wa Bunge mojawapo ya sifa ni kuwa na kazi halali zinazotuingizia kipato kama hawa Wenyeviti wa Vitongoji ambao sisi tunalipwa, wao hawalipwi. Je, Serikali iko tayari kuleta sheria ili waweze kulipwa mishahara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa viongozi hawa ndiyo wanaohamasisha maendeleo kama ujenzi wa zahanati, shule za msingi, sensa na kusimamia amani, je, Serikali iko tayari iko tayari kuendelea kuwalipa posho? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, napenda nimhakikishie kwamba wakati wowote Serikali inapopata

mapendekezo huwa inayafanya kazi. Kwa hiyo, mara tutakapopata mapendekezo kutoka kwenye vikao halali vinavyohusika tunaweza wakati wowote tukafanya marekebisho ya sheria kutohana na muktadha wa muda utakavyokuwa na mapendekezo yatakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu kulipa posho, Serikali ilishatoa Mwongozo tangu mwaka 2003 kwamba yatumike mapato ya ndani kulipa posho kwa viongozi hawa na posho zile zimeainishwa. Kwa hiyo, ni jukumu la Wakurugenzi wa Halmashauri na Mheshimiwa Mbunge namwomba sana asimamie kwenye jimbo lake na watumie Mwongozo huo kuhakikisha kwamba viongozi wetu hawa wanalipwa posho.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda, Mbunge wa Kigoma Kusini.

Na. 179

### **Kuligawa Jimbo la Kigoma Kusini**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

Jimbo la Kigoma Kusini lenye ukubwa wa kilometra za mraba 10,178 lina jiografia mbaya na idadi ya wakazi wake ni kubwa sana:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuligawa jimbo hilo na kuanzisha halmashauri nyingine ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma za kijamii kiurahisi?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo katika Tarafa ya Nguruka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali refu la

Mheshimiwa Hasna Sudi Katundu Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kuyagawa majimbo ya uchaguzi kwa kuzingatia vigezo vya idadi ya watu, jiografia, hali ya mawasiliano, ukubwa wa jimbo na uwezo wa ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Jimbo lolote ligawanywe, Tume hutoa tangazo kuhusu nia hiyo. Baada ya tangazo, mapendekezo hujadiliwa katika vikao vya Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa na hatimaye kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo hutangaza jimbo jipya baada ya kupata kibali cha Rais.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyozingatiwa katika kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua elfu hamsini, kata zisizopungua tatu, eneo lisilopungua kilomita za mraba mia moja na hamsini, viwanja viliviyopimwa visipungue asilimia 30 ya eneo lote, uwepo wa mpango kabambe wa uendelezaji wa mji (*master plan*) na huduma za jamii za kukidhi ukuaji wa mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo ya kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo yanapaswa kuanzia kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa kwa kuzingatia vigezo hivyo kwa mujibu wa sheria. Mapendekezo ya vikao hivyo huwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kumshauri ipasavyo Waziri mwenye dhamana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

nyongeza. Natambua kwamba Jimbo la Kigoma Kusini linakidhi vigezo vyote vya kugawanywa na kuwa majimbo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kwa mfano, Mkoa wa Katavi una kilometra za mraba 45,000 *population* 564,000. Jimbo hili la Kigoma Kusini lina vigezo vyote na tayari tulishafanya vikao kuanzia kwenye Vijiji, Kata, Baraza la Madiwani, DCC, vikao vikaenda mpaka kikao cha Mkoa kwa maana ya RCC na tayari tulipeleka Wizara ya TAMISEMI. Tume ya Uchaguzi mwaka 2015 waliliweka kwenye *website* yao kuonesha kwamba wako tayari sasa kuligawa, kama taratibu zote zilishafanyika na tulishawasilisha kwenye Wizara ya TAMISEMI, kwa nini walipotangaza majimbo mengine 2015 hawakuligawa jimbo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nguruka ilishafuata taratibu zote za kisheria na vigezo vyote inavyo kwa maana tuna kata nne na vigezo vya kisheria vinasema lazima tuwe na kata tatu. Je, kwa nini sasa Wizara ya TAMISEMI wasiamue tu rasmi kutangaza kwamba Mamlaka ya Mji wa Ngaruka sasa tayari inaweza kuanzishwa rasmi? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali refu jibu, kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, nina wasiwasi aliposema kwamba ana uhakika Jimbo la Kigoma Kusini limekidhi vigezo vyote, lakini nilipokuwa najibu swali la msingi nilizungumza kigezo kimojawapo ni ukubwa wa ukumbi wa Bunge. Sasa sijaelewa kama kigezo hicho nacho tayari kimefikiwa kwa kuangalia ukubwa na viti vilivymomo ndani ya Bunge kama kweli vinaweza vikakidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimhakikishie tu kwamba kwa mawasiliano zaidi na kuwapa uhakika wananchi wa Kigoma Kusini tutapeleka barua Tume ya Taifa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Uchaguzi ili kusudi watupe mrejesho mzuri zaidi wa hatua ambayo imefikiwa mpaka sasa hivi. Nina uhakika 2020 bado iko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu Nguruka kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, naomba sana arejee jibu langu la msingi nimesema kwamba vikao vinatakiwa vianzie kwenye Serikali ya Kijiji, Halmashauri ya Kijiji ikae ipeleke kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji upitishe, upeleke kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata iende kwenye Halmashauri, iende Mkoani ndio ije kwetu kwa ajili ya kumshauri Waziri mwenye dhamana na Waziri mwenye dhamana ni Rais. Kwa hiyo, itakapofika kwetu tutatoa ushauri, naomba sana awe na subira.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Wilaya ya Tunduru ni mionganini mwa wilaya kubwa ina kilometra za mraba 18,786 sawa na Mkoa wa Mtwara wenye wilaya sita. Je, Serikali haioni wakati sasa umefika wa kugawa wilaya hiyo kulingana na majimbo yaliyopo, kuna Jimbo la Tunduru Kusini na Jimbo la Tunduru Kaskazini maeneo haya sasa yakapata wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe taarifa tu kwamba Jimbo la Sikunge ambako mimi natoka lina kilometra za mraba 27,873 sasa yeye kilometra za mraba 18,786 anaweza akasubiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape *comfort* wananchi wa Tunduru kwamba maeneo haya Serikali inafahamu kwamba ni makubwa, lakini kwa sasa hivi mzigo uliopo kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba inaziwezesha wilaya mpya ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, tuna wilaya kama sita

ambazo zimeanzishwa hivi karibuni zipate majengo, vifaa vya uendeshaji, zipate watumishi, huo mzigo bado ni mkubwa sana na halmashauri mpya vilevile. Kwa hiyo, tukimaliza kuziwezesha hizi halmashauri mpya na wilaya mpya zikapata vifaa na majengo yakakamilika kabisa hapo ndiyo tutakuja kwa awamu nyininge sasa ya kuanzisha wilaya mpya na halmashauri mpya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kata za Isaka, Mwalugulu, Isakajana pamoja na Mwakata walishakamilisha mchakato wa kuanzisha Halmashauri au Mamlaka ya Mji Mdogo wa Isaka na taratibu zote ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezielezea hata hapa hadi kufika hatua ya kufika kwenye ofisi ya Waziri mhusika wameshafikia. Nataka kujuu tu ni lini sasa hatimaye Mamlaka ya Mji Mdogo wa Isaka itaanizhwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, anataka kujuu ni lini, *please* mjibu kwa kifupi sana, kama bado mwambie bado.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Ezekiel Maige kwamba maombi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Isaka yameshapokelewa, yanafanyiwa kazi, lakini tunawaomba wananchi wasubiri pale ambapo tutakuwa tayari mara moja tutatangaza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Manispaa ya Moshi Mjini tayari imekidhi vigezo vyote na kikubwa zaidi ina Milima Kilimanjaro ambayo ni *highest pick in Africa*. Nataka kujuu *process* inaendelea vipi mpaka sasa hivi bado hatujapata majibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamwelewa vizuri Mheshimiwa Susan Lyimo kwa sababu Moshi tayari ni Manispaa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuipandisha kuwa jiji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay* kuipandisha kuwa jiji. Pamoja na alivyosema kwamba imekidhi vigezo lakini bado hatujapata maombi rasmi kutoka kwenye vikao vinavyohusika kwa hivi karibuni....

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kama anazungumzia maombi ya zamani lakini ya hivi karibuni hatujapata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ukishamjibu maombi hamjapata basi, unaenda kukaa tu wewe.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

Na. 180

**Serikali Kurejesha Mikopo Kwenye  
Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile *LAPF, PSPF, PPF, NSSF* na *NHIF* mesaidia sana kutoa mikopo hasa kwa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya jamii:-

Je, Serikali imefanya juhudhi gani kurejesha mikopo hiyo kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Serikali ilifanya uhakiki wa deni la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii linalotokana na mikopo ya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ili kuandaa utaratibu wa malipo. Jumla ya deni lililowasilishwa Serikalini kwa ajili ya uhakiki kwa mifuko yote ni shilingi trilioni 2.1 na deni liliokubalika baada ya uhakiki ni shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uhakiki kukamilika, Serikali ilianza kuandaa utaratibu wa kulipa deni hilo kwa kutumia hati fungani maalum zilizotarajija kuiva ndani ya kipindi cha kati ya miaka mitatu (3) na 20. Hata hivyo, wakati zoezi la kuandaa hati fungani likiendelea, Serikali ilipendekeza na Bunge lako Tukufu kuridhia mapendekezo ya Serikali ya kuunganisha Mifuko ya Pensheni na kuunda Mifuko miwili mmoja kwa ajili ya sekta ya umma na mwingine kwa ajili ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo, ilisababisha Serikali kusitisha zoezi la kuandaa na kutoa hati fungani maalum hadi hapo taratibu za kuunganisha Mifuko ya Pensheni zitakapokamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili ni la muda mrefu sana kabla hata dhana ya kuunganisha Mifuko ilikuwa haijafikiwa, ndio linakuja leo. Pamoja na mambo hayo nitakuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la trillioni 2.1 ndani yake kuna malimbikizo makubwa ya riba ambayo yamesababishwa na Serikali kwa kutokulipa kwa muda mrefu. Mifuko bado haijaunganishwa lakini riba haisubiri Mifuko kuunganishwa inaendelea. Ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha kwamba Mifuko hii inaunganishwa haraka ili kunusuru riba hii isiongezeke? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sheria tayari imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais na kanuni zimeshakamilika. Ndani ya mwezi huu wa Tano Serikali inazipeleka kanuni kwa wadau ili tuweze kupata maoni yao na sisi kama Serikali tunatambua umuhimu wa kuiwezesha Mifuko kwa madeni yao haya, tuko tayari kulipa pale kanuni zitakapokuwa zimekamilika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, deni linalipwa, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Nagu.

Na. 181

### **Kupungua kwa Ruzuku za Pembejeo Wilaya ya Hanang**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Wilaya ya Hanang ni mionganini mwa Wilaya zinazozalisha kwa wingi nafaka za mahindi, ngano na shayiri lakini inashangaza kuona kuwa ruzuku ya pembejeo imepungua kutoka vocha 20,000 kwa mwaka 2012/2013 hadi vocha 10,000 mwaka 2014/2015:-

(a) Je, ni kwa nini vocha zimepungua na lini Serikali itaanzisha mfumo mpya wa pembejeo?

(b) Je, Serikali inatumia utaratibu gani kuhakikisha kwamba Mawakala wa pembejeo hawawauzii wananchi kwa bei kubwa kuliko bei ya soko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, bajeti ya ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha ilitokana na mchango wa fedha za Serikali na Benki ya Dunia hivyo kupelekea kuwa na vocha nyingi ambapo Wilaya ya Hanang kaya 20,000 zilinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwaka 2015/2016 bajeti ya ruzuku ya pembejeo kwa kutumia vocha ilitokana na mchango wa Serikali pekee na hivyo kupungua kwa idadi ya vocha zilizotolewa, ambapo idadi ya kaya katika Wilaya ya Hanang ilipungua na kufikia kaya 10,000 ikilinganishwa na mwaka ule wa 2012/2013.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha mfumo wa usambazaji wa pembejeo kwa wakulima, kuanzia msimu wa 2017/2018, Serikali inatumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja kwa maana ya *Bulk Procurement System*, ambao umeongeza upatikanaji wa mbolea kwa wingi, bei nafuu na kwa wakati. Aidha, kwa kutumia utaratibu huo, bei za mbolea aina ya *DAP* na *Urea* zimepungua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja hutoa bei elekezi kwa kuzingatia umbali kutoka makao makuu ya wilaya kwenda kwenye kata na viji. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (*TFRA*) inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na pindi ukiukwaji wa bei elekezi unapobainika hatua stahiki zinachukuliwa kwa wahusika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali langu vizuri. Swali la kwanza, kama Waziri alivyoeleza ni kwamba mfumo umebadilika lakini kama ilivyo kule Hanang bei bado haijashuka na madhumuni ya kuwa na mfumo huu wa sasa ni kushusha bei. Nataka kujua kwa nini bei haijashuka mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, mfumo wa sasa unapaswa kuwafikia wakulima wote badala ya ule wa ruzuku kufikia watu wachache peke yake. Hata hivyo, nataka kujua kwamba huu ununuzi wa pamoja wa mbolea kama kweli umewanufaisha watu kama wanavyotarajia na kama Serikali inavyotaka na kama sivyo watuambie ni msimu upi mfumo huo wa sasa utanufaisha wakulima wote kuliko ilivyokuwa pale awali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo amekuwa akishugguhulikia suala zima la mbolea na mfumo wa pamoja na ukizingatia yeye alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maswali yake mawili ya nyongeza ni kwamba ni kweli bei haijashuka kwa sababu mfumo huu tumeuanza sasa hivi na matokeo yake mazuri tutayaona kuanzia msimu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile swalı lake la pili ni kwamba mbolea yetu ambayo tunasema ina bei elekezi ya Serikali tunapaswa tuwaambie wananchi wote wasubiri msimu unaotakiwa ili iuzwe kwa pamoja lakini vilevile hata wale wazabuni wetu tunataka wawe wanafanya *order* kwa wingi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nitoe ushauri, hata wale wafanyabiashara kwenye yale maghala

yao wajenge kwa wingi ili maghala yale kulekule katika halmashauri wawe wanazalisha ili huu msimu unapofika basi wananchi na wakulima wetu waweze kupata mbolea zile kwa wakati na kwa pamoja inavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joram, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Hawa.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Wakulima wa zao la chai, hasa wakulima wadogowadogo wamekuwa wakinunua pembejeo kwa bei ya juu sana. Ni lini Serikali itatoa mbolea ya ruzuku, kwa maana ya pembejeo ya ruzuku kwa wakulima hawa wadogo kama ilivyo kwenye mazao mengine ya korosho na pamba, ili waweze kupata faida kutokana na kilimo hiki cha chai? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwaambie kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote, msimu huu tumeamua kwamba hakutakuwa na bei yoyote ya ruzuku kwenye mbolea. Ndiyo maana hata kwenye *sulphurambayo* ilikuwa inatolewa kwa ruzuku, safari hii tumeamua kwamba na yenyewe iwe inauzwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, Mheshimiwa Naibu Waziri anafanya kazi nzuri, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa butura ulikuwa unamsaidia sana mkulima wa kahawa Mkoa wa Kagera kupunguza ukali wa maisha wakati anasubiri kuvuna

kahawa shambani. Je, Serikali imejipangaje kumsaidia huyu mkulima baada ya kuzuia uuzaaji wa butura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Anajibu Waziri husika, haya kubwa lao, majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, butura ni mfumo ambao wakulima wamekuwa wanauza mazao kabla hawajavuna na ni mfumo ambao umewanyonya kwa miaka mingi. Ndiyo, walikuwa wanapata fedha lakini fedha wanayopata hailingani na thamani ya mazao yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ni mfumo ambao sasa hivi Serikali inahakikisha kwamba hautaendelea. Badala yake Vyama vya Ushirika vimeshawishiwa na tunavisaidia kuweka utaratibu ambao utakuwa unaweza kuwawezesha wakulima wenyewe shida ndogondogo badala ya kuuza mazao kwa bei za chini sana ambazo wananyonywa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salome, jiandae Mheshimiwa Hawa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utii wa mgongo wa nchi hii uko kwenye kilimo. Tunategemea kilimo ili tuweze kupata maendeleo kwenye nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome uliza swali, wewe swali unachomekea halafu unaleta utaalami.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali. Shinyanga na Kahama tunaongoza kwa kilimo cha mpunga na mahindi. Mpaka sasa ninapoongea ruzuku imepungua kwa zaidi ya 50%. Nini mpango wa Serikali kuongeza ruzuku ili tuweze ku-*improve* kwenye kilimo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Wajiandae Mheshimiwa Hawa, Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Aisha Matembe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amezungumzia kwenye zao la mpunga na mahindi na juu ya kuongeza ruzuku. Nilipokuwa najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli nimesema kabisa kwamba hatutakuwa na ruzuku kwa mwaka huu kwa sababu mazao yote yawe ya kimkakati, yawe yale ya nafaka, wote watakuwa wanunuia isipokuwa kwa bei elekezi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa kama swali lako ni hilohilo basi ukae tu, uliza kama ni jipya. (*Kicheko*)

**MHE. HAWA S. MWAFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Chama cha Msingi cha Imalamakoye AMCOS kimesababishia hasara kubwa wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Urambo ya zaidi ya Dola 19,500 sawa na Shilingi za Kitanzania milioni 40 na zaidi na hivyo kusababisha kushindwa kununua pembejeo kwa ajili ya kilimo chao cha tumbaku. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa illi Chama hiki cha Imalamakoye kiweze kuwalipa pesa zao waweze kupata pembejeo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii pia na ye ye kumpongeza kwa jinsi anavyofuatilia suala zima hili la tumbaku. Ni kweli kwamba hii *AMCOS* ya Imalamakoye ambayo ameisema imekuwa ina matatizo, kumekuwa na ubadhirifu katika na mpaka sasa hivi tunapozungumza ni kwamba Mwenyekiti wa Bodii ameshashtakiwa na kesi hii iko Polisi, uchunguzi unaendelea kufanyika. Mara itakapobainika basi hatua kali sana za kisheria zitachukuliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Msimu uliopita mbolea na mbegu Mkao wa Rukwa hazikufika kwa wakati na hazikuwa na *impact* yoyote. Je, msimu unaokuja atatuhakikishia kwamba mbolea na mbegu zitafika kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Wajiandae Mheshimiwa Aisha na Mheshimiwa Chegeni.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi la Mheshimiwa Dkt. Nagu, nilijibu kabisa kwamba Serikali imeshajipanga kuhakikisha kwenye msimu ujao mbolea inafika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aisha, Mheshimiwa Chegeni na Mheshimiwa Katani.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

**MWENYEKITI:** Naomba muulize maswali mafupi.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkao wa Singida unazalisha kwa wingi mazao ya biashara na chakula kama vitunguu, mahindi, alizeti na viazi vitamu. Tatizo kubwa liliopo kwa wakulima wetu ni bei kubwa ya pembejeo pamoja na zilizopo sokoni kukosa ubora. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa bei zilizokwu nzuri lakini zina ubora wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pembejeo zinanunuliwa lakini sisi kama Wizara ya

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kilimo tuna Mfuko wetu ule wa Pembejeo ambao tunatoa mikopo yake kwa asilimia saba au nane kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni na Mheshimiwa Katani.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa swalii zima limejikita kwenye mambo ya pembejeo; na kwa kuwa wakulima wengi sana wa mazao kama ya pamba, muhogo, chai na hata korosho, wamekumbwa na tatizo la wadudu waharibifu. Kwa mfano, wakulima wa pamba na wakulima wa mahindi wanazumbuliwa na yule *fall armyworm* wakulima wa muhogo wanazumbuliwa na *cassava mealybug*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kumwondolea adha mkulima ambaye anajitahidi kulima sana lakini anazumbuliwa na hawa wadudu au viwavijeshi ambao ni waharibifu zaidi? Nataka tamko la Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *American fall army worm* wameonekana kwa mara ya kwanza nchini mwaka jana. Jitihada ya Serikali iliyofanyika ya kwanza ili kuwa ni kuhakikisha elimu inawafikia wakulima wote namna ya kukabiliana na hawa wadudu. Kwa hivyo, tulichokifanya ni kueneza hii elimu lakini na kufanya utafiti wa haraka kubaini ni aina gani ya dawa inayoweza kuuwa hawa wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa hiyo tumekwishaitangaza ili mwananchi akiona mazao yake yanashambuliwa atumie dawa hiyo kuuwa hawa wadudu. Tunafanya hivyo na kwa visumbufu vingine vyamea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mheshimiwa Ngombale na siyo Mheshimiwa Katani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mwaka huu ilijielekeza kwamba sisi wa zao la ufuta tutatumia Stakabadhi Ghalani...

**MWENYEKITI:** Ulikuwa unasemaje?

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mheshimiwa Vedasto Ngombale sio Mheshimiwa Katani.

**MWENYEKITI:** Basi kaa chini kama siyo Mheshimiwa Katani. (*Kicheko*)

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Katani hayupo kwa leo. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Haya, endelea basi.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru baada kuwa sasa umetambua jina langu vizuri. Ninachosema ni kwamba Serikali ilielekeza mwaka huu katika zao la ufuta utaratibu wa manunuzi utafanyika katika Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na kwamba mikoa yote inayolima ufuta itatakiwa kuingia katika mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninavyozungumza ufuta umeshakuwa tayari na kuna baadhi ya mikoa tayari wameshaanza kuuza katika mfumo holela na Serikali iko kimya haijasema chochote. Naomba kufahamu, je, tutaingia katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani au tutaendelea katika utaratibu ule amba tulikuwa tumeufanya mwaka jana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali hilo ni jipya, lakini lijibu kwa sababu wewe ni mtaalamu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli kwamba, ufuta ni moja ya zao ambalo Serikali ilidhani na inatarajia kuliweka kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, lakini ili uingie kwenye huo mfumo yako maandalizi ya msingi ambayo lazima yafanyike vinginevyo mfumo hautafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi tunakamilisha hayo maandalizi, tutakuwa na mku الوا wa wakuu wa mikoa yote inayolima ufuta ili tujiridhishe kwamba maandalizi hayo yako *in place* tuweze kuanzisha mfumo wenye.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Injinia Ngonyani.

Na. 182

### **Ujenzi wa Chuo cha VETA Namtumbo**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Namtumbo:-

(a) Je, gharama za ujenzi wa chuo hicho hadi kinakamilika ni kiasi gani?

(b) Je, ni lini ujenzi wa chuo hicho utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** aliibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inategemea kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha VETA cha Wilaya ya Namtumbo kwa makadirio ya Sh.6,321,320,292.40.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi ilianza mwezi Machi, 2017 na inakadiriwa kuchukua muda wa miezi 18. Hivyo, ujenzi wa chuo hicho unategemewa kukamilika ifikapo Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Elimu ya Ufundı na Mafunzo ya Ufundı Stadi, itaendelea na ujenzi wa vyuo hivyo kwa ajili ya kuandaa Rasilimali Watu watakaotumika katika viwanda ili kufikia lengo la Serikali kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025. Aidha, vyuo hivi vitasaidia kuwapatia vijana wetu ujuzi utakaowawezesha kujajiri na kuajiriwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wanamatumbo hawafahamu ni majengo gani yanayojengwa na wapo wanaosema kwamba linajengwa jengo la bwalo la chakula, nyumba za wakufunzi, nyumba za kulala wanafunzi, kwa hiyo wanahisi tu hawajui. Je, Serikali iko tayari kuwaeleza wananchi wa Namtumbo kwanza, hizo hisia zao kama ni sahihi na kama sio sahihi ni majengo gani yanayojengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Profesa Ndalichako alipofika Namtumbo watu walikuja kupata taarifa baada ya yeye kuondoka na walipobeba ngoma zao kwenda kumshangilia wakakuta hayupo, je, yupo tayari hicho chuo kitakapokamilika ama yeye, kwa sababu wakimwona yeye ni sawa wamemwona Mheshimiwa Rais au kiongozi yejote wa ngazi ya juu aje akifungue kile chuo ili wale wananchi waondoe kiu yao ya kutaka kuwaona viongozi wao wanaowapenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni majengo gani yanajengwa katika ujenzi unaoendelea, naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa majengo ambayo yanajengwa ni jengo la utawala, karakana za ufundi seremala, uashi, bomba, umeme wa majumbani na maabara ya komputa. Majengo mengine ni pamoja na madarasa, maktaba na stoo ya *generator* lakini katika awamu zitakazokuja tutajenga majengo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili kama Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda wakati wa ufunguzi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa namna Serikali inavyotilia mkazo suala la ufundi na namna ninavyomfahamu Mheshimiwa Waziri anavyosisitiza masuala hayo Wizarani, nina hakika kwamba atakuwa tayari kwenda katika ufunguzi lakini hata baada ya kusikia kuna ngoma hata mimi nafikiri nitaungana naye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekwenda, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea kwa niaba yake Mheshimiwa Mwambe.

Na. 183

**Ujenzi wa Barabara ya kutoka Kimara  
Mwisho-Barabara ya Nyerere**

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. SAED A. KUBNEA)**  
aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete iliahidi kujenga kwa lami barabara ya kutoka

Kimara Mwisho kupitia Mavulunza – Bonyokwa Segerea hadi kuungana na barabara ya Nyerere yeny urefu wa Kilomita 4.7 na ambayo imekasimiwa kwa *TANROADS*:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo kwa lami kama ambavyo iliahidiwa miaka mitano iliopita?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hiyo ili kupunguza tatizo la foleni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, lenye kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Kimara Mwisho kupitia Mavulunza - Bonyokwa hadi Segerea hadi kuungana na barabara ya Nyerere yeny urefu wa kilomita nane (8) unategemea kuanza mara baada ya kukamilisha utekelezaji wa mpango wa sasa wa ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano Jijini Dar es Salaam unaendelea vizuri. Mpaka kufikia mwezi Aprili, 2018, ujenzi wa barabara ya Banana - Kinyerezi – Kifuru – Marambamawili - Msigani hadi Mbezi Mwisho yeny urefu wa kilomita 17, ambayo inaunganisha barabara ya Nyerere na Morogoro umefikia asilimia 90. Kwa sasa ujenzi unaendelea ili kukamilisha sehemu ya barabara iliyobaki yeny urefu wa kilomita mbili (2) kuanzia Msigani mpaka Mbezi Mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa barabara hii kutaunganisha barabara ya Nyerere, Morogoro na Bagamoyo kupitia barabara ya Mbezi Mwisho, Goba, Tangi Bovu ambayo ujenzi umekamilika.hata hivyo, Serikali inaendelea

kutenga fedha za matengenezo ya barabara ya kutoka Kimara Mwisho – Bonyokwa - Segerea ili kuhakikisha inapitika vizuri wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, ukiangalia majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba baada ya kukamilika barabara ya Kinyerezi - Mbezi ndipo wanapotegemea kuanza ujenzi wa barabara hii inayoongeleta hapa na Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba hizi ni barabara mbili tofauti na mahitaji ya wananchi wale ni tofauti. Tunataka kufahamu ni lini Serikali *specifically* itaanza ujenzi wa barabara inayotajwa ilioyahidiwa miaka mitano iliyopita? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, suala lililopo Jimbo la Ubungo linafanana moja kwa moja na masuala yaliyopo katika Jimbo la Ndanda, Mkoa wa Mtwara kwamba Serikali iliahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Mtwara Mjini – Nanyamba – Tandahimba – Newala - Masasi mpaka Nachingwea kuja kutokea Nanganga. Sasa tunataka kufahamu pamoja na mkandarasi kuwepo pale ambaye anasuasua kwenye kazi hii, ni lini Serikali *specifically* itaanza ujenzi wa barabara inayotokea Masasi kwenda Nachingwea kuja kutokea Nanganga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu na umeona Wabunge walivyosimama hapa kuhusu barabara. Wengine mtasubiri utekelezaji wa bajeti.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika barabara ambazo nimezitaja awali ndiyo zilikuwa na matatizo makubwa na ndiyo zilikuwa kipaumbele. Niseme tu kwamba nafahamu

maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia ni korofi na kama nilivyosema tutaendelea kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo matatu ambayo tulikuwa tunaendelea nayo kuhakikisha kwamba barabara hii inatoa huduma iliyokusudiwa wakati sasa tukikamilisha hii barabara ni fursa tosha kuja kuijenga barabara hii. Yako maeneo pale Kwa Bichwa, Kwa Mahita na eneo la Makange Sekondari ndiyo zilikuwa sehemu korofi. Alikuwepo mkandarasi anaendelea kurekebisha maeneo yale lakini kutokana na mvua nyingi zilizonyesha amesimama kidogo ili hali ya hewa ikiwa nzuri hii barabara tuiimarishe halafu baadaye sasa wakati barabara hizi zinakamilika ni fursa tosha kuja kuijenga hii barabara kama ahadi ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Ndanda kuja Nachingwea kupitia Nanganga kama tulivyoizungumza katika bajeti tumetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kipande hiki kutoka Nachingwea - Nanganga na Nachingwea – Ruangwa – Nanganga. Mheshimiwa Mbunge anafahamu pia liko daraja katika Mto Lukuledi tunaendelea kulijenga na hii ni sehemu ya kukamilisha barabara hii anayoitaja ili sasa tuweze kuunganisha kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsihi tu Mheshimiwa Mbunge avute subira na wananchi wa Ndanda wategemee kwamba barabara hii tunaenda kuikamilisha ili waendelee kupata huduma kama wananchi wengine katika maeneo ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, jiandae Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekita, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na juhudzi za Serikali za kuweka barabara nyingi za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam hatua ambayo naipongeza, lakini ninalo swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nzasa - Kilungule kuungana na Buza ni muhimu sana kwa wakazi wa Mbagala katika kuondoa msongamano. Je, Serikali lini itaanza ujenzi wa barabara hiyo? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, wajiandae Msabaha, Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa amekuwa akifuatilia barabara nyingi lakini nimhakikishie kwamba katika harakati za kukwamua msongamano katika Jiji la Dar es Salaam barabara 12 zimekamilika. Ziko barabara 10 ambazo mpaka kufikia mwezi Aprili tunaendelea nazo lakini ziko barabara nyingine ambazo tutazishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali iko committed kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linafunguka. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge hii barabara anayoizungumza kutoka Nzasa – Kilungule - Jeti Kona itashughulikiwa na mradi wa DMDP. Nitajaribu kufuatilia baada ya mkutano wa leo ili nione hatua ilivyo na nitampa mrejesho lakini niombe tu tuendelee kushirikiana na kupeana taarifa kwa sababu lengo la Serikali ni kurekebisha maeneo mbalimbali ili yaweze kuitika vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msabaha, jiandae Mheshimiwa Hussein.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nimuuilize Naibu Waziri swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa hizi barabara zimekuwa zikijengwa kwa gharama kubwa sana, halafu zinaharibika kwa muda mfupi, je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha wakandarasi wote wanaojenga barabara hizi wanachukuliwa hatua na kurudia ujenzi ili kuepusha kutumika tena gharama nyingine ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kuna baadhi ya maeneo baada ya barabara kutengenezwa zinaharibika, lakini ni hali ya kawaida kwa sababu ziko sababu nydingi ambazo zinaweza kusababisha miundombinu hii kuharibika. Ndiyo maana baada ya ujenzi wa barabara katika kipindi cha maisha ya barabara tunatenga fedha kwa ajili ya kufanya *rehabilitation* na baada ya miaka 20 tunafanya matengenezo makubwa kwa maana kwamba ule muda wa maisha ya barabara unakuwa umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali...

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Hussein na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alikuja jimboni na akaahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama – Nyang’olongo – Bukwimba - Kalumwa - Busolwa hadi Busisi Sengerema na Rais wa Awamu ya Tano pia aliahidi hivyo hivyo. Je, Serikali ni lini itatenga fedha ya upembuzi yakinifu ili kuanza kujenga barabara hiyo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hii barabara Mheshimiwa Mbunge tumezungumza mara nydingi, ni barabara ambayo inaenda kuunganisha pia katika Jimbo la Msalala kuja Kahama Mjini. Kwa hiyo, kama tulivyozungumza tutaangalia sasa namna nzuri tuweze kuiingiza kwenye usanifu, kwa sababu zile barabara ambazo zinakwenda kuunganishwa na barabara hii Mheshimiwa Mbunge, unajua ile barabara inayokwenda

Geita ni muhimu sana kwamba tutaweza kuwa na kipande cha kwenda Sengerema. Ni kipande kifupi Mheshimiwa Mbunge kinahitaji *commitment* ya fedha siyo nyingi sana. Kwa hiyo, azidi kuvuta subira tutaendelea kutazama kwenye bajeti zinazokuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. Naomba nimuulize swali dogo Mheshimiwa Naibu Waziri. Barabara ya Kitunda – Kivule - Msongora mkandarasi yupo *site* kwa zaidi ya mwaka mzima sasa, lakini hajatekeleza kazi ile hata zaidi ya asilimia 20, amechimbachimba na kuiharibu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kwenda Kivule ili akaangalie usumbufu ambao wananchi wanapata na kulazimisha ujenzi ufanyike haraka illi watu wapate barabara ya kupita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lake uko tayari kwenda, ni hilo tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niko tayari na inawezekana kesho pia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wetu mdogo, inatosha. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Deo Ngalawa.

Na. 184

#### **Hitaji la Bandari – Wilaya Ludewa**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Bandari katika mwambao wa Ziwa Nyasa kutoka moja kwenda nyingine zipo kwa umbali mrefu sana hususan upande wa Wilaya ya Ludewa; hii imekuwa ni kero kubwa kwa sababu hakuna miundombinu ya barabara ambayo ingerahisisha huduma ya usafiri:-

(a) Je, ni lini Serikali itatupatia bandari katika Vijiji vya Nkanda, Nsele, Kyaghomi, Makonde na Yigha?

(b) Je, ni lini huduma za usafiri wa meli zitaanza tena ili kupunguza kero ya usafiri kwa wananchi waishio kandokando ya Ziwa Nyasa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) ina mkakati wa kuboresha na kujenga miundombinu ya bandari na gati mbalimbali katika Ziwa Nyasa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali kuititia *TPA* ilitenga fedha kwa ajili ya kuendeleza Bandari za Mbambabay, Itungi, Kiwira, Ndumbi, Manda, Matema, Liuli na Lupingu Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hiyo, bado kuna timu toka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania inafanya usanifu wa awali katika vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mbunge vya Nkanda, Nsele, Kyaghomi, Makonde, Yigha na maeneo jirani. Baada ya usanifu wa awali, Serikali itatambua maeneo gani yanafaa kuweka vituo vya kushusha na kupakia abiria na mizigo ili kuwaondolea adha abiria katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado inaendelea kumalizia ujenzi wa meli ya abiria itakayotoa huduma katika eneo la Ziwa Nyasa, hivyo tunatumaini wananchi watapata huduma ya usafiri wa meli kabla ya mwaka huu 2018 kwisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kutokana na usanifu ambaao unafanyika sasa na timu ya wataalam wa bandari ili eneo hili liweze kupatiwa vituo vya kushusha na kupakia abiria, je, timu hii ni lini itamaliza kazi hiyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tayari kuna tengo la mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kujenga gati katika Bandari za Lupingu na Manda. Je, wananchi hawa ambaao walipisha maeneo haya watalipwa lini fidia yao ili waendelee na shughuli nytingine? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA - NAIBU WAZIRI WA UJENZI,  
UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia sana huduma ya usafiri wa majini lakini huduma ya usafiri wa nchi kavu. Niseme tu kwamba zoezi hili litakamilika kwa muda mfupi kwa sababu hivi ninavyozungumza wataalam wanaelekea maeneo haya na najua adha wanayoipata wananchi kule ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, litakapokuwa limekamilika, siyo lazima vijiji vyote alivyovitaja tuweze kuweka vituo vya kushusha na kupakia lakini wataweza kutambua maeneo gani ambayo yatawafanya wananchi hawa wasisafiri sehemu ndefu sana kwa ajili ya kupata huduma. Kwa hiyo, avute subira na sisi tutampa mrejesho. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo haya watoe ushirikiano ili tupate *information* za kutosha tuweze kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wale wananchi ambaao wanapisha maeneo yao kwa ajili ya maendeleo na sisi kama Serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba fedha zikipatikana tunawalipa mara moja. Kwa sababu tunajua kwamba fidia kama itachelewa kulipwa pia huduma itachelewa kwenda kwa wananchi hawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Susanne Peter Maselle.

Na. 185

**Matumizi ya Nyavu Haramu za Uvuvi za 'Single'- Mwanza**

**MHE. SUSANNE P. MASELLE** aliuliza:-

Mnamo tarehe 30 Januari, 2017, wavuvi wa maeneo ya Igombe na Ilemela Jijini Mwanza walikamatwa na kunyang'anywa nyavu, mitumbwi na mashine za mitumbwi yao na Maafisa wa Uvuvi wakidai wanatumia nyavu haramu ambazo ni "double" huku Serikali ikitaka watumie "single":-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kutoa taarifa, elimu na muda kwa wavuvi pindi inapotaka wavuvi wafanye mabadiliko katika shughuli au zana zao za kazi?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa elimu kwa wavuvi wa Igombe na maeneo mengine ya Mwanza kuhusiana na uvuvi wa kutumia nyavu za *single* badala ya *double* ili wafanye kazi zao kwa uhuru bila bughudha ya kukamatwakamatwa?

(c) Je, Serikali inataka wavuvi wavue samaki katika kina kipi cha maji na katika kina cha mita 50 na kuendelea watumie nyavu za mita ngapi kwenda chini?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa taarifa na elimu kwa wavuvi kuhusiana na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi kujitia mikutano, vipindi vyta redio na runinga. Pia, leseni za uvuvi huonyesha masharti yanayopaswa kufuatwa ili kuwa na uvuvi endelevu. Kimsingi

elimu kwa wavuvi hutolewa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na wakati wanapopewa leseni na wakati wa kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kutumia Maafisa Uvuvi wa Idara, Manispaa ya Ilemela na Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (*BMU*) imeendelea kutoa elimu kwa wavuvi wa Igombe na maeneo ya Mwanza juu ya katazo la matumizi ya nyavu za kuunga kwa maana ya *double*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wanaweza kuvua katika tabaka lolote la maji kwa kutumia nyavu zinazoruhusiwa. Isipokuwa hawaruhusiwi kuvua katika maeneo ya mazalia ya samaki na maeneo tengefu. Aidha, katika kina cha mita 50, wavuvi wanapaswa kutumia nyavu zillizoruhusiwa zisizozidi macho au matundu 26 kwenda chini kwa upande wa Ziwa Victoria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susanne.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa nini operesheni za Serikali dhidi ya uvuvi haramu zimekuwa zikijikita katika kutekeza zana haramu za uvuvi badala ya kujikita katika kuwasaidia wavuvi hawa waweweza kupata zana hizi halali kwa urahisi na kwa bei nafuu kwa kuwaondolea kodi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa uvuvi haramu unaelezwa kama moja ya tishio la kutoweka kwa samaki adimu kama ningi, nembe, gogogo, ngogwa, domodomo, sangara, njegele na sato katika Ziwa Victoria. Je, kuna mkakati wowote wa kusaidia samaki hawa kuzaliana tena ili kuendeleza fahari ya ziwa hilo na mazao yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini operesheni za Serikali zinajikita kuteketeza nyavu badala ya kuwapa nyavu halali? Operesheni za Serikali zinafanyika kwa mujibu wa sheria na operesheni hii inayofanyika kwa maana ya Operesheni Sangara inafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na.22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapa nyavu za bei nafuu wavuvi ni utaratibu ambao tunao pia na ndiyo maana tumetoa punguzo la kodi na hata kuondoa baadhi ya kodi katika vifaa hivi vya uvuvi ili kusudi kuweza kuwasaidia wavuvi wetu. Kama haitoshi tumeanzisha programu maalum ambazo kwa kutumia hata Mifuko yetu ya kijamii kama vile *NSSF* kuwafanya wavuvi waweze kujiunga katika vikundi ili waweze kupata mikopo na kuweza kununua nyavu kwa bei nafuu na vifaa vingine kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni kutoweka kwa samaki kama vile gogogo, nembe na furu. Tumeendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa kutumia taasisi yetu ya utafiti ya *TAFIR*/ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kulinda rasilimali hizi za nchi kwa ajili ya vizazi vya leo na vizazi vijavyo. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote waweze kutuunga mkono katika jambo hili kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Bilago na Mheshimiwa Sware.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Serikali imekuwa ikichoma haya makokoro kila mara tani na tani, si muda muafaka sasa Serikali ikashughulika na wale wanaoingiza na wanaotengeneza hizi nyavu haramu nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashughulika na ndiyo maana mwaka huu mwanzoni tumekamata nyavu nyingi sana za wazalishaji wa *Sunflag* kule Arusha ambazo tumeziteketeza. Tumeteketeza nyavu za waagizaji kutoka nje ya nchi badala ya ku-deal na wavuvi wadogo wadogo tu. Kwa hivyo, tunashughulika na wazalishaji, waagizaji na wauzaji pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sware, jiandae Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sware jiandae, Mheshimiwa Bilago, vipi?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sware, jiandae baadaye Mheshimiwa Bilago.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Napenda kujua kwa nini Serikali hajikiti katika kuviimarisha Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvubi yaani *BMU's* ili kuweza kuwa na uhakika wa uendelevu wa usimamizi wa rasilimali hizi na wenyewe kuleta tija? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi, jiandae Mheshimiwa Bilago.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *BMUs* zipo kwa mujibu wa Sheria ya Uvubi Na 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake lakini pia inatambulika na Sheria ya Ugatuaji wa Madaraka kwa maana ya *D by D*. Sisi tunaendelea kuzitumia *BMUs* na katika maboresho yetu ya sheria ambayo tunayategemea kuingia katika

mwaka huu tutahakikisha kwamba tunazipa nguvu zaidi na mwongozo zaidi ili *BMUs* ziweze kufanya kazi vile ambavyo inatakiwa kwa sababu *BMUs* ni mali ya wananchi wenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Kakonko ina wafugaji wa samaki waliojunga kwenye vikundi katika Vijiji vya Nagwijima, Kasanda na Nyabibuye. Swali langu, Waziri yuko tayari kuwasaidia mikopo, ruzuku au chochote kile watu hawa ambao wametumia nguvu yao na nguvu ya Mbunge kutokana na Mfuko wa Jimbo ili waweze kuendeleza ufugaji wa samaki? (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko tayari kama Serikali kuwasaidia wafugaji wa samaki na ndiyo maana katika mapendelekezo ya sheria na bajeti mwaka huu atakuja kuona kwamba tumependekeza kuhakikisha kodi na tozo mbalimbali zinazofanya tasnia hii ya ufugaji wa samaki isisonge mbele ziweze kupunguzwa ama kufutwa ili kusudi tuweze kuwasaidia wafugaji wa samaki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na maswali yote yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni:-

Wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wajasiriamali walioshiriki kwenye Tamasha la Sanaa na Utamaduni la Jumuia ya Afrika ya Mashariki liliofanyika Mjini Kampala nchini Uganda mwezi Septemba 2017. Karibuni. (*Makofî*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Wageni nane (8) wa Mheshimiwa Hussein Amar ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 46 wa Mheshimiwa Omari Kigoda ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Handeni, Mkoa wa Tanga. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 43 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Kwaya ya Uvuke kutoka Kanisa la Anglikana la Jijini Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 34 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wana maombi kutoka Jijini Dodoma. Karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofi*)

Wageni wanne (4) wa Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* ambao ni wafanyakazi wa *Bank of Africa (BOA)* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 50 wa Mheshimiwa Ahmed Shabiby ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mkoani Morogoro. (*Makofi*)

Wageni wawili (2) wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea ambao ni rafiki zake kutoka nchini Uhlanzi. (*Makofi*)

Wageni watano (5) wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni familia yake kutoka Tunduru, Mkoani Ruvuma. (*Makofi*)

Pia kuna Wageni 35 wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni wachezaji na viongozi wa Timu ya *Majimaji Rangers*. Timu hii ni Mabingwa wa Soka la Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Wageni watatu (3) wa Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete kutoka *International Republican Institute (IRI)*. Karibuni. (*Makofii*)

Wageni waliotembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 66 na Walimu watatu (3) kutoka Shule ya Msingi *Canon Andrea Mwaka* ya hapa Jijini Dodoma. Karibuni. (*Makofii*)

Wanafunzi 19 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara – *CBE* cha hapa Jijini Dodoma. Karibuni. (*Makofii*)

Utambulisho wa Mtumishi wa Mungu Mwalimu Christopher Mwakasege katika Ukumbi wa Bunge. Mwalimu Mwakasege yupo katika *Gallery* ya Spika muda huu tunaomba tumtambue, karibu Mwalimu Mwakasege. (*Makofii*)

Tangazo la Ibada kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuhudhuria ibada katika Ukumbi wa *Basement* leo siku ya Ijumaa tarehe 4 Mei, 2018, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana. Leo tutakuwa na Mtumishi wa Mungu Mwalimu Christopher Mwakasege katika Ibada hiyo. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Mwalimu Christopher Mwakasege akiambatana na Mke wake Diana Mwakasege na timu yake. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Tayari.

**MWENYEKITI:** Jamani nimetangaza mwanzo na sasa naagizwa kutangaza mgeni wa Spika. Spika ndiye mwenye nyumba likija tangazo lake lazima niliseme. (*Makofii*)

Tangazo la mechii za kirafiki, Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anapenda kuwatangazia Wabunge wote na wananchi kwa ujumla kwamba kesho tarehe 5 Mei, 2018 katika Uwanja wa Jamhuri

wa Dodoma kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club (Ndugai Boys)* na *BOA Bank*, mechi itaanza saa 10.00 jioni. Aidha kuanzia saa 1.30 jioni kutakuwa na mchapalo kwa Waheshimiwa Wabunge wote utakaofanyika katika hoteli ya *Royal Village*. (*Makofi*)

Pia tarehe 6 Mei, 2018 siku ya Jumapili kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Ndugai Boys* na *Ilala Veterans* katika Uwanja huo huo wa Jamhuri kuanzia saa 10.00 jioni. Mechi zote zitatangazwa mubashara kupitia Kituo cha *Azam Television*. Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa ujumla mnakaribishwa kushuhudia mechi hizo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Kalanga, Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Hasna. Tuanze na Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Kanuni ya 68(7) siwezi kuisoma kwa sababu ya muda. Wakati Naibu Waziri anajibu swali langu la nyongeza kupitia swali la 181 kuhusu mbolea na mbegu katika Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine, Serikali ilikuwa inatoa majibu haya haya kila mwaka lakini hakuna hata mwaka mmoja mbolea na mbegu zilifika kwa wakati katika Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine katika nchi hii na kusababisha shida kwa wakulima wanakuwa kama wanyonge wakati wanalima kwa nguvu zao wenyeewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa Serikali inihakikishie kwamba msimu unaokuja mbolea na mbegu zitafika kwa wakati ama sivyo wajizulu kuanzia Waziri, Naibu

Waziri na Makatibu wao kwa sababu imekuwa ni shida sana kwa wakulima, kila mwaka inatokea hivi. Majibu ya Waziri ni haya haya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako wanipe jibu la uhakika kwamba msimu huu haitakwenda mbolea kwa kuchelewa katika mikoa yote ya wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Keissy ushaeleweka.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7). Kulikuwa na swali namba 182 lilitojibwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na kwa kuwa swali hili la Wizara ya Elimu linaonesha umuhimu wa teknolojia katika kukuza elimu lakini kwa kuwa kwa hivi sasa katika mitandao kunaoneshwa vitabu vya elimu ambavyo kwa kweli mimi naviita ni vya hovyo ambavyo havifai kabisa na huenda vimetengenezwa kwa teknolojia mbovu au kwa makusudi au kwa kupotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itoe uafanuzi nini kauli ya Serikali kuhusu vitabu hivi ambavyo havifai kabisa vinavyosambaa katika mitandao. Naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kwa haraka natumia Kanuni ya 68(7), niko nayo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wanalipa kodi. Hata hivyo, katika siku za karibuni kila wananchi wanapoenda kufanya malipo mbalimbali ya Serikali wanaambiwa kwamba mtandao upo chini. Mfano mzuri ni kodi ya ardhi, mpaka Mheshimiwa Waziri amelazimika kuongeza siku mpaka tarehe 30 Mei, 2018 kwa sababu kila unapoenda kufanya malipo mtandao uko chini hali ambayo

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

inawafanya wananchi wavunjike moyo kufanya malipo ya Serikali. Sasa ni nini kauli ya Serikali katika jambo hili, je, ni hujuma ama ni uzembe ama ni nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasna, jiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali langu namba 179, kwenye maswali mawili ya nyongeza niliyoyaauliza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kitu tofauti kabisa na kile nilichouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia kwamba vigezo vyote anavyovihitaji yeye tulishafanya na tayari *document* zillishakwenda Wizara ya TAMISEMI. Nilichotegemea, Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie kwamba *documents* walishazipokea na kwamba lini taratibu za kugawanya jimbo na kuutangaza Mji Mdogo wa Nguruka zitafanyika, lakini badala yake amejibu kitu tofauti kabisa yaani kama vile anaturudisha tukaanze mchakato mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ni huu, jana baada ya majadiliano hapa Bungeni nilikwenda Ofisi ya Habari ya Bunge kutaka mchango wangu kama ambavyo ni haki ya kila Mbunge kupata mchango wake. Hata hivyo, baada ya kufika pale niliambiwa mchango wako utauchukua baadae. Kwenye Wizara ya Sheria na Katiba niliongea Bungeni hapa, nilipokwenda kuulizia wakaniambia na jana wameniambia pale sijui mchango wako na wa Bashe una tatizo gani, kila mkiongea Bungeni huwa hazifiki huku. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako kwamba majadiliano ya Bunge haya ni huru na mimi ni Mbunge, Waandishi wa Habari wamekwenda jana wamenyimwa *clip* za Wabunge wote wa *Opposition* ambao tumetoa michango yetu ndani ya Bunge hili hata Mheshimiwa Haonga wamenyimwa *clip* yake. Kama Bunge sasa limefika kwenye nafasi hata michango yetu ndani ya Bunge ambayo ni majadiliano huru na ushauri kwa Serikali tunaweza tukanyimwa, basi tungeni kanuni hata kuruhusu tu mtupe hizo *clip* zetu tupelekee wake zetu kama kwenye *public* nzima hamtaki ziende huko. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lema umeeleweka, Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) juu ya suala ambalo lilitokea humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Sima waliomba mwongozo wa Kiti chako kutaka kufahamu kuhusu sintofahamu kubwa iliyopo juu ya mishahara ya watumishi baada ya agizo la Mheshimiwa Rais siku ya Mei Mosi. Ongezeko la mishahara ni haki na lipo kisheria na watumishi wanapostaa fu mafao yao yanakokotolewa kwa kutumia mshahara wao wa mwisho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejapata tamko na Bunge lako linajua na jukumu la Bunge ni kuvisimamia na kuielekeza Serikali. Tunatambua vigezo na umuhimu wa mambo yanayofanyika, je, nini muhimu sasa, tuache watumishi hawa wanaumia kwa sababu tunataka kununua ndege na kukamilisha mradi wa *Stieglers Gorge*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako Serikali itoe tamko kuhusu suala hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka. Mheshimiwa Komu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7). Humu Bungeni kuna kitu ambacho kwa maoni yangu naona kama Kiti kinafanya *double standard*. Kwa sababu jana wakati Mheshimiwa Esther Matiko anachangia alimtaja *IGP* na *RPC* wa Dodoma, Kiti kikaamuru kwamba maneno hayo yafutwe kwa sababu watu hawa hawana fursa ya kujitetea humu ndani. Nakumbuka jana Assumpter Mshana, *DC* wa Kibaha alitajwa humu ndani na hakuna chochote kilichosemwa kwamba kifutwe. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Sixtus Mapunda akichangia alitaja mataifa nane yanayotuzunguka akasema yana matege na yana chokochoko. Akataja kuanzia Kenya mpaka Msumbiji lakini hakuna kitu chochote ambacho kilitolewa kama katazo. Wakati huo huo kipindi fulani Mheshimiwa Naibu Spika akiwa amekaa hapo alikataza, wakati Mheshimiwa Mbarawa akiwa anasoma hotuba yake kwamba tusitaje majina ya nchi nyingine kwa sababu kidiplomasia inaweza ikatuletea matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ni wakati gani tunaruhusiwa kumtaja mtu humu ndani au Taifa lingine humu ndani ili hili Bunge liwe na *standard* fulani ambayo tutakuwa tunaitumia. Naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natumia Kanuni ya 68(7). Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili ni chombo cha wananchi. Siku chache zilizopita wakati wa Wizara ya Elimu kulitokea mjadala mkubwa hapa kuhusu walimu waliotolewa sekondari kupelekwa *primary*. Tarehe 1 Mei Rais aliagiza kwamba watumishi wa umma wasihamishwe bila kulipwa stahiki zao na Waziri wa TAMISEMI aliwahi kujibu

humu ndani kwamba walimu wote waliohamishwa kule wapewe stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako sasa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na maeneo mengine ya nchi yetu karibu walimu 64 kutoka Monduli ambao wamehamishwa tangu Januari kutoka sekondari wamepelekwa katika shule za msingi wametii agizo la Serikali, wanafanya kazi, lakini mpaka leo Serikali hajjawalipa hata shilingi moja na kila mahali wakienda wanatishiwa kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Rais na Mawaziri hazitekelezwi na kama Bunge hili linapuuzwa, hivi wananchi wetu wa kawaida ambao hawawezi kufika hapa na kutoa malalamiko yao ni lini haki zao zitatekelezwa? Serikali hii ambayo matamko mpaka ya Rais, kama Rais hasikilizwi kwenye nchi, nani mwingine anayesikilizwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba Walimu hawa wanalipwa lini. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuhusu mbolea.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki moja na nusu iliyopita nililitangazia Bunge Iako Tukufu kwamba tutafanya semina ya Bunge zima ili kueleza namna gani mfumo wa uingizaji wa mbolea nchini unavyofanya kazi. Natumaini tukishafanya semina hiyo, maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala la mbolea yatapata majibu yake na ni wakati huo ambao Bunge pia litapata nafasi pana ya kutushauri kama kutaonekana yapo mambo ya kushauriwa ili tuweze kurekebisha au kwenda vizuri na uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea kwa ukweli tunajipanga na ni matamanio yetu pia kwamba iwe inapatikana muda wote bila kusubiria msimu au sijui kitu gani kwamba mtu akihitaji mbolea aende dukani aikute anunue.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ume-save kujiuzulu hapo.  
(*Kicheko*)

Suala la Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa ufanuzi kuhusu mwongozo ambao umeombwa na Mheshimiwa Martha Mlata wa vitabu ambavyo vimekuwa vikisambaa mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimepata nafasi ya kuona kitabu cha kiingereza cha darasa la tatu kinachosambaa mtandaoni ambapo ni kitabu ambacho kilikuwa na makosa ambayo yamekwishafanyiwa marekebisho na wahusika tayari wamekwishachukuliwa hatua. Pia kipo kitabu ambacho kinasambaa kinaonesha mwili wa binadamu na kwa kweli mishale ile imewekwa hovyo hovyo. Kitabu hicho hakijawahi kuwa sehemu ya vitabu ambavyo vimetolewa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona kwamba watu wameamua kutunga vitu ambavyo vina lengo la kuichafua Serikali na kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viro hapa leo. Kwa hiyo, naviagiza mara moja vitafute watu ambao wanatengeneza hizi taarifa za kughushi na kuchafua Serikali ili wachukuliwe hatua kwa sababu huo ni uhalifu. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, vyombo vyote viro hapa mmesikia, watu wanaichafua Serikali kwenye mitandao.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwa mwongozo wa Mheshimiwa Chumi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie.

**MWENYEKITI:** Hukusikia swali? Ameulizia kuhusu mitandao ya ulipaji kodi, wananchi wanakwenda kulipa za ardhi lakini mitandao haifanyi kazi na nyie ndiyo mnahusika na tenda hizo za mitandao.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea na tunalifanyia kazi kwa sababu nimelisikia hapa na sisi tunaendelea kulifanya kazi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na mwongozo wa Mheshimiwa Hasna Mwilima kuhusu swali na majibu, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie tena wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini kupitia kwa Mheshimiwa Mwilima kwamba wanipe muda nirudi ofisini mchana, niite *documents* zote ili niweze kumpa taarifa sahihi zaidi jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine la uhamisho wa Walimu Iilzungumzwa na Mheshimiwa Kalanga. Nitoe tu msisitizo kwamba maelekezo ya Serikali yanabaki pale pale kwamba Walimu wanaohamishwa ni lazima walipwe posho lakini kwa mujibu wa sheria. Kuna Walimu ambao wamehamishwa ndani ya kijiji, shule ya sekondari ipo kwenye kijiji kile kile na anahamishiwa kwenye kijiji kile kile, huyo halipwi, hata *disturbance allowance* halipwi kwa sababu haami nyumba, nyumba yake inaendelea kuwa ile ile. Mtu anayelipwa *disturbance allowance* ni yule ambaye anahamisha mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu wa sheria lazima ufuatwe, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema mwongozo wako tutaufanyia kazi, nalichukua.

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwambe swali lako na mwongozo wako ulishatolewa majibu na kwa mujibu wa kanuni zetu jambo ambalo lilishafanyiwa maamuzi halijadiliwi tena Bungeni. Kwa hiyo limekuwa ni *redundant*.

Mheshimiwa Komu kosa ulilolifanya umekituhumu Kiti, Kiti hakituhumiwi kwa mujibu wa Kanuni zetu. Kama una shida na Kiti unakwenda kwenye Kanuni ya 5(4), unaandika barua kwa Katibu. Siku zote huwa nawapa mifano rahisi sana ya mpirani, *referee* huwezi kumtuhumu kwa jambo lolote, *referee* anaandikiwa barua kwenye Kamati Maalum ya Saa 72. Kwa hiyo, Mheshimiwa Komu nawe mwongozo wako ni *redundant*.

Mheshimiwa Kalanga Walimu shule za msingi, Mheshimiwa Kakunda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshalijibu.

**MWENYEKITI:** Umeshalijibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ungesubiri nikuite sio unajibu tu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Waheshimiwa umeibuka mchezo sasa wa miongozo kuwa kipindi kingine cha maswali na majibu, leo niwaambie ndio mwisho. Kuanzia Jumatatu tunakwenda kwa mujibu wa Kanuni jambo lillotokea ndani Bungeni mapema, tumelewana?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Mambo  
ya Ndani ya Nchi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, ajiandae Mheshimiwa Selemani Said Bungara, maarufu Bwege.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kunijalia asubuhi hii afya na uzima nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojuja Wizara ya Mambo ya Ndani ni mionganini mwa Wizara za Muungano. Kwa hiyo, taasisi zake zote zilizomo katika Wizara hii zinapaswa zifanye kazi katika maeneo yote ya Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia kuhusu Jeshi la Polisi ambalo kwa mujibu wa utaratibu ndiyo ambao wanalinda mali na raia wa nchi hii kwa ujumla. Pia tamko hilo liko *supported* na Ibara ya 15(2)(a) na (b) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Nasema hivyo kwa sababu nataka kuelewa hili jukumu la kulinda raia na mali zake lipo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar au kuna mpaka baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu inaonekana dhahiri chombo hiki kikija katika maeneo ya Zanzibar labda kuna vyombo vingine ambavyo vimepewa majukumu haya ya kufanya kinyume na ule utaratibu wa kuweza kulinda raia na mali zao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano hai wa siku ya Alhamisi, tarehe 5 Aprili, katika Kijiji cha Mitambuuni, Jimbo langu la Mtambwe, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, kama alivyosema Mheshimiwa Khatib jana vijana sita wadogo kabisa, *innocent*, wapo mbali kabisa na hata maendeleo ya teknolojia maana hakuna umeme, hawana *television* wala hawana habari yoyote, ambao wana umri kati ya miaka 16 na mkubwa wao ana miaka 30 wamekamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwenda watu sijui tuite ambao hawajulikani wakiwa na magari manne yenye namba za *private*, namba ambazo baadhi ya majirani walizichukua, wakawagongea, wakawachukua vijana hawa, nyumba tofauti wakawafunga vitambaa vyta uso, wakawasweka katika magari wakaenda nao mahali pasipojulikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hao wakapelekwa katika nyumba, kwa sababu wamefungwa hawakujuwa wamekwenda wapi. Kulipokucha asubuhi wazee wao na jamaa zao wakaenda katika Kituo cha Polisi cha Wete ambapo ni Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba kuuliza, kwa sababu tumezoea mambo haya lakini mara nyingi tunazoea Polisi wanawachukua watu wanakwenda nao vituoni, lakini walipofika pale wakaambiwa hapa hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaenda Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Chakechake napo wakaambiwa watu hao hawapo. Vijana hawa baada ya siku nne vijana watatu katika sita, majina ninayo hapa, alfajiri wakatupwa mahali mbali kabisa na makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipokuja vijijini wakaeleza wakasema kwa kweli sisi tunashukuru hatukufanyiwa mateso lakini wenzetu ambao tumebagulia wapo katika vyumba tofauti wana mateso ya ajabu. Sasa *just imagine* hali ya wazee na jamaa itakuwaje watoto wao wameambiwa

wapo katika mateso makubwa kama hayo. Wale vijana watatu wakakaa ndani kwa siku 11 kuanzia tarehe 5 mpaka Jumapili ya tarehe 15 na wao wakaenda wakatupwa mahali wakiwa wamefungwa mikono na vitambaa vyaa uso. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni msiba mkubwa nchi kama Tanzania ambayo tunajivunia ni kisiwa cha amani, miaka 54 ya Muungano leo wanakwenda maharamia kwenda kuwachukua vijana wadogo. Waliporudi tulipokwenda kuwaona kwa kweli hali zao haziridhishi, wakikueleza mateso waliyoyapata basi huwezi kustahamili, unaweza kutoa machozi. Kwa kweli hali ni mbaya, wamepigwa kila eneo la mwili wao. Kwa hiyo, unaweza kujiuliza nyuma ya Jeshi la Polisi kuna nani ambaye ni *super power ana-organize* uharamia huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uharamia ambao kwa kweli unasikitisha mno. Kamishna wa Zanzibar yupo hapa ampelekee shukrani zetu *RPC* wa Kaskazini, katupa ushirikiano siku zote tulipokuwa tunakwenda lakini yeze muda wote alikuwa na yeze anasikitika, mimi hawa watu sinao jamani nendeni mkakague katika maeneo yangu yote, lakini unamhisu kuna jambo ambalo limefichika nyuma yake, anajua baadhi ya mambo. Yeze anasema hanao lakini anatupa moyo baada ya siku mbili au baada ya siku ngapi mtawapata watu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi tumepeleka hata namba za gari, hapo ndiyo mwanzo, kama ni upelelezi unaanzia hapo. Tungetarajia kwa kupitia namba za gari zile watu hawa wangekuwa *traced* na wakajulikana na tunasikia wamehojiwa lakini mpaka leo wanadunda, hakuna ambaye amepatikana na ameshtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo maana tukauliza, je, wajibu na jukumu la Jeshi la Polisi hasa kule Zanzibar kuna watu mme-*delegate powers* kwao, wao ndiyo washughulikie

usalama lakini wakati huo huo washughulikie mateso ya watu? Hapa ndipo ambapo tunapata shaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamuuliza Waziri *Inshallah* akija hapa kutoa majumuisho, ni lini hawa watu ambaao hawajulikani wataanza kujulikana na mateso haya yatakoma lini. Au kama hiyo haiwezekani basi atamke hapa leo akija Mheshimiwa Waziri kwamba sasa jukumu la kujilinda liwe lenu wenyewe wananchi. Tukishapata kauli hiyo tutajua namna gani ya kuweza kukaa kulinda wananchi, kujilinda wenyewe na mali zao, vinginevyo kwa kweli itakuwa hatuwafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungeomba kabisa nchi hii ni yetu sote, kama kuna mtu yejote na kwa kawaida kila raia ni mtuhumiwa mtarajiwa. Mimi naweza kutuhumiwa leo lakini kuna utaratibu, niitwe polisi au popote pale nikahojive ikionekana labda kuna makosa nipelekwe katika vyombo vyta haki (mahakama).

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kwenda kumgongea mtu usiku ukamfunga kitambaa ukaenda ukamtesa bure. Mtakuja kuwaona wananchi ni wabaya kumbe wabaya wakati mwingine ni Jeshi la Polisi. Hii ni kwa sababu wao wameshindwa kuwalinda wananchi pamoja na mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niseme kwamba pamoja na yote hayo, tunaona kwamba polisi wana matatizo mengi katika maeneo yao ya kazi. Hata bajeti yao ya mafuta ni ndogo mno. Kwa mfano, hata tulipowaita wao kwenda katika *site* watu wale walipokuwa *dumped* kikwazo kilikuwa ni mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selemani Bungara, ajiandae Kanali Masoud.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na uhai ili nichangie katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu, inapambana au inakataza dhuluma na uonevu, lakini katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani inaonesha badala ya kulinda wananchi imekuwa wao ndio kipaumbele cha kuwatesa wananchi. Mtu ye yote mwenye dhuluma silaha zake ni mbili; silaha ya kwanza kutamanisha, maana yake kutoa rushwa, silaha ya pili ni kutisha na kuua. Tumefanikiwa Tanzania kwa kutumia silaha hizo za rushwa kuwanunua Wapinzani na kuwatesa watu, mmefanikiwa Serikali ya CCM kutufikisha watu wa Tanzania kuwa waoga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni ajabu kwa watu wa Serikali na watu wa CCM kuitetea Serikali ya CCM ambayo inawatesa Watanzania, hatuoni ajabu. Na hata enzi hizo wakati wa Firauni pamoja na ubaya wake Firauni lakini kulikuwa na wapambe wake waliokuwa wanamtetea; hii ina maana kwamba kila mtawala atatetewa na watu wanaomfuata nyuma yake hata kama akiwa mbaya, kwa hiyo, hatuoni ajabu kwa yote yanayofanyika katika nchi hii kuna watu wanatetea kwamba mambo mazuri tu. Hatuoni ajabu kwa jambo hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawaambia viongozi wa CCM na Serikali yake kwamba mikono yenu imejaa damu na kama ingelikuwa Watanzania... (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, jielekeze kwenye hoja ambayo iko mbele yako.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo tunachoangalia hapa ni amani na utulivu na huu ni wakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Najielekeza katika mada yangu, lakini ninachosema mikono yenu imeingia damu na sisi tunaweza tusiwape mikono kuanzia leo.

**MWENYEKITI:** Hebu ukiwa unachangia nitazame mimi, usitazame chini.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka nikutazame? Unataka usikie? *Insha Allah.*

**WABUNGE FULANI:** Anasomaa!

**MBUNGE FULANI:** Hasomi bwana!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mambo ya Ndani...

**MBUNGE FULANI:** Anasoma!

**MBUNGE FULANI:** Wewe vipi wewe?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Waziri wa Mambo ya Ndani...

**MBUNGE FULANI:** Hajui kusoma jamani.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, katika hotuba ya Waziri Mkuu nilimwambia kuna vijana wangu wawili ambao wamewachukua mpaka leo hawajawarudisha na alisema atakuja kunjibu katika Wizara yake leo; naomba leo jibu langu nilipate, wako wapi na lazima wapatikane. Vijana hao ni Ali Mohamed Shari na Yusuf Kipuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna viongozi wamekamatwa kule Rufiji, leo nitakutajia viongozi 12, wamewakamata hatujui walipo. Wa kwanza Ziada Nongwa, huyu ni Diwani wa Viti Maalum kwa Tiketi ya CUFna ana mtoto mchanga, wamemkamata wamemchukua hajulikani wapi alipo, ni mama huyu. Nitaona ajabu sana akinamama wa CCM, mama mwenzenu tena Diwani kakamatwa hajulikani alipo, mseme hiyo ndiyo kazi tu, hapana; kwa hiyo, Ziada Nongwa Viti Maalum. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Moshi Mchela, Mwenyekiti wa Kitongoji na ni mwanamke vilevile; Braziluli Lyango na mkewe; Jumanne Kilumeke, Mwenyekiti wa Ikwiriri; Kisangi Athumani, Mwenyekiti wa Kijiji na Katibu wa Vijana wa CUF; Kazi Mtokela, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikwiriri; Mtuko Astella, Katibu wa CUF, Kata ya Ikwiriri; Khamisi Nyumba Mkali, ni Katibu wa CUF, Wilaya ya Rufiji; Baratu Kisongo, Ikwiriri; Kanjoma Mlanzi, mfanyakishara Ikwiriri; Abdallah Mkiu na Salim Mkiu, Mwenyekiti Mstaafu wa Umwe, wote hao wamewakamata, wako wapi? Waleteni mahakamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba anapofika hapa atuambie wako wapi na lini watawafikisha mahakamani, wazee wao wanalia watoto wao hawawaoni. Namwomba sana Mheshimiwa Nchemba, tuwajue hawa watu wako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niongelee kuhusu Mashekhe, sisi ni Waislam na Muislam ni ndugu kwa Muislam mwenzake, ukimuua Muislam mmoja umetuua wote, sisi ni ndugu, hatuwaelewi Serikali ya CCM, hatuwaelewi, kwa nini wanawatesa Mashekhe; kwa nini wanawafunga Mashekhe? Wanawachukua Mashehe wanawaweka ndani hawawapeleki Mahakamani, kwa nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waislamu wote tushikamane kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika *Quran* yetu, tupambane na Serikali ya CCM. Mtume amesema mdhalimu ye yote anapofanya udhalimu wake tuseme na tukishindwa kusema tuuondoe udhalimu huo kwa mkono wetu; kasema Mtume. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Waislamu wa Tanzania tuutoe uongozi wa Serikali ya CCM kwa mkono wetu kwa kutumia kura, tutumie kura tuitoe Serikali ya CCM, inatuonea Waislamu kwa nini? Tumekosa nini? Mashekhe wetu Zanzibar wako ndani, Arusha wako ndani, Lindi wako

ndani, kwa nini? Kila Ijumaa tuombe dua Serikali ya CCM itoke madarakani, inatuonea Waislam kwa nini, tuna kosa gani sisi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *wamandharaba nafsi laa yabuk*, ajipigae mwenyewe halii, tuiondoe Serikali ya CCM madarakani, Waislam tuungane, tushikamane na Muislamu yeoyote atakayesema kwamba Waislam wakae mahabusu huyu sio Muislam, *kafir*.

**MBUNGE FULANI:** *Takbir!*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Tunaomba sana Waislam tushikamane, wametugawanya kwa makusudi, wametugawanya...

**MBUNGE FULANI:** Waambie.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** BAKWATA inaisherehekeea Serikali ya CCM, wengine sisi tukisema hatuonekani...

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Tunaomba sana Waislamu kama kuna Waislamu kweli tushikamane, Waislam tunateketetea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Tunateketetea waislamu.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante; Mheshimiwa Kanali Masoud, jiandae Mheshimiwa Janeth Massaburi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka niombe mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na nilikuwa naomba nimsikilize mchangiaji mpaka atakapomaliza ili niweze kumwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, maneno ambayo alikuwa anayatumia mchangiaji wakati akichangia ni maneno ambayo kwa kweli ni mazito sana. Ni maneno ambayo yanakiuka misingi ya Katiba, misingi ya umoja wa Taifa letu, maneno ambayo yamejaa uchochezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili kwanza halijawahi kufanya uchaguzi kwa misingi ya kikabila ama misingi ya udini. Taifa hili limeishi katika umoja. Leo Mheshimiwa Mbunge anapohamasisha Wabunge na Watanzania wenye imani ya dini fulani moja waungane pamoja haya ni maneno makubwa na ni maneno ya uchochezi mkubwa sana. (*Makofi*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hiyo aya ya Mwenyezi Mungu tushikamane katika kamba ya Mwenyezi Mungu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge angeweza kuchangia vizuri tu hoja yake, lakini maneno haya ambayo ameendelea nayo wakati akichangia siyo maneno ya kuendelea kuvumilika ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba, kwa mujibu wa kanuni tulizonazo utupe mwongozo, ni kweli maneno haya yanastahili kusemwa ndani ya Bunge hili kwa niaba ya Watanzania wote? Kama hayastahili ni lazima yaondolewe katika mjadala wetu wa leo ili tuendelee kubaki wamoja,

tuendelee kujenga mshikamano katika Taifa letu na tusigawanywe kwa misingi ya kidini wala imani tulizonazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kuwa, nakwenda kuipitia *Hansard* na kutazama maneno yote ambayo kwa kweli yalikuwa ni ya uchochezi au maneno ambayo yameathiri *atmosphere* ya Bunge na haturuhusiwi kikanuni, tutayaufuta katika *Hansard* yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe rai vilevile; tunapochangia humu ndani tusiwe na hisia za kidini. Kama kuna watu wako mahakamani, kama watu wako chini ya uchunguzi, tuviachie vyombo vifanye kazi na pale...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MWENYEKITI:** Sasa mimi nikisimama ninyi hamruhusiwi hata kusema kitu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mwongozo wangu ni kuwa ntautoa baada ya kupitia *Hansard* na kupitia vizuri maneno ya Mheshimiwa Bungara. Hata hivyo, nitoe tahadhari vilevile, Bunge hili hatutaruhusu maneno yoyote ya uchochezi au ya kuhamasishana kidini au kuhamasishana kwa jambo lolote. Kama kuna hoja Mbunge anayo aiweke Mezani vizuri alete hoja yake, na itajibiwa na Serikali wakati wana-*wind up* leo jioni. Mheshimiwa Kanali Masoud.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Magufuli, kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya kwa Taifa letu. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na muhimu sana wanayoifanya kwa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa lolote duniani, ulinzi una nyenzo muhimu ambazo ukitaka ufanikiwe katika ulinzi lazima uzikamilishe ndiyo utapata mafanikio mazuri. Nyenzo ya kwanza katika ulinzi ni watu kwa maana ya askari wenyewe, lazima upate askari wenyewe nidhamu, wenyewe mafunzo na wenyewe afya ili waweze kufanya kazi vizuri wakati wote wanapokuwa katika kazi zao za kila siku. Kwa maana hiyo lazima kwanza maslahi ya askari wetu yaangaliwe vizuri ili kuyafanya hayo matatu yaweze kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lazima uwe na vifaa vya kutendea kazi ambavyo vitawasaidia askari hao kufanya kazi kwa weledi na kwa ucharaka. Mambo mengi tunayalamikia wakati mwingine yanababishwa na ugumu na changamoto walizonazo askari wetu katika kukamilisha vifaa vyao vya kufanya kazi. Niombe sana Serikali ijitahidi kabisa kuhakikisha fedha tunazopitisha katika Bunge basi zinapelekwa kwa wakati ili ziweze kuwasaidia wenzetu kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasikiliza michango mingi ya wachangiaji kuanzia jana hadi leo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wapo wenzetu walifika mbali sana jana na kutaka kumkosoa Mungu ambaye kwa kweli huwa hakosolewi na mtu ye yeyote. Katika dini yetu tunaambiwa ukimkuta mwenzio anakosea mwombee dua, usishindane naye wala usibishane naye, mwombee dua ili anyooke aende katika njia iliyonyooka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo Tanzania kuanzia sisi viongozi na hata wananchi wa kawaida, kila mtu sasa hivi anajifanya yeye polisi, kila mtu anajua kazi ya

polisi. Nataka niwaambie, kazi ya polisi ni kazi ya kitaalam yenye kutaka mtu ajifunze ajue jukumu lake na afanye vile inavyotakiwa. Utamkosoa polisi wewe kazi hujui, huwezi kufanya kazi ya polisi kama hujafunzwa, ni kazi inayohitaji ujuzi na utaalaman wa hali ya juu sana. Upelelezi ni kazi kubwa na inahitaji vitu vingi tu ambavyo hatuwezi kuvieleza katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi nawaomba, hasa Mheshimiwa Kamanda wa Polisi, Inspekte Jenerali, namwomba afanye kazi yake kulingana na Katiba na sheria, wala asiogope kitu. Namwona ni dereva mzuri, dereva mzuri aliyebeba abiria ni yule ambaye akisimamishwa mahali pasipostahili, akipigiwa debe na kondakta asimame mahali pasipostahili, hasimami. Dereva mbaya ni yule anayesimamishwa mahali ambapo hapastahili akasimama akasababisha ajali na vifo na mambo kadhaa. Kamanda Sirro aendelea na kazi yake, asibabaishwe na wapiga debe ambao hawafahamu nini wanalolifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge niliona michango yao wakichangia hapa wakilalamika sana, wanasema polisi wametumia nguvu kubwa kufanya mazoezi kwa kusikia habari za maandamano na vitu kadhaa. Sasa hili ndiyo nilizungumza mwanzo; kazi ya polisi ni ya kitaalam, ukigundua mahali panaashiria jambo baya moja ya namna za kuzuia uhalifu ni mazoezi. Ukishaona hapa mahali panaweza pakatokea jambo baya, polisi pigi zoezi na watu wanakaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hivyo, hatukuona maandamano, hatukuona kitu kwa sababu ya mazoezi tu. Naomba ndugu zetu wa polisi waendelee kufanya kazi zenu bila ya kujali, bila ya kubugudhiwa na bila ya kubabaishwa na maneno ya watu humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tunajua kazi hizi ni ngumu na kila anayesimama, hapa Jeshi la Polisi, Jeshi la Polisi, hawazungumzii idara nyingine, Wizara hii ina idara nyingi

tu, lakini ni polisi tu na kwa sababu watu wengine wanataka wafanye wanayoyataka ambayo hayatakiwi kufanywa ndani ya nchi hii. Sasa wewe utafanya jambo ambalo halitakiwi halafu uachiwe, hatuwezi kukubali; kila anayefanya kosa, awe CCM awe nani, wewe shughulikia halafu tutakuja kujuana mbele huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana katika mchango kuna Mbunge mmoja alichangia na niendelee kusositiza tu, Kituo chetu cha Polisi Mikese, nimeshuhudia, ni shuhuda katika ajali iliyotokea hivi karibuni, tulikuwemo na mimi nilikuwemo na nilibahatika kupanda lilelile gari la polisi, lile gari dereva anashikilia gia, ukiachia gia gari linatoka mpaka tukafika tulikokwenda, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ni mahali pa muhimu ambapo kwa kweli panatakiwa magari ya uhakika ya kufanya kazi. Kwa hiyo, niwaombe sana, Mheshimiwa Waziri akiangalie sana kile kituo na pale pana ajali nyingi zinatokea kila mara, niwaombe sana wawasadie gari linalofaa kwa ajili ya kufanya kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuzungumza ni kuhusu Magereza, maana wengi wamekwenda kwenye polisi lakini ni kwa sababu ndiyo wanayoyaona humo barabarani na sehemu nyingine, wengine tulishayaona mpaka ya Magereza sasa. Hali ya magereza yetu hapa nchini, makazi yao kwa kweli hayaridhishi, nimeshafika mwenyewe binafsi nimeona, nimefika mpaka kwenye gereza na nikafika kwenye nyumba ya Mkuu wa Gereza. Kwa umri wangu na urefu nilionao kwenye nyumba ile siwezi kupita kama sijainama, nyumba haifai, aibu na inatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana kwa kweli, Mheshimiwa Waziri na hasa tuwaambie wenzetu, fedha zinapopitishwa Bungeni Wizara ya Fedha ijitahidi kupeleka kwenye Wizara hii ili angalau wapunguze matatizo. Nina imani kabisa kama fedha tunazozipitisha hapa zitakwenda kwa wakati katika Wizara mambo mengi tunayoyazungumza

hana mwakani hatuwezi kurudia kuyazungumza. Tujitahidi kuwapatia fedha ili watatue matatizo yao na hatimaye tufike kule tulikokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu usafiri kwa baadhi ya vituo vya polisi hapa nchini. Mimi mwenyewe katika Jimbo langu la Mfenesini ninacho kituo cha polisi, nimeshazungumza sana hapa na nakumbuka inakaribia miaka kumi ama zaidi kituo kile hakina gari, kuna wakati nilishatumia gari langu pia kufanya kazi za polisi. Kwa hiyo, niombe sana Wizara hii iangalie vituo vyetu, hasa Kituo hiki cha Polisi cha Mfenesini ambapo kwa kawaida ni njia kuu ya watalii wote wanaokwenda Kaskazini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri ukweli kabisa, ilishawahili kutokea, watalii walismama kituoni wakaomba kwenda kujisaidia, askari wale nawasifu sana, ni waelewa, waliwaambia kituo chetu hakina choo. Ilikuwa ni bora kuliko wangewaruhusu kwenda kwenye hicho choo, maana ingekuwa ni aibu ya kutisha kabisa. Niombé sana, licha ya usafiri lakini na majengo ya askari wetu hawa yachukuliwe umuhimu wake nayo, warekebishiwe ili waweze angalau kufikia kiwango fulani cha kuwasaidia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo pia kwa jeshi letu la Zimamoto ambalo huwa mara nyngi halizungumzwi hapa na hawalizungumzi pengine kwa sababu hatujawahili kuyaona matukio yanayotoa ya moto na wakashindwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati. Hawa wana matatizo mengi hawa ndiyo hasa wanatakiwa waangaliwe zaidi licha ya matatizo ya majengo lakini bado hata bado vifaa vyao vya kufanya kazi ni pungufu mno. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara iendelee kuchukua juhudzi za pekee kuwasaidia wenzetu wa Zimamoto ili angalau nao wafikie kiwango fulani cha kutenda kazi sawa kwa weledi na kwa ufanisi mkubwa zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na niwashukuru wenzangu waliochangia Wizara hii. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Masaburi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kuweza kunipa fursa hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa zawadi ya uhai na kuweza kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara kuititia jeshi la polisi itupatie taarifa ya kifo cha Chacha Wangwe, tunaomba taarifa ya kifo cha Mchungaji Mtikila, tunaomba taarifa ya watalii waliomwagiwa tindikali kule Zanzibar, tunaomba taarifa ya Makanisa yaliyochomwa moto Zanzibar. Tukumbuke nchi yetu iko hapa kwa mkono wa Mwenyezi Mungu na tangu kuhasisiwa kwake tangu enzi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, enzi ya Mzee Mwinyi, enzi ya Mzee Mkapa, enzi ya Mzee Kikwete na sasa hivi enzi ya ndugu yetu Dkt. John Pombe Magufuli. Hawa wote wamewekwa hapa kwa ruhusa na mkono wa Mwenyezi Mungu na ndiyo maana hata ukiangalia maisha yao ni ya kawaida sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ndugu zangu tusitumie fursa ya viongozi wetu kukaa kimya na kuweza kuwatukana hovyo hovyo. Tulikuwa tukintukana Mheshimiwa Kikwete sana, mpole tukamhujumu hata kwenye miradi yake, lakini Mwenyezi Mungu alikuwa amemsimamia alikuwa upande wake. Vilevile Rais wa Awamu ya Tano kuna mkono wa Mwenyezi Mungu na nasema watapambana lakini hawatashinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukeni ndugu zangu tulipa kuitetea na kuilinda katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana hiyo tulisema totalinda Muungano kwa gharama yoyote. Tarehe 26 Aprili ni siku ambayo tunakumbuka Muungano wetu ulioasisiwa na ndiyo maana yale mazoezi na *parade mlizoziona* ndiyo gharama za

kulinda Muungano. Kwa hiyo, tumesikia watu wana sema gharama zimekuwa kubwa tungejenga shule. Ile ni sehemu ya kulinda Muungano wetu ndiyo gharama zenyewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ni yetu sote humu ndani tuko kama mia tatu na kitu, lakini tukumbuke Watanzania wako zaidi ya milioni 60 sisi tunajiona kama tuna haki zaidi ya Watanzania walio wengi. Kuna wakulima, wavuvi, wamachinga, watu wasio na vyama, wenye dini, wapagani, kila mtu ana haki na hamasa ambazo zinatolewa kwa kutubagua sisi tunaomba zishindwe katika jina la Yesu na hazitafanikiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza /GP wetu na Makamanda wote wa Mikoa yote na Wakuu wa Mikoa kwa kazi nzuri sana wakiongozwa na Waziri, Naibu Waziri bila kumsahau Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. Wamefanya kazi nzuri sana kuhakikisha nchi inakuwa salama, bila amani hatuwezi kulima, bila amani hamna kwenda shule, bila amani hakuna kustarehe, bila amani hamna kuzaliana, bila amani hamna kizazi endelevu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusitanie amani kwa kutumia dini, kwa ku-*convince* watu kwamba dini fulani inaonewa, hakuna! Mbona wewe kama dini unabaguliwa mbona uko humu ndani? Tuko dini tofauti humu ndani, kama kungekuwa kuna ubaguzi tusingekuwepo. Tusitanie amani kwa sababu tuna dhamana ya kulinda uhuru wa nchi hii tuweze kurithisha na vizazi vijavyo. Tumeikuta nchi hii ikiwa na amani, kama mnatumika na maadui wa ndani na wa nje waambieni Tanzania haitaniwi, iko imara, hakuna utani katika masuala ya amani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iongeze bajeti ya kutosha katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, tunaomba magari yaongezwe, tunaomba mafuta yaongezwe, tunaomba makazi yao yaboreshwe na kujengwa nchi nzima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba maslahi ya askari; katika nchi nyingine nimetoa mfano kadhaa kule Marekani bajeti yao ya kwanza yenye kipaumbele ni ulinzi bila ulinzi yote hayawesi kutekelezeka, mbona wewe nyumbani kwako unafunga mlango, mbona unajenga geti, mbona unaweka walinzi, tusitaniane katika mambo ya ulinzi wa nchi na wala hatutishwi, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hatutishwi na tupo imara. Mmetushika pabaya katika masuala ya amani hatutaniwi, sisi tutatoka kwenye Bunge hili na kizazi kitaendeleza ulinzi kwa sababu Mungu yuko pamoja na sisi kwa sababu Mungu ni wa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Jeshi la Zimamoto, kama alivyosema Mjumbe aliymaliza kwa kweli limekuwa lina mwamko mdogo na hasa kwenye Wizara yenye dhamana ya kupanga bajeti katika Jeshi hili. Tunaomba Jeshi la Zimamoto lipewe fedha za kutosha, sisi sote hapa majanga ya moto huwa yanatokea huko mtaani na majumbani kwetu, jeshi lipewe vifaa, magari ya kutosha, majengo yako marefu sana Dar es Salam, Dodoma Makao Makuu, jengo la Bunge hivi tuna vifaa vy'a kisasa vy'a kutosha kukabiliana na janga la moto, vifaa vy'a uokoaji au ikitokea majanga tunaita watu kutoka South Afrika? Naomba jeshi hili liimarishwe kama vilivyo vikosi vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji, naomba idara hii pia iongezewe bajeti ya kutosha kukabiliana na wahamiaji haramu, Dar es Salaam kule mkienda Kariakoo unakuta sura tofauti maana yake sisi Watanzania tunajuana. Nimwambie Mheshimiwa Waziri, wako wengi Dar es Salaam bila kutaja ni mataifa gani, mimi nakaa maeneo ya Segerea kule. Siku hizi kuna majirani wageni tunashangaa, tutumieni sisi Wajumbe wa Mabalozi wa CCM tunaweza kuwaambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiongelee Jeshi la Magereza; Jeshi hili lionezewe bajeti ya kutosha ili wajenge makazi ya askari wapatiwe usafiri unakutana na askari magereza anaomba lifti, unakuta pale askari magereza amekaa kona

anaomba lifti ni jambo la aibu mno. Anakuwa mnyonge, matokeo yake ndiyo huwa wanatukanwa hovyo hovyo. Naomba watoe pesa tuwekeze kama tunavyowekeza kwenye *Stiegler's Gorge*, katika masuala ya ulinzi yapewe kipaumbele, miradi hii yote mikubwa haiwezi kutekelezwa kama hamna ulinzi wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema sisi tutakuwepo, tutaondoka watakuja wengine, lakini kizazi cha Watanzania cha sasa na cha kijacho kinatutegea sisi, ulimi wetu tuutumie vizuri, tukiongozwa na roho ya Mungu, tusitumie dini kudanganyana hapa, hata mpagani anaweza kuona ufalme wa mbingu wewe ambaye unasema unadini ukapelekwa motoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulembo, wajiandae Mheshimiwa Ritta na Mheshimiwa Zito.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nichukue fursa hii kuwapongeza ndugu zangu walioko Wizara ya Mambo ya Ndani Mheshimiwa Mwigulu, Naibu wake Mheshimiwa Masauni, Katibu Mkuu Wasaidizi wao wote, Makamishna Jenerali walioko hapo juu, Ma-RPC, Maafisa Uhamiaji katika Mikoa. Wizara nzima nawapongeza sana kwa kazi kubwa mnayoifanya kutulinda katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hilli la ulinzi hasa polisi, wachangiaji wengi wamesema nani halindwi, nani kafanyiwa hivi, nani kafanyiwa hivi, mimi nataka niende Kibiti tu kidogo. Polisi walifanya kazi kubwa sana Kibiti inatakiwa tuwapongeze wote tulimo humu ndani. Kazi yao walifanya ni kubwa, ilifika mahali mtu ukitaka kwenda Kibiti inabidi utafute polisi wa kukusindikiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani wengine walimaliza kusema kwamba sisi Serikali haitutaki, haiwi hivi

nataka kuuliza swali moja hasa kwa Wabunge, askari polisi mmoja anapokufa ni kwamba alikuwa vitani, Kibiti wamekuwa askari kama sikosei kati ya 20 mpaka 25 haikutugusa, haionekani kama walikuwa vitani, wakapata shida na wala hata humu ndani hatukuitana kuchangiana hata elfu kumi kumi ya kusaidia familia zao. Ni watoto wetu wale! Ni wapiganaji wa nchi hii ndiyo kiapo chao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakaa hapa kuna watu wanabeza polisi. Hata ukiwa na Mmasai anakulinda huwezi kubeza polisi. Wasemaji wamesema polisi ni *professional*, haiwezekani kila mtu anaweza kwenda nyumbani akavaa akaitwa polisi. Kwa nini tunawafanya watu wa kawaida polisi? Naomba Waheshimiwa Wabunge polisi pamoja wanalipwa kwa kodi zetu hata nyie Wabunge humu mnalipwa kwa kodi ambapo hata polisi anakatwa makato yake, si ndiyo? Maana yake leo mtu anasema kodi yetu, nani halipwi kwa kodi? hata sisi mshahara tunaopata ni kodi ya polisi ipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili ni letu sisi wote, lakini wachangiaji wanasema polisi kwa kodi zetu, kodi ni yetu sisi wote kama polisi anavyolipwa mshahara, kama wewe unavyolipwa posho, tuna haki ya kuthamini polisi. Naendelea kusema tukitoka nje hapa tunalindwa na polisi, popote unalindwa na polisi, lakini polisi hawa hatuwathamini wala hatuwapi *value*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, napenda niwapongeze matrafiki wote Tanzania wanaofanya kazi ya usalama barabarani. Sisi Wabunge tukienda na magari yetu *traffic* akikusimamisha, unasema naitwa Mbunge, kwani ukiitia Mbunge ndio uvunje sheria? Nani amekwambia kuna mahali imeandikwa Mbunge avunje sheria? Tunawadharau wale watu hatuwapi haki, hata kama wewe ni Mbunge una haki nayo, basi simamisha gari msikilise jieleze mpe thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Mheshimiwa *IGP* Sirro, hawa Wabunge wanaofanya makosa barabarani

wakienda wawapeleke mahakamani. Ndiyo, kwa kuwa hakuna mahali mtu ameambiwa avunje sheria, sheria hii inatuhusu sisi wote. Unaona watu wanafanya vitu vya ajabu eti kwa sababu wanatumia nembo ya Ubunge, Ubunge siyo *certificate* ya kwenda kufanya makosa kwa kuadhalilisha wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sehemu ya pili upande wa polisi, polisi kuna ile kitu wanaita *Police General Order* kwa maaskari wetu, wanakaa miaka 12 ndio wanaangia kwenye ajira, hii nyingine ni mkataba mkataba. Nafikiri wangefanya utarabu tulete sheria huku au tufanye marekebisho tuwape nafasi yao. Kwa sababu kama tunafanya hivyo hapa katikati wakiondoka kuna mambo mengi wanayapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa polisi niende suala lingine ambalo ni gumu. Kwenye kitabu cha bajeti cha Waziri hapa nilipoangalia kwenye eneo la maendeleo kwenye ukurasa wa 51, polisi wamewapa hela kidogo. Pale Makao Makuu ya Polisi kuna jengo fulani pale linajengwa miaka mingi *forensic bureau* haliishi, kwa nini Mheshimiwa Mwigulu jengo hili haliishi? Kwa nini kwenye bajeti hii hatulioni? Jengo hili ni muhimu sana kwa nchi za wenzetu kwa sababu gani, mtu akipata ajali, mtu akiuawa usiku kuna mahali anapelekwa ajue, mitandao ipo, tutakwenda kuangalia wapi, kwa nini jengo hatulipi bajeti? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo matatizo mengi katika nchi hii watu wanaauawa, watu wanaonewa, watu wananyang'anywa mali zao, lakini hawana mahali pa kwenda. Naomba Mheshimiwa Mwigulu wakati akija hapa anijibu *forensic bureau* ya Makao Makuu pale inakwisha lini? Huo mradi ni mkubwa sana katika nchi za wenzetu, huwezi kutambua jambo mpaka uende kuazima kwa rafiki yako itakuaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana, inawezekana hatuoni umuhimu, lakini nina uhakika eneo hili

ni muhimu. Hawa watu wenu wa Kibiti wangekuwa wanapatikana, mitandao ya simu ingekuwa inapatikana polisi wajitegemee wenyewe, kwa nini wawe na mawazo ya kupiga hodi kwa watu wengine? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akija nafikiri majibu yake yatakuwa mazuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Uhamiaji. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Kamishina wa Uhamiaji, hongera sana mama, ameonesha mabadiiliko, anafanya kazi. Pia katika pongezi hizo nimpongeze tena Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani niliuliza hoja hapa Bungeni kuna vijana wetu walifukuzwa pale polisi kwa kufoji viza, yule aliyesababisha wafoji viza akapigwa *Pi* Uhamiaji wakawa bado wanamshikilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Naibu Waziri na Jenerali wa Uhamiaji, yule mtu baadaye walikamilisha utaratibu akarudi kwao, basi watoto wetu wamefukuzwa na ye ye ameenda kwao. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa usikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uhamiaji kuna tatizo, tena si dogo kubwa sana. Namwomba Kamishna atoke Ofisini, atembelee Mikoa ya Tanzania yote ajue pamekaaje. Kwenye *border* kuna shida, kuna shida sana ukienda Namanga, ukienda Mtukula, ukienda Songwe pale kuna shida kubwa. Pamoja na hayo kila siku tunawakamata Waethiopia, tunawakamata Wasomali, lakini humu ndani kuna watu wanaishi bila utaratibu na wako wanalindwa na Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa nikasema kuna mtu amekuja hapa nchini anaitwa Mhasibu, leo ni *group Meneja* miaka 20, anaitwa Vedagiri yuko kwenye kampuni ya *Alpha Group*. Mtu yule anaishi kwa utarabu gani lakini niliposema neno lile kuna Wabunge humu niliwigusa wenyewe matakwa na watu kwa sababu ni wafanyabiashara wakubwa nafikiri wana mambo yao pale wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoongelea ni Utanzania kwenye uhamiaji. Baada ya kumtaja huyo nimeletewa wengine zaidi ya 20, wanaishi humu wanaonekana kama Watanzania, lakini hatuwafuatilii! Ukienda kwenye Idara ya Uvuvi, Mheshimiwa Mwigulu nimewaambia waanzie Mtwara mpaka waje Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli Watanzania hawana uwezo wa kuuza bucha za samaki? Hawa Wahindi wanaouza bucha za samaki wanawapa vibali gani? Uhamiaji wanawaona? Ni Wizara ya kazi ndiyo wanashirikiana na Wizara hizi ni mtambuka, lakini kazi haiwezi kuwapa kibali mpaka uhamiaji waseme anatakiwa kuwepo nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa eneo la Uhamiaji kwa nini wanashughulikiwa Waethiopia, Wasomali, ndiyo wanaguswa huku, lakini hawa wengine tunaoishi nao nchini kwa sababu wana mapesa, wamekaa zaidi ya miaka 20 mpaka wanaingia kwenye siasa zetu nani awe CCM, nani awe CHADEMA, wanawaangalia tu hawasemi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sasa namkabidhi Mheshimiwa Waziri, Kamishna Jenerali hajashindwa inawezekana alikuwa hajui wakae mezani wanipe majibu. Bahati mbaya nikilisema nitaenda nalo mpaka mwisho kwa sababu sitaliacha kama sitapa majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawalinda Wahindi humu, hawana vibali, hawana nini, wanakamata Wasomali akina Bashe waliozaliwa nchini, ndiyo wanahangaika nao. Akguswa mtu wewe njoo, wewe njoo, lakini hawa wanaotoka nje hawafanyi nao kazi kwa nini? Uhamiaji ni pazuri, siwezi kumsema Jenerali huyu mpya ana siku chache, lakini pale kuna mizizi mibaya, ukienda sehemu ambako kuna wakimbizi, ukienda sehemu ambazo zina mipaka watu wa Uhamiaji wale ni hatari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize kati ya Uhamiaji na Polisi; nimeona *IGPSirro* mwili wake mzuri, Kamishna Jenerali

wa Uhamiaji mzuri, Magereza mzuri, hawa wenye vitambi vikubwa vinakaa kwenye meza kuliko vyetu ni mapolisi kweli au...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati, jiandae Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaa! Nimemaliza?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Naomba nimirungulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu na nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimwia Dkt. Mwigulu, Naibu Waziri na pia nimpongeze *IGP* Sirro na Makamanda wote bila kumsahau Kamanda wa Uhamiaji, dada yetu Kamanda Anna Makakala, mwanamke mwenzetu kwa kazi ambazo wamekuwa wakizifanya kulitumikia Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye alikuwa Iringa kwa siku tano. Amefanya kazi nzuri sana na niseme kwamba wananchi wa Iringa kwa kweli wametambua uwepo wake na wametambua kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya kwa wananchi wetu. Nimpongeze sana *RPC* wa Mkoa wa Iringa, Kamanda Bwire kwa kuhakikisha kwamba usalama umekuwepo kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza naomba kumpongeza sana Mchungaji Msigwa, narudia tena, nampongeza sana Mchungaji Msigwa, Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kutambua kazi nzuri ambazo zinafanyika kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano na kumtambua kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Pombe Magufuli anafanya kazi bila kubagua, bila ubaguzi na maneno haya mazuri

ameyaongea mbele ya Waziri wetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, mbele ya Mheshimiwa Susan Mgonukulima na Wabunge na wananchi wa Iringa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nasema sasa Mheshimiwa Msigwa ameanza kukomaa kisiasa. Nashindwa kushangaa, Wabunge wengine wa Upinzani wanapokutana na Rais waseme haya maneno, wamwambie ukweli, lakini wanapoingia humu ndani kwenye Bunge wanaanza kusema tofauti, sasa huo unakuwa unafiki. Hata jana eti wanasema kwamba Rais wetu hakosolewi, mbona mkikutana sasa hamumkosoi? Mnasubiri mpaka muingie humu Bungeni muanze kukosoa, muanze kutukana, mnataka kiki au mnataka nini? Jamani mimi nawaombeni, upinzani wa kweli ni kusema ukweli lakini upinzani wa kweli siyo kuanza kusema vitu ambavyo siyo vya ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze mchango wangu; nizungumzie changamoto ambazo ziko katika Mkoa wa Iringa. Mkoa wa Iringa una changamoto kwa kweli, askari wetu wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana, lakini bado wanaishi kwenye makazi duni. Haya maneno tumeshayazungumza muda mrefu, askari bado nyumba zao siyo nzuri sana kuanzia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto bado hawajaweza kujengewa nyumba nzuri kama ambavyo zilivyo za wanajeshi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba Serikali yetu kwa kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa na askari wetu, basi wajengewe makazi ambayo yanalingana na kazi zao kwa sababu tunapozungumzia makazi pia tunamzungumzia na yule mwanamke ya wale watoto ambao wanaishi kwenye zile nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali hii ingalie umuhimu wa askari wetu kwa kuwajengea nyumba nzuri kwa sababu nyumba ambazo ziko pale Kihesa, mimi nakaa pale Kihesa, ni nyumba ambazo zimejengwa muda

mrefu sana, zingeweza zikabomolewa, zikajenga maghorofa kama ambavyo zimejengwa kwenye sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *OC* zao za Mkoa wetu bado zinatakiwa ziletwe za kutosha. Stahiki zao zilipwe mara moja kwa sababu wamekuwa wakidai kwa muda mrefu. Upandishaji wa madaraja na vyeo jamani uende kwa muda, wapandishwe kwa muda kwa sababu askari wetu nao wanahitaji wapate stahiki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini nizungumzie Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Zimamoto wenzangu wengi wameshalizungumzia nimpongeze Kamanda Andengenyé, lakini askari wetu wa Iringa, Kamanda wetu James anafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Wana vituo vitano nya zimamoto lakini kuna gari moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa una uwanja wa ndege, Mkoa wa Iringa una misitu kule Mufindi, kule Kilolo ambapo mara kwa mara ajali za moto zinatokea lakini magari yao ni mabovu sana. Kuna mlima ule wa Kitonga kumekuwa kunatokea ajali mara kwa mara hakuna *crane* ya kusaidia kuondoa magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wamekuwa mara nyingi kwenye Mto Ruaha watoto wetu wa shule wanazama, tunapata ajali, wananchi wanazama, hawana hata vifaa nya uokozi nya maji. Kwa hiyo ningeomba kwa kweli hili Jeshi la Zimamoto hebu liangaliwe, lipewe pesa ya kutosha ili wananchi waweze kuishi bila ya kuwa na matatizo yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishauri halmashauri zetu tunapotenga haya maeneo basi tuweke na maeneo kwa ajili ya kuonesha huduma hii ya zimamoto kwa sababu tumeona sasa hivi miji inakua, lakini inapotokea ajali haya magari yanashindwa kupita kwenda kuokoa. Hata hapa Dodoma ilitokea siku ile walibomoa nyumba. Kwa hiyo, niombe Halmashauri zetu pia zitenge maeneo kuhakikisha kwamba magari ya zimamoto yanakwenda kufanya kazi zao

vizuri. Vilevile naona magari yale ya washawasha yanatumika kuzima moto. Sasa naomba Jeshi letu la Zimamoto wapewe magari ya kutosha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Kamanda wa Jeshi la Magereza na hasa wa Mkoa wetu wa Iringa, Kamanda Mwakajungu anafanya kazi nzuri sana. Nilishakwenda kutembelea Magereza, chakula kizuri sana lakini wafungwa hawana *uniform* kwa kweli, wanavaa kwa shida. Iringa ni mji ambaao una baridi sana, wapewe masweta na mablanketi, kwa kuwa unakuta wafungwa wanaugua *pneumonia*. Kwa hiyo, wanatumia pesa nyangi kuwatibu badala ya kuzuia na wanapata matatizo makubwa sana kwa kuhudumia hayo matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niendelee kuzungumzia kwamba Wilaya ya Kilolo ni Wilaya ya muda mrefu sana bado haijaweza kujengewa Ofisi ya Wilaya. *OCD* anakaa mbali na *DC*, kwanza hawana vifaa vyta kutosha kwenye ile Wilaya, kwa sababu hawana mafuta, vilevile hawajawahi kujengewa nyumba za kuishi, siku zote wamekuwa wakiishi kwenye maeneo ye makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari amepanga kwa mwananchi, je, yule mwananchi akifanya kosa na yeye amepanga kwake kweli atam-report? Kwa hiyo, niombe kwa kweli Jeshi la Polisi liangalie, askari wote waishi kambini kwa sababu wakati mwininge wanakuwa hawana usafiri. Kwa mfano, Kilolo, Makao Makuu ya Polisi ambayo wamepewa yako mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuzungumza kuhusiana na maandamano. Kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuondoa haya maandamano, kwa sababu kwenye Mkoa wetu wa Iringa, maandamano haya yametuletea hasara kubwa sana, yalisababisha hata gari la zimamoto lilipigwa vibaya sana, lilivunjwa vunjwa kwa ajili ya maandamano. Vilevile barabara nyingi sana ziliweza kuchomwa wakati huo na kusababisha hasara sana kwenye Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gumu sana ambalo akinamama wote kwa kweli tumelipongeza kuhusu maandamano, watoto wengi sana walivunjwa miguu, waliumia sana na hawakuweza kupatiwa msaada wowote. Kwa hiyo, nasema kwamba wananchi waandamane kwa kufanya kazi, wasiandamane kwa kuharibu vitu na niwaombe hata wanasiasa wenzangu tufanye hawa watu waandamane kwa kufanya kazi, nafikiri itakuwa busara zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee kuhusiana na mtandao wa wanawake, maana yake sisi ni wanawake, nilikuwa mgeni rasmi kwenye shughuli ya sikukuu ya mtandao wa wanawake. Kwa kweli walionesha wanafanya kazi nzuri sana. Kila idara wapo lakini cha kushangaza /GP yuko hapa, ukitembea kule kote hawapati vile vitochi, vitochi hivi vinapewa kwa masharti, naona wanashika tu wanaume. Walikuwa wanasema kwamba hata wanawake wanaweza wakashika vile vitochi wakafanya kazi vizuri tu. Sijajua kwamba wanapewa kwa masharti vitochi ama walipewa kwa waganga wa kienyeji. Kwa hiyo, niombe hata wanawake pia wapewe vitochi siyo kwamba wanaume tu siku zote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto, wajjandae Mheshimiwa Juma Othman Hija na Mheshimiwa Khamis Mtumwa.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Mafungu takribani sita ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza nianze kurejea kwenye Katiba, Ibara ya 15 ambayo inasema kwamba kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru. Ibara ya 15(2) inasema:

*"Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote*

*kukamatwa, Kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Katiba yetu ambayo inatuongoza na sote hapa tumeiapa kuilinda na kuitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwakumbushe na hasa niwakumbushe wana CCM. Kwenye hotuba ya Mwalimu Nyerere alipokuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mwaka 1987 kwenye Mkutano Mkuu alisema "Panapokuwa hapana haki wala imani na matumaini ya kupata haki, hapawezি kuwa na amani, utulivu wa kisiasa na hatima yake panazuka fujo, utengano na mapambano" haya ndiyo maneno ya Baba wa Taifa, amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumza kwa mara ya kwanza tokea Mbunge mwenzetu ashambuliwe kwa risasi. Tumekaa humu ndani kwa mara ya kwanza kwa maana ya bajeti, tunakwenda kupitisha zaidi ya shilingi bilioni 596, asilimia 63 ya bajeti yote ya Wizara ya Mambo ya Ndani inakwenda Jeshi la Polisi mpaka leo Jeshi la Polisi halijaweza kufanya uchunguzi na kujua ni nini ambacho kilitokea Mbunge mwenzetu akapigwa risasi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakutana hapa tunataka tuwatengee fedha Jeshi la Polisi lakini tuna watu ambao wana miaka inakaribi miwili wamepotea hawajulikani wako wapi akina Ben Saanane. Mwandishi wa Habari, Azori Gwanda juzi mkewe amapata mtoto, mtoto hamuoni Baba yake na Jeshi la Polisi halina maelezo yoyote ambayo limeyatoa mpaka sasa hivi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa hotuba ya TAMISEMI na Utawala Bora nilizungumza kuhusu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, Ndugu Kanguye ambae ni Diwani wa Chama cha Mapinduzi, wiki iliyopita Mama mzazi wa Ndugu Kanguye amefariki dunia, amefariki

dunia akiwa hajui mwanawewe yuko wapi. Waziri wa Utawala Bora alituambia kwamba siyo kazi ya Usalama wa Taifa kukamata tukasema sawa, hii Serikali moja, Wizara ya Mambo ya Ndani itakuja, Wizara ya Mambo ya Ndani imekuja haya watueleze! Kama siyo kazi ya Usalama wa Taifa ni kazi ya Polisi, Polisi watueleze kwamba Ndugu Kanguye yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni mlolongo wa mambo mengi ambayo yanaweza yakatuletea shida kubwa sana katika nchi. Mbunge wa Kilwa, Ndugu Bungara amezungumza kwa hisia na wakati mwingine muache watu wazungumze kwa hisia kwa sababu watu wanapozungumza kwa hisia ndiyo wanaongea yale mambo ambayo yanawahusu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Mbunge Bungara ana mwongozo unamsubiria; kwa hiyo, nakuomba elekeza hoja yako kwenye mambo yako.

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 Juni, 2017, mama mmoja anaitwa Ziada Salum wa Kitongoji cha Maparani, Kibiti alichukuliwa na jeshi la Polisi saa 6.00 mchana na leo ni miezi 11 mama huyu hajaonekana yuko wapi. Siku hiyo hiyo kuna mtu anaitwa Rukia Muhoni na Tatu Muhoni ni ndugu hawa, walichukuliwa na Jeshi la Polisi mpaka leo hii tunavyozungumza miezi 11 hawajaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina orodha hapa, nina watu 348 wa Wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji na hapa hatujajumlisha watu ambao wanatoka Kilwa. Kuna mtu jana hapa alizungumza kuna zaidi ya watu 1000 wamepotea, inawezekana orodha niliyonayo hapa na nitampatia Waziri, watu 348 na katika hao watu 68 wamethibitika wamekufa. Tunaomba Serikali itueleze nini kinaendelea Wilaya za Kusini ya Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, dakika tano zako zimekwisha. Mheshimiwa Juma Othman Hija, ajiandae Mheshimiwa Khamis Mtumwa. Mnataka dakika kumi msikilizie ndani au msikilize nje? Mheshimiwa Zitto Kabwe zima *microphone* yako.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii kutoa michango yangu katika Wizara hii kubwa katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha uwezo mkubwa wa kuongoza nchi hii na *Insha Allah* Mwenyezi Mungu ampe kila la kheri katika kufanikisha suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, namshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa umahiri wao mzuri wa kuwasilisha hotuba hii ambayo imebeba mambo mengi katika nchi yetu hii. Nchi yetu hii ni kubwa lakini hotuba yao hii ni fupi sana lakini ime-cover kila kitu katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, nawapongeza watu hawa kwa umahiri wao huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itakwenda kwenye kukumbusha masuala ambayo nimekuwa nikiyazungumza mara nyingi kwenye vipindi vyetu vyaa maswali na majibu. Suala la kwanza ni kuhusu kituo changu cha Mkokotoni, kituo hiki ni mionganoni mwa vituo vikongwe sana katika nchi yetu hii. Ni kituo chakavu kabisa, kinahitaji matengenezo ya kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ilianzisha jengo pale katika kituo hiki, lakini mpaka sasa hivi jengo lile limekwama, hatujui nini kinaendelea. Jengo limebakia kama gofu, hatujui hatima ya jengo lile. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuiomba Wizara ikamilishe jengo lile ili askari wetu pale wapate makazi mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu pale wana hali ngumu sana, katika mvua hizi ambazo zimenesha juzi, askari wetu imebidi wahamie chumba cha mahabusu kufanya kazi, *imagine* chumba cha mahabusu askari wetu wamehama kwenye Ofisi yao wanatumia chumba cha mahabusu kufanya kazi katika kituo kile. Kwa hiyo, naionomba Wizara ikamilishe masuala yale ili askari wetu wale waweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimekuwa nikizungumza kila siku ni kituo cha Polisi katika Kisiwa cha Tumbatu. Suala hili nimekuwa nikizungumza kila siku kuiomba Wizara kwamba itujengee kituo katika Kisiwa cha Tumbatu. Jiografia ya Kisiwa cha Tumbatu inahitaji huduma zote pamoja na huduma za usalama. Masafa kutoka Mkokotoni mpaka Tumbatu ni *almost* kilomita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linapotokea neno Kisiwa cha Tumbatu inabidi askari watoke Mkokotoni waende Tumbatu, wavuke kwa kutumia bahari. *Imagine* kama kuna kitu kimetokezea kule hatuombi kitokezee, lakini mpaka wakifika pale Tumbatu basi lilitokozee limeshaathiri sana. Kwa hiyo, naionomba suala hili kwa mara nyingine kwamba Wizara itujengee kituo katika Kisiwa cha Tumbatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni vitendea kazi katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Waheshimiwa wengi hapa wamesimama wanazungumzia vitendea kazi wamekuwa wanaomba magari na vifaa vingine, lakini Wizara hii ina tatizo moja kubwa sana la vitendea kazi hasa kwenye *stationeries*. Mwaka jana nilipata bahati mbaya, niliibiwa simu yangu nyumbani kwangu nika-report polisi Dodoma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofika pale kituo cha polisi Dodoma nilitakiwa nichukuliwe maelezo, basi askari pale hata *stationery* hawana, *stationery* ya kuandika ile *report* yangu hawana mwisho niliona kwamba kwa kweli ni kitu cha

aibu, askari pale wanatumia *order paper* hizi zetu za Bunge, ndio wanaandikia *report* zetu. Kwa hiyo, Wizara iwasaidie siyo Dodoma tu lakini nchi nzima kwamba kuna tatizo la *stationeries* katika vituo vyetu hivi vya Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo leo nataka nichangie ni kwamba utaratibu wa viongozi wetu wa Wizara hii kutembelea katika mikoa. Mheshimiwa Waziri mara baada ya kuchaguliwa alikuwa na utaratibu mzuri wa kutembelea katika mikoa yetu na wilaya zetu. Namwomba Waziri utaratibu wake ule uwe utaratibu wa kudumu aendelee nao katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khamis Mtumwa jiandae Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi, kwa kutuwezesha kuwa wazima wa afya na kuweza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo anafanya ya kutuletea maendeleo katika Taifa letu na kusimamia amani ya nchi yetu hii. Kwa kweli Mheshimiwa Rais anastahiki pongezi sana tena sana kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya za kuweza kuhakikisha Taifa letu hili linasimama kwa amani na Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na /GP na Makamishna wote, hongera sana kwa kazi ambayo wanaifanya ya kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa na amani sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia sasa kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika kipengele cha hali ya usalama nchini. Katika taarifa yake ukurasa wa tano, Mheshimiwa Waziri amesema matukio ya uhalifu yamepungua na kutoka mwaka 2017 kutoka matukio ya 56,913 yamepungua hadi kufikia matukio 47236 mwaka 2018. Hongera sana kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri zaidi kwamba ili matukio haya yapungue zaidi ni vyema sasa Mheshimiwa Waziri Wizara yake ikaendelea kuimarisha vifaa vya utendaji kazi katika Jeshi la Polisi na hasa kwenye kipengele cha mafuta ili kuhakikisha maeneo yote ambayo yanatokea matukio mbalimbali, Jeshi letu la askari la Polisi liweze kufika vizuri na kuweza kufanya kazi katika maeneo hayo ili kupunguza haya matukio yetu ya uhalifu ambayo yanaendelea kutokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuchangia kuhusiana na suala la *basic training* za polisi. Hawa kuruta wanapofanya mazoezi wakati wapo katika *training* zao wanakimbia kwa kutumia viatu vya kiraia pamoja na *tracksuit* hizi za kiraia. Sasa unapofika wakati wa *field* yenye we utamkuta askari amevaa lile *bullet proof* ambalo halipungui kilogramu 10 au amechukua mashine ya *SMG* isiyopungua kilogramu saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vyema hawa askari wakaweza ku-cope na haya mafunzo ambayo wanayapata. Kwenye mafunzo hawachukui hivi vifaa lakini kwenye *field* utakuta wanabeba hivi vifaa na utawakuta wamevaa mabuti na *helment* karibu masaa yote ya kazi wanatakiwa vifaa vile wawe navyo. Kwa kweli ili kuwajengea mazingira mazuri ya kuweza kupambana zaidi na kuweza kuzoea vile

vifaa ambayo wanavitumia ni vyema wakati wa *training* vilevile waweze kupata hivyo vifaa ili waweze kufanya mazoezi vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nichangia kuhusiana na suala la ujenzi wa nyumba za askari na vituo vya polisi. Mwaka jana tumemwambia Mheshimiwa Waziri kwamba hizi nyumba za askari hasa katika iji letu hili la Dodoma zimakaa kama *incubator* ambapo ukapeleka mayai yako pale baada ya muda utapata vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu kweli kwa sababu askari wetu wanafanya kazi nzuri, lakini wanapoenda kulala siku za joto inakuwa balaa, siku za baridi inakuwa balaa, maana yake juu kuna bati, pembeni kuna bati na chini kuna bati. Sasa kama mtu ana mke ana watoto sijui wanaishi katika mazingira gani katika nyumba zile ni vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vema nyumba hizi tukazifanyia ukarabati zikaendana na hadhi ya Jiji la Dodoma. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutenga zile billioni 10 za kuhakikisha kwamba askari waweze kuishi vizuri na ningewaomba sana hizi nyumba 400 kila mkoa ambazo zimebekwa humu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ziweze kuonekana kwa vitendo. Kwa sababu mwaka huu umetuambia nyumba 400 kila mkoa ningeomba sana mwakani nyumba tusije tukazizungumza tena hasa katika hili Jiji la Dodoma askari wetu kukaa kwenye nyumba za *incubator* za kuzalishia vifaranga vya kuku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna suala la huduma za maji na umeme. Mwaka jana nilimshauri sana Mheshimiwa Waziri, hizi huduma ni bora wangekopi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JW) wanafanyaaje na wao wakachukua hizi wakafanya, kwa sababu huduma za maji na huduma za umeme kwa kweli ni gharama kwa askari mwenyewe kulipa. Imefika mahali miaka iliyopita wanafika askari wanastaafu wanakopesha pesa zao mfukoni kulipia huduma za maji na umeme katika vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri askari wetu hawa pesa ambayo wanapata ni ndogo sana halafu pesa hiyo hiyo takribani huduma ya maji Mheshimiwa Waziri anaijua, haipungui shilingi 50,000 au 60,000 kwa mwezi na huduma ya umeme karibu 50,000 au 60,000. Ukiangalia mishahara yao ni midogo, kidogo linakuwa ni suala gumu zaidi kwa askari wetu hao. Naomba sana Mheshimiwa Waziri suala hili akalichukua akalifanya kazi endapo mwakani akija atuambie kwamba amefanya kama JW wanavyofanya kuhusu suala la maji na suala la umeme kwenye huduma hizi za malipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia la *uniform*, askari wetu wanunua wenyewe, ni nadra sana kupewa viatu bure kama ulivyokuwa unavaa wewe, ni nadra sana kupewa hizi *uniform* bure kama ambavyo wanavyopata kwa mgao ambao wanapopewa mara nyingi wanakuwa wanatumia pesa zao za mshahara sasa kujinunulia hivi vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri tu kwenye hotuba yake, kuna viwanda ambavyo vinatengeneza viatu na kuna viwanda ambavyo vinatengeneza nguo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hili alibeve ili sasa migao itakapotoka itoke kwa wakati na nguo hizi na vifaa wasiwe wanunua wenyewe waweze kununuliwa na jeshi letu la polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mishahara na posho za askari nalo hili imekuwa ni shida sana, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri aziangalie kama alivyosema kwenye maelezo yake wakati anahutubia hapa, kwamba yale masuala madogo madogo amezungumza nao. Mwakani naamini yale masuala madogomadogo hatosema amezungumza nao atakuja hapa atatuambia masuala madogo madogo tulishamalizana nao ili na wao waweze kufanya kazi vizuri kama Jeshi letu la Polisi ambao wanatulinda sisi tunalala kwa amani, wao wanapata shida, lakini mishahara yao bado na hali zao za mambo madogo madogo ambayo yapo zinakuwa vilevile zipo katika hali ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri suala hili alichukue *serious* kweli kwa sababu wenzetu hawa wanafanya kazi kubwa sana ya kulinda amani ya nchi yetu lakini posho zao na maslahi yao yanakuwa na shida. Hata wenzangu wamezungumza kuhusiana na suala la askari anapandishwa cheo anakaa miaka chungu mzima hapati matunda ya kile cheo ambacho anakipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na namwelewa utendaji wake mzuri na Mheshimiwa Naibu Waziri watalizingatia hili, tuone sasa haya madeni ambayo askari anadaiwa yakamilike na hayo mambo mengine mazuri yapatikane vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia katika Kitengo cha Upelelezi, Mheshimiwa Waziri upelelezi hauwezi ukafanyika bila fedha, lazima zipatikane fedha, hawa askari wetu waweze kufanya upelelezi vizuri, vinginevyo kitengo hiki kitakufa kabisa. *Information is money*, huwezi ukaenda kwa mtu ukamwambia akupe taarifa au uka-collect *information* bila kuwa na fedha, lazima uwe na pesa kidogo umpatie maji ya kunywa kidogo, umpatie mtu kidogo vitu fulani ili aweze na yeye kumtengeneza ili akupe *information* Mheshimiwa Naibu Waziri anajua sana kazi hizi wameshazifanya sana wanazielewa. Kwa hiyo, nawauomba sana Kitengo hiki cha Upelelezi ili kiweze kufanya kazi vizuri...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, ajiandae Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. KHAMIS MTUMWA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia leo

kusimama hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara ambayo ina maisha ya wananchi moja kwa moja kwa sababu inalinda raia lakini inalinda na mali zao. Kwa hivyo hapo utaona ugumu wa kazi hii wewe unayelindwa una mali, anayekulinda hana mali. Kwa hiyo, hii Wizara kwa kweli ina kazi ngumu . (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri tumeona kuna mambo mazuri ambayo yameelekezwa kwa Jeshi letu la Polisi. Tunaomba mambo hayo yafanyike kwa utaratibu kama yalivyopangwa. Mheshimiwa Waziri nimshukuru mwaka jana katika mchango wangu nilizungumzia Kituo cha Polisi Dunga na nimepata habari kwamba tayari ujenzi umeanza. Kwa hiyo namshukuru na nampongeza Mheshimiwa Waziri na naomba fedha zipelekwe kwa wakati ili ujenzi uweze kuendelea vizuri na kile kituo kimalizike kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mkao wangu wa Kusini Unguja tuna upungufu mkubwa wa magari kwa ajili ya kufuatilia shughuli mbalimbali za maaskari. Mkao wetu una vituo vingi lakini kuna ukanda mkubwa wa utalii, hatuna magari, baadhi yamekuwa yakinumika magari yetu kuwasaidia askari ni wajibu wetu. Kwa hiyo, tunaomba katika haya magari ambayo nimeyaona katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, basi na Mkao wetu wa Kusini wasisahau kutuletea magari hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vie nimeona kuna ujenzi wa nyumba za maaskari, Mkao wa Kusini na kuna baadhi ya vituo vinahitaji kusaidiwa nyumba za askari, kwa hivyo nayo wasitusahau pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nizungumzie, nataka nisifu Wizara hii, kazi ya kulinda raia na

mali zao ni kazi kubwa. Kwa hivyo, bado namwomba Mheshimiwa Waziri, elimu ya kutii sheria bila shuruti iendelee kutolewa kwa wananchi wetu, kwa sababu maelezo yanayoelezwa humu ndani inaonesha wazi kwamba bado wananchi wanataka kupata elimu ya kutii sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi na raia ni ndugu, ni kama watoto pacha sisi tunawategemea lakini kwa kweli kumekuwa na manung'unico mengi ambayo mengine hayana ukweli, mengine yanaweza yakawa yana ukweli fulani, kwa hiyo, ipo haja ya elimu kutolewa kwa raia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nilipongeze Jeshi la Polisi, Zanzibar kulikuwa na wakati mgumu sana, lakini tunashukuru Jeshi la Polisi waliweza kuzuia ugumu ule na sasa tunaishi kwa amani na utulivu. Wizara wanafanya kazi nzuri lakini kwa kuwa kuna wahalifu wengine hawataki kuona uzuri huu, tunaomba kila mtu achukue nafasi yake sisi raia tuna nafasi ya kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi tushirikiane nao na wao wanayo nafasi ya kushirikiana na sisi na wao washirikiane na sisi vizuri. Jeshi hili lisiwe na uadui kwa raia na sisi raia tusiwe na uadui kwa Jeshi la Polisi kwa sababu tukilikosa kwa kweli hatuwezi kuishi hata kidogo, tunauona umuhimu wa Jeshi la Polisi pale yanapotokea matatizo, lakini tumekuwa tunawalaamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, pia wako askari walikufa katika kutekeleza majukumu yao na wengine waliuawa kama walivyouawa raia wengine, halifurahishi kwa sababu uhai wa mwanadamu hauna thamani ya kitu chochote. Hata hivyo, haya mambo yaende sambasamba, sisi raia tuweze kutii bila shuruti, nao askari baadhi yao kwa sababu na wao ni binadamu kama sisi na wao bila shaka wengine wana upungufu, yule mtu mmoja asiharibu Jeshi zima la Polisi ambalo linafanya kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waendelee na kazi nzuri, yale madogo madogo ambayo yanalamikiwa tuyafanyie uchunguzi na tuyachukulie hatua. Kuna askari wanafanya kazi nzuri na wamekuwa wakidai posho zao muda mrefu. Mheshimiwa Waziri amefanya ziara Zanzibar na Mheshimiwa Naibu wake amefanya ziara, lakini hata Wakuu wa vikosi nao wamefanya ziara na wamekuwa wakiwaahidi, kwa hiyo tuwatimizie yale matakwa yao ambayo bado hawajafanikiwa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kidogo inaleta huzuni kwa sababu ninapoona mwenzangu tumeingia kazini wote mwaka 2013/2014, wao wamepata zile posho, wengine hawajapata, kwa kweli haileti picha nzuri na wako hawa wanaopata posho ya kazi maalum. Kuna wengine wamepata, lakini wengine hawajapata na wote wameanza kazi pamoja, wameingia kazini pamoja, wamefuatilia, wamekwenda mpaka Makao Makuu, lakini majibu hakuna. Kwa hivyo tuwatazame hawa watu, yale manung'uniko madogo madogo tuweze kuyaondoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya askari wa *FFU* Machui, walishiriki katika ile Operesheni Tokomeza na wao pia wanasema hawakupata posho zao mpaka sasa hivi. Mambo mazuri mengi wanayafanya, lakini haya madogo madogo najua yako ndani ya uwezo wao, kwa hivyo tujitahidi na wao tuwakamilishie ili mambo yaweze kwenda vizuri, lakini kiujumla Jeshi la Polisi wanafanya kazi nzuri. Kazi mnayoifanya tunaiona, tusingeweza kuishi kwa amani na utulivu kama hawapo, kuwepo kwao kuna umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, yale niliyozungumza kuhusu vituo vyaa polisi wayatekeleze. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia, wajiandae Mheshimiwa Upendo Peneza na Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayofanya. Pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote Serikalini kwa kazi kubwa wanayofanya. La kwanza nizungumzie kwamba katika Wizara ambazo zina changamoto lukuki katika nchi hii ni Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Wabunge wenzangu wote wamezungumza suala la miundombinu ya majengo kwenye makazi ya askari, maofisi na hata magereza na vituo nya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mwaka wa tatu sasa, changamoto ya Wizara hii haiwezi kutatuliwa kwa jinsi tunavyokwenda, hali ni ngumu sana, fedha ni kidogo. Tulifanya ziara Mtwara na Lindi tukakuta viporo nya miradi ambayo hata kwenye kitabu cha bajeti baadhi yake haikuwekwa. Sasa Waziri tungependa atuambie ile miradi tuliyotembelea japo yeye hakuja ni kwa namna gani Serikali sasa inatatua changamoto ya hizi Wizara kwenye miundombinu ya majengo yale kwa sababu tumeshawekeza na sasa hakuna utekelezaji wa ukamilishaji wa hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais kwa hela aliyotoa kwa ajili ya Makao Makuu Dodoma lakini fedha zile hazitasaidia kwenye miradi ambayo tumekagua. Wizara hii Jeshi la Zimamoto, Polisi na Magereza magari yake ni mabovu sana na hasa kwangu kule Mbulu, hayana matairii, hayana muda wa matumizi, muda wa matumizi wa hayo magari umeshakwisha. Kwa hiyo, Waziri aje atuambie ni kwa namna gani angalau tunakombolewa kwenye tatizo kama hili la ubovu wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba matumizi ya magari ya Serikali ni miaka mitano. Kwa hiyo, inapokuwa zaidi ya miaka mitano yale magari yanakuwa hayana tena hadhi ya matumizi katika utendaji wa Serikali na hasa askari. Magari ya askari ni magari yanayotakiwa yaye mapya, watakapoitwa mwendo wao ni wa kasi, wanakimbia, kuna roho za watu juu ya yale magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yanapokaa muda mrefu na yamechakaa, kule kwangu Wilaya Mbulu, magari yote matatu, majimbo yote mawili yamechakaa. Nimeomba miaka mitatu sasa na leo tunapitisha bajeti hakuna gari, lakini kwenye makazi, ni mahali gani tutakwenda, kule Mbulu tukienda Magereza haifai, imejengwa toka ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Wilaya hakifai, kimechakaa, majengo mengine yale ya makazi ya askari hayafai, wangeenda waandishi wa habari tungejificha. Nafikiri hata hayo yanayojengwa anzeni na Makao Makuu ya Maafisa wa majeshi yetu yaliyo chini ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waende kwenye ngazi ya mikoa kujenga nyumba za Makamishna wa Mikoa, waende kwenye ngazi za Wilaya tupeleke tuanze kwenye ngazi za Wilaya tupeleke tuanze kwenye ngazi za maafisa ili hata wale askari wa kawaida wakipangisha, basi na yale majengo yafanane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari ni utii, askari ni uhodari, askari ni uaminifu wanatupigia saluti, wanampigia Waziri saluti, mtu yoyote saluti mwenye mamlaka kwake, siku moja na sisi huko tunakokwenda kwa Mwenyezi Mungu wao watapewa ufalme huo, tutawapigia wao saluti. Nadhani mambo haya sio mambo ya mchezo wakati fulani tunapoyaongea, yanahitaji sana kuangaliwa na kwa namna gani tunatatua basi hata kwa awamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia kuna askari wachache wanaochafua majeshi yetu ziara ya viongozi Waziri, Inspeksa Generali, *RPC* akutane na baadhi ya viongozi na baadhi ya wanajamii na viongozi wa madhehebu ili masikio yake pia yapate kusikia eneo hili kuna matatizo gani, kukagua tu askari na kupita hakusaidii kuona sikio lako, kisogo chako kina kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna Wabunge wameongea mambo hapa, kama hayana ukweli wafute zile kauli. Mfano, Mheshimiwa Zitto anazungumza watu 68

wameuawa, watu mia tatu na kitu hawaonekani, aisaidie Serikali upelelezi kwa sababu sisi tunazungumza kwa niaba ya Watanzania, mambo haya yanapotosha umma . (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kwamba, wakati huu ambapo tunaelekea kwenye kupidisha bajeti, mambo ni mengi, lakini tuyaweke kwenye vipaumbele, kuna baadhi ya mambo tumetembea sisi na Mheshimiwa Waziri, tumetembelea Wizara hii, tumeona mambo mengi sana, tumeona miradi viporo, tumeona hakuna namna ya utatuzi, basi tutafute njia mbadala ili tuweze kukamilisha hiyo miradi ambayo tulitarajia kwa namna ya pekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nalipongeza Jeshi la Polisi kwa sababu kazi hii wanayofanya sio rahisi. Kama tunavyozungumza sisi ni kazi ngumu sana, unapolala yeye anakulinda na mali yako, unapoamka yeye anaendelea kukulinda, lakini mazingira yao hayafanani na kazi wanayofanya. Kwa hiyo, nadhani hatujawatendea haki askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa dakika tano, ni ya kuishukuru Serikali, mimi nilitaka dakika 20 za kuizungumzia Wizara hii na kwa namna ya pekee nimwambie hatuwatendei haki askari. Mheshimiwa Mwigulu, yeye kama Waziri, ajitazame, atafakari maneno tunayoyazungumza hapa. Mengine yeye ni mtu mzima, aende kuyachambua kuna mambo ambayo yana ukweli kabisa na yafanyiwe kazi na yeye kama kiranja wa Wizara hii kwa nafasi yake anapaswa kuangalia Watanzania wanasesma nini. Mengine yanababishwa na askari kutokana na mazingira ya kazi yao. Kazi inapokuwa ngumu, mazingira yanapokuwa si rafiki, lazima mtu anashawishika kwenda kufanya mambo mengine ambayo hayana maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba watuangalie kwenye ngazi za wilaya, mikoa, na ngazi za Taifa ili tuweze kufanya kazi hii kwa weledi na askari wawe na amani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha, mchango wako ni mzuri mpaka umejisahau.

Mheshimiwa Upendo Peneza, ajiandae Mheshimiwa Mariam Msabaha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii nami kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 3(1) inasema Tanzania ni nchi ya kidemokrasia inayofuata mfumo wa vyama vingi. Maana yake ni kwamba vyama vyote ambavyo viko Tanzania vyote vinasajiliwa kulingana na Katiba na sheria ambazo ziko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo tungetegemea kwamba sheria ambazo zinaruhusu vyama vyaa siasa kufanya mikutano ya hadhara iweze kuheshimiwa ili wananchi wakapate fursa ya kusikiliza vyama hivi vyaa siasa lakini pia vile vile kutimiza wajibu ambaa upo kutokana na Sheria ya Vyama vyaa Siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha ni kwamba Jeshi letu la Polisi na mtakubaliana na mimi kwamba Vyama vyaa Upinzani havina uadui wowote na Jeshi la Polisi na ndio maana pamoja na kwamba katika bajeti hii upinzani hatujawa na hotuba mbadala kwa sababu ya changamoto zilizopo, lakini kwa miaka mingi ambayo imekuwa ikipita upande wa upinzani umekuwa ukitoa maoni namna gani ya kuboresha maisha ya askari wetu. Tumekuwa tukifanya hivyo kwa sababu tunatambua kazi kubwa walionayo ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo maoni kutoheshimiwa, leo Jeshi la Polisi limekuwa ni sehemu ya kukandamiza demokrasia ndani ya nchi hii. Jeshi la Polisi limekuwa pale mtu anaposimama na kuikemea Serikali, mtu anaposimama na kuonesha kwamba hapa Serikali imekosea, mtu huyo anabadilika na kuwa adui, ataitwa mchochezi, ataitwa majina ya kila namna ili mradi tu kuhakikisha kwamba uongozi au Awamu hii haisemwi, haikoselewi badala yake ni kusifiwa tu kwa mema tu wanayoyafanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo hatutaweza kwenda na kama Jeshi la Polisi sasa hivi kwa kazi ambayo inaifanya, mfano, kama dada mmoja ametangaza maandamano ya tarehe 26, viongozi wangu wa Geita, Katibu wangu, wamekamatwa kana kwamba ni sehemu ya Mange Kimambi. Uwoga ambaao unatengenezwa ni kana kwamba wananchi wa Kitanzania hawaruhuswi kusema na kuikosoa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tutakubali kwenda kwa kile tu ambacho kinasemwa na Rais, kwenda kwa kile tu ambacho Serikali inasema, basi hatutafika na tunaendelea kurudi nyuma. Jeshi letu la Polisi leo kwa kazi yote ambayo wameifanya na nitasema tu kwamba kipindi cha nyuma tukiwa na /GP Said Mwema alianzisha mpango wa kutengeneza jamii iwe na urafiki na polisi wetu. Mpango ambaao sasa hivi unaendelea kurudi nyuma hatua nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakandamiza demokrasia Polisi wale wa ngazi za chini wanajengeka ubabe wa hatari. Raia wamekufa mikononi mwa polisi, kijana wa Mbeya ameuawa mikononi mwa polisi, ndugu yake Heche ambaye amezikwa jana ameuawa mikononi mwa polisi kwa kuchomwa kisu. Hatuwezi kuwa na Taifa ambalo watu ambaao tunategemea watulinde na mali zetu ndiyo wanaotuangamiza na kutufanya tufe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanaanza kwa sababu ya ubabe ambaao umeanza wa kushughulikia

viongozi, watu ambao wanatoa mawazo mbadala, sasa yanaenda mpaka kwa raia ambao kwa namna moja ama nyingine inawezekana wana ukosefu katika maeneo yao, ubabe wa hatari unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina sababu ya Jeshi la Polisi kujitengenezea uadui kwa sababu hawana nyumba za kutosha, wanaishi na sisi kwenye jamii, ni ndugu zetu, ni waume zetu, ni shemeji zetu. Tungependa tuishi nao kwa amani, hakuna haja ya kuua watoto wetu akina Akwilina halafu leo jalada hilo linafungwa kana kwamba polisi wameshindwa kufanya uchunguzi hata baina yao wao wenyewe kumtambua ni nani halisi aliyepega risasi na kumuua Akwilina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishia kumfariji mama kwa sababu anatoka familia ya kimaskini na hakuna la maana lolote linalofanyika. Kesho, keshokutwa, Watanzania ambao wameumizwa na Jeshi la Polisi kutochukua hatua yao, watatumia nguvu kuwashughulikia watu, watawaua polisi jambo ambalo halitakuwa jema. Sasa ni vyema tukachukua hatua hiyo mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hiyo ambayo si halali ya kukandamiza demokrasia nchi hii ambayo polisi wamekuwa wakiifanya, kule Geita kuna mauaji ya akinamama ambayo yanafanyika. Sasa hivi mama akienda shambani kule Nyangh'wale anatekwa, anavunjwa shingo, wanauawa. Wanatafutwa akinamama wajawazito na akinamama tu wengine katika maeneo ya shamba, suala ambalo limejenga hofu kubwa sana. Sasa ningeomba hii nguvu kubwa ambayo inatumika kudhibiti maandamano ya magari yote hayo tunayaona barabarani, polisi na vifaa vyao hebu vitumike basi viende Nyangh'wale, hawa akinamama wafanye shughuli zao kwa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nitamuomba kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba anijibu kama mtu anayetegemea kuwa Rais ndani ya nchi hii siku moja.

Alitutangazia kwamba alikuwa na nia na alishiriki kwenye kura za maoni ndani ya chama chake, kwa hiyo, sidhani kama hiyo nia imekufa mapema hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba Wabunge wa Viti Maalum wapo humu Bungeni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara 66 na Ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazungumza uwepo wa Wabunge wa Viti Maalum ambao majina yao yanapendekezwa na vyama vyao na baadaye wanapatikana na kuunda ile asilimia isiyopungua 30 ya watu ambao wako ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na Wabunge wengine wa Viti Maalum ambao tuko huku ndani tumekuwa tukizuiwa kufanya mikutano yetu ya hadhara. Namwomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Wabunge wa Viti Maalum tunaambiwa tufanye kazi, sisi sio Wabunge wa vyumbani, tufanye kazi chumbani tuongee na akinamama na hili linaleta mtazamo mbaya hata katika jamii, ndiyo maana Wabunge wa Viti Maalum wengi wamekuwa wakidhalilishwa kwa sababu watu hawajui kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaache wanawake wafanye kazi, wafanye mikutano, wawawakilishe wananchi ili wananchi waone kama kweli hawa ni Wabunge ambao wapo kwa ajili ya kuwawakilisha. Badala yake tunaonekana kama tuko tu kumaliza mishahara ya Serikali, "unalipwa milionio 12, unalipwa milioni 12" sasa sawa! Kazi yangu haithamiwi, siruhuswi kufanya kazi, sasa kwa nini nakuwa Mbunge? Kwa sababu kama unalipwa ujira basi ufanye kazi inayopaswa kufanyika na tunahitaji kuwakilisha wananchi wote. Watu wafanye mikutano katika maeneo yao. Kwa hiyo, naomba sasa sheria za nchi yetu ziheshimike, watu wawasikilize wananchi, huwezi ukaja humu ndani ukamwakilisha mwananchi ambaye hujamsikiliza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Viti Maalum wafanye mikutano katika maeneo yao, kama ni katika mikoa na kuweza kuwawakilisha wananchi. Badala yake tutasema

kwamba Serikali ya Awamu hii ya Tano ipo kukandamiza wanawake, Serikali ya Awamu hii ya Tano ipo kuzuia maendeleo ya wanawake, badala yake tutasema kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano inataka kutengeneza mazingira magumu ya wanawake kuwa Wabunge kwa sababu katika siasa tunasema *it's all about visibility*, nani kakuona hata katika Viti Maalum, badala yake sasa kama tunawafunga watu, ngono zitatumika, rushwa ya hela itatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawatisha jamii kutafuta nafasi za kugombea. Tuwaache wanawake waonekane na hata kuzuia mikutano ya hadhara, inaathiri hata vijana wengine wasionekane kwa sababu kwa vijana kama mimi tumekuja humu ndani ya Bunge kwa sababu ya kazi ambazo tumefanya, tumefanya mikutano, jamii imetuona ikatuamini. Kwa hiyo, si tu kwa hivi wanavyovunja sheria za nchi, lakini pia wanaathiri ndoto za akinamama, wanaathiri ndoto za vijana ambao wangependa siku moja kuwa viongozi ndani ya nchi, kuwa viongozi wema ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nategemea kwamba, katika majibu ambayo kaka yangu atanipatia asinijibu kwa kutoa sababu kama zile alizojibu kipindi kile Katiba na Sheria. Tuweke mstari wa mbele kama tunataka kuendelea na kama unategemea au siku moja unataka kuwa kiongozi wetu, basi *show the art* kwa majibu unayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msabaha, wajiandae Mheshimiwa Mary Muro, Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama katika Bunge lako hili Tukufu na leo ikiwa ni siku *Al-jumaa* kwa hiyo *Insha Allah* Mwenyezi Mungu atasimama na mimi, nitakayoyaongea, Serikali itayachukua wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwape pole viongozi wangu wote ambao wamepitia misukosuko kwenye Jeshi la Polisi na ambao hata wengine sasa hivi wapo magerezani wanatumikia vifungo na wengine ambao wapo kwa mashtaka mbalimbali ndani ya magereza. Niliwahi kusema hapa ndani ya Bunge hili, nikasema sheria za wafungwa na magereza na haki zao zifuatiliwe na wapate faragha ya kukutana na wapenzi wao, sasa viongozi wote tunaelekea huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la haki za raia na vifo vinavyotokana na ukatili wa Jeshi la Polisi. Si vibaya ndugu zangu kuwasema kidogo na kuwakosoa kidogo, polisi unavyoenda kupambana na raia, raia hana silaha na najua Jeshi la Polisi wamefundishwa namna ya kupambana na raia ambaye hana silaha na ambaye hawezi kukuhujumu wewe na kuna vilungo maalum ambavyo wamefundishwa namna ya kupambana na hawa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naona wanakokwenda si kuzuri, wanakamata watu, wahalifu, wahalifu hawana silaha, mhalifu hana chochote, hana hata sindano, lakini kinachofuatia anapata kipigo ambacho ni kitakatifu. Akishapata kipigo kile ambacho kimemsababishia maumivu, wanampeleka wanaenda kumweka *lockup* au rumande, kokote kunakostahili kuwapeleka watu wale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hakuna matibabu, hapa wanakiuka haki za binadamu na sitaki muende huko. Raia, askari huwezi kufanya kazi, hasa Kitengo cha Upelelezi bila kuwa na rafiki raia ambaye ni mwananchi, ndio na wewe unapata uafueni wako wa kufanya kazi. Taarifa utazipata wapi? Taarifa lazima uzipate kwa kupitia kwa raia na ndio maana tunasema polisi wasijenge uhasama na wananchi wasiokuwa na silaha, wasiokuwa na mbinu za kutumia silaha, ni lazima wajenge urafiki ambapo na wao wapate wepesi wenu wa kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wana changamoto, kuna wengine wana vyeo lakini stahiki zao hazilingani na vyeo vyao. Niombi Serikali iongeze mishahara na iangalie namna gani wanavyopandisha madaraja ya maaskari hawa nao wapate stahiki zao, sio kuwatumia kwa matukio tu mbalimbali bali nao wapate stahiki zao ili wapate kufanya kazi kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo waende labda Marekani waangalie askari wanavyofanya kazi. Waende japo hata Kenya wakaangalie askari wanavyofanya kazi, wanafanya kazi kwa kuipenda, kwa hiyo askari wetu wasifanye kazi kwa kulazimishwa kuifanya ile kazi na sidhani kama kuna wanasiasa ambao watawafundisha kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavyokamata wahalifu, wale wahalifu wakishawakamata, ambaye labda kesi hii kaifanya kweli kweli, mpe ile kesi ambaye anastahili kupewa kesi ile, wasimbambikizie kesi. Haya mambo ya kuwabambikizia wananchi kesi, wananchi sasa wanafika mahali wanajenga hofu na Jeshi la Polisi. Wakumbuke bado askari wengi hawajajengewa nyumba, wanaishi uraiani, watoto wao wanasma uraiani. Tunujuana Watanzania, kwa hiyo, wakiijenga mazingira yale, kinafika kipindi sasa na Watanzania nao watakosa uvumilivu kwa sababu wataona, kwa nini mzee wangu kafanyiwa kitendo hiki? Kwa hiyo, mtoto anakuwa anajenga chuki na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahabusu; mahabusu wana haki kama binadamu wengine, lakini sasa mahabusu hawa wanavyopelekwa huko mahabusu, unakuta kwa kweli mahabusu wanakaa dirisha lile ni dogo sana, japo wamefanya makosa. Wengine nimesema wanakuwa wanabambikiziwa makosa, wote wanaokwenda kule mahabusu sio wote wana hatia, sasa unakuta kule mtu analetewa chakula, choo chake kiko pale pale, mazingira sio rafiki na mahabusu. Mlo wake anapata mara moja, hao wengine pia hawana ndugu wa kwenda kuwaangalia kule kuwapelekea chochote. Wale askari ambao wanakaa na wale mahabusu, hawana fungu la kuhudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali ihakikishe sasa wanatenga bajeti ya kutosha. Hii bajeti ambayo tunaisimamia ndani ya Serikali tuhakikishe inapelekwa kwa wakati muafaka ili angalau sasa Serikali na askari hawa ambao wanahusika na mahabusu, mahabusu nao wapate haki zao, kwa sababu unavyomkamata mhalifu sio wahalifu wote wanandugu, wahalifu wengine hawana ndugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie, kuna wale watu ambao wanakamatwa na makosa madogo madogo. Yale makosa madogo madogo tunaweza kuangalia sasa wale ambao wanapelekwa magerezani, wanajazwa magerezani tukaangalie zile kesi za kuku, kesi sjui za nazi, hawa wapewe adhabu ndogo ndogo ili kupunguza msongamano wa magerezani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaongelea kuhusu Chuo cha Mafunzo Ziwani. Hiki Chuo cha Mafunzo Ziwani ni chuo kizuri sana na ni chuo cha zamani na wengi wanatambua. Hiki chuo jamani naona wamekisahau kwa sababu wako askari wengi nao wanatoka huku bara wanapangiwa kwenda Zanzibar. Hata hivyo, sasa hivi hiki chuo kinapoteza hadhi, chuo hiki kiko tangu enzi za mkoloni, tangu enzi za muasisi wa Taifa lile, Mzee Karume lakini zile nyumba ni za siku nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna hospitali, hospitali ile sio inahudumia tu polisi na familia zao, hapana! Hospitali zile zinahudumia mpaka raia ambao wanatoka pembezoni ambao ni majirani wa chuo hiki. Sasa naomba Serikali wahakikishe wanavyotenga bajeti, bajeti hii wahakikishe na upande wa pili inavuka ili kutatua zile kero ambazo zinakabili chuo hiki cha Ziwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mikese, kiko barabarani. Nimshukuru afande ambaye ni Mkuu wa Kituo hiki, amekuwa msaada mkubwa sana, wangeangalia ni namna gani hata waweze kumwongeza angalau chochote. Mheshimiwa Mwigulu, huyu askari amekuwa hana itikadi ya

kazi, anafanya kazi yake kwa weledi mzuri sana, lakini kituo hiki ni cha tangu enzi za Mjerumani. Pale hakuna gari na pale pamekuwa panatokea ajali mara kwa mara na hata viongozi wengi wamekuwa wanapata ajali sana pale ile barabara ya Mikese, si usiku, si mchana. Sasa kituo hiki hakina nyenzo, kituo hiki ukiangala kinavuja, waende siku za mvua waangalie pale panavyovuja, panavuja, majengo yote yanavuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wanafanya kazi katika wakati mgumu, hakuna magari ambapo utasikia ajali imetokea labda Morogoro kwa mbele kule, wanatakiwa watoke pale kituoni, wafuate majeruhi, au kuna wengine wamegongana na pikipiki, lakini gari hakuna, mafuta hakuna, nyenzo hakuna. Unakuta sasa wengine wanatoa pesa zao mfukoni, tusifike huko. Kwanza nimshauri Mheshimiwa Rais...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mary Muro, wajiandae Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze nami kuchangia mada iliyoko mezani. Kwanza ningependa kusema amani ni tunda la haki, mahali popote pale ambapo haki haitatendeka ni kwamba amani haiwezi kupatikana. Tutacheza, tutasema, tutachangia, tutafanya tufanyavyo lakini kama watendaji hawatatenda haki hakuna amani itakayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu kumekuwepo na kamata kamata, mauaji na hao wasiojulikana na vyovyote vile na wale wanaouawa mikononi mwa polisi. Hivi kama ungeweza kufikiria mtu anauawa mikononi mwa polisi, halafu useme kwamba kuna amani hao waliopata huo msiba wa kuuawa huyo ndugu yao mikononi mwa polisi wawachukulieje polisi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kabisa tutakaa tukafikiria hivi kama kweli tunataka kuzungumzia habari ya amani, tuangalie haki inatendeka kwa kiasi gani, ndipo tutaweza kusema kwamba sasa hivi Tanzania tuna amani ya kutosha kwa sababu haki inaenda sambamba na amani. Huwezi kupata amani kama hutendi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama inataka kuhubiri amani tuone haki ikitendeka kwa watu wote na vyombo vyetu nya ulinzi vitende haki kwa wananchi ndipo tutasema kwamba Tanzania sasa hivi ina amani. Hatuwezi kusema *theorywakati practical/hazipo*. Niishauri Serikali kama kweli Mheshimiwa Waziri wetu ana nia ya dhati ya kurejesha amani ile tuliyokulia sisi kwa umri huu, haki itendeke kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia ubambikaji wa kesi, kijana anashikwa, kwanza utaratibu wa polisi kuwakamata wahalifu ni mbovu, kwa sababu sheria zinasema kabisa kwamba utamkamata, utamfikisha mahali akajieleze halafu kesi iende mahakamani, lakini mtu anampiga mhalifu, anageuka yeye kuwa ndio mahakama na kumsababishia maumivu na wakati mwingine kumsababishia kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu zingine polisi wamempiga mpaka kijana mmoja anafika hospitalini anakufa, kwa sababu tu polisi hawajui kazi yao kwamba akishamshika mtuhumiwa huyo sio mhalifu tayari, mahakama ndio itakayosema kwamba yeye ana uhalifu na aingie jela. Hata hivyo, unakuta kwamba polisi anachukua hatua ya kumwadhibu wakati yeye siyo mahakama, tutasemaje kuna amani kama kuna mambo haya yanatendeka? Hiyo amani ambayo tunaihubiri ni ipi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia upekuzi. Jamani hivi kweli unapoenda kumpekua mtu kuna sheria, tuna vitambulisho, unatakiwa kama ni kwenye mtaa kuna Serikali ya Mtaa, inatakiwa ishuhudie mtu anapekuliwa, lakini mtu anaingia yeye kama ni polisi anaanza pekupeku

anaingia chooni, anaingia chumbani, anaingia huku, sehemu zote anaingia kwenye nyumba ya mtu. Hivi huyo mtu anajisikiaje, maana yake hata ile *dignity* yake inapotea. Kwa nini tufanyiwe hivi wananchi wa Tanzania, huko tulikotoka hatukushuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina miaka yote hii sijawahi kuona Serikali ambayo inaruhusu mtu apekuliwe, ukiuliza unaambiwa nimeambiwa kutoka juu, huko juu ambako kupo juu sana, tunajua kabisa juu anakaa Mungu peke yake. Siku hizi anashusha *directive* kwamba sasa utafanya hivi na hivi ni kweli au huko juu anakoeleza kila siku ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri akija hapa atuambie huko juu wanakosema kila siku juu ni wapi huko tukakujue. Kama ni imbinguni tujue kitabu kinasema nini, Mungu alishusha biblia, alishusha maelekezo kwamba taratibu za kidini zitaenda hivyo. Huko juu sasa hivi ambako kila kitu juu, juu, ni wapi? Maana yake tumekuwa hatuelewi huko juu ni wapi? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho ningependa kusema ni upepelezi wa kesi. Mahabusu anakaa miaka sita kwa sababu upelelezi haujatimia, huyo mahabusu akishakaa miaka sita aje ahukumiwe anakuwa na miaka mingapi au akutwe hana kosa analipwa fidia? Kama sio uonezi. Tunataka kuchambua kwa sababu nimesema kabisa amani ni tunda la haki, kama watu hawa hawatendewi haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naapa hakutakuwepo na amani katika nchi hii mpaka tufike hapo, kwa sababu haki isipotendeka, amani natokea wapi wakati watu wanalamika kila kona kwamba nimefanyiwa hivi, mimi unajua ilikuwa iwe hivi, nimefanyiwa hiki, kwa nini ifike mahali hapo, kwa nini tusione kwamba nchi ya amani haina migogoro, haina mambo ya kubambikiziwa, haina mambo ambayo ukiangalia kwa macho hata hivi unaona kabisa kwamba hii sio haki mtu kutendewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea kuhusu watoto magerezani. Tunafahamu kabisa kwamba magereza yetu yanafanya kazilakini Serikali ina mpango gani juu ya watoto wale walioko magerezani ambao wanazaliwa magerezani. Hivi kweli mtoto afungwe pamoja na mzazi wake kwa kosa ambalo hakufanya. Kwa nini isitokee kwamba mtu akishajifungua apewe kifungo cha nje ili yule mtoto aweze kupata haki za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale Ruanda nimekuta mtoto amefungwa na mzazi wake, akipita pale mlangoni kuingia na mtoto ananyoosha mikono hivi kuingia kama mfungwa, ametoka shule anaingia na yeze kama mfungwa, huyu mtoto anajifunza nini labda katika maisha yake atakuwa amejifunza nini? Serikali jamani tunaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasema kwamba kuna amani, huyu mtoto anayejifunza mambo mabaya ya gerezani atakapokuwa atakuwa mbaya kuliko baba yake au mama yake aliyeingia gerezani, kwa sababu atakuwa amejifunza ukatili. Kwa nini ifike mahali tumfunge mtoto yule ambaye hajafanya kosa? Kwa nini tusichukue hatua zingine za kum-rescue yule mtoto ili aje awe kijana mzuri au kijana bora katika maisha yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anapo-*windup* atuambie hawa watoto watafungwa magerezani mpaka lini? Kwa sababu kama ni makosa walifanya wazazi wao na wakati mwingine mimba zenyewe zinapatikana humo humo magerezani, sasa yeze amekosa nini? Hajaingia jela yeze na wala mahakama haikumhusu yeze, kwa nini afungwe kama mfungwa wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kuhusu matumizi mabaya ya silaha au nguvu inayotumika na polisi katika kukamata mtu. Ifike mahali Serikali watueleze vizuri hivi anaponikamata mimi na begi langu kwa kunikwida na kunipiga na kunifanyaje wakati sina silaha, sina nguvu

kama ye ye ambaye amejifunza nguvu za kumkamata, mtu ni nini hiki kinatendeka jamani? Tunatambua amani huyu mtu anayefanyiwa haya ndani ya moyo wake anafurahi au ndugu zake wanaoona anatendewa hayo wanafurahi? Kama hawafurahi, hawana amani hawa watu, hawana furaha na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tufike hapo, kwa nini tusifike mahali pa kufanya yale tuliyokuwa tunafanya enzi zetu miaka hiyo. Serikali zilikuwa zinafanya mambo haya haya na watu hawa hawa tulipo tumeshuhudia mengi, haya tunayoona ni mageni. Mtu anakuja anakamatwa au polisi wanatawanya maandamano au wanatawanya watu ambao wako mikusanyiko. Hii mikusanyiko haina silaha, haina chochote unaamua kutumia risasi ambazo tunazinunua kwa pesa nyngi kufyatua na kuumiza watu ambao ni nguvu kazi. Hivi tunaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukiuliza hivi kwa nini mnafanya hivi? Eti kutoka juu, mbinguni? Yaani iwe ndio kinga tunataka kujua kutoka juu, huko juu kuna nini? Tunajua huko juu anakaa Mungu peke yake, Mheshimiwa Waziri atueleze huko juu kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukamataji holela nimeshangaa kitu kimoja jamani. Sisi tulikuwepo hapa Bungeni siku moja tunashangaa watu wanakamatwa, Wabunge wanakamatwa wanaambiwa kwamba sijui wamempiga Shonza tulishangaa na ile *immunity* iko wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Papian, wajandae Mheshimiwa Taska Mbogo na Mheshimiwa Saddifa.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nishukuru na kupongeza Hotuba ya Waziri kwa maneno mazuri na jinsi ambavyo amejipanga na timu yake kwa ajili ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kiteto tuna Kituo cha Polisi ambacho kimechakaa na ni muda mrefu, nataka niombe Waziri mwenye dhamana atakapopata muda basi tutembelee pale, tumpitie *RPC* wetu, twende pale tufanye kikao tuzungumze, tuone lile jambo tunaliwekaje, yawezekana tukafanya marekebisho ya muda wakati tunafikiria kufanya marekebisho ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema jambo moja la magereza. Niombe Kamishna wa Magereza, haya magereza mengi yangefanya shughuli za kilimo yangeweza kusaidia sana. Pale Kitengule Karagwe lile gereza kule Kagera kuna mvua ambazo ni za misimu yote miwili. Ningombwa hili gereza liweze kutumika kwa ajili ya kilimo cha kuzalisha mbegu kwa sababu wana mashamba makubwa na ni mazuri na hakuna *contamination* ya majirani kwa ajili ya kufanya ile *pollution* ya mbegu ili iweze kutoka mbegu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe huyu Kamishna wa Magereza azungumze na watu wa ASA hiki kitengo chetu cha mbegu na mimi nitakwenda kama Mjumbe wa Kamati ya Kilimo kama kushauri kwa gharama zangu na timu ya kule ambayo ni ya kilimo ya magereza ili tuweze kukaa chini tuone tuainishe namna gani, hawa watu wanaweza kuzalisha mbegu kwa ajili ya Serikali na wananchi wetu na kwa ajili ya Serikali ili tuweze kupata mapato. Hata hivyo, gereza litapata faida kubwa sana kwa kuzalisha mbegu badala ya kuzalisha yale mahindi 60,000 au 70,000 ambao kwa sasa yawezekana haiwalipi kama magereza pia hailipi kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya suala la Uhamiaji. Uhamiaji wanafanya kazi nzuri na kubwa sana lakini shida kubwa wanayoipata, mimi naona kwenye bajeti hapa Mheshimiwa Waziri atakapokuja aniambie maana nimekusudia kushika shilingi. Hizi pesa alizowapangia ni pesa ndogo sana, hawa watu hawawezi kufanya kazi kwa kiwango ambacho wanafanya na shughuli nydingi walizonazo ambazo ni ku-*control* mipaka yetu yote, kulinda ndani, kukamata wahalifu na wahamiaji haramu wakaweza

kufanya hili jambo. Kwa bajeti hii hakuna kitu kitakachoendelea *unless in between tuangalie ni namna gani* Serikali inaweza kuongezea hawa watu bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano mpakani tunao watu wengi ambao wanaingia, hizi nchi jirani ambazo tumepakana nazo kwa kuwa Tanzania tumepakana na nchi nyngi. Kuna malalamiko mengi ambayo watu wanaingia na kumetokea watu; Mheshimiwa Waziri mwenyewe anakumbuka alienda kuchoma silaha pale Kigoma, watu wameingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hawa watu wanapoingiza hizi silaha wanakutana na raia wetu wanakaa nao, wanazungumza, wanakula nao, wanahifadhi hizo silaha, leo uhamiaji wanapokwenda kukamata wananchi na baadhi ya Wabunge wanalamika kwamba wale watu wamewaonea, *its quite impossible*, lazima Uhamiaji wachape kazi na waendelee wasirudi nyuma na wasikatishwe tamaa na wasonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri juu ya jambo la Uhamiaji. Kuna haja ya Uhamiaji kukaa na Wabunge wa Mikoa ya mipakani, Kagera, Kigoma, Tunduma na kwingineko ili kunapotokea zile *complains* angalau waweze kukaa wakubaliane baadhi ya mambo ambayo *technically* lazima yafanyike kwa wananchi ili kudhibiti usalama wa wananchi na raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea malalamiko mara nyngi wanasema mtu amekamatwa, amehojiwa, ameshinda kituoni, amefanya nini. Labda niseme hiyo ndio kazi ya Uhamiaji waliosomea ni kukuita na kukuhoji na kukuruhusu urudi nyumbani au ulale ndani, hiyo ndio kazi waliosomea hakuna nyngine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikueleze ukweli hatuna haja ya kukimbia na kuficha haya. Niliwahi kupigwa ile fomu ya kujaza ya uhamiaji, sasa nilipopewa kwanza nikajifikiria nikasema sasa hapa nafanya? Fomu ile kama sio raia wa

Tanzania, niseme, huwezi kujaza ile fomu. Kama sio raia wa Tanzania halali ile fomu *page* ya kwanza tu chali, lazima uombe kwenda kukojoa mara mbili. Sasa ndio maana unaona...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa mzungumzaji anayeongea kama aliweza kujaza ile fomu natamani arudie tena kujaza.

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo taarifa gani? Waheshimiwa nitaomba msipoteze muda wa kiti, endelea Mheshimiwa Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu naomba nisiendelee naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema Idara ya Uhamiaji kazi yake ni kuita mtu, ni Mbunge uitwe, ni kiongozi wa dini uitwe, ni Waziri uitwe, wewe ukifika pale chukua fomu yako jaza ukimaliza tawanyika, unahofu nini? Unahofu nini na kulalamika kwamba kwa nini umehojiwa, unahofu nini? Kama una hofu *it means* wewe sio kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Idara ya Uhamiaji, kwanza hii bajeti ni ndogo, ndio maana nasema nakusudia kushika shilingi, waongezewe pesa ili wakamate wengi, wahoji wengi. Maana kuna *intervention* ya watu wanaingilia kwenye hii mikondo na kutafuta kutengeneza umamluki na uharamia wa kutafuta hawa watu waendelee kupoteza laini, wanasema watu wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawa Mbunge pale Dosidosi, Kiteto pale mpakani na Kongwa, nimefika pale Wahabeshi wamepita pale, mmoja kat iao akawa

amezidiwa, ameumwa wherever kwenye gari, gari limeharibikia upande wa pili wakaisogeza, mtu wamemwacha porini amekufa na gari iko *sealed*. Leo unauliza watu wanakufa, wanaokufa ndio hao wanaotoka nje, sio Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katikati, hapa Kiteto, Kongwa hii hapa, *semitrailer* imepaki pembeni, watu wameshushwa, ni Wahabeshi wamejaa gari zima wengine wame-*faint*, wengine wamekufa, hao hao ndio wanaokufa ambao sasa sisi hatuwezi, nchi au Uhamiaji au Polisi haiwezi kulaumiwa kwamba watu wanakufa, wanaokufa ni watu wa nje ambao still *Tanzanian*...

## KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni Mbunge anapozungumza...

**MWENYEKITI:** Kanuni ipi?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 64 anapaswa kuthibitisha, naomba nimalize. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anazungumza sasa hivi atuthibitishie kuwa watu wote waliookotwa *Coco Beach* na kwenye *beach* nyingine zozote ni Wahabeshi au ni wahamiaji. Atuthibitishie kwa sababu sisi tunavyofahamu hakuna uchunguzi wowote uliofanywa na Jeshi la Polisi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kwanza umetumia kanuni ambayo sio inayotakiwa na kama kanuni ya kusema uwongo, wewe uliyesimama ndiye unayetakiwa umthibitishie yule. Kaa chini Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Papian endelea.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kuzungumzia na huyo aliyenipa taarifa, hao wote

wanaokufa mimi nilitarajia yeye atusaidie, aende aiambie polisi kwamba jamani kuna mtu amekufa hapa, ni Mtanzania, jamani fatilieni hili, kwa vyovyyote vile atakuwa anawajua, huyu aisaidie polisi. Nataka kuishauri idara yetu hii iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kushauri hawa watu wa NIDA wa vitambulisho. Kwenye hii mikoa ya mipakani watu wanazungumza lugha moja wanazungumza wanaelewana huku na huku, niombe kwamba... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na dunia kwa kutujalia uhai mpaka leo tumeweza kuwa humu ndani ya Bunge tunachangia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia napenda kuwaambia Watanzania wote kwamba tulinde amani tuliyonayo na tulinde kwa bidii kwa sababu amani ikipotea haina cha Mkristu, Mpagani, Muislam wala mtu wa aina yoyote, wote tutazama kwenye hiyo bahari. Amani ikipotea ina maana Watanzania wote tutazama kwenye hiyo bahari. Naomba Watanzania wasisikilize maneno, waendelee kuilinda amani tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuchangia mjadala ulio mbele yetu. Napenda kumpongeza kwanza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya. Napenda vile vile kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa nafasi zao tofauti na Wizara zao tofauti kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu na Naibu wake Mheshimiwa Masauni kwa kazi nzuri wanayoifanya. Napenda pia kupongeza Jeshi la Polisi kwa kulinda raia na mali zao au zetu kwa ujumla. Napenda vile vile kulipongeza Jeshi la Magereza kwa kuwalea wafungwa Magerezani na kuwafundisha tabia njema wanapotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Idara ya Uhamiaji kwa kulinda mipaka yetu ya Tanzania na kulinda wahamiaji wanaoingia ndani ya nchi yetu. Pia napenda kupongeza Jeshi la Zimamoto kwa kusaidia maafa ya moto yanapotokea nchini mwetu Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye kuchambua hoja moja moja za Idara hii. Nianze na Idara ya Uhamiaji. Naomba Idara ya Uhamiaji ifanye kazi kwa weledi. Ihakikishe nchi yetu ya Tanzania haiingiliwi na wahamiaji haramu, iwadhibiti wahamiaji haramu wote waaoingia ndani ya nchi hii. Ihakikishe nchi yetu ya Tanzania siyo kisiwa cha kupokea maharamia na Alkaida wanaotoka nchi nytingine. Ihakikishe nchi yetu ya Tanzania siyo kisiwa cha kupokea dawa za kulevya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Idara ya Uhamiaji wafanye kazi kwa weledi kwa kuangalia mipaka yote na nawaomba wasifanye kazi kwa *computer*, waende *field*. Wasifanye kazi kwa kuingia ofisini na kucheki *computer* unaona kwamba kuna usalama. Waende *field* wakakague mipaka yetu. Wachukue ramani ya Tanzania na waangalie mipaka ya Tanzania yote imekaaje? Waitembelee kwa kuionna *visible* siyo kwa kukaa kuiangalia kwenye *computer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mkurugenzi wa Uhamiaji kwa sababu ni mama tumeona mabadiliko anayoyafanya, atendee haki kiti chake; atembelee mipaka ya nchi yake ya Tanzania aijue, asifanye kazi kwa *computer* pamoja na timu yake yote ili nchi yetu iweze kuendelea kuwa na amani hii

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, haiingii akilini; juzi juzi hapa kuna wananchi walishikwa pale Dar es Salaam wako kwenye nyumba, ina maana hawa *Immigration* na Polisi kulikuwa na uzembe fulani ndijo maana hawa watu waliweza kupenyeza mpaka kuwa kwenye nyumba ya mtu, walishikwa wakiwa wanagombania chakula, ndijo maana wakafahamika kwamba wako pale, ina maana hapa Jeshi la Polisi na Uhamiaji halikufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, haiingii akilini kuona wahamiaji haramu wanashikwa Dar es Salaam. Wamepitaje Tanga, wamepitaje Moshi mpaka wanakwenda kufika Dar es Salaam? Naomba warekebishe hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie suala la Polisi. Polisi wanafanya kazi yao vizuri, lakini naomba wajirekebishe wawe rafiki na raia. Naomba nichangie hasa upande wa *traffic*. *Traffic* wamekuwa wakiwa-harass sana hawa vijana wa bodaboda kiasi kwamba wanawakimbia mpaka wanaenda sehemu nyingine na kuweza kusababisha ajali. Vijana wale wanatafuta maisha, kwa hiyo, wanahitaji tu kupewa semina ili waweze kufanya kazi zao vizuri za bodaboda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kuhusu *traffic*, unaposhika gari njiani, mimi mwenyewe nimewahi kukamatwa, tumelipa *fine* ya Sh.30,000/= lakini hatukupewa *receipt*, tumepewa *notification*. Sasa tunajuaje hiyo hela kama imefika Wizara ya Mambo ya Ndani? Naomba Mheshimiwa Mwigulu wale *traffic* amba wanakamata magari njiani, wapewe mashine wanapokamata magari watoe *receipt*. Wasitoe ile karatasi ya *notification*. *Notification* siyo *receipt*. Unapodai *receipt* wanakwambia kwamba *receipts* utaipata mbele ya safari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikamatwa hapa kutoka Chemba tukaambiwa tutakuta *receipt* Chemba, tumefika pale Chemba wala gari la Polisi lilikuwa halipo. Kama vitendea kazi hamna, naomba Mheshimiwa Mwigulu hawa *traffic* wasikamate magari.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Tauhida hayupo; Mheshimiwa Dkt. Kafumu hayupo; Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza nianze kuipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Jeshi la Polisi; *IGPSirro* pamoja na Makamishna na Makamanda wote katika ncni yetu. Tuko katika kipindi ambacho tunaona kabisa kwamba kuna *transformation* kubwa imefanyika. Matukio mengi tuliyozoea kuyaona hata katika ajali, lakini pia uhalifu kwa maana ya wizi katika mabenki, lakini pia ujambazi wa kutumia silaha, kwa kweli yamepungua kwa kiasi kikubwa sana. Sasa hatuwezi tukabeza hizi jitihada pamoja na kwamba changamoto zipo na sitarajii sisi kama viongozi tuamini kwamba changamoto zitakwisha kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawapongeza na tunawaomba waongeze weledi katika kushughulikia matatizo mbalimbali hasa kwa maana ya kwamba sasa hivi kutokana na ukuaji wa teknolojia, uhalifu nao unakua. Tukisema tunajiunga katika kanda na uhalifu na wenyeve pia wanajiunga, wana kanda zao; tukisema tuko katika *block* fulani na wenyeve pia uhalifu unazidi kuongezeka. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tunakuwa na jeshi lenye weledi na kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kushauri kwa sababu ndiyo kazi yetu ya msingi kama Wabunge,

kushauri na kuisimamia Serikali. Katika eneo la ushauri nianze na Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto bado liko karne nyuma zaidi ya karne tuliyokuanayo. Bado vifaa wanavyotumia kuzima moto haviendani na teknolojia ilivyokua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona sasa hivi tunayo majengo marefu sana hasa katika Majiji Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha ambako kuna majengo marefu, lakini utashangaa bado Zimamoto wana magari ambayo hayawezi kuzima moto hata ambao uko ghorofa ya pili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwamba kikosi hiki cha Zimamoto kiboreshw, kiwe na vifaa vyatikisa ambavyo vinaendana na wakati tulionao. Pia, katika Jiji kama la Dar es Salaam ambalo linazidi kupanuka, hatutarajii kuwaona Zimamoto bado wakiwa pale pale walipokuwa tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatarajia kuwaona Zimamoto wakiwa na vituo labda maeneo kama Mbezi, Mbegala, Kigamboni, Bunju na maeneo mbalimbali ambayo hata ikihitajika huduma ile gari linafika kwa wakati. Sasa hivi bado wako maeneo yale ya kule Mjini llala ambapo hata akiitwa kuzima moto Mbegala, anatumia hata saa mbili kufika huko na hiyo tija haiwezi ikaonekana. Kwa hiyo, suala la msingi kwanza tuboreshe hii huduma kwa maana ya kuwapa vifaa vinavyoendana na wakati, lakini pia wajaribu ku-decentralize hii huduma kuelekea huko ambako makazi ya watu yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la *breakdown*. Unapopata ajali katika Jiji la Dar es Salaam wanatumia *breakdown*, hizi *Land Roverza* zamani. Zile *Land Rover* sidhani kwamba hata zinalipa kodi kwa maana ile ni biashara, lakini sidhani kama wako katika mfumo rasmi kwamba wanalipa hata mapato ya Serikali. Kwa sababu umbali ambao hauzidi kilometra moja wanachukua

Sh.80,000/= kuvuta gari ambalo limeharibika ama lime-park eneo ambalo haistahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwaso wangu hapa ni kwamba je, kwa vijana hawa tuliokuwa nao kama Mawaziri, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa *Engineer Masauni*, bado Taifa hili tuna haja ya kuwa na *breakdown* aina ya *Land Rover* zile kweli? Yaani *Land Roverile* ikaanze kuvuta *BMW* ya shilingi milioni 200 inavutwa na gari ambalo thamani yake haifiki hata milioni 12?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa kuna tatizo. Lazima tuje na ubunifu kwa sababu hii wanaifanya kama biashara. Basi tujaribu kuitangaza hii biashara watu wenye uwezo watuletee *breakdown* za kisasa ambazo unapakia gari juu ya gari. Hili tuliangalie kwa makini sana. *Breakdown* hizi, zenyewe zinaharibu hayo magari wakati wa kuyapakia au wakati wa kuyavuta. Wanatumia minyororo ambayo ni teknolojia ya zamani sana kiasi kwamba utakapoona lile gari linavyovutwa, japokuwa wewe ni binadamu, lakini unaumia kwamba hapa kitu kinachofanyika siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na eneo hilo waliangalie, wao ni vijana lazima walete ubunifu kwenye hii Wizara. Tumeona Mheshimiwa Augustine Mrema aliyahi kukaa kwenye Wizara hii na akatengeneza jina, nao tunatarajia wafanye vitu ambavyo vinaonekana ili viweze kuwatangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie suala la Gereza la Kilimo, Mnaro. Nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri mara kadhaa kwamba Gereza hili ni miongoni mwa Magereza machache ya kilimo katika nchi hii na kule kuna *scheme* za umwagiliaji, lakini Gereza hili ni chakavu kwa sababu ni la siku nyingi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza nadhani mwaka 1973 ndiyo Gereza hili limejengwa. Kwa hiyo, wanahitaji kuboresha miundombinu ya Gereza. Pia, nimewahi kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba

ikama ya wafungwa pale ni ndogo. Hili ni Gereza la Kilimo, tunahitaji tuone wanalima. Tunahitaji tuone wanazalisha; ni kilimo na ufugaji unaendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza lina uwezo wa kuchukua wafungwa mpaka 100, lakini walioko pale ni wafungwa 38. Siku moja Mheshimiwa Matiko hapa alisema kuna msongamano Gereza la Tarime, Rorya, nikamwambia sasa si awahamishie kule watusaidie kwenye shughuli za kilimo Lushoto? Hii iwe tu wazi kwamba kwa nini wafungwa ni wachache, ni kwa sababu watu wa Lushoto sio watu wa matukio. Kwa hiyo, ndiyo maana kule Magerezani huwezi hata kuwakuta Wasambaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Kituo cha Polisi cha Mlalo. Kuna wakati kulitokea suala hili la ugaidi katika maeneo ya Mapango ya Amboni na wale watu walifika katika Milima ya Usambara. Kituo cha Polisi Mlalo kilikuwa hakijajenga amari, kwa hiyo, hatukuwa na sehemu ya kuhifadhia silaha. Sasa tumeshajenga tunaomba kikaguliwe...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje, dakika tano.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii. Kwanza niwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP*, Kamishna *General* wa Magereza, Kiongozi wa Zimamoto, Kiongozi wa Uhamiaji kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Askari wote, wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiona mtu anapambana na Polisi, nashangaa kabisa. Hawa ndio wanaotulinda. Hata

hana Bungeni, saa 24 wanalinda hawa vijana. Nchi yetu hii unatembea saa 24 hata saa 8.00 usiku, usalama upo tu kwa sababu ya hawa Askari. Naomba waongezewe posho zao na wajengewe makazi bora. Sasa hivi makazi wanayokaa kwa kweli yanatisha. Hawa ni binadamu, lazima tuwaheshimu tuwajengee makazi bora kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Wilaya ya Mpwapwa ina Kata 33, lakini Vituo vya Polisi viko viwili tu pamoja na Makao Makuu ya Polisi Mpwapwa, cha tatu; Kibakwe pamoja na Kipogoro. Kile Kituo cha Kibakwe hawana usafiri. Waliwahi kupewa pikipiki na ile pikipiki imeharibika. Kwa hiyo, naomba *IGPtusaidie* gari; eneo lile ni kubwa sana, pamoja na Kituo cha Polisi Kipogoro. Wanashughulikia maeneo yote ya Mtera kuhusiana na uvuvi haramu, kwa hiyo, naomba wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mpwapwa Mjini ndio Makao Makuu ya Polisi Wilaya. Kituo kile kina zaidi ya miaka 30 hakijafanyiwa ukarabati, paa linavuja. Naomba *IGP* akitoka hapa atembelee Kituo cha Polisi Mpwapwa. Zile nyumba wanazoishi Askari kwa kweli hazifai, wanaishi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango wa kujenga nyumba 400 kila mkoa, naomba Wilaya ya Mpwapwa isisahaulike. Tuwajengee Polisi nyumba nzuri hasa hapa Mkoa wa Dodoma. *RPC* anafanya kazi nzuri, mkoa wake una amani kabisa na utulivu, sisi Wabunge tupo hapa, hatujawahi kutoa malalamiko yoyote kwa *RPC*, lakini tunaishi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri Askari wote, *IGP* na vyombo vyote vilivyo chini ya Jeshi la Polisi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majina ya wachangiaji ya mchana yamekwisha. Saa 11.00 tutaanza na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Naibu Waziri Kakunda, Mheshimiwa

Waziri Profesa Kabudi, Mheshimiwa Waziri Jenista, Mheshimiwa Naibu Waziri Masauni na mtoa hoja Mheshimiwa Mwigulu.

Waheshimiwa Wabunge, nataka nitoe angalizo au taarifa kwenu. Waheshimiwa Wabunge mnaposoma Katiba ndani ya Bunge, muisome vipengele vyote. Msisome tu.

Sasa Mheshimiwa Zitto alisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 15, kila mtu ana haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

*"Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa uhuru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeoyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo (islipokuwa, hapa hamsomi) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria. (Makofi)*

Subiri. Ibara ya 16, Mheshimiwa Zitto tulia. "Kila mtu anastahili kuhestimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake. Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa ibara hii, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria."

Hivi, hamsomi. Toka dunia ianze enzi ya *Roman Empire, Vikings* kulikuwa na utaratibu wa sheria. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza. Tulitaja majina ya Waheshimiwa wawili. Tunaanza na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Kabla ya yote, nataka nimpongeze Mwenyekiti wetu na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na viongozi wa CHADEMA ambao kwa sasa wako katika kadhia ya kuripoti Polisi kila Ijumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie suala la Zimamoto. Zimamoto mwaka 2016/2017, Bunge lilitenga pesa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua magari mawili ya Zimamoto, lakini pesa hizo hazikuweza kutoka sawasawa na Bunge liliivyopitisha. *Tender Board* ilikaa wakazungumza na Wizara ya Fedha pesa ziweze kutoka, zilitoka shilingi milioni 117 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia viwanda, viwanda na moto ni vitu vinaenda pamoja. Kama hutaweza kutenga pesa kwa ajili ya magari ya Zimamoto unakuwa hujafanya sawasawa katika utekelezaji wa kuleta maendeleo. Mwaka 2017/2018 Serikali lilitenga shilingi bilioni 3.5, haikutoka hata senti tano kwa ajili ya watu wa Zimamoto. Jeshi hili ninavyoliona ni kama Jeshi ambalo limesahaulika sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu kabisa kwamba Jeshi hili hata ukiangalia mavazi yao, ni chakavu kuliko majeshi mengine. Sasa sijajua tunawaweka katika ma-grade kwa sababu gani? Kwa hiyo, naomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kujibu hoja, tunataka kujua hizi pesa tunazopitisha kama Bunge, halafu hazitumiki na wala hazitoki, Wizara ya Fedha haitoi pesa. Kama Bunge limepitisha, kwa nini Wizara haitoi? Namwomba Mheshimiwa Waziri aje atoe majibu anapokuja kuhitimisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia jengo la Mchicha. Unajua Zimamoto mpaka sasa hivi wanapanga na kuna jengo tayari Serikali imeshaweka pesa pale, jengo halijakwisha, limechakaa na safari hii hakuna hata senti tano iliyotengwa kwa ajili ya jengo lile. Sijajua tunawaza nini na

tunafikiria nini kwa ile pesa tulioizamisha pale Mchicha, mpaka leo hiyo pesa hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi kuna wakati niliwahi kuongea na *IGP* nikamwambia kwamba Jeshi linafanya kwa *professionalism*. Unapokuwa na jeshi lazima na intelijensia inafanya kazi yake kwa makini kwa kufuata weledi wa kile walichosomea. Leo hii Jeshi la Polisi linafanya kazi na mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binti mdogo anaitwa Mange Kimambi anaanzisha maandamano mtandaoni, leo wanalitoa Jeshi sehemu za siri kulileta barabarani. Sidhani kama wako sahihi. Wakitokea Mange Kimambi 10, wanataka kuniambia watashinda wakifanya mazoezi barabarani? Sidhani kama wako sahihi. Mheshimiwa *IGP*, naifikiri inabidi kujitafakari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri Mwigulu alipokuwa Singida sikumbuki ilikuwa hafla gani, alizungumzia kuhusu waandamanaji na akasema waandamanaji watakapoandamana inaweza ikatokea kupigwa risasi. Sasa sijajua kwamba anaota au sijajua kama ye ye ni Mfalme Njozi, sijafahamu. Ninachojua, Polisi kazi yake ni kulinda raia. Maandamano mimi naona wanazungumzia kama ni dhambi au kitu kibaya. Jeshi la Polisi kazi yake kufanya intelijensia. Elimu waliyosomea ipo kwa ajili ya kuzuia mabaya, wala haipo kwa ajili ya kutetea kwa kutumia vitu vya kufikirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa Waziri, Mheshimiwa Mwigulu, ye ye ni kiongozi wa wote. Hisia zake za kichama ajitahidi kuzidhibiti zisiweze kumtoa kwenye reli. Naomba afanye kwa weledi, ataacha alama katika jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapolalamika, Polisi wanaposema wamefanya utafiti na kugundua kuwa kutatokea hali mbaya, sijaelewa huwa inaangalia upande mmoja, au ni pande zote. Kiongozi wa Chama cha Upinzani,

kiongozi wa Jimbo kwa maana ya Mbunge, anaandika barua ya kufanya Mkutano ambao huo wameuruhusu, lakini Polisi inatoa majibu ndani ya masaa mawili kabla ya Mkutano kusema kwamba tumegundua amani haitakuwapo. Kwa kweli nashindwa kuelewa. Mikutano hii akifanya Polepole intelijensia haioni ubaya, lakini akifanya mtu wa CHADEMA Mheshimiwa Heche, intelijensia inaona ubaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, nataka kuwaambia, siku zote ubaya wa kidogo kidogo huwa unajenga chuki ndani ya watu. Mheshimiwa Bwege mchana wa leo amezungumza na mkamshutumu kwamba anaongea kwa hisia, lakini kumbukeni mabaya huwa hayatokei isipokuwa yamefanywa kidogo kidogo mwisho wa siku yakawa makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ni la wote na wala siyo *favourites* kuwepo hapa. Ni haki yetu na wajibu wetu na kwa sababu walikubali vyama vingi, wakubali kumeza vidonge vyama vingi. Polisi watuachie CCM tukae nayo pembeni sisi wenyewe tufanye nao siasa, wao wakae pembeni. Kwetu sisi CCM ni wepesi kama karatasi wakikaa pembeni; lakini wakitulazimisha na sisi ni binadamu, tutatafuta njia mbadala ili kuhakikisha tunafikia wapi tufike kwenye malengo tunayoyataka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Uhamiaji, dada yangu kiongozi wa Uhamiaji anafanya kazi vizuri, lakini bado kuna maeneo madogo madogo hasa kwenye biashara ya kujenga nyumba za Uhamiaji, asimamie vizuri pesa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Jeshi la Magereza, wako vizuri, wanafanya vizuri. Tatizo lao Magereza pia ni kama la Zimamoto kutokua na vifaa vya kutosha ikiwemo nyumba za kuishi, lakini *uniform* ni kilio kikubwa sana kwa wafanyakazi hao. Magari kwa Magereza ni shida. Ukienda mikoani, wanahitaji kupeleka wafungwa kwenye

kesi, hawana magari. Sasa sijajua tunategemea nini? Kesi zitaendaje? Watafanyaje kama hatutaliwezesha jeshi hili kufanya kazi zao? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba uhalifu umeongezeka kama wanavyosema, lakini Magereza mengi yana vyumba vidogo. Magereza mengi hayana vyumba vya mahabusu vya wanawake. Wanawake kwa mfano ukienda Gereza la Kyela, hakuna sehemu ya kuweka wanawake, wanaenda kulala Tukuyu. Ni mwendo mrefu sana na wakati huo huo hawana gari la kuchukua hao watuhumiwa na kuweza kuwapeleka Tukuyu na Kyela. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja atuambie amejipanga vipi kuondoa changamoto hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nafikiria sisi kama Bunge hatujajipanga sawasawa kuisimamia Serikali. Ni mara nyingi tumepitisha bajeti lakini bajeti hizi hazitoki. Bajeti hizi, pesa hazitoki, ni hadithi. Watu wetu wanakuja hapa Dodoma, tunakaa nao, tunawasililiza kwenye Kamati, tunakubaliana. Ikifika kwenye utekelezaji, hiyo imekuwa ni shida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu linapopitisha bajeti, tunataka tukija kwenye mwaka mwingine wa fedha hizo pesa zifanye kazi na ziwasaidie watu wetu kufanya kazi zao na waweze kufanikiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono Kambi Rasmi ya Upinzani, najua hatujaleta maoni yetu, lakini bado tunaamini kwamba maoni yetu yangali yanaishi hata yale ya mwaka 2017 yanaweza kuendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru. Ahsanteni. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini nianze kabisa kwa kuwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara hii, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na kaka yangu Yussuf Masauni kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuhakikisha nchi yetu bado ipo na ulinzi na usalama na amani ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Kamanda Sirro, Kamanda wangu wa Mkoa wa Kanda ya Dar es Salaam, Mambo Sasa na Kamanda wangu wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamanda Jumanne. Kwa sisi ambao tumetoka kwenye hekaheka za chaguzi muda siyo mrefu tunajua umuhimu na thamani ya kazi za Watendaji wetu wa Ulinzi na Usalama. Kwa kweli nawapeni pongezi nydingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwa mkweli. Nimefurahishwa sana na nimejifunza kitu kikubwa sana kutoka kwa kiongozi wangu, Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa alipokuwa anaongea mbele ya Mheshimiwa Rais. Kwa kweli nimejifunza kwamba sisi kama Wabunge, kama Wanasiasa pamoja na hitilafu zetu za Vyama, pamoja na tofauti zetu bado tunahitaji kuheshimiana. Nam-*promise* kwamba kwa kuwa amemheshimu kiongozi wetu wa nchi, amemheshimu ni kiongozi wangu wa Chama nami nam-*promise* nitamheshimu kiongozi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mchango wangu katika Jeshi la Polisi. Pamoja na kazi nzuri wanayotufanyia Polisi wetu, bado wana changamoto nydingi. Kwetu pale Dar es Salaam bado tuna changamoto ya vituo chakavu vya ofisi za vituo vidogo vya Polisi, tuna changamoto ya samani za Watendaji wetu wa Polisi na changamoto ya usafiri. Polisi pamoja na Magereza wote wana changamoto ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie wenzangu, bajeti hii sitegemei upande ule kule kwamba wataikataa kwa sababu itaenda kutatua matatizo ya kuongeza magari. Tuliona lilitokea tatizo hapa, kiongozi wetu na wale baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu watuhumiwa walicheleweshwa kwenda Mahakamani wakakosa dhamana ikabidi walale ndani kwa sababu ya kukosa magari na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna nzuri ya kuondoa tatizo lile ni kuitisha hii bajeti ikawa ni bajeti ambayo inaenda kufanya kazi badala ya kwenda kwenye Balozi za watu wengine na kuomba labda watusaidie, kwa sababu hapa ndiyo mahali pake. Nategemea kwamba bajeti yetu itapita bila shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wetu walikuwa wanapata *ration* na wanaendelea kupata lakini wanapata mwisho mwezi na majeshi yetu mengine haya. Ni vizuri kwa sisi ambaao tunafanya nao kazi, tunazungumza nao, wanaomba sana hii *ration* itolewe kati ya mwezi na isiwe mwisho wa mwezi, kwa sababu ikitolewa katikati ya mwezi ina manufaa makubwa sana kwao. Kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu alichukue hili kwamba ni hitaji la vijana wetu wa ulinzi na usalama, wanaomba *ration* zao zipatikane katikati ya mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge, vijana wangu wa Dar es Salaam pale wengi wanaendesha bodaboda. Hivi sasa imekuwa bodaboda na Jeshi letu la Polisi wanawindana kama chui na paka. Namwomba kiongozi wetu wa Jeshi la Polisi badala ya kuwatazama vijana wale kama maadui na badala ya kuwawinda kama chui anavyowinda mnyama, wawafundishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua vijana damu inachemka kuna makosa mengi wanakosea, wakati mwingine wanashindwa kufuata sheria, kuvaan kofia ngumu, kuendesha wakiwa na ndala, natambua na hata mimi mwenyewe najitahidi sana kuwaelimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Jeshi la Polisi lichukue hili kama ni *task* maalum, kwa sababu wale vijana ni wetu, wamejajiri, wanatoa service na wanahudumia watu wetu. Huu upungufu wao basi, Jeshi la Polisi kama walivyoanza kufanya kuandaa baadhi ya semina mbalimbali, kuanza kuwaelimisha kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani; pili, kuwafundisha maadili ya usafirishaji; na tatu, kuwaeleza kwamba watakapofanya kinyume na utaratibu, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ili vijana wale wapate kujifunza. Naamini wakijifunza wanaweza kukafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami natambua kwamba Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa sana katika *operation mbalimbali*. Nakumbuka kuna kipindi *Panya Road* walisumbua pale siku moja tu mji mzima uliharibikiwa. Hata wale ambao wanatazama hii dhana ya ulinzi na usalama na kutazama Polisi kama ni watu ambao hawana faida sana, nawashangaa kwa kweli. Nawashangaa kwa sababu naamini Polisi kama wangepata kupumzika siku moja tu na wahalifu wangejua siku hiyo moja wanayopumzika Polisi, nafikiri tungejua thamani ya Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tulipokuwa kwenye kampeni, wakati tunamaliza pale Polisi walitusaidia sana. Wakati mwingine wakijua kwamba chama fulani wanapita njia fulani wanakuja kutuzuia sisi wengine tusingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana siku liliptokea tukio lilitokea laiti sisi vyama tungekutana pale, kwa kweli lingetokea jambo moja kubwa sana. Nafikiri tusingesema tunayosema sasa. Kwa juhudhi zao Jeshi letu la Polisi wamefanya kazi kubwa, nami nasema waendelee kufanya kazi kubwa. Huu upungufu unaotokea, siupuuzi na wao wasiupuuze, wautazame kwa jicho kubwa, waondoe upungufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wajumbe wenzangu wengine wamesema kwamba watu waliokufa wakaokotwa *beach* wamefika 1,000 na wengine wanaamini wale walikufa

Tanzania, wengine tunaamini sio Watanzania kwa sababu mahali wanapokufa watu 1,000 Tanzania hii wenyе ndugu zao wangeonekana. Haiwezekani leo tunazungumzia mfano suala la Benny Saanane, tunazungumzia mfano suala yule mwandishi aliyepotea, halafu tukaacha kuzungumzia watu 1,000 waliopotea, kwa kweli haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonekana, tukubaliane na kama tulivyopewa taarifa, hawa ni watu wahamiaji haramu wanaotupana, watu wanasafirishwa kwenye malori, wakishakufa wanatafuta mahali pa kuwa-dump. Haiwezekani kwamba wale wawe Watanzania halafu ndugu na jamaa wasionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo kwa kweli siyo sahihi. Tusije tukalipaka tope Jeshi letu kwa ajili tu ya kutaka kutia uzito wa jambo. Kimsingi tuzungumzie hoja iliyopo, kuna watu wamepotea na watu wakipotea Polisi wanashirikiana nasi kutafuta, haina maana kila aliyepotea kafichwa na Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hapa limesemwa, jambo kubwa sana. Siku za nyuma kuna wachangiaji wameshawahi kuchangia suala la... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Huyu alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

### **MICHANGO WA MAANDISHI**

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ukiukwaji wa haki za raia wa Mkoa wa Kigoma

na kusumbuliwa kuwa siyo raia wa Tanzania. Kakonko kila basi linasimamishwa na kukaguliwa na Maafisa wa Uhamiaji. Abiria wanavuliwa nguo za juu, yaani *t-shirt* au blauzi ili kuona chanjo iko mkono gani kulia au kushoto? Huu ni udhalilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachukua rushwa kwa kila raia atakayekosa kitambulisho na kushushwa kwenye gari la abiria. Wamekamatwa wanaodhaniwa kuwa raia na kufungwa kwenye *container, barrier* ya Kihomoka Kakonko. Huu ni udhalilishaji wa hali ya juu. Je kufunga binadamu kwenye *container* ni halali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Mtende iliishia kumaliza maji Kambini (*underground water*) kisha wakaja kuomba wachimbe visima vitano kwenye Vijiji vya Kasanda, Kazilamihunda, Kewe, Juhudi na Nkuba. *TCRS* waliomba kuchimba visima, hivyo waliweka mkataba kuwa wakipata maji lazima wapate *host community* kwanza (vijiji vitano) kabla hayajapelekwa kambini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maji kupatikana, *TCRS* walidai hawana bajeti ya kupeleka maji kwenye vijiji vitano kinyume na mkataba. Kijiji cha Kasanda walipata maji toka *Water Mission Gate9* na Mkuba *Gate2* tu, maji ambayo hayatoshi kabisa na ni kinyume na mkataba. Wananchi wana hasira, chuki na *TCRS* pamoja na wakimbizi waliochukua maji yao bila wao kupata, jambo ambalo litaleta mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi 92 wanaodai fidia ya mazao mpaka sasa hawajalipwa. Suala hili nillifikisha Wizarani ili liweze kufanyiwa kazi, lakini hadi sasa wananchi hao hawajapata fidia yoyote wakati mazao yao yaliharibiwa. Hili linazidi kuongeza chuki kwa wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu kwenye *barrier* ya Kihomoka Kakonko, hutumiwa na Polisi, Uhamiaji na Maliasili. Matumizi yenye uharibifu ni rushwa kwenye magari ya mizigo, abiria wanaodhaniwa kuwa sio raia, rushwa kwa bodaboda, rushwa kwa wafanyabiashara wanaopita *barrier* hiyo, rushwa

kwa wanaobeba mbao, mkaa na kadhalika na kupiga watu bila sababu. Nashauri *barrierhii* ifungwe, kwani haitendi haki bali kuwafaidisha Polisi na Uhamiaji kwa kujipatia kipato kisicho halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Kakonko na nchini kote wanakamata bodaboda wasio na hatia na kuwaomba rushwa kila wakati na kufanya zoezi hili, ni shamba la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wengi wa Kakonko wanaomba rushwa kwa raia wanaopatikana na tuhuma mbalimbali na hakuna dhamana bila rushwa. Kituo cha Polisi kina kesi za kubambikiza ili mtu atoe rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Polisi wengi kukaa muda mrefu Kakonko (*overstay*).

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuyasema mambo matatu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mchinga, bado kina changamoto nyangi ingawa kimekitajwa katika ukurasa wa kumi wa kitabu cha hotuba. Kituo kile kimejengwa tangu mwaka 2002, lakini hadi leo bado hakijakamilika; Askari wamehamia pale lakini hawana nyumba hata moja ya kuishi. Hivyo wanaishi Lindi Mjini na wanalahizimika kuja asubuhi na jioni kurudi Lindi. Inapofika wakati wa usiku ikitokea dharura ya kuhitajika huduma za Kipolisi wananchi hawawezi kupata huduma hiyo. Naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri itenye fedha za angalau nyumba tatu za kuishi Askari pale Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu Kituo cha Polisi Rutamba. Kituo hiki pia kipo Jimbo la Mchinga. Kituo hiki kinakabiliwa na changamoto kubwa ya makazi ya Askari, hakuna nyumba za makazi ya Polisi, lakini pia jengo lenyewe la kituo limechakaa na halikidhi haja ya kuwa Kituo cha Polisi. Naomba watutengee pesa za kujenga jengo la Kituo cha Polisi Rutamba pamoja na nyumba za Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwamba, magari ya Polisi Lindi (Wilaya) yote yamechakaa, hivyo yanaharibika mara kwa mara. Askari Polisi hamwapi *OC*, hivyo mara kwa mara wamekuwa wakitusumbua sisi Wabunge tuwape fedha za matengenezo ya magari yao pamoja na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuuliza Mheshimiwa Waziri, kwa nini wanawatesa hivi Askari na kulidhalilisha Jeshi wakiacha mafao yao ambayo bado machache? Hata magari yao ya kufanya kazi nayo ni shida pia. Waone aibu, watengeneze magari ya Askari, ya Ofisi ya *OCD* Lindi pamoja na kupewa mafuta yatakayowezesha kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la haki za kiraia na vifo vinavyotokana na ukatili wa Jeshi la Polisi, kuna baadhi ya Polisi wanafanya matukio ya kikatili kwa raia wa nchi hii. Tunasisitiza kuwa Katiba yetu inaruhusu mfumo wa Vyama Vingi vyta Siasa na sheria zetu zinatoa haki na wajibu kwa vyama hivyo katika kuendesha shughuli zao za kisiasa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila raia yupo na haki ya kujumuika na kuijunga na chama chochote. Vilevile kuna baadhi ya Askari wanawapa mateso baadhi ya raia ambao kwa namna moja au nytingine wanahusiana na Vyama vyta Siasa vyta Upinzani, bali ni kukiuka haki ambazo sisi wenyewe tumezikubali kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 Februari, ulifanyika uchaguzi wa marudio katika Majimbo na baadhi ya Kata nchini. Ikumbukwe uchaguzi wowote unatoa wajibu na haki kwa Vyama vyta Siasa vinavyoshiriki uchaguzi. Moja ya haki za vyama na Wagombea wanaoshiriki uchaguzi ni pamoja na haki ya kuwa na Mawakala katika kila Kituo cha Uchaguzi na Wakala wa ziada kwa mujibu wa uchaguzi na sheria. Kauli za Jeshi ni kuwa maandamano ni kosa la jinai na hata

kusema neno "maandamano" kwa sasa inaonekana ni kosa la jinai huku wakijua ni haki ya kikatiba na kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Jeshi la Polisi na Wasaidizi wa Polisi na Kanuni za Kudumu za Polisi. Baadhi ya vituo vingi vya Polisi nchini vimegeuka sehemu ya kutesa raia badala ya lengo la msingi la ulinzi na usalama wa raia wa jeshi hilo. Kwa hali hii wananchi wanakosa imani na Jeshi la Polisi na kuamua kuchukua sheria mikononi mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukiukwaji wa haki za mahabusu katika Vituo vya Polisi, Askari anapomkamata mtuhumiwa, ni vizuri kumjulisha makosa yake. Ni haki ya mtuhumiwa kujulishwa makosa yake ili ajue sababu ya yeye kukamatwa. Kumekuwa na utaratibu ambao umeanza kuzoeleka katika utendaji wa Jeshi la Polisi ambapo watuhumiwa wanakamatwa bila kujulishwa makosa yao, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya sheria. Mawakili au ndugu wanapohoji ni kwa nini watuhumiwa wanashikiliwa bila kuelezwa makosa yao, wanajibiwa kuwa wanasubiri maelekezo kutoka juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko juu ni wapi? Au Jeshi la Polisi limerekebisha sheria bila kuletwa Bungeni kwa kutengeneza mamlaka nyingine ambazo siyo kwa mujibu wa sheria? Ni lazima mtuhumiwa yeoyote yule afikishwe Mahakamani ndani ya saa 24, isipokuwa kwa makosa ambayo adhabu yake ni kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti haya yamekuwa magumu katika Vituo vya Polisi vingi nchini ambapo Jeshi la Polisi limekuwa likiwashikilia watuhumiwa zaidi ya masaa ambayo yanatakiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kawaida kwa wanachama au Viongozi wa Vyama vya Upinzani kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu bila kupelekwa Mahakamani, wanarudia kauli ileile ya tunasubiri maelekezo kutoka juu.

Ukiukwaji huu wa sheria siyo tu kwa wanasiasa wa Vyama Upinzani, hata kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Wapo baadhi ya watu wameshikiliwa kwenye Vituo vya Polisi mbalimbali kwa zaidi ya miezi miwili bila kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhoji kuwa pamoja na ubovu wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ambayo kimsingi inatakiwa kufutwa kabisa (kwani hauridhishi), hakuna kifungu chochote cha sheria ambacho kinawapa Jeshi la Polisi mamlaka ya kuwashikilia watuhumiwa wa makosa hayo ya mtandao kwa muda mrefu bila kuapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Polisi (Jeshi lisiojulikana) watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Kumeibuka vikundi vya watu ambao hufanya matukio ya utekaji, utesaji, kuua na kushambulia watu mbalimbali. Serikali kuititia Vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama imekuwa ikiwaita watu hao kuwa ni watu wasiojulikana. Zipo taarifa kuwa watu hao wasiojulikana wanaovamia wananchi huwaeleza kuwa ni Maofisa wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala la haki ya kupata dhamana kuwa kama ni zawadi ya Polisi. Uharaka wa Jeshi la Polisi kuapeleka Mahakamani watuhumiwa baada ya kupata wito wa Mahakama Kuu ni ishara kuwa hawana sababu wala nia njema ya kuwashikilia watuhumiwa. Huu ni ukiukwaji wa haki wa wazi unaofanywa na Maafisa wa Jeshi la Polisi. Hili limekuwa likijirudia mara kwa mara na kuonekana kama jambo ambalo ni halali mbele yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana ya Jeshi la Polisi siyo zawadi, ni haki ya msingi kabla mtuhumiwa hajahukumiwa na Mahakama. Vilevile ni vizuri Jeshi la Polisi lisikamate watuhumiwa mpaka pale uchunguzi au upeletezi wao utakapokamiliika. Hii ni kwa sababu kumekuwa na

sababu za mara kwa mara zinazotolewa watuhumiwa wengi kuendelea kusota Magerezani kwa sababu za kutokamilika kwa upelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kwa mahabusu na Magereza yetu nchini. Magereza yetu nchini yana msongamano mkubwa wa wafungwa, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndani ya Magereza kuna wafungwa wengi ambao wamefungwa muda mrefu kwa makosa madogo mdogo na hivyo kusababisha msongamano pasipo ulazima wowote. Yapo makosa mengi yanayofanana katika jamii ambayo yanaweza kabisa kurekebishiwa bila watuhumiwa kufikishwa Mahabusu au Magerezani. Vijana wengi ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa, wanaishia Magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iendelee kutekeleza adhabu mbadala kwa wafungwa ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa wafungwa na Mahabusu Magerezani. Pia naomba Serikali isimamie marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya Magereza na katika maeneo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Usalama barabarani wanatakiwa kutoa elimu na kuonesha kuhusu makosa madogo madogo barabarani. Wananchi wengi wanalamika kutozwa pesa za faini ya makosa ambayo hayahitajiki kupigwa faini zaidi ya kupewa elimu ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Askari kupewa idadi ya makosa ambayo wanatakiwa kutoza faini kwa siku. Faini za usalama barabarani zinaweza kuleta chuki katika jamii kwa sababu ya hisia zinazojengeka kwa wamiliki wa magari. Ni vizuri Serikali kuismamia ipasavyo Sheria ya Usalama Barabarani iliyopo na kurekebishiha sheria hiyo ili kudhibiti na kupunguza makosa ya barabarani.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwanza kwa Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayofanya. Pili, nampongeza Waziri Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kazi yake nzuri anayofanya. Pia namshukuru sana kwa kutupatia gari la Kituo cha Polisi Mtowisa, ahsante sana. Hata hivyo, palipo na mazuri hapakosi changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kwela yapo mauaji ya mara kwa mara. Kwa mfano mwezi wa Pili Ndugu Paul Kisiwa, Mwenyekiti wa Kamati wa Chama cha Mapinduzi Kata ya Mtowisa ameuawa kinyama na watu wasiojulikana. Mwezi huu tarehe 2 Mei, 2018 Ndugu Benedict Chapewa, Mtendaji wa Kata ya Mwadui na aliyekuwa Katibu Mwenezi 2010 - 2015 ameuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kukomesha mauaji haya kwa kujenga Vituo vya Polisi kwa na kuvipatia bunduki. Jambo la kushauri ukanda ule wa bonde la Ziwa Rukwa kuwe na Wilaya ya Kipolisi hii ni kutokana na jiografia ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaomba Serikali kusaidia vituo ambavyo vimeanzishwa kujengwa na wananchi. Vituo cha Polisi vya llemba, Milepa na Kipeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri kwa kazi wanazofanya. Wizara hii ina changamoto nyingi sana. Hata hivyo, nawapongeza Majeshi yetu yote ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto. Kufuatia bajeti ya Wizara hii naomba kuwasilisha changamoto za Gereza Kuu la Kitai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni uchakavu wa nyumba za watumishi. Hakuna uhaba wa nyumba za watumishi katika Gereza hilo, isipokuwa eneo la Gereza hilo

lina tatizo la mchwa. Nyumba nyingi mapaa yake yameliwa na mchwa, hivyo zinavuja na hivyo zinaweza kuanguka wakati wowote na kuhatarisha maisha ya watumishi na familia za wanaoishi katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna uchakavu wa jiko pamoja na mesi ya chakula. Paa nalo limeliwa na mchwa, mesi haina sakafu, wafungwa wanapikia nje kwani jiko limevunjika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa mlango wa Gereza; lango kuu la Gereza hilo ni chakavu sana kiasi kwamba inawapa ugumu sana wa ulinzi wa wafungwa. Lango hilo linahitaji ukarabati mkubwa sana. Uchakavu wa uzio (*fence*) iliyopo ni ya miti ambayo siyo imara, hivyo *fence* au uzio huo unahitaji kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu tatizo la maji safi na salama. Gereza lilifanikiwa kuchimba kisima. Kinachohitajika ni jenereta ama umeme juu ili kusukuma maji hayo kwa matumizi ya Gereza hilo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati ili afanye hima kupeleka umeme katika Gereza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upungufu wa sare za Askari na wafungwa. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri alingalie hili, kwani wafungwa wamekosa *uniform* kiasi cha *ku-repair* sare hizo kwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ukosefu wa gari kwa ajili ya kazi za utawala. Gereza hili halina kabisa gari, jambo ambalo linaleta ugumu sana katika kutekeleza majukumu ya kiutawala. Naomba hili lipewe kipaumbele kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba Vituo vyetu vya Polisi vya Mbinga Wilayani; Kituo cha Polisi, Maguu na Kituo cha Litembo, vitengewe fedha kwa ajili ya ukarabati pamoja na kupatiwa vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mambo yafuatayo yazingatiwe hasa katika Mkoa wa Kigoma na Jimbo la Kasulu Mjini.:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umaliziaji wa nyumba za Polisi Kasulu Mjini zipo *Blocks* nne zinazohitajika kukamilishwa ujenzi wake. Nyumba hizi zina uwezo wa kuishi zaidi ya familia 20 za Askari Polisi. Tafadhalii kamilisheni nyumba hizo kwani ni muhimu sana kwa utendaji kazi wa Jeshi la Polisi. Barua ya mchanganuo nimeiwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hatua zaidi tangu mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo umuhimu wa kuongeza idadi ya Askari katika Wilaya ya Kasulu ambayo ni kubwa na ina changamoto nyingi sana, pamoja na kuwa na Kambi kubwa ya Wakimbizi ya Nyarungusa. Wilaya inastahili kupewa kipaumbele cha Askari na vitendea kazi vingine kama magari ya doria na motisha kwa Askari hawa. Wilaya ya Kasulu ni tofauti kabisa na Wilaya nyingine kwa sababu zake za Kijirografia na idadi kubwa ya watu. Kasulu pekee ina idadi ya wakazi zaidi ya 800,000 hadi milioni moja sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ni Mkoa uliopo mpakani na nchi jirani za *DRC*, Burundi na Zambia kwa upande wa Kusini. Watu tumeingiliwa sana tangu miaka ya uhuru 1961, wakati idara ya uhamiaji wanafanya doria zao za kusaka wahamiaji haramu, wakimbizi wa wageni wakazi. Naomba sana yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Idara itumie weledi zaidi kuliko hisia, watu watambuliwe kwa hoja na siyo kwa sura zao au lugha zao za asili;

Idara itumie viongozi wa Serikali waliopo katika maeneo na kamwe Maafisa hawa wasivamie watu barabarani, sokoni na kwenye nyumba za starehe;

Wageni wakazi na wahamiaji haramu wanaweza kufichuliwa na viongozi wa Serikali za Mitaa katika sehemu zao;

Vizuizi barabarani siku za masoko na gilio siku ya minada kamwe zisitumike kunyanyasa raia halali wa Taifa hili kwa sababu tu wanaishi mpakani mwa nchi yetu;

Vitendo vya rushwa, uonevu na unyanyasaji kamwe visipewe nafasi katika misako ya Idara hii ya Uhamiaji;

Makamanda wa Wilaya na Vituo wawasimamie vijana wao kutenda haki na kwa mujibu wa sheria zetu; na

Pia Idara ya Uhamiaji Kasulu wapewe vifaa vya kazi, mfano magari na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza linafanya kazi njema sana katika mazingira magumu. Jeshi hili kule Kasulu wapewe vitendea kazi ikiwemo nyumba za kuishi. Pia Wizara iboreshe makazi ya Askari wa Jeshi hili ili ubora wa Jeshi hili uonekane dhahiri mbele ya Jamii. Jengo la Magereza Wilaya ya Kasulu ni jengo la siku nyingi sana tangu Wakoloni wa Kijerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hili lipo katika Mji wa Kasulu. Nashauri *strongly* Magereza haya yahamishiwe nje ya Mji wa Kasulu. Maeneo yapo mengi; maeneo ya Tarafa ya Makele yanafaa sana kujenga gereza la kisasa. Magereza ya sasa yaliyopo yanaweza kuendelea kutumika kwa ajili ya mahabusu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia changamoto za kiutendaji Polisi - Kaskazini Pembra kuhusu mafuta, vipuri na umeme. Polisi wetu wanapatiwa lita 900 badala ya mahitaji ya lita 3,000. Vilainishi (*lubricants*) na *spare* wanapewa shilingi milioni 1.5 badala ya shilingi milioni 4.5 ya mahitaji. Umeme

wanapatiwa Sh.400,000 kwa mwezi wakati mahitaji ni shilingi milioni 2.4 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Maofisa wa Polisi Wilaya ya Wete linavuja, jengo la utawala la Polisi Kaskazini Pemba ni chakavu, jengo la Askari Polisi - Konde ni chakavu, Bweni la Askari wetu ni bovu, nyumba za Askari *FFU* ni chakavu zinahitaji ukarabati wa miundombinu ya majitaka na makaro na kuezekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Maafisa na Askari kutolipwa mishahara kulingana na vyeo vyao kwa muda mrefu, wastaifu kuchelewa kulipwa mafao yao bila ya sababu ya msingi, kutolipwa posho mbalimbali kama za nyumba, upelelezi, nguo na malipo ya uhamisho huchelewa sana. Vile vile kuna uchache wa Askari ambapo Askari wengi wanahamishwa na kustaafu bila ya kupatiwa mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Ofisi ya Teknohama Mkoa ipatiwe vifaa vya kisasa pamoja na *computer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri asimamie upatikanaji wa stahiki za Idara ya Uhamiaji Makao Makuu kama vile vinywaji.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kulinda amani na usalama. Nashauri pamoja na kazi nzuri inayofanywa, Polisi wasichukue sheria mkononi mwao kama vile anapotokea mhalifu badala ya kumpeleka Mahakamani hupigwa na kufia mikononi mwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo hivi vimeshamiri na pia imetokea kwenye Jimbo langu Kijiji cha Kilambo, Kata ya Kala ambapo mtuhumiwa wa wizi kijana alipigwa na Polisi na akapoteza maisha. Haya yanatokea sehemu mbalimbali nichini na yanalamikiwa sana. Nashauri Polisi wasitumie nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko kuwa watu wanapotea, wanatekwa na wengine hawajapatikana. Vitendo kama hivi siyo utamaduni wa Tanzania. Tanzania irejeshe taswira nzuri iliyojengeka miaka ya matumizi ya vyombo vyao kutafsiri sheria, yaani Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri ya kuendelea kulinda raia na mali zao ambapo mpaka sasa raia na mali zao wapo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Waziri anipe bati kwa ajili ya kuezeka kwenye vituo vya polisi vilivyojengwa na wananchi vya Tarafa ya Kate, Mji Mdogo wa Kate na Tarafa ya Wampembe, Kata ya Kala na Kijiji cha Mpasa wananchi wasikate tamaa maana wao wameona umuhimu wa kuwa na huduma ya Polisi lakini wameshindwa kuezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Nkasi hawana nyumba za kutosha. Pia Polisi Nkasi hawapati fedha ya mafuta na badala yake wanakuwa wanaomba ombo wakipata dharura. Naomba Polisi Nkasi waongezewe gari ili ipelekwe Wampembe kwani ni mbali na Makao Makuu na ni mpakani.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi Wilaya ya Igunga linafanya kazi nzuri katika kulinda raia, lakini Jeshi hilo lina changamoto nyingi sana zikiwemo ukosefu wa miundombinu kwa ajili ya kutenda kazi zao. Wilaya ya Igunga ina Kata 35, lakini ina vituo saba tu vya Polisi vya Igunga, Nanga, Simbo, Igurubi, Simbo, Sungwizi na Choma. Vituo hivi vyote vinatumia magari mawili tu yaliyopo kituo kikuu cha Wilaya Mjini Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wetu wanafanya katika mazingira magumu sana. Kuna wakati wanalazimika kukodi pikipiki hata baisketi kwenda kukamata wahalifu. Hii ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wanaishi Mtaani na wengine wanaishi kwenye nyumba mbaya sana (*Line*

*Police*). Hii haikubaliki. Naomba sana Serikali ijenge nyumba za Askari wetu kwani wanaishi kwa taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi, Igunga hakina jengo la utawala kwa ajili ya upelelezi. Tumeanza kujenga kwa kuchangishana na sasa tumefikia kupaua. Tunaomba Wizara ituunge mkono kwenye ujenzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Wilaya ya Igunga ni dogo sana. Linahudumia wafungwa zaidi ya 200 badala ya wafungwa 100. Pia kuna Gereza kwa ajili ya akinamama. Kwa hiyo, tunalazimika kupeleka mahabusu na wafungwa Gereza la Nzega. Gereza hilo halina jengo la utawala, pia halina ngome. Ngome yake ni miti, aibu kubwa. Nilishawahidi kumwomba Mheshimiwa Waziri atutembelee mara kadhaa lakini sijafanikiwa. Tafadhali Mheshimiwa Waziri aje Igunga ajionee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Viongozi wa Gereza la Igunga wakashirikiane na viongozi wa Wilaya wakiwemo Wabunge. Tumeanzisha ujenzi wa jengo la utawala ili kuondokana na aibu hii kwa kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo na michango mingine. Tumekamilisha ujenzi wa msingi. Tunaomba Wizara ikamilishe jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Askari Magereza nao hawana nyumba za makazi. Tunaomba wajengewe nyumba kwani wanateseka sana mitaani. Tafadhali tusaidieni Igunga Gereza letu lipo katika hali mbaya.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wanapostaafu hawapatiwi haki zao stahiki kwa wakati. Kwa mfano, waliostaafu mwaka 2017 mwishoni wanatakiwa wahame kwenye nyumba za Polisi kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Jeshi letu la Polisi kuwa chini ya Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya (Kamatitazza Ulinzi na Usalama) linawaweza katika hali ngumu kiutendaji (Rejea Ibara ya 147 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Himo kinafanya kazi kubwa (huduma eneo la mpakani na nchi jirani), hawana vitendea kazi vya kutosha hasa magari; Ofisi ni ndogo na ni chakavu; makazi yao hayatoshelezi na chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, weledi wa Jeshi letu la Polisi uwekwe msisitizo hasa mahusiano na jamii (elimu endelevu)

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwapongeza Watendaji na Viongozi wote wa Wizara hii wakiongozwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na vikosi vyote vilivyoko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijana wetu waendesha bodaboda hasa walioko Mkoa wa Dar es Salaam, kwa asilimia 90 hawana usikivu na utu wa kutosha kwa Jeshi la Polisi, kuititia Idara ya Usalama Barabarani kwa kutozingatia usalama wa raia wakati wawapo barabarani. Vijana wengi wa bodaboda huendesha wakati wakiwa wamekunywa pombe au kuvuta bangi. Hali hiyo husababisha ajali nyingi za bodaboda na hivyo kuua na kujeruhi wananchi wengi wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jeshi la Polisi kuititia Idara ya Usalama barabarani liangalie upya jinsi ya kuzuia ajali zilizokithiri katika Mkoa wa Dar es Salaam zinazofanywa na vijana waendesha bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Makamanda wa Usalama Barabarani katika Mkoa wa Dodoma kutokana na waendesha bodaboda kutii kwa kufuata Sheria za Usalama Barabarani. Vijana wa Dodoma tumewaona wakisimama kwa kuwapisha wananchi kuvuka kwa dakika mbili mpaka tatu. Kwa kitendo hicho sisi tunaotoka Mkoa wa Dar es Salaam imetushangaza kuona vyombo vya moto (pikipiki) kusimama kwa adabu na kuheshimu watu wasipatwe na ajali na kuacha ulemavu na hata vifo kwa raia wetu wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifanye utaratibu wa kuwapatia fedha Idara ya Upelelezi kwa ajili ya mafunzo mbalimbali ikiwemo kuepuka kulaumiwa kwa baadhi ya Maafisa Upelelezi ambao wanachafua Jeshi letu kwa kupokea rushwa kutoka kwa walalamikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya baadhi ya Wapelelezi kutotenda haki kwa walalamikaji wakati wanapokwenda kushtaki katika Vituo ya Polisi. Wapelelezi hao hubadili kibao kwa walalamikaji na kutoa upendeleo kwa watuhumiwa. Hali hiyo inaashiria kuna mkono wa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jeshi litafute jinsi ya kukomesha tabia hiyo kwa baadhi ya Maofisa hao Wapelelezi. Pia Maofisa hao wapatiwe usafiri na fedha za mafuta na makazi bora ili waweze kutimiza wajibu wao wa kazi kwa ufanisi na tija. Kwa kuwapatia nyenzo au vitendea kazi kutaweza kuepusha vishawishi kwa wahalifu/watuhumiwa kwa kuwashawishi Maofisa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kituo cha Polisi Segerea (jirani na Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Segerea) kijengwe au kimaliziwe na kupatiwa samani, gari na Askari wa kutosha ili waweze kuimarisha ulinzi katika eneo hilo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia kuwapongeza wote waliohusika na utekelezaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mwigulu na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Masauni kwa kuliongoza vizuri Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na taasisi zote za Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na watumishi wazalendo wa Wizara, lakini wapo wachache ambao wanaharibu taswira ya Wizara. Viongozi wa juu wa Wizara wapite katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, wasikilizeni kero za wananchi kuhusu utendaji wa baadhi ya Maafisa wa Polisi, Magereza na Uhamiaji ili waweze kuzitafutia ufumbuzi na nydingi zimesemwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja ambalo limenitokea jana shambani kwangu; Askari walivamia wakampiga mke wa mlinzi ambaye ni mjamzito, wakavunja mlango kwa madai kwamba wanakagua mali ya wizi na hawakukuta chochote. Walitaka kuchukua dawa za mazao ambazo bado hatujazilipia na yule mama akawaambia kwamba watafungwa kwani dawa zina deni, ndipo wakaziacha. Kwa bahati nzuri, mume wangu aliweza kwenda kuripoti kwa mkuu wa kazi wa Askari hao, wakaitwa na kuomba radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba sana Mawaziri wetu wakemee mmomonyoko wa maadili unaoendelea mionganini mwa Askari wachache kwani jambo baya husambaa na kusikika kwa haraka kuliko jema liililo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza taarifa za kupungua kwa uhalifu ikiwemo makosa ya usalama barabarani. Naamini chanzo kikuu cha mapato kwa Jeshi la Polisi ni faini na kwa uchache stika. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, lengo la kukusanya shilingi bilioni 73 halikutimia na badala yake zimekusanya shilingi bilioni 43. Sasa kama makosa yamepungua ina maana faini pia zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipate maelezo ya kuridhisha ni kwa nini Wizara kwa mwaka 2018/2019 imeongeza makadirio ya mapato kufikia shilingi bilioni 84? Je, kuna chanzo gani kipyaa cha mapato? Vinginevyo wananchi watalazimishwa kulipa faini isivyo halali. Leo nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa jitihada mbalimbali za kuwezesha Wizara na Taasisi zake zote zinazotekeleza majukumu yake pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ione namna ya kuongeza fedha katika Wizara na Taasisi zake ili majukumu ya kazi zao yatekelezwe kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lipatiwe zana na vitendea kazi vyta kisasa ili Jeshi hili liweze kukabiliana na majanga, maafa na matukio mbalimbali yanayotokea nchini yanayohitaji uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lipatiwe vitendea kazi ili liweze kukabiliana na uhalifu na ulinzi wa nchi, wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba wahamiaji haramu wakikamatwa warudishwe kwao au waachiwe waendelee na safari yao nje ya nchi yetu kuepusha mlundikano wa mahabusu katika Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari ye yeyote ambaye anakiuka maadili ya kazi yake kwa kuchafua Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na kadhalika, wachukuliwe hatua za kinidhamu ili kulinda heshima ya majeshi yetu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawatakia utekelezaji mwema. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mafia kijiografia ni kusini na inahudumiwa na kituo kimoja cha Polisi cha Wilaya. Mapema mwezi wa Nne mwaka huu, gari pekee linalohudumia kituo hicho aina ya *Land Cruiser (Pick Up)* liliipata ajali ya kutumbukia baharini kwenye Bandari ya Kilindoni, Mafia. Kwa kuwa kina cha maji kilikuwa ni kikubwa, gari lile limeharibika sana kiasi cha kutoweza kutengenezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hii, Wilaya ya Mafia haina gari la Polisi; na kutoptana na jiografia yake, hatuwezi hata kuazima gari kutoka Wilaya jirani. Mbaya zaidi, wahalifu wamechukua fursa ya kufanya uhalifu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie gari lingine, kwani hali inazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie Kituo kidogo cha Polisi katika Tarafa ya Kivungwe, Kata ya Kivungwe. Hii inatokana na ukweli kwamba umbali kutoka kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya ni mkubwa, wananchi wanalazimika kusafiri masafa mrefu kufuata huduma hii ya Kipolisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mashehe wa Uamsho linaingia mwaka wa tano sasa bila ya kujulikana hatma yao. Mashehe hawa wamekaa rumande kwa muda mrefu na mmoja wa wake wa Mashehe hao amejiua kutoptana na kushindwa hali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wapiga kura wangu watatu kutoka Wilaya ya Mafia wanashikiliwa rumande mwaka wa pili huu sasa kwa tuhuma za ugaidi. Tunaomba haki itendeke kwa mujibu wa sheria za nchi. Kama hawana hatia, basi waachiwe huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inabeba usalama wa Taifa. Kwa maana hiyo, kama Wizara hii

ikiendelea kufanya vibaya kama ilivyo sasa, usalama wa Taifa utazidi kuwa hatarini. Uizingatia kuwa usalama wa Taifa tunahitaji Serikali iangalie changamoto zifuatazo ili kunusuru Taifa; udhibiti wa uhalifu, mauaji, kubambikiziwa kesi, usalama mipakani, usalama wa wafungwa Magerezani, dawa za kulevyta na matumizi ya nguvu kwa wananchi kupitia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji katika Taifa letu imekuwa ni changamoto kubwa ambayo kimsingi mpaka sasa wananchi wamebaki hawana majibu ya mauaji ambayo yameshatokea, lakini taarifa za matukio haya haya na ripoti inayoeleweka; tukio la Mheshimiwa Tundu Lissu kupigwa risasi mpaka sasa Serikali imeshindwa kutoa majibu ya tukio hili na kuwataja wahuksika hasa wa shambulio hili. Je, ni lini Serikali itatoa taarifa ya jambo hili ili wananchi waondokane na hofu iliyopo kwamba Serikali inaficha wauaji hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu kupotea kwa Ben Saanane, kupotea kwa mwandishi wa habari Azory, maiti zinazookotwa bila taarifa kamili, kubambikiziwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kupitia bajeti atuambie ana mkakati gani wa kuhakikisha Vituo vya Polisi na baadhi ya Polisi wanachukuliwa hatua kwa makosa ya kubambikizia kesi wananchi na wananchi wakitoa taarifa za matukio haya hawapati msaada kutoka Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tanganyika ina malalamiko na kesi nyingi za wananchi kubambikiziwa kesi na badala yake watuhumiwa wanaombwa pesa na Askari ili wamalize kesi hizi. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani hamwon kwamba baadhi ya Polisi wasio waaminifu wanachafua Jeshi la Polisi? Mr. Said Anganisye ana kesi katika Kituo cha Polisi Kata ya Kabungu, Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya bodaboda Mwakagana (Wilaya ya Mpanda) Polisi anashutumiwa

kumpiga bodaboda mpaka kumuua na Polisi anajulikana kwa jina la Deus lakini mpaka sasa tunavyoongea wananchi hawana majibu ya vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya magereza yetu bado yana changamoto kubwa kwa maana ya kukosa vyumba vyakusaidia kutosha pamoja na usafi; vyumba havina hewa na uchakavu wa magodoro yenye magonjwa. Wafungwa hawa pamoja na kwamba wanapewa adhabu, basi zisihusiane na kimazingira bali pia Wizara iangalie haki za binadamu. Kwa kuangalia utesaji na kazi ngumu sana wanazofanya wakiwa Gerezani, badala yake Serikali itumie wafungwa kufanya kazi za kimaendeleo zaidi na siyo mateso wanayopata ambayo hayana tija kwa Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchache wa vitendea kazi na sare za wafungwa ni aibu kwa Serikali kwa kushindwa kuwapa sare wafungwa na kupelekeea Askari Magereza kuwapa nguo zao binafsi kama makoti na nguo za ndani. Mjitätahidi kutatua jambo hili. Ni udhalilishaji kwa wafungwa kukosa hata nguo za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze ulinzi mipakani na mikoa inayopakana na nchi jirani kama Katavi, hali ni mbaya.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama katika nchi yetu ni tete. Watu wengi wamekuwa wakitekwa na kuuawa na hata wengine wanauawa na Polisi kama vile Suguta Chacha, mdogo wake Mbunge mwenzetu, ameuawa na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hali hii inaharibu kabisa hali ya amani na utulivu. Naiomba Serikali mchukue mkakati wa makusudi kuhakikisha mnakomesha hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge, hasa Wabunge wa Upinzani, wamekuwa wakizuiwa kufanya mikutano. Polisi wamekuwa wakiwaandikia barua ya kuwazuia wasifanye mikutano. Hii siyo sahihi kabisa. Huko ni kukiuka Katiba ya nchi yetu. Naiomba Serikali ichukue hatua ya makusudi kuhakikisha inatenda haki kwa watu wetu na hasa kuwaruhusu Waheshimiwa Wabunge wafanye mikutano kama Katiba inavyodai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wa barabarani wanafanya kazi ya *TRA*, wanasumbua sana madereva. Madereva wananyanyasika, kulipa faini kila Kituo cha Polisi, pia kama hawana pesa za rushwa wananyang'anywa kadi za gari na leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwasaidie vijana wetu wanaoendesha bajaji, bodaboda na magari madogo ya mizigo; wanatozwa pesa bila sababu. Naomba Serikali isimamie Polisi wa Usalama Barabarani wasiwapige viboko madereva. Huo kwa kweli ni uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iache kutumia Polisi kwa kuwadhalilisha Wabunge wa Upinzani kwa kuwakamata kamata ovyo, hata kuwapiga makofi, mfano, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanya Jeshi la Polisi, lakini kwa muda mrefu jeshi hilli lina upungufu wa vituo vya Polisi kwenye maeneo yetu pamoja na vitendea kazi. Naomba Serikali itengeta fedha za kutosha kwenye maeneo yetu na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na upungufu wa nyumba za Askari. Kila mmoja wetu anafahamu mazingira wanayoishi Askari hawa. Ni muda muafaka kwa Serikali kuja na mkakati kabambe wa kujenga nyumba za kutosha kwa ajili ya Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka ya hivi karibuni kumeripotiwa mauaji na kupotea kwa raia hapa nchini. Kuna maiti zinaokotwa kwenye fukwe za bahari, watu wanapotea na kutekwa, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa Jeshi la Polisi halijawakamata na kuwapeleka wahuksika wa matukio haya Mahakamani. Ukimya huu unawatia wasiwasi wananchi, maana hawaoni hatua zozote zikichukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne ilihamasisha sana dhana ya Polisi Jamii na ulinzi shirikishi kwa maana kwamba suala la usalama ni suala la kushirikiana kati ya jamii na Jeshi la Polisi. Kwa siku za hivi karibuni, tumeshuhudia dhana hii kuanza kupoteza maana kutokana na matendo yanayofanywa na baadhi ya Askari Polisi yanawakatisha tamaa wananchi. Naomba Wizara iangalie upya mahusiano ya Jeshi la Polisi na wananchi ili kuhakikisha usalama wa raia wetu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 kulikuwa na kampeni kali ya kupambana na dawa za kulevyu ilioyendeshwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Wote tulishuhudia orodha ndefu ya wafanyakiashara na watumiaji wa dawa za kulevyu na wengine kuitwa Polisi kuhojiwa na kupimwa mikopo. Nataka kujua katika ile orodha, ni wangapi wamefikishwa Mahakamani? Utumiaji wa dawa za kulevyu umepungua kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto halina magari na vifaa vyta kutosha kukabiliana na majanga yanayotokea kwenye jamii yetu. Serikali ijitahidi kulipangia fedha za kutosha ili liwe na magari na vifaa vyta kutosha vyta uokozi.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nami kushiriki katika kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri yenye mlengo chanya, hotuba hii inakwenda kutekeleza yale yote yaliyoainishwa

katika llani ya Chama cha Mapinduzi ili kuleta mapinduzi makubwa ya kiutendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua katika kuliboresha Jeshi letu la Polisi ili lifanye kazi zake kwa uwezo wa hali ya juu kwa kuwapatia vifaa vyakisasa vya mawasiliano na vya kiuchunguzi ili liweze kupambana na ujambazi na matukio mengine ya kihalifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napongeza kwa kujenga Kituo cha kisasa cha Mawasiliano (*Call Centre*) Dar es Salaam ili kuwezesha wananchi kutoa taarifa za matukio mbalimbali kwa urahisi. Haya yote ni maboresho ya hali ya juu kwa Jeshi letu la Polisi ili kuliwezesha kufanya kazi zake pasipo shaka yoyote na kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua kuboresha idara nzima ya uhamiaji kwa kuzinduliwa kwa Mradi wa Uhamiaji Mtandaoni (*e-Immigration*), vilevile kwa kuzinduliwa pasi mpya ya kusafiria ya kielektroniki ya Kimataifa ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nzima ya kuzinduliwa kwa pasi hii ni kupunguza vikwazo vya kusafiri mipakani baina ya raia wa nchi wanachama, pia kuimarisha mahusiano na shughuli za kiuchumi baina ya nchi wanachama. Pia naipongeza Serikali kwa kufungua ofisi zaidi za uhamiaji kwenye baadhi ya wilaya lakini naishauri izidi kufungua ofisi zaidi ili kuweza kuwasogezea wananchi huduma karibu na kudhibiti uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwa na changamoto mbalimbali, mfano katika mazoezi muhimu ya kitaifa, kama zoezi la uandikishwaji wa Vitambulisho vya Taifa, Kadi ya Kupigia Kura, kumekuwa na matukio mbalimbali ya baadhi ya wahamiaji wasiokuwa waaminifu kujaribu kujipatia Kadi za Kupigia Kura na Vitambulisho vya Taifa, hali hii inatuonyesha kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatuonesha kwamba usimamizi wa masuala mazima ya uhamiaji bado kuna changamoto kubwa ya kudhibiti wahamiaji haramu na hii ni hatari kubwa kwa mustakabali wa Taifa letu. Kama hali hii ikiendelea basi nchi yetu inaweza siku kutokea tukatawaliwa na kiongozi ambaye si Mtanzania halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kujikita zaidi katika kudhibiti uhamiaji haramu na si kufanya kazi kwa mazoea, operesheni za mara kwa mara ziwe zinafanyika nchi nzima ili kuwabaini wahamiaji haramu. Tunapenda watu watakaoishi nchini kwetu kwa kufuata taratibu, sheria na miongozo na si watu wanaotaka kupita njia za panya na kujipatia uhalali wa kujita Watanzania. Tujifunze kupitia nchi jirani, ama kwa nchi za wenzetu jinsi gani wanavyoweza kudhibiti wahamiaji haramu, Tanzania isiwe shimo la watu kuja na kujiamulia wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza mazuri yote ya kuiboreshaji yanayoendelea kufanya na Serikali yetu lakini sina budi kueleza changamoto zinazolikabili jimbo langu na ningependa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa anipe majibu ya changamoto ninazokwenda kuziainisha. Eneo la Kibaha Vijijini ni kubwa kijigrafia, gari liliopo la polisi ni moja na ni chakavu haliwezi kabisa kufika maeneo yote ya vijijini na ukizingatia eneo ni kubwa na ukizingatia tena Kibaha Vijijini barabara zake ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba katika bajeti hii kupatiwa magari zaidi ya polisi ili yaweze kufanya doria na kuhakikisha hali ya kiusalama inazidi kuimarika. Naiomba Serikali kupitia Wizara inieleze hapa ni lini sasa Wizara itatupatia magari hayo ili jeshi letu liweze kufanya kazi zake bila vikwazo vyovyyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hakuna makazi ya askari na kuwafanya askari wetu kuishi maeneo tofauti tofauti ambayo ni mbali na eneo lao la kazi. Kuna nyumba ya askari iliyojengwa lakini bado haijkwisha na imekwama kwenye hatua za umaliziaji, nyumba hii ikiisha itasaidia sana askari

wetu kuweza kupata makazi bora. Naiomba Serikali kupitia Wizara inieleze ni lini nyumba hii itakamilika na ikizingatiwa imesalia sehemu ya umaliziaji tu. Naiomba Wizara inipe majibu pale Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya uboreshaji wa majeshi yetu lazima tuzingatie na kuyapa kipaumbele pia maeneo yenye changamoto mbalimbali kama maeneo ya vijijini, lazima tuwapatie vitendea kazi vyatya kutosha kama magari, askari wa kutosha na nyumba za kuishi. Maeneo ya vijijini pakikosekana doria za kutosha na askari ni maeneo ambayo wahalifu huweza kujificha kwa urahisi na kupanga mipango hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi naishauri Serikali kuyapa jicho la tatu maeneo hayo ili kuwawezesha askari wetu kufanya kazi kwa urahisi ili kuwawezesha kufika maeneo yote yanayowazunguka. Hata hivyo, napenda kuwapongeza askari wote pamoja na wa jimboni kwangu Kibaha Vijijini kwa kuendelea kufanya kazi ingawa kuna mazingira ambayo si rafiki, hii yote wanaonyesha uzalendo wa hali ya juu katika kulitumikia Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuona mmomonyoko wa kasi wa kimaadili na wa ghafla wa Jeshi la Polisi na kushamiri kwa kasi vitendo vyatya uvunjivu wa haki za binadamu. Polisi waliokuwa kimbilio leo wanakimbiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mwanza mtoto anafariki kisa mama yupo mahabusu na mtoto hawezikupewa matibabu; Ndugu Saguta Heche amekamatwa, amefungwa pingi na anauawa; Polisi na bodaboda kana kwamba hawajui sheria, kama mtu hajataka kutii hiyo Sheria ya Usalama Barabarani si anafikishwa mahakamani; na upelelezi unaogusa Afisa wa Jeshi la Polisi haukamiliki au unachukua muda mrefu, liko wapi faili la Akwilina?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu vyombo vya dola kugeuka wanasiasa, hii inafanyika makusudi kabisa. Tumezoea kuambiwa dola ina mkono mrefu lakini leo ndiyo tumelewa maana halisi ya neno hilo. Dola ina mkono mrefu dhidi ya wenye mtazamo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kuendelea kukamata vijana wadogo wanaoandika tu kwenye mitandao, mbona hawamkamati Musiba? Je, ni kwa kuwa anaongea wanachotaka kukisikia? Mheshimiwa Tundu Lissu kisa kaandika tu meseji kwenye *group* wanamkamata, akina Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mbowe na wengine, ina maana hao Polisi hawajawahi kumsikia Musiba?

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu kwa kazi kubwa ya kutunza amani nchini, Mheshimiwa Waziri hongera sana na ni ukweli usiopingika kwamba, kazi nzuri inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Polisi hasa Dawati la Jinsia kwa kazi nzuri wanayofanya, limekuwa kimbilio la wanyonge na wenye manyanyaso mbalimbali. Dawati hili lilitoa takwimu juu ya ukatili majumbani, wanawake wanaoteswa, wanaopigwa, kubakwa na kuuawa zinatisha lakini takwimu za watoto wanaoteswa, wanaolawitiwa/kubakwa ni kubwa mno. Napenda kujua Wizara ina mpango gani ili kudhibiti ukatili mkubwa wanaofanyiwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku wanakamatwa wahamiaji haramu wanaoingia nchini kinyume na utaratibu. Hawa watu wanaweza kuingia na kuingiza silaha kitu kinachohatarisha usalama wa nchi yetu. Najua mipaka yetu iko *porous*, napenda kujua Jeshi la Polisi/Wizara wana mpango gani wa kudhibiti uingizaji wa silaha kupitia mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu Waziri Mheshimiwa Injinia Masauni kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo matatu. Kwanza ni kuongeza askari Kituo cha Polisi Nanyamba. Kituo cha Polisi Nanyamba kilijengwa miaka mingi kuhudumia wakazi wa Nanyamba kama tarafa. Mwaka 2015 ilianzishwa Halmashauri ya Mji Nanyamba na Jimbo la Nanyamba. Kituo hicho sasa kimechakaa na idadi ya askari ni wachache. Naomba idadi ya askari iongezwe, kituo kipyaa kijengwe na wapewe na usafiri ili waweze kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la watu na uhalifu na wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni ujenzi wa nyumba za askari. Kuna upungufu mkubwa wa nyumba za askari katika Mkoa wa Mtwara na katika Halmashauri ya Mji Nanyamba. Katika Halmashauri ya Mji Nanyamba hakuna nyumba ya askari na kuna kituo cha polisi. Naomba mgao wa nyumba mpya kwa Mkoa wa Mtwara na Jimbo la Nanyamba kwa ajili ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni changamoto za ulinzi na usalama kwa maeneo ya mpakani. Kuna changamoto ya usalama kwa maeneo tunayopakana na nchi jirani ya Msambiji. Naomba askari wa Nanyamba wavezeshwe vitendea kazi ili waweze kufanya *patrol* maeneo ya Kifaya ambako kuna mwingiliano na wenzetu wa Msambiji.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Majukumu ya jeshi hili ni kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya uokoaji pale inapotokea majanga. Jeshi hili umuhimu wake unaonekana zaidi pale panapotokea majanga, hata hivyo umuhimu wake haupewi uzito kutokana na kutopewa fedha za kutosha na vitendea kazi ili waweze kufanikisha majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ihakikishe inalisaidia au inalipatia Jeshi la Zimamoto na Ukoaji fedha za kutosha na vitendea kazi vya kisasa ili utekelezaji wa majukumu uwe na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, vituo vya polisi nchini. Vituo vya polisi nchini vingi vina uchakavu wa kutisha. Vituo hivi vimekuwa vikihifadhi wahalifu pamoja na uchakavu huo jambo ambalo ni hatarishi kwa usalama. Umuhimu wa kukarabati vituo hivi ni jambo ambalo haliepukiki. Jeshi lipange kimkakati wa ukarabati wa vituo hivi kwa awamu ili kuwa na vitu bora na vinavyokidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Jeshi la Magereza. Jeshi hili lina jukumu la kuwahifadhi wafungwa na kutazama mahitaji yao kwa ujumla, lakini majukumu haya hayatekelezwii ipasavyo kwa ufinyu wa bajeti na vitendea kazi ili kufanikisha majukumu yake. Msongamano ni mkubwa katika magereza yetu, magari ya kupeleka wafungwa mahakamani ni machache na mabovu sana. Nashauri Serikali itenye fedha za kutosha ili kukabiliana na upungufu mkubwa uliopo katika hili Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, vitambulisho vya uraia. Vitambulisho vya uraia ni haki ya kila Mtanzania kwa kuwa ndicho kinachomtambulisha. Zoezi hili licha ya kushushwa kwenye wilaya zetu limekuwa la kusuasua na kuleta usumbufu na urasimu usiokuwa na ulazima. Wananchi wametakiwa kuchangia fedha ili kupata vitambulisho hivyo. Kwa nini Serikali inachangisha wananchi wakati ni haki ya wananchi kupatiwa vitambulisho. Serikali inawajibika kuwapatia vitambulisho bila vikwazo kwa kuwa Serikali inakusanya kodi ambazo zinapaswa kuwashudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea ukurasa wa kumi wa hotuba ya Waziri kuhusu ujenzi na ukarabati wa nyumba za polisi. Tunapenda

kujua kati ya nyumba 400 zinazotarajiwa kujengwa kama Vituo yya Polisi Bassotu na Endasak vinahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama fedha zilizotolewa za maendeleo kiasi cha Sh.38,285,682,000/= zinahusiana na ujenzi na ukarabati wa nyumba za polisi. Kama ndivyo, je, Vituo vya Polisi katika Wilaya ya Hanang, Mkoani Manyara vina kiasi gani cha fedha za ujenzi na ukarabati? Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja, naomba kujua kama Vituo vya Polisi Bassotu na Endasaki vimetengewa fedha, kwani Kituo cha Bassotu Wilayani Hanang Mkoani Manyara, wamepewa barua ya kuondoka katika nyumba ambayo waliomba kuishi kwa muda kama kituo cha polisi. Je, lini kituo hicho kitajengwa na nyumba za polisi kwa ajili ya usalama wa raia na mali zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni usafiri. Kutokana na kuwa na eneo kubwa la ulinzi kunatakiwa usafiri wa uhakika kwa polisi wetu wanaoishi kwenye vituo ambavyo viro pembezoni na mbali na makao makuu ya Polisi Wilaya. Kwa hiyo, naomba kupatikane gari ambalo litawasaidia Polisi Bassotu ili waweze kulinda wananchi, raia na mali zao kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ajira. Naomba askari wa kutosha wa kike ili kuhifadhi hadhi ya wanawake kwani wanawake ni wengi sana kuliko wanaume.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia mateso wanayoyapata Askari wa Kituo cha Mkokotoni Kaskazini A Unguja. Kituo cha Polisi cha Mkokotoni kiliteketetea kwa moto usiku wa tarehe 27 Desemba, 2017 saa 7.30. Ujenzi wa kituo ulianza mara moja kwa lengo jema kujenga kitu bora daraja (A) na kuwaondolea usumbufu askari wetu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kituo kiungue huu ni karibu mwaka wa tisa (9) ujenzi haujakamilika. Mazingira wanayofanya kazi ni magumu sana kiasi cha kuhatarisha afya zao. Mfano mdogo mapokezi (*reception*) ni banda la mabatijuu, chini, pembeni yaani limeezekwa kwa mabati, kuta zake mabati. Wakati wa joto kali askari wanapata shida kwa joto kali kiasi cha kusababisha uharibifu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka tisa ni kipindi kirefu kufanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi kwa afya za askari. Wabunge tumekuwa tukiuliza sana kuhusu kituo hiki lakini majibu ni yale yale, mwaka wa fedha 2016/2017 ukimalizika unaambiwa 2017/2018 lakini hakuna linalofanyika. Naomba sana na kwa heshima kubwa tuone huruma askari ni binadamu wanahitaji kupewa moyo. Nataka kujua ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliuliza kuhusu deni la mkandarasi wa ujenzi wa Kituo cha Mkokotoni, Naibu Waziri akajibu bado hajalipwa. Inawezekana kutolipwa kwa mkandarasi huyu ni sababu ya kutokamilika kwa jengo hili. Hata hivyo, huyu ni mfanyakiareshara, kumcheleweshea kumlipa ni kumuua kibiareshara. Mkandarasi huyu anaumwa, afya yake si nzuri, anataka matibabu hali yake ngumu, je, ni lini Serikali itamlipa deni lake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 25 Septemba, 2017, Mzee Ali Juma Suleiman alivamiwa nyumbani kwake Mtoni Kidatu Unguja saa 5.30 usiku na kundi kubwa la watu ambao wengine wana mapanga, marungu na silaha za moto. Kama kawaida ya mtu ye yote mwenye kuvamiwa aliomba msaada kwa kupiga kelele nyingi pamoja na watoto wake. Ili kuzuia jamii isisogee kutoa msaada zilipigwa risasi za juu, wakamchukua na kwenda kumtesa, akaokotwa kupelekwa Mnazi Mmoja siku ya tatu alifariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza Zanzibar kisheria umiliki wa silaha za moto ni vyombo vyaa

usalama pekee. Inapotokea tukio kama hili risasi kama tatu mpaka nne zinapigwa halafu vyombo vyote nya ulinzi vinakaa kimya bila wasiwasi wowote, hili linatia wasiwasi mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Ali Juma Suleman alihojiwa akiwa hospitali na vyombo nya habari alisema na kutilia wasiwasi Jeshi la Polisi kuhusika kwao katika uvamizi uliomkuta. Jambo la kusikitisha na kwa mshangao mkubwa mpaka muda huu Jeshi la Polisi halijakamata mtu ye yeyote kuhusiana na tukio hili. Serikali inatuambia nini kuhusu dhuluma hii mbaya kabisa?

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi, mwangi wa rehema. Pia nakushukuru kwa kupata fursa hili ya kuchangia kwa maandishi hoja iliyopo mezani sasa. Napenda kuzungumzia Vitambulisho nya Uraia; pigwapigwa inayofanywa Zanzibar na Vikosi nya SMZ wakati huohuo Polisi wanawalinda wapigaji na kuwekwa ndani Mashekhe kwa kipindi kirefu bila kujali sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na vitambulisho. Kuhusu suala hili japo halijakaa sawa kabisa, bado kuna Watanzania wengi hawajapatiwa vitambulisho ilhali tayari wameshatimia umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pigapiga inayofanywa kule Zanzibar na Vikosi nya SMZ inatisha. Baya zaidi Askari Polisi ambao wao ndiyo wenye dhamana ya kulinda raia na mali zao huwa wao Polisi wanawalinda hawa wapigaji ambao ni Vikosi nya SMZ. Kama kuna makosa yoyote yanayofanywa kwa mujibu wa sheria basi watu hawa wapelekwe Mahakmani. Haya wanayoyafanya Vikosi nya SMZ hawana mamlaka ya kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zanzibar limekuwa ni jambo la kawaida kupigwa, kutekwa, kupotezwa na hata kutupwa vichakani. Baya zaidi kuna mtu amepigwa

nyumbani kwake usiku na Polisi na baadaye akakimbizwa hospitali na baada ya siku kama ya tatu mzee yule akafariki. Tunakwenda wapi Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu Mashekhe waliokekwa ndani kwa miaka kadhaa sasa. Hivi ni upelelezi wa aina gani hadi leo ushahidi haujakamilika? Inashangaza sana. Wabakaji, wahuni, walawiti watoto, wote hawa ushahidi umethibitika lakini kwa Mashekhe ambao kimsingi hawana makosa yoyote mpaka leo bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapita katika kipindi kigumu sana kwa ongezeko la uhalifu hasa dhidi ya haki za binadamu. Yamekuwepo matukio mengi ya watu kutekwa, kupotezwa, kuuwawa na miili yao kuopolewa kutoka baharini na kwenye mito. Taharuki ni kubwa kwamba watu hawa wasiojulikana hawatambuliwi wala kukamatwa na vyombo vyetu vya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matukio makubwa ni kama la Mheshimiwa Lissu kumiminiwa risasi hadi leo hakuna hata mtuhumiwa mmoja aliyekamatwa. Kibaya zaidi matukio haya yote yanayowapata wananchi hakuna hata siku moja mkuu wa nchi au Waziri wa Mambo ya Ndani amejitokeza na kuzungumza na wananchi kuhusu matatizo hayo na kuwapa *a sense of comfort* kuhusu usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa kwa kiongozi wa juu kuzungumza na wananchi kuhusu usalama wa nchi. Ili haki ionekane kutendeka wananchi wapate taarifa mara kwa mara kuhusu kukamatwa kwa watu hao wasiojulikana wanaoharibu taswira ya Jeshi la Polisi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na mhimili wa Mahakama wawaachie wafungwa, mahabusu wanaotuhumiwa kwa makosa

madogo madogo yanayodhaminika watumikie kifungo cha nje. Kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza msongamano mkubwa kwenye magereza na kupunguza gharama na kuepuka magonjwa ya maambukizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto liwezeshwe kwa kupatiwa rasilimali ya kutosha kama watumishi na zana za kazi ili kuwawezesha kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye Wizara, taasisi, majengo ya biashara na huduma kudhibiti majanga ya moto ambayo siku hizi yamekuwa yanatokea mara kwa mara. Kinga ni bora kuliko tiba, kuzuia majanga ya moto ni jambo muhimu sana kama hatua ya kulinda usalama wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu na naomba kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu mauaji ya raia Abilah Abdureheman wa Mtwara Mjini. Kijana huyu aliuawa na Jeshi la Polisi tangu tarehe 25 Machi, 2018 ufukweni/pwani ya Mtwara Mjini Kianga. Nimeongea sana kuhusu suala hili ila bado sijapata majibu ya Serikali na hatua kwa wahusika ni zipi maana Waziri aliahidi kuunda tume mpaka sasa hakuna majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali (Waziri) atoe majibu stahiki juu ya mauaji haya kwa kijana ambaye hakuwa na hatia kwa kisingizio kuwa alikuwa mvuvi haramu. Suala hili limeleta tataruki kubwa sana Mtwara Mjini, Serikali lazima ifanye uchunguzi wa kweli na wahusika wachukuliwe hatua na mimi kama mwakilishi wa wananchi nipate majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, napenda kuongelea Kituo cha Polisi Mtwara (Wilaya) ambacho kiko mbioni kubomoka. Kituo cha Polisi Wilaya ya Mtwara ni kibovu sana, zege inakatika na siku yoyote itabomoka. Naiomba

Serikali ikarabati haraka kituo hiki kwani askari wetu watapoteza maisha muda wowote baada ya kuwabomokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niongelee kuhusu kukosekana kwa samani katika Kituo cha Wilaya ya Mtwara. Kituo hiki hakina meza na viti ambavyo vinaweza kukidhi mahitaji ya polisi wanapotoa huduma. Polisi wanasimama muda wote wanapohudumia wananchi. Naomba ziletwe meza na viti katika kituo hiki cha Polisi Wilaya kwani hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne nitaongelea kuhusu nyumba za bati za Polisi wa Mtwara. Nyumba za bati kwa polisi ni hatari sana. Mtwara Mjini zipo nyumba nydingi za bati mpaka leo. Hali hii inatisha sana kwani umeme unaweza kuangamiza maisha ya askari wetu mara moja. Naomba pesa ziletwe Mtwara Mjini kwa ajili ya kujenga nyumba bora za polisi badala ya hizi za bati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, niongelee kuhusu bodaboda na polisi. Mtwara Mjini wahalifu wengi wameingia kwenye kazi ya bodaboda na uhalifu umepungua sana Mtwara Mjini kwa kuwa wahalifu wana kazi ya kufanya. Jambo la ajabu askari wetu ambao hawaitakii mema amani yetu wanawasumbua sana bodaboda tena bila sababu. Askari wanawafukuza kana kwamba wameua, wanakamata pikipiki hovyo na kutoza *fine* ovyo tena bila sababu. Bodaboda anatakiwa apeleke Sh.40,000 kwa tajiri wake kwa wiki lakini anashikwa na polisi anatozwa Sh.120,000 au Sh.90,000 kwa kisingizio kuwa amefanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Polisi zimejaa pikipiki nydingi sana. Polisi hawatoi elimu, wananyang'anya pikipiki za maskini, wanaziacha zinaoza katika vituo vy'a polisi. Hali hii haikubaliki hata kidogo. Naitaka Serikali iangalie suala hili kwa jicho la kipekee kabisa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nydingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu

Waziri na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge limekuwa linatenga fedha nyingi sana kwa ajili ya *NIDA* kuendesha zoezi la kuandikisha raia ili kupatiwa vitambulisho vya uraia. Zoezi hili lilianza mwaka 2011 na lilitegemewa kukamilika ndani ya miaka miwili. Leo ni zaidi ya miaka nane (2011-2018), naomba Serikali ieleze Bunge zoezi hili limefikia hatua gani? Watanzania wangapi wamepatiwa vitambulisho mpaka sasa na ni lini zoezi hili litakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari polisi wamekuwa wanapanda madaraja wanakaa miaka mingi bila kupandishwa mishahara yao na maslahi mengine. Wapo askari waliopanda madaraja tangu 2010, 2015 mpaka leo hawajaboreshewa mishahara yao. Jambo hili linawanyima haki zao lakini pia linakatisha tamaa ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana la watuhumiwa kuwekwa *lock-up* za polisi/mahabusu kwa zaidi ya saa 48 kinyume na sheria. Polisi wanawaweka watuhumiwa mahabusu siku 7 - 14 bila kuwapeleka mahakamani. Serikali ilieleze Bunge na kutoa kauli kuhusu tatizo hili ambalo tunalisemea kila leo lakini bado linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto halitengewi fedha za kutosha kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Jeshi hili halina ofisi/vituo wilayani bado wamo kwenye ofisi za mikoa kwa maeneo mengi. Hakuna vitendea kazi vya kuokoa na kupambana na majanga ya moto, magari ni machache na hata pale wanapoitwa wanafika hawana maji. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Jeshi la Zimamoto linakuwa na vituo katika wilaya zote hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua hatuna nyumba za kutosha za askari polisi. Askari wengi wanakaa mitaani jambo ambalo ni hatari sana kwa usalama wao na

familia zao. Serikali haijawahi kujenga nyumba za polisi Wilaya ya Kaliua kwani chache zilizopo ni juhudzi za viongozi wa Kaliua na wananchi. Serikali sasa itengete fedha za kujenga nyumba za askari pale Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Kaliua hakina vitendeza kazi vya kutosha. Gari ni moja, pikipiki ni mbili tena mbovu, hakuna komputa hata moja na mafuta yanayotengwa kwa ajili ya gari hilo ni kidogo mno. Wilaya ya Kaliua ni kubwa sana hivyo matukio ya uhalifu ni mengi sana. Serikali itoe kipaumbele kwa Wilaya ya Kaliua kupatiwa vitendeza kazi ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi hutumia nguvu kubwa sana hasa wakati wa kukamata wahalifu wasiokuwa na silaha. Wanaumizwa kwa vipigo wakati hawajathibitishwa kama wamekosea. Wapo raia wengi wameumia na wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya matumizi ya nguvu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kaliua, Kata ya Ushokora tuelekezwe kutenga eneo kwa ajili ya kujenga gereza. Tangu 2014 mpaka leo hakuna lolote linaloendelea pale. Wananchi waliokuwa wanatumia eneo hilo walinyimwa kutoliendeleza hata kwa kilimo. Serikali itueleze nini hatma ya eneo lile na nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Kaliua panajengwa gereza?

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu hali ya amani nchini. Nashauri Serikali kuangalia upya juu ya suala zima la chanzo cha amani kama kipo vizuri. Chanzo cha amani ni haki. Haki ni tunda la amani, bila haki haitatokea hata siku moja amani ikawepo. Kamata kamata ambayo inaendelea hapa nchini na mauaji yanayoendelea yanachochaea uvunjifu wa amani. Niishauri Serikali kuangalia kuna shida gani inayosababisha watu kuuliwa katika mazingira ya kutatanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya polisi kubambikia kesi wananchi na kuwafanya kukaa mahabusu

kwa miaka sita bila kesi zao kumalizwa mapema. Niishauri Serikali kuangalia juu ya mahabusu hawa kwani huongeza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali juu ya polisi kutumia nguvu nyingi kwenye mambo ya kawaida, mfano, unapozua au kutawanya waandamanaji wasio na silaha kwa bunduki na risasi za moto mpaka kufikia kuua kama alivyouwa Ndugu Akwilina. Maandamano ya CHADEMA yalikuwa ya amani, hayakutakiwa kufyatuliwa risasi za moto. Polisi wameshindwa kufanya kazi ambayo wana wajibu nayo wanafanya kazi ya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya polisi wanavyowachukua watuhumiwa ndivyo sivyo, ni hatari sana kwani huwapiga watuhumiwa ambao hawajahukumiwa, hivyo kupewa hukumu na polisi kitu ambacho si haki. Je, kama haki haikutendeka, amani itatoka wapi? Hawa polisi wanaishi na wananchi huko kwenye jamii, hivyo itafika siku ambapo jamii itachoka na kupambana na polisi huko huko kwenye jamii.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchimba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri, lakini naomba kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ifunge vifaa vya kudhibiti mwendo katika magari ya mizigo (malori) maana mara nyingi husababisha ajali.

(ii) Ili kuondoa sitofahamu kwa Watanzania, Kitengo cha Madawa ya Kulevyta pindi wanapoteketeza madawa hayo mfano *cocaine* na *heroine* ioneshe hadharani kama wanavyoonesha bangi.

(iii) Serikali iharakishe upelelezi katika kesi zinazowakabili wananchi. Upelelezi uwe unafanywa kwa haraka ili kuepusha mlundikano wa kesi na mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu.

(iv) Kikosi cha Zimamoto hususan Mkoa wa Dar es Salaam kimebuni mradi wa kuwauzia wafanyabiashara vifaa vyta kuzimia moto (*fire extinguishers*). Hii hupelekeea kuongezeka kwa uitiri wa kodi kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wawaendee wenyewe nyumba (wamiliki wa majengo) wanununue *fire extinguisher* waweke katika *corridors* za majengo na siyo ndani ya maduka. Maana wakati mwingine moto hutokea nyakati za usiku wakati mmiliki wa duka yupo nyumbani amelala. Kwa hiyo, *fire extinguisher* haina msaada wowote maana ipo ndani ya maduka siyo nje katika *corridor*.

(v) Askari wa usalama barabarani (*traffic*) ni kero sana kwa watumiaji wa vyombo vyta moto. Mara nyingi kuna makosa mengine askari wa usalama barabarani anapaswa kumwelimisha anayeendesha chombo cha moto na siyo kosa la kutoza faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi inaonesha kabisa wapo barabarani kuisaidia Serikali kukusanya mapato ya nchi na siyo kuelimisha jamii au madereva katika kulinda usalama wao na mali zao. Serikali itoe semina kwa askari wa usalama barabarani ili wawe na weledi na kujua majukumu yao na siyo kuleta kero kwa watumiaji wa vyombo vyta moto.

(vi) Kuna baadhi ya askari wetu wamepandishwa vyeo lakini mishahara yao haijapandishwa. Suala la kupandishwa cheo kwa askari liende sambamba na kuongezwa mishahara.

(vii) Serikali ipunguze gharama za kupata *passport* ya Sh.150,000 maana ni ghali mno ukizingatia kipato au kima cha chini cha Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwombea Mheshimiwa Waziri kila la kheri na Mungu ampe umri mrefu na afya njema katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mheshimiwa Mwigulu pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Lushoto kilijengwa toka mwaka 1890 na kimejengwa na mkoloni. Mpaka sasa hakijafanyiwa hata ukarabati lakini *DC* anayeitwa Majidi Mwanga alipata pesa kuitia wafadhili na kujengwa jengo moja la utawala ambalo limejengwa mpaka kufikia usawa wa lenta. Mpaka sasa ni miaka minne imepita bado jengo liko vile vile na linazidi kunyeshewa na mvua. Kwa hiyo, niiombe Serikali ipeleke pesa za kumalizia jengo lile ili lisije likaangushwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, kuna shida kubwa sana ya nyumba za watumishi. Nyumba zile za polisi ni za tangu mkoloni, zimechoka mno hazistahili kuishi askari wetu. Pamoja na hilo, askari wameamua kujenga nyumba za mabanzi ili waweze kuishi humo lakini kiuhalisia nyumba hizo za mabanzi hazistahili kuishi askari wetu ambao wanafanya kazi ngumu mno. Hivyo basi, niiombe Serikali angalau askari wetu wapate hata nyumba tano.

eshi la Magereza nalo gereza lao ni la muda mrefu pamoja na nyumba wanazoishi askari wetu siyo nzuri kabisa na hata nikisema hazistahili kuishi askari namaanisha. Hivyo basi, niiombe Serikali yangu Tukufu iiangalie Lushoto kwa jicho la huruma ili tuweze kuokoa maisha ya askari wetu. Kwani kwa maisha wanayoishi askari wetu wanawenza kupata magonjwa na kuhatarisha maisha yao ukizingatia nyumba zile walizojenga hazina hata sehemu ya kuchimbia choo kwa ujumla nyumba zile hazina vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Lushoto inajulikana kuwa ni ya milima na mabonde na wilaya nzima ina wakazi zaidi ya milioni moja lakini Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Magereza hawana vitendea kazi. Hivyo basi, niiombe Serikali yangu ipeleke magari kwa ajili ya askari polisi na askari magereza. Hasa hawa magereza hawana kabisa

magari wanapata tabu sana hasa katika utafutaji wa kuni. Hii imepelekea wafungwa kutembea umbali mrefu kufuata kuni na hii ni hatari kwa askari wetu wanaweza kutorokwa na wafugwa. Kwa hiyo, Serikali ituangalie Lushoto kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia ya askari wetu wasio waaminifu kuwanyanya raia wetu kwa kuwalazimisha wawape rushwa. Wakikataa au kama hawana ndiyo wanaanza kuwabambikia kesi au kuwapiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, askari wetu hawa hasa hawa askari trafiki wanawanyanya vijana wa bodaboda na vijana wanaoendesha *Noah*. Imefikia hatua hata kama dereva amepaki gari askari hutoa *plate* namba za gari tena kwa kuitoa kwa nguvu hadi ikatike na kusababisha uharibifu wa *plate* namba hiyo. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu ikemee kitendo hiki kinachofanywa na askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu Tukufu itujengee vituo vidogo vya polisi katika maeneo ya Makanya – Kwemakame na Gare, kwani maeneo haya yana watu wengi sana na pia ndiyo maeneo ambayo yana matukio mengi ya kihalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali yangu Tukufu, hizi pesa zinazokusanywa vituo vyetu vya polisi zote zisiende Serikali Kuu. Angalau zibaki hata 30% ili vituo vyetu viweze kukidhi mahitaji yao madogo madogo kama mafuta ya magari na kununua *stationary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitambulisho vya Taifa, kazi hii inasuasua sana na huku wananchi wetu wanatuuliza kila siku. Hivyo basi, niiombe Serikali yangu ihmize mamlaka hii inayoshughulika na vitambulisho hivyo iongeze kasi hasa katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia uhai hadi kuona siku hii ya leo. Jeshi la Polisi ni taasisi muhimu kwa ajili ya ulinzi wa raia na mali zao. Jeshi hili liachwe huru kabisa lifanye kazi yake kwa mujibu wa taratibu na sheria zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lisitumike kisiasa na watawala wote waache kutoa maagizo kwa jeshi hili lifanye kwa matakwa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya wanapofanya ziara zao vijiji wanaandamana na magari ya polisi kiasi cha kuwatia wananchi hofu. Mbona sisi Wabunge tunafanya ziara bila polisi na usalama upo wa kutosha? Kutembea na mapolisi ni matumizi mabaya ya Jeshi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuhusu vitambulisho vya uraia (*NIDA*). Mradi huu ultengewa fedha za kutosha lakini wakati wa utekelezaji wake wananchi wetu katika Wilaya ya Karatu walichangishwa fedha kwa kila mmoja Sh.1,000/= kama sharti la kupata kitambulisho. Kwa nini wananchi wachangishwe wakati Serikali ilitoa fedha kwa mradi huu? Naomba kupatiwa ufanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ilitoa ardhi eneo la Njiapanda (Bashay) ekari 60 kwa Jeshi la Magereza ili kujenga Magereza ya Wilaya ya Karatu. Hadi leo bado magereza hayo hayajajengwa. Jeshi la Magereza kama halihitaji lirudishe eneo hilo kwa halmashauri.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pili, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba za Polisi, kwa kuwa nyumba wanazoishi askari polisi zina hali mbaya sana mbovu na hazina hadhi ya kuishi askari polisi na kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga nyumba 400, kila Mkoa

na kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi, je, ujenzi wa nyumba hizo utaanza lini ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa ambapo nyumba za Askari Polisi ni mbovu zimechakaa na hazifai kuishi askari ikiwemo jengo la kituo cha polisi ambapo wakati wa kipindi cha mvua paa linavuja sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Mpwapwa halina ukuta wa ngome na hivi sasa maaskari magereza wanajitolea kujenga ukuta (ngome) na mimi kama Mbunge nilichangia mifuko 25 ya *cement*. Je, Serikali imetenga shilingi ngapi kwa ajili ya ujenzi wa ngome ya gereza la Mpwapwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji, kwa kuwa *passport* zinabadilishwa na kwa kuwa sisi Waheshimiwa Wabunge hatujabadilishiwa, je, Idara ya Uhamiaji itabadilisha lini *passport* za Waheshimiwa Wabunge na hizi za sasa zinaruhusiwa kutumika kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto, kwa kuwa magari ya zimamoto katika miji mingi ni machache sana na matukio ya moto ni mengi hapa nchini. Je, ni Serikali itanunua magari ya kutosha kuzimia moto katika miji yote Tanzania ikiwemo Makao Makuu ya Nchi Dodoma. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja Serikali kununua gari moja la kuzimia moto kila Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii, kwa kazi nzuri inayofanywa na watumishi wa Wizara hii kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, AGPna watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iwe inakumbuka ahadi zake *Budget* 2015/2016, 2016/2017, niliomba fedha za ujenzi wa vituo vyatupu, Nyamuswa na Mugeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya makazi ya nyumba za askari polisi ni mbaya sana, tunaomba suala hili Serikali ilione na kulfanyia kazi haraka. Jimbo la Bunda ni wakulima wa pamba, naomba Kituo cha Polisi, Kata ya Haonyori, ambayo wakazi wake ni wakulima wazuri wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba askari watumie weledi wao wakati wa kufanya *operation*. Tarehe 12 Novemba, 2018, kulitokea mauaji ya watu wawili katika mapigano ya vijiji viwili, Remung'orori na Mekomariro lakini askari walikuja kufanya *operation* katika tukio hili, walichukua bidhaa zote madukani, walikunywa bia zote katika baa na kupekua masanduku na kuchukua fedha *clip* zipo na tukio hili siyo zuri, askari watumie weledi.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za askari na vituo vya polisi, Jimbo la Tunduru Kusini ina tarafa tatu katika tarafa hizo ni moja tu Tarafa ya Nalasi ina vituo vya polisi lakini Tarafa ya Lukumbule na Tarafa ya Namasakata haina kituo cha polisi hivyo wananchi wanalazimika kufuata huduma hiyo Tunduru Mjini, zaidi ya kilometra 60 mpaka 80. Tunaomba angalau kila Makao Makuu ya Tarafa kuwa na kituo cha polisi ukizingatia kuwa tarafa hizo zinapakana na Msumbiji hivyo kuna mwingiliano wa watu kutoka Msumbiji na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya uhamiaji; Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na Mto Ruvuma kwa maana ya Msumbiji kuanzia mwanzo mpaka mwisho, lakini hamna kituo chochote cha uhamiaji jambo ambalo linaleta kero kwa wananchi wa Tunduru mara wanaposafiri kwenda Msumbiji kwa sababu tunaingilia sana kati ya Msumbiji na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Msumbiji kuna askari wengi sana wa Uhamiaji na polisi

wanawanyanya sana wananchi wanaovuka mpaka kwenda Msumbiji wakati wao wakija kwetu hamna mtu anayebugudhiwa. Hivyo naomba angalau Kituo cha Uhamiaji katika Kijiji cha Lukumbule ili kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Boma la Polisi Lukumbule, wananchi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilianzisha ujenzi wa kituo cha polisi Lukumbule tangu 2011, mpaka leo kituo hicho hakijakwisha, limejengwa boma tu halijaezekwa mpaka leo. Hivyo tunaomba Serikali itusaidie kumalizia kituo hicho ili kiwasaidie wananchi wa Kata za Lukumbule na Mchasi ambao wapo zaidi ya umbali wa kilomita 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya polisi Tunduru; katika Halmashauri ya Tunduru illkuwa na makazi ya polisi lakini yaliungua na moto zaidi ya miaka mitano iliyopita lakini nyumba zile mpaka leo hazijajengwa tena na askari wale sasa wanakaa uraiani. Hivyo tunaomba askari wetu wapatiwe makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa askari polisi pamoja na vifaa vyta kufanya kazi, Tunduru hatuna polisi wa kutosha kuhimili eneo kubwa la Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Hivyo, tunaomba tuongezewe askari ili waweze kuhudumia wananchi wetu pamoja na mali zao. Vilevile kuna tatizo kubwa sana la usafiri, pindi matukio ya uhalifu yanapotokea, askari hawafiki kwa wakati kutokana na tatizo la usafiri. Wakati mwingine hata mafuta ya kuweka kwenye gari wanakuwa hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la fedha za uendeshaji wa ofisi; polisi wamekuwa ombaomba wa mafuta kwa ajili ya magari yao kutokana na ukosefu wa fedha za kununulia mafuta ya magari. Hivyo, tunaomba Serikali ipeleke fedha za OC ili polisi wafanye kazi zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la rushwa, wananchi wengi sana wanalamikia Jeshi la Polisi kutokana na rushwa

inayoendelea, wananchi kwao limekuwa kawaida kuombwa rushwa mshtaki na mshtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasema kuingia polisi bure ila kutoka polisi lazima uwe na pesa. Jambo hili linalichafua jeshi la polisi. Vilevile bado kuna malalamiko ya rushwa kwenye Jeshi la Polisi la Usalama Barabarani kwani kuna askari wa usalama barabarani wamefanya kazi hiyo kama mradi wao wakujipatia kipato kisicho halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linachafua sana Jeshi la Polisi la Usalama Barabarani; kwa mfano kila basi linalotokea Ubungo linatozwa zaidi ya Sh.20,000 la sivyo gari/basi halitoki. Vilevile vituo vyote vya ukaguzi vya mabasi kila basi linatozwa Sh.5,000 mpaka Sh.10,000, la sivyo basi linacheleweshwa kwa visingizio mbalimbali. Tunaomba jambo hili likomeshwe. Vitendo hivyo viro kwenye vituo vyote vya mabasi yanayosafiri kwenda sehemu mbalimbali ya Mikoani na Wilayani.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

- (i) Uchunguzi wa mauaji ya raia (MKIRU - Mkuranga, Kibiti na Rufiji);
- (ii) Suala la uraia wa watu wa Kigoma;
- (iii) Kupotea kwa Ben Saanane, Azory Gwanda na Simon Kanguye bila taarifa yotote ya polisi kuhusu uchunguzi wa kupotea kwao. Pia uchunguzi kuhusu kupigwa risasi Tundu Lissu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya Watanzania 380 wanatajwa kupotezwa 'MKIRU', Bunge lichunguze kama liliyochunguza Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 12 Juni, 2017 mchana Bi, Ziada Salum wa kitongoji cha Maparoni Wilayani Kibiti alikuwa nyumbani kwake akipika chakula cha familia yake,

wakati ambao Jeshi la Polisi lilitifika na kumchukua kwa ajili ya kwenda kumhoji. Ni Miezi 11 leo tangu Bi. Ziada Salum achukuliwe, hajarudishwa mpaka leo, familia yake hajaarifiwa chochote, bado imekaa na matarajio kuwa ipo siku atarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi huo wa Juni, 2017, si Bi Ziada tu aliyechukuliwa na kutokurudishwa mpaka leo, kwa staili ya namna hiyo ni wengi mno. Wakiwemo kina mama wa familia moja, Rukia, Muhohi na Tatu, Muhohi wa kitongoji cha Msala, hapo hapo Wilayani Kibiti, wao wakichukuliwa kwenda kuhojiwa na Jeshi la Polisi 26 Juni, 2017 na mpaka leo hawajarudishwa. Kaka yao Nassoro Muhohi yeye alichukuliwa 27 Juni, 2017 kisha kuachiwa (najua kwa kumtaja hapa Bungeni anaweza kuchukuliwa tena na mara hii kupotea kabisa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitongoji hiki cha Msala kimewapoteza wengi, akiwemo Jumanne Rashid Pango, aliyechukuliwa naye siku moja pamoja na Rukia na Tatu Mhohi. Ni miezi zaidi ya 10 leo, watu hawa wote Jeshi la Polisi halijawarudisha, lakini pia halijatoa maelezo yoyote kwa ndugu zao juu ya walipo na lini watawarudisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kina Muhohi si ndugu pekee waliochukuliwa na Jeshi letu la Polisi na kutokurudishwa mpaka leo, katika Kata ya Mjawa, Wilayani Kibiti ndugu watatu wa familia moja nao walichukuliwa 2 Juni, 2017, hao ni Hamisi Omari Nyumba na mwanawewe, Sadam Hamisi Nyumba pamoja na nduguye, Juma Omari Nyumba. Nao Jeshi la Polisi limebakia nao mpaka leo, halijawarudisha, hatujui kama bado wako hai ama ni sehemu ya miili iliyo koto wa kwenye fukwe zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hao tu, 10 Julai, 2017, katika Kitongoji cha Nyantimba, Wilayani Rufiji, Jeshi la Polisi liliwachukua watu watatu, bwana Hamis Mketo, Bi Tabia Nyarwamba na Bi. Pili Mkali nao wakielezwa wanakwenda kuhojiwa, kama ilivyo kwa hao wengine, nao hawajarudishwa mpaka leo, zaidi ya miezi tisa sasa. Orodha

niliyonayo hapa ni kadhia 68 za namna hii, kadhia 62 zikiwa zimezithibitisha, kadhia nane nikiwa naendelea na uchunguzi. Kwa sababu ya muda niishie kutaja hao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhia za namna hii ni nyingi mno na yejote kati yetu, akipata wasaa tu wa kwenda MKIRU (Mkuranga, Kibiti na Rufiji) ataaelezwa mambo haya kwa undani, makadirio ni kuwa zipo kesi zaidi ya 380 za namna hii za watu kuchukuliwa na kutorudishwa kwa zaidi ya miezi 10 sasa, hizo ni tofauti na zile za watu waliokamatwa, kuteswa na kisha kuachiwa au wale waliojeruhiwa kwa kupigwa risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo MKIRU tu, bali ukanda wote wa Kusini, wiki mbili zilizopita, Mbunge wa Kilwa Kusini Mheshimiwa Suleiman Bungara 'Bwege' (*CUF*) naye alieleza kadhia za watu 10 wa Jimboni kwake Kilwa, kuchukuliwa Msikitini na Jeshi letu la Polisi, kupigwa risasi wengine kutokurudishwa mpaka leo na kuhisiwa kuwa wameuawa, wengine kurudishwa wakiwa na vilema vyta kukatwa masikio, kuchomwa ndevu kwa moto na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua haja ya kudhibiti hali mbaya ya usalama iliyojitokeza mwaka jana. Mauaji yale ya Askari Polisi na raia yaliyokuwa yakiendelea MKIRU yalipaswa kukomeshwa, lakini bado ukomeshwaji husika ulipaswa kufanyika ndani ya utaratibu wa kisheria tuliojiwekea kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya yanayoripotiwa sasa kutoka MKIRU, ni dhahiri kuwa utaratibu wa kisheria ulikuukwa, haki za binadamu zilivunjwa, raia wema na wasio na hatia waliuawa na jeshi ambalo lilipaswa kuwalinda na wananchi wengi wakiwa wamepotea tangu wachukuliwe kwenda kuhojiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya namna hii si mapya hapa nchini mwetu, hayana nia nzuri ya kudhibiti jambo bayo, bali hutumika kuwaumiza wananchi. Mwaka 2013 nchi yetu ilikumbwa na janga kubwa la ujangili, tembo

na faru wetu wakiuawa na magenge ya wahalifu. Kwa nia njema ya kudhibiti ujangili huo, Serikali kwa kutumia majeshi yetu, ilianzisha Operesheni ya kutokomeza Ujangili huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kifupi cha Operesheni husika, malalamiko juu ya wananchi kubakwa, kuteswa, kuuawa, kuporwa mali zao na mengine mengi mabaya ya unyanyasaji wa raia yaliripotiwa. Unyanyasaji na ukiukwaji huo wa haki za binaadam wa wananchi wetu uliripotiwa Wilayani Babati, Mkoani Manyara; Tarime, Mkoani Mara; Kasulu, Mkoani Kigoma; Meatu, Mkoani Simiyu; Ulanga, Mkoani Morogoro; Urambo na Kaliua, Mkoani Tabora; pamoja na maeneo mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya wananchi yaliletwa hapa Bungeni. Bunge letu lilichukua hatua juu ya malalamiko hayo. Kwanza kwa kuitaka Serikali kusitisha Operesheni Tokemeza na kisha kwa kuunda Kamati Teule ya Bunge, kuchunguza juu ya utekelezwaji wa Operesheni Tokomeza. Kamati Teule ilithibitisha ukweli wa madai ya wananchi kunyanyaswa, kuuawa, haki zao kubinywa na kadhalika na hatua kadhaa njema zilichukuliwa ili kurekebisha jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya MKIRU ni makubwa mno, unyama unaoripotiwa kufanywa huko na vyombo vyetu vya ulinzi na usalalma hata hauelezeki, umehusisha kupotezwa kwa watoto, akinamama na wazee, haukujali jinsia wala rika, kadha chache nilizozielezea hapa zimeonesha taswira ya maumivu na ukubwa wa jambo hilo, zaidi taarifa juu ya kupotea kwa watu zaidi ya 380 zikishtusha na kuamsha hisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano Mkuu wa CCM wa mwaka 1987, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alisema yafuatayo:-

*"Panapokuwa hapana haki, wala imani na matumaini ya kupata haki, hapawezi kuwa na amani wala utulivu wa*

*kisiasa. Hatima yake patazuka fujo, utengano na mapambano”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wa MKIRU na Kusini kwa ujumla ni ndugu zetu, kaka na dada zetu, ni Watanzania wenzetu ambao tuko humu Bungeni kuwawakilisha. Unyama huu unaosemwa kufanywa dhidi yao umewaondolea kabisa Haki yao ya uhai, umewaondolea Imani ya kupata ulinzi wa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, Bunge letu lichunguze jambo hili kuwapa Matumaini ya kupata haki, ili wasibaki na vinyongo na ili wasichague fujo, utengano na mapambano kama njia ya kuponya majeraha yao na kudai Haki zao zilizominywa. Sisi Bunge tunao wajibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo basi, kwa maelezo hayo nillyoyatoa, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa taarifa kwamba nitatoa hoja binafsi kutaka Bunge lako Tukufu Kamati Teule kufanya uchunguzi kuhusu kadhia za Mauaji, kupotea, kupigwa Risasi, kuteswa watu wa MKIRU na Kusini kwa ujumla. Ni imani yangu kuwa Wabunge wenzangu wataunga mkono jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa kigoma si Watanzania? Uhamiaji na *NIDA* watueleze tukatafute nchi yetu? Jambo la pili ninalotaka kulizungumzia ni juu ya suala la uraia kwa watu wa mikoa ya mipakani mwa nchi, zaidi kwetu sisi watu wa Mkoa wa Kigoma. Nchi yetu inapakana na nchi majirani nane, zikiwemo nchi za Kenya na Uganda upande wa kaskazini; Msumbiji, Malawi na Zambia upande wa kusini; na Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa upande wa magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa upande wa magharibi, hasa tunaopakana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi ndio tunaosumbuka na haya masuala ya uraia kwa kiasi kikubwa kuliko watu wengine wa mikoa ya mipakani. Kiasi kwa sasa limekuwa ni jambo la kawaida kabisa kwa mtu ye yeyote mwenye asili ya Mkoa wa Kigoma,

aliyekwaruzana au kusigana na Serikali kuitwa na kuhojiwa na Idara ya Uhamiaji au kutakiwa kuthibitisha uraia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya matukio ya namna hiyo ndefu sana, sina haja ya kuisema hapa, lakini wahanga wa karibuni wa kadhia za namna hiyo ni Abdul Nondo, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, UDSM na kiongozi wa Mtandao wa wanafunzi nchini, *TSNP*; pamoja na Askofu Mkuu wa Kanisa la *Full Gospel Bible Fellowship (FGBF)*, ndugu Zacharia Kakobe, ambao wote wallitwa kuhojiwa na Idara ya Uhamiaji kwa sababu ya misigano walijonayo na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo la watu wengi wenye asili ya Mkoa wa Kigoma, wenye mikwaruzano na Serikali kuitwa kuhojiwa na Idara ya Uhamiaji, sasa limeibuka tazito kubwa zaldi na hili linatuhusu karibu wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma, ugumu katika upatikanaji wa vitambulisho vyta Taifa kutoka *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kigoma tunasumbuliwa mno kupata vitambulisho, katika wakati ambao ni 13.4% tu ya Watanzania wote ndio wana vyeti vyta kuzaliwa, haitegemewi kuwa hicho kitumike kuwa kikwazo cha sisi kunyimwa vitambulisho. Zaidi hata wananchi wanaokwenda na viapo nao wanasumbuliwa, wakati wanatumia gharama kubwa kuvipata viapo husika, wakivifuata mjini kwenye huduma ya Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kigoma ni maskini, mkoaa wetu ni moja ya mikoa masikini zaidi nchini, ni mkoaa pekee hapa Tanzania ambaohaujaunganika kwa mtandao wa barabara za lami na mikoa mingine nchini, haya pekee yalitosha kuifanya Serikali kututazama kwa jicho la huruma. Lakini sivyo, hata Utanzania wetu, uraia wa nchi yetu tunahojiwa, tukinyanyaswa na kutendewa kama watu wa daraja la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuyaoni haya kwa Wadigo wa kule Horohoro, au Wamasai wa Longido, kama

ambavyo hatuyaoni haya tunayotendewa watu wa Kigoma, kwa watu wa Nachingwea na Nanyumbu, au Nyasa na Tunduma. Kwa nini sisi tu watu wa Kigoma tunasumbuliwa zaidi kuhusu masuala ya uhamiaji? Kwa nini sisi watu wa Kigoma ndio tunapata zaidi tabu kupata vitambulisho vyta Uraia kutoka *NIDA*? Kwa nini ni sisi tu? Naamini Waziri atakuja na majibu juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge tulipuza kupotea kwa Saanane, tusipuuze kuchunguza kupotea kwa Azory na Kanguye. Mwaka jana Aprili, 11 nilizungumza humu Bungeni wakati nikichangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, juu ya kupotea kwa ndugu Ben Saanane, kijana wa Kitanzania, kupotea ambako kulihusishwa na Idara ya Usalama wa Taifa, ikielezwa kwamba alishikiliwa na kisha 'kupotezwa' na watu wanaohisiwa kuwa ni Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu yale, nilitoa wito kwa Bunge lichukue hatua kufanya uchunguzi juu ya jambo hilo, kwanza ili kupata ukweli juu ya matukio yaliyokuwa yameanza ya watu kupotea tu bila maelezo ya kina, pamoja na kulinda hadhi ya Idara ya Usalama wa Taifa ambayo ilitajwa kuhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya kuwa wito wangu wa Bunge kufanya uchunguzi haukupata uungwaji mkono. Wakati natoa hotuba ile, ilkuwa ni miezi sita tangu ndugu Saanane apotezwe, leo ni mwaka mmoja na nusu, familia yake, ndugu na wazazi, wamebaki na simanzi ya kutojua nini kimetokea kwa kijana wao. Idara yetu ya Usalama wa Taifa imebaki na doa la kuhusishwa na kupotea kwake na nchi yetu imechafuka, kwa taswira yake kuwa ni nchi ya usalama na amani kupotea na Bunge letu likionekana dhaifu kwa kutochukua hatua ya kuchunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndani ya Bunge hili tunayo dhima na wajibu, tumekasimishwa na Watanzania wenzetu mamlaka na madaraka ya kuwasemea, kuisimamia Serikali kwa niaba yao, kuhakikisha juu ya usalama wao. Kwenye jambo hili la ndugu Saanane tumeshindwa kutimiza wajibu

wetu, tumeshindwa kuhoji juu ya usalama wake, hasa ikiwa Idara yetu ya Usalama wa Taifa ndiyo inayotajwa juu ya kupotea kwake, hatujafanya kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kwetu kuhakikisha tunachunguza suala la ndugu Saanane kumetoa mwanya wa matukio ya namna hiyo ya watu kupotezwa tu kuendelea bila kukoma, sasa karibu yataonekana ni matukio ya kawaida. Labda kwa kuwa Saanane ni kijana wa upinzani tuliona tu kuchunguza juu ya kupotea kwake, tukidhani ni jambo lingeishia tu kwa watu wa upinzani, lakin kupuuza kwetu kumepelekeea kupotea kwa ndugu Simon Kanguye, huyu ni Diwani wa CCM na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya kupotea kwa ndugu Kanguye hayana tofauti na mazingira ya kupotea kwa ndugu Saanane, yeye aliiwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, kukutana na *DSO*(Afisa Usalama wa Wilaya) wa Kibondo, tangu hapo hajaonekana, akiwa amepotea siku moja kabla ya ziara ya Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa hapo kwenye Hamashauri ya Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanguye amepotea tangu Julai, 2017, miezi miwili na siku10 tangu Bunge likatae wito wangu wa kuchunguza kupotea kwa Ben Saanane. Naamini sisi Bunge tungechunguza juu ya kupotea kwa Ben labda asingepotea, labda angekuwa na familia yake, au barazani na Madiwani wenzake kule Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni miezi tisa na nusu tangu Kanguye apotee, mkewe na wanawe wamekwenda kila mahali kutaka msaada wa kupatikana kwake, mie huyu ni mjumbe mwenzangu wa RCC, nimehoji huko, sijapata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miezi minne tangu kupotea kwa Kanguye, akapotea Azory Gwanda, baba, mume na Mwandishi wa Habari za Uchunguzi, akiandikia hasa Magazeti

ya Kampuni ya Mwananchi, kupotea kwake kumehusishwa na habari za Kibiti ambazo amechunguza na kuandika mno. Kama ilivyo kwa Saanane na Kanguye, maelezo ya kupotea kwa Azory (kwa mujibu wa mkewe) yamehusisha tena watu wetu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama, waliomchukua 21 Novemba, 2017 nyumbani kwake na kutokuonekana mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni miezi mitano na nusu tangu Azory apotee, mkewe, dada yetu Anna Pinoni aliyejewa mjamzito, amejifungua Februari mwaka huu, binti yao sasa ana miezi mitatu, mnaweza kuwaza huzuni, upweke, mfadhaiko na msongo wa mawazo aliyonayo mama huyu. Kuachwa mjane, kuachwa na ujauzito na sasa kulea mtoto akiwa mpweke bila ya mzazi mwenzake. Mimi nikiwaza jambo hili naumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge letu haliwezi kuwa msaada kwa Anna Pinoni, kuibana Serikali ieleze alipo mumewe, kuhakikisha anarudishwa kwake salama ili asibaki mjane binti yake asibaki yatima, basi litapoteza maana na uhalali wake kwa wananchi wanyonge. Hali ya mke wa Azory ndiyo aliyonayo mke wa Kanguye pamoja na watoto wao, ndiyo waliyonayo wazazi wa Ben Saanane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge hatukutimiza wajibu wakati wa suala la Ben Saanane, tuutimize sasa kwa kuchunguza matukio haya ya watu kupotezwa huku vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vikihusishwa. Narudia wito wangu kwenu Wabunge wenzangu, kwa heshima na taadhima, tuunde Kamati Teule ya Bunge kuchunguza mambo haya, huu ni wajibu wetu kwa wananchi wenzetu. Tuutimize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge natoa taarifa kwamba nitatoa hoja binafsi kutaka Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule kufanya uchunguzi kuhusu vitendo vya utekaji, upotezwaji na mauaji dhidi ya raia (likiwemo suala la Ben Saanane, Simon Kanguye na Azory Gwanda).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Waheshimiwa Wabunge wenzangu wataniunga mkono kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mauaji, utekaji na uteswaji unaendelea kwenye Wilaya za Kusini Pwani (Mkuranga, Kibiti, Rufiji – MKIRU). Natambua umuhimu wa kudhibiti usalama wa ndani yetu lakini nalaani mauaji ya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalitaka Bunge kuunda Kamati Teule kuchunguza vifo vya raia Wilaya za MKIRU na Kilwa. Watu takribani 348 wamepotea/kufa ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za inayoitwa *Task Force* inayoteka, kutesa na kuua watu ni lazima ichunguzwe na Kamati Teule ya Bunge. Bunge haliwezi kuacha raia wake wanauawa hovyo kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi.

**MHE. ABADALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na nchi na muweza wa mambo yote. Aidha, nakupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi ni chombo muhimu sana katika kila nchi duniani kote. Ni chombo cha ustawi wa jamii kinachostawisha amani na usalama, kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa polisi ni chombo kinachotegemewa katika hali zote, ni matumaini ya wananchi wote kupata huduma na utumishi uliotukuka wa Jeshi la Polisi na Vitengo vyake vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko mengi ya Jeshi la Polisi kutumika vibaya au kisiasa zaidi. Naishauri Serikali chombo hiki kitumike vizuri kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi. Ikiwa Polisi watafanya kazi zao kwa weledi na

kutumia taaluma zao, jambo hili likifanyika vyema amani na utulivu wetu wa nchi utatengamaa. Waepukane na dhana ya kuwa Polisi wanaweka taaluma zao nyuma na kufanya kazi zao kwa kufuata maagizo kutoka upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za polisi, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu nafasi za kuajiriwa vijana katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani hususan Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Sote tunafahamu sana kwamba kuna kasma maalum ya nafasi za ajira za Polisi na Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mkoa kuna idadi yake maalum inayotengewa lakini kuna malalamiko kwamba inapofika wakati wa mahojiano ili kupata nafasi hizo kuna mambo mengi yanayofanyika ambayo sio mazuri ili kuziparanganya nafasi hizo na kukoseshwa nafasi hizo wale wanaostahiki. Yasemekana kwamba watoto wa wakubwa ndio huchukua nafasi nyingi hata kama si wakazi wa mikoa husika. Mambo haya hasa huwa yanatokea Mikoa ya Zanzibar yaani Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya yanatendeka naiomba Serikali na Wizara husika kulishughulikia jambo hili ili kuzifanya nafasi hizi ziende kwa walengwa na kuondoa malalamiko ya siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya kihalifu na utekwaji wa raia. Jambo hili ni tatizo kubwa na sasa limekuwa likilalamikiwa sana na raia. Ni ukweli usiopingika jambo hili linaleta usumbufu kwani tuhuma zinakwenda kwa askari wetu na Serikali inalijua lakini jawabu la Serikali ni kwamba matendo hayo huwa yanafanyika au yanafanywa na watu wasiojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa kutumia weledi wa askari wetu kuwabaini watu hawa wanaofanya matendo haya ya uharamia na kuwabaini watu wasiojulikana na kujua ni akina nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la matendo maovu yanayotendwa na watu wasiojulikana tunaiomba Serikali ije na majawabu maridhawa na watu wasiojulikana iwe sasa ni watu wanaojulikana ili ufundi na weledi wa polisi wetu uwe wa manufaa zaidi.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Wizara kwa kuendeleza vyema kulinda usalama na raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabumbilisho vya Taifa (*NIDA*), zoezi la kuandikisha watu na kupata vitambulisho vya Taifa linaendelea katika mikoa mbalimbali nchini, lakini changamoto iliyopo ni uhaba wa fedha za kuendeshea zoezi mpaka inalazimu Madiwani, Wabunge na Watendaji wa Wilaya, Kata na Vijiji kuchanga pesa kusaidia chakula na malazi jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji na mazingira hayo yanaweza weka ushawishi wa watendaji kutoa utambulisho kwa watu wasio na sifa yaani njia ya rushwa kutokana na malipo ya makarani kuwa madogo yaani shilingi elfu kumi kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji zoezi kwa kata ni ngumu kutokana na kata nyingine ni kubwa inaleta usumbufu kwa wazee, wagonjwa, mama wajawazito, hivyo zoezi liwe linazingatia umbali kati ya kijiji na kijiji ndani ya kata. Tunahitaji Waziri atoe tamko la namna bora ya kuendesha na pia upatikanaji wa vifaa na fedha ikiwemo magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni ya Askari Polisi katika *TRC*, jeshi la polisi hutumika na Shirika la Reli katika *escort* za treni na mkataba ni kuwa walipwe posho lakini kuna madai ya muda mrefu kati ya Askari na *TRC* mpaka kupelekeea kufungua kesi Dodoma Mahakama Kuu. Naomba Serikali ifanye mazungumzo na *TRC* ili kuwe na malipo kwa wakati na madeni ya nyuma yalipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Nsimbo, Halmashauri ya Nsimbo Kituo cha Polisi ambacho bado

hakina vifaa vya kutosha kuanzia gari, pikipiki na hifadhi ya silaha. Tunaomba Wizara isaidie vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za barabarani, sheria zinazosimamiwa na Jeshi la Polisi juu ya makosa ya barabarani zinaingiliana na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD* hivyo ni vyema Serikali ikafanya sheria hizo ziwe chini ya Wizara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Sheria za Barabarani, wananchi wengi hawazijui kanuni hizi. Mfano makosa ya gari na dereva, makosa katika mmiliki na Dereva mwajiriwa. Sheria iboreshwe ili kosa la Dereva lisiwe la mmiliki.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia kwa maandishi siku hii ya leo. Pia nipongeze Wizara kwa jitihada inazofanya lakini, pamoja na jitihada za Serikali bado katika nchi yetu kuna changamoto nyingi zifuatazo ambazo napenda kuiomba sana Serikali izifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maslahi ya Polisi, Polisi ni watu muhimu sana katika nchi yetu kwani ndiyo wanaotulinda raia na mali zetu, lakini kulinda hata amani ya nchi yetu, lakini polisi hawa hawana maslahi mazuri ya mishahara yao. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa polisi kupelekea kuishi kwa shida, hii ni hatari kwani inaweza pelekea wao kuingia katika vitendo vya kiuhalifu kama unyang'anyi wa silaha, upokeaji wa rushwa ili wajiongezee kipato. Niombwe sana Serikali kuboresha mishahara ya Polisi kwa haraka, hii i tawaongezea munkari ya kufanya kazi kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Polisi, maeneo mengi ya nchi yetu makazi ya polisi kiukweli ni duni sana na hayaridhishi kabisa. Polisi wanaishi katika mabanda yaliyojengwa kwa mabati. Hii siyo sawa, polisi wapatiwe

nyumba nzuri za kudumu na wao waishi kwa heshima. Leo Mkoani kwangu Kigoma polisi wanaishi katika nyumba duni sana humo humo baba, mama na familia hakuna usiri. Kiukweli hali si nzuri kabisa. Niiombe sana Serikali ijenge nyumba za kudumu na nzuri katika mikoa na wilaya zote nao polisi waishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakavu wa vituo vya polisi, vituo vingi vya polisi vina hali mbaya sana hasa mikoani. Unaweza jiliza hiki ni kituo cha polisi au ni kitu gani? Kituo chakavu sana, hawa polisi nao ni binadamu wanahitaji kufanya kazi katika mazingira mazuri na hata raia wanaokwenda kupata huduma pale wahudumiwe katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya upoteaji wa watu, sasa hivi hali inatisha sana. Kumejitokeza matukio makubwa na ya kuhuzunisha sana, watu wanapotea na kuuawa mara kwa mara na watu ambao hawajulikani. Hali hii imezua taharuki sana kwa wananchi. Serikali niiombe sana kuhakikisha watu hawa wanaofanya vitendo hivi wanakamatwa kwa haraka na kuchukuliwa hatua kali mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia kubambikiziwa kesi na polisi. Baadhi ya polisi wamekuwa si waadilifu na kupelekea kulichafua Jeshi la Polisi kwani kumekuwa na malalamiko mengi sana toka kwa wananchi hasa vijijini. Wanabambikiziwa kesi na baadhi ya polisi wasio waadilifu kwa lengo la kujipatia pesa. Niiombe sana Serikali kuliangalia suala hili kwa jicho la pili kwani wananchi wengi wanateseka sana, mtu anapewa kesi kubwa wakati hahusiki. Hasa tulipo mipakani kama Kigoma, wafugaji, wavuvi wamekuwa wakibambikiziwa sana kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi kujichukulia hatua dhidi ya raia wanapowakamata. Ninavyofahamu mimi kazi ya polisi ni kulinda raia na mali zake. Polisi anatakiwa kuhakikisha anamlinda raia asipate tatizo lolote lile hata anapomkamata amefanya kosa lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la polisi kumlinda mhalifu (raia) na kumfikisha kituoni akiwa salama pamoja na mali zake. Hata hivyo, polisi wamekuwa wanaua raia kwa kuwapiga mpaka kupoteza maisha. Hii ni hatari sana sana kupita maelezo. Hata kama raia amekosea ni jukumu la polisi kumlinda na kuhakikisha anafika kituoni salama. Tumeona Musoma Polisi kamchoma kisu raia, kweli polisi wanafikia huku? Hii ni hatari kubwa na inasikitisha sana. Niombi Serikali hii sikivu polisi hawa wachukuliwe hatua kali mara moja iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto kubwa sana katika Jeshi la Zima Moto, maeneo ya Wilayani hakuna vifaa vyta zima moto viro mikoani tu. Hii ni hatari sana lakini hata maeneo ambayo yanazima moto bado changamoto ni kubwa, vifaa wanavyotumia kwani inategemea ukubwa wa moto. Niombe sana Serikali iweke vikosi hivi vyta zima moto katika maeneo yote ya Wilayani na mijini pia, majengo yawepo ya kutosha. Niombe sana Serikali ijenge majengo ya kutosha, vifaa vyta zimamoto vyta kutosha katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamiaji maeneo mengi hayana ofisi. Niombe Serikali ijenge ofisi za uhamiaji za kisasa hasa katika Mikoa iliyopo mpakani kama Kigoma, Kagera, Tunduma, lakini utoaji *passport* umekuwa wa shida sana na bei ya kupata *passport* ni kubwa kwa raia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na mchangwo wangu katika Wizara hii kwa kuishauri Serikali kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa wakati hasa miradi ya nyumba za Askari Polisi na Magereza kwani askari wetu kuishi uraiani kunawaondolea weledi wao na pia kuhatarisha maisha yao, kufuatia mazingira ya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na ujenzi wa nyumba za askari vilevile ingeanza ujenzi wa vituo vyta polisi vyta Wilaya mfano hadi leo Wilaya ya Liwale haina jengo la Kituo cha

Polisi cha Wilaya. Jengo linalotumika ni jengo la mtu binafsi ambalo lilipangishwa kwa iliyokuwa Benki ya *NBC*, jengo hilo sasa ni chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza hayana hati miliki ya ardhi, mahali pengine hata jengo la magereza halina hati miliki licha ya kuwa na majengo yaliyokamilika. Mfano, Gereza la Wilaya ya Liwale lililoanzishwa mwaka 1982 lakini hadi leo jengo wananolitumia ni la tope lenye uzio wa miti. Hata hivyo, wenyewe mashamba yaliyotwaliwa kipindi hicho bado hadi leo hawajapewa fidia za mashamba yao. Gereza lina miaka 36 sasa lakini wenyewe mashamba hawajapata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma magereza zetu zilikuwa zinajitegema kwa chakula. Je, ni kwa nini sasa magereza zimekuwa mzigo mkubwa kwa Serikali kulisha wafungwa wakati magereza nyingi nchini zina mashamba makubwa na viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali? Kuna umuhimu gani wa kuaweka wafungwa magerezani kisha iingie gharama kubwa ya kuwatunza wafungwa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa upeletezi wa kesi mbalimbali nchini. Jambo hili limekuwa likichelewesha kesi nyingi kuamuliwa mahakamani. Ni kwa nini kesi hizo zisiwekewe muda maalum ili ikifikia muda huo, basi kesi hiyo iweze kufutwa kwani haina ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kesi mahakamani kwa muda mrefu kwa kukosa upeletezi, jambo ambalo linaashiria rushwa na kuwanyima haki raia wema. Hata hivyo, wakati mwingine kuchelewa kwa kesi nyingi ni kutokana na matamko ya kisiasa, kwani wako viongozi wanaowaweka ndani bila maelezo ya kutosha na kuwaamuru askari kuwa hakuna kumwachia huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekwa na kupotea watu, kumekuwa na matukio mengi nchini ya kutekwa na kuuawa

kwa watu wetu, lakini jeshi la polisi na watu wa usalama wako kimya sana na siyo jeshi la polisi tu, hata viongozi waandamizi ndani ya Wizara hii wamekuwa kimya sana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya mauaji nchini sasa limekuwa ni jambo la kawaida. Cha kusikitisha zaidi ni pale Jeshi la Polisi linapohusishwa na mauaji hayo na huku wengine wakibambikiziwa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi hili pia linahusishwa na utekaji nyara wa raia wema kwa kisingizio cha taarifa za intelejensi. Jambo hili kama wasemaji wanakuwa kimya jamii huamini kinachoandikwa kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ni mgumu sana na watu wengi bado hawaelewi kinachofanyika kwani ni zoezi linalochukua muda mrefu sana na wala hatujui zoezi hili litakwisha lini. Kila mwaka fedha nyngi zinatengwa kwenye mradi huu lakini utekelezaji wake ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi vya Jeshi la Polisi, kumekuwa na uhaba mkubwa wa vitendea kazi katika Jeshi letu la Polisi hasa upande wa magari, mfano Wilaya ya Liwale haina gari la polisi, Wilaya yenye kata 20, tuna gari moja tu. Ikumbukwe kuwa Wilaya ya Liwale ina kituo kimoja tu cha polisi, hivyo kulingana na Jiografia ya Liwale gari la polisi ni muhimu sana hasa kwa Tarafa za Kibutuka na Makata ambako hakuna vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi kuzuia mikutano, kumekuwa ni jambo la kawaida sasa Jeshi la Polisi kuzuia mikutano bila sababu japo Sheria haisemi hivyo. Kwani Sheria inawataka watoe ulinzi kwani hata hao wanaoomba kufanya mikutano wajibu wao ni kutoa taarifa polisi na si kuomba kibali cha polisi, hivyo polisi kuzuia mikutano husika ni kukiuka sheria na kuwanyima raia kupata taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi kutumia nguvu kubwa, kumekuwa na matumizi makubwa sana katika kuwakamata washtakiwa au watuhumiwa japo bado hawajathibitka kufanya kosa analotuhumiwa nalo. Matumizi haya ya nguvu pasipohitajika yamekuwa yakiwaletaa hasara kubwa raia kwa kupoteza mali zao na hata wengine viungo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya nguvu hizi ni kuwafanya raia wachukie Serikali yao na Jeshi la Polisi kwa ujumla wake. Watuhumiwa wengi hufika vituoni wakiwa na majeraha makubwa na wengine kuibiwa mali zao.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi kubwa ya kuendelea kulinda amani na utulivu nchini. Naomba Jeshi la Polisi llendelee kuboresha maslahi ya watumishi wake ili waweze kuitenda kazi yao kwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba askari wa barabarani (*traffic*) wachukue muda mwinge kufanya kazi ya kuwaelimisha wananchi badala ya kutafuta makosa na kutoza faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iweke mkakati wa kujenga Vituo vya Polisi kila Kata hususan Kata za Singida Mjini.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maelezo yangu binafsi kuhusu hoja iliyopo mbele ya Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban mwaka mzima nimekuwa nikiomba Jeshi la Polisi likague Kituo cha Polisi Mlalo ili baada ya kukaguliwa tuweze kupata silaha. Nimejaribu kufuatilia jambo hili kwa muda mrefu lakini Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Niombe sasa Wizara, jambo hili lifanyike kwa wakati ili kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo letu la Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mlalo lenye Tarafa tatu, Kata 18, Vijiji 78 na Vitongoji 600 lina vituo viwili vya Polisi, lakini kwa bahati mbaya vituo hivyo havina silaha. Ni jambo haya sana hasa ikizingatiwa kuwa Jimbo lenyewe liko katika mpaka na nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Kilimo Mng'aro limechakaa sana kwa sababu limejengwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza. Pia, gereza hili lina upungufu wa wafungwa chini ya ikama. Uwezo wa gereza ni kuweza kuweka wafungwa 100 lakini kwa sasa wafungwa wapo 38 hivyo kulifanya gereza hili kufanya kazi zake chini ya ufanisi hasa ukizingatia ni gereza la kilimo.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia kuhusu Jeshi la Polisi. Zamani wananchi walliamini Polisi ni sehemu salama lakini Awamu hii ya Tano mambo yamebadilika, Polisi siyo sehemu salama tena maana matukio mengi ya vifo yametokea mikononi mwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kuna kijana anaitwa Allen aliuawa akiwa mikononi mwa Polisi Mjini Mbeya. Pia hivi karibuni mdogo wake Mbunge wa Tarime Vijijiini, Mheshimiwa John Heche pia amechomwa kisu akiwa mikononi mwa Polisi, tena akiwa amefungwa pingu. Matukio haya yanalidhalilisha Jeshi la Polisi kwa kukosa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia ukimya wa Jeshi la Polisi kuhusu matukio mbalimbali ambayo yametokea katika nchi yetu. Mfano, Mheshimiwa Nape Nnauye alitishiwa bastola mchana kweupe; Mheshimiwa Lissu alimiminiwa risasi 38 mchana kweupe Mjini Dodoma, kifo cha mwanafunzi wa *N/T* ambaye alipigwa risasi wakati wa kampeni za uchaguzi wa Jimbo la Kinondoni, mauaji ya Kibiti, kupatikana kwa maiti katika fukwe za Coco Beach, lakini mpaka leo hakuna taarifa yoyote kuhusu matukio haya. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake atolee ufanuzi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia suala la Askari Polisi kuwashikilia watumishi zaidi ya saa 48 bila kuwapeleka Mahakamani. Ni kwa nini Jeshi la Polisi linafanya hivi? Namwomba Mheshimiwa Mwigulu akija atueleze ni sheria gani ambayo inaruhusu Jeshi la Polisi kuwa-*detain* watuhumiwa zaidi ya saa 48 bila kuwapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yake katika kipindi cha bajeti cha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Wizara hii kwa kazi kubwa wanazofanya katika kuendelea kudhibiti vitendo vibaya, viovu vinavyofanyika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Lindi. Kwa kweli wamethibitisha uchakavu wa nyumba za maaskari wetu zilivyochochaka, inatia huruma sana. Naiomba sana Serikali katika nyumba hizi zitakazojengwa katika kipindi cha bajeti hii ya 2018/2019, tupate mgao wa nyumba kwa ajili ya Polisi wetu na Askari Magereza katika Wilaya za Lindi Manispaa na Wilaya ya Nachingwea; naiomba Serikali kusikia kilio chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

Ni lini Polisi watatoa *EFD Machines* wanapokusanya faini? Ni lini ombi letu la Magereza Babati kutugawia eneo la makaburi litatekelezwa? Ni lini Serikali itatupa fedha za kumalizia jengo la *RPC Manyara*? Ni lini Sheria ya Zimamoto itarekebishwa?

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu. Niwapongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu wake na Watendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa na muhimu ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kuchangia kwa kuzungumzia masuala ya Wilaya za pembezoni kama vile lleje ambako tuna changamoto nyingi za kiusalama kwa sababu tuko mpakani na Malawi na Zambia, pia, kuna mwingiliano mkubwa wa wageni toka Somalia, *DRC Congo*, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zetu ni kuwa lleje yenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,906 na yenye jilografia ngumu ya millima na mabonde na raia wake ambao wako mbalimbali sana na kwenye umbali mrefu katika kata na kata, kijiji na kijiji, ina kituo kimoja tu cha Polisi miaka takribani 44 ya Wilaya hii kongwe. Hiki ni kikwazo kikubwa kwa utoaji huduma, Kituo Kidogo cha Polisi cha Isoko wananchi wametumia nguvu zao kukijenga na kupaua. Tunaomba Serikali iwaunge mkono kukimalizia na kujenga nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya lleje ina upungufu mkubwa wa Askari, Wilaya nzima tuna Askari 58, karibu *ratio* ya 1:5,000 askari kwa wananchi kwa *projection* ya mwaka jana, hivyo kuhatarisha ulinzi na usalama. Kituo chetu kimechakaa mno kwa sababu ni cha miaka mingi mno. Tathmini tuliyofanya tunahitaji milioni 38 kufanya ukarabati wa kituo pekee kilichopo lleje. Tuna nyumba 10 za Askari ambazo zinahitaji ukarabati mkubwa na hazitoshi kwa mahitaji ya makazi ya Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha lleje kina upungufu mkubwa wa vitendea kazi, mafuta, spea tairi za magari na hata magari ya kufanya kazi na hiki ni kikwazo kikubwa kwa utendaji wa Askari wetu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu mno. Maslahi na vyeo vya

Askari wa lleje bado ni duni sana na kwa kuzingatia ugumu wa maisha ya lleje wanahitaji kuhamashishwa na kupewa stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyetu havipokei fedha ya kutosha kuendesha ofisi na hii inasababisha askari kuomba msaada wa Mbunge mara kwa mara ili waweze kufanya kazi. Tumeshawapatia mashine ya kudurusu ya kisasa, *laptop, printer* na *scanner*, vilevile nimechangia *ma-box* ya *rim* za karatasi, nimechangia matairu ya gari na kukarabati gari la Polisi, pia, nimechangia matengenezo mengine. Hii haipaswi kuwa kazi ya Mbunge, lakini kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa wananchi na mali zao imebidi iwe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya Jeshi la Zimamoto kuna haja ya kuhakikisha kuwa, kila jengo la biashara linajengwa liwe na ngazi ya dharura nje ya jengo kila ghorofa. Nyumba nydingi kwa sasa hazizingatii hili, tunataka Waziri atoe tamko kuhusu hitaji hili muhimu kwa usalama wa watu na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunamwomba Mheshimiwa Waziri aje kutoa tamko la kuagiza kila jengo, hasa la kibashara, kuwa na vitambuzi Moshi (*smoke detectors*) ili itoe taarifa ya awali kung'amu dalili za moto ndani ya nyumba, vilevile kuhakikisha vifaa vya kuzimia moto vinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Traffic Police* bado ni tatizo kubwa, kuna haja ya kuweka vifaa barabarani na kupunguza askari hawa ambao muda mwangi wanajali kuchukua rushwa badala ya kuelekeza watumiaji wa barabara kuzingatia usalama na kuwachukulia hatua madhubuti. Bado magari yasiyo na ubora wa kutumika yanaendeshwa, ilhali Askari Usalama wamejazana barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara itafute Mwekezaji wa kuja kuwekeza kwenye vifaa vya ukaguzi wa magari kabla ya kuyapa leseni; vilevile waweke kamera barabarani na kutumia teknolojia ya kuwezesha kutambua

magari yanayoendeshwa ili kutoa udhibiti na adhabu husika. Umefika wakati sasa ukaguzi ufanywe kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Polisi wetu hawajaweza kushughulikia ipasavyo matukio ya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia ambayo yanaongezeka hata kuathiri watoto wachanga. Tunamwomba Waziri aoneshe kuguswa kwakwe na hili ili wananchi hasa wanawake wapate faraja kuwa mateso wanayopata mikononi mwa wanaume wao na watoto wao yatashughulikiwa kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Kilwa wapo vijana wawili wamechukuliwa na vyombo vyaa dola (Polisi), vijana hao ni Ndugu Ali Mohamed Shari na Ndugu Yusufu Kiduka. Vijana hawa tangu wamechukuliwa hawajulikani walipo, wazee wao wananiulizia na wamenitura wanataka kujua wapo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, walikamatwa na Polisi tunahitaji wapelekwe Mahakamani. Pamoja na hawa waliokamatwa Kilwa, pia wapo wananchi wamekamatwa Wilaya ya Rufiji, pia nao hawajapelekwa Mahakamani na jamaa zao hawajui walipo, wengi wao ni viongozi wa Serikali na Chama cha Wananchi ambao ni hawa wafuatao:-

Ndugu Ziada Nongwa, Diwani Viti Maalum; Ndugu Moshi Machela, Mwenyekiti wa Kitongoji; Ndugu Jumanne Kilumike, Mwenyekiti Ikwiriri; Ndugu Kisinga Athumani, Mwenyekiti Kijiji na Katibu wa Vijana *CUF*; Ndugu Kazi Mtoteka, Mwenyekiti wa Kijiji; Ndugu Mtuku Astera, Katibu *CUF*, Kata Ikwiriri; Ndugu Khamisi Nyumba na mwanawewe Katibu *CUF*, Wilaya ya Rufiji; Ndugu Blasil Linyago na Mkewe; Ndugu Baruti Kongoi, Ikwiriri; Ndugu Konjoma Milanzi, Mfanyabiashara, Ikwiriri; Ndugu Abdala Mkuu na Ndugu Salum Mkuu, Mwenyekiti Mstaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hawa wote wamekamatwa, lakini hawajapelekwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Mheshimiwa Waziri nahitaji kujua wapo wapi na lini watafikishwa Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yako napenda kupata majibu. Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Kilwa, Kijiji cha Chumo, siku ya Ijumaa tarehe 21 Julai, 2017, Polisi walivamia msikiti wa Ali Mchumo usiku na kushambulia kwa risasi za moto na kusababisha kifo cha muumini Ismaili Bweta na kupoteza jicho kwa muumini Mbaraka Saburi. Je, Serikali inasema nini kuhusu wahanga hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani. Naomba kuwasilisha.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishaji vyeo Jeshi la Zimamoto; Askari walipandishwa vyeo baada ya mafunzo mwaka 2016 na walipewa barua za kupanda vyeo, lakini hawajabadilishiwa mshahara mpaka leo na badala yake kuna barua ya kufuta vyeo vilivyopanda. Naomba kujua lini Askari hawa watarejeshewa vyeo na mabadiliko ya mishahara yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Kituo cha Polisi Kati Geita; katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali iliahidi ujenzi wa kituo hiki. Naomba kufahamu lini ujenzi huu wa kituo cha Polisi Kati Geita Mjini utaanza, ikiwa ni pamoja na jengo la zimamoto na magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa magari, lipo tatizo kubwa la usafiri kwa Jeshi la Polisi Mkoani Geita. Mfano *OCD* Geita anategemea gari la *FFU* Kasamwa inapotokea ugeni wa viongozi hali za doria zimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mlundikano wa mahabusu na ubovu wa Magereza; hali katika Gereza la Geita ni mbaya sana, idadi ya mahabusu ni wengi na hii

imetokana na utaratibu mbaya wa kesi za kawaida ambazo zingeweza kumalizwa na wahusika, kulazimu kupelekwa Polisi na Mahakamani ambapo matokeo yake mahabusu mwenye kesi ya kuku kutumia gharama kubwa bdala ya faida inakuwa hasara. Naishauri Serikali kuleta mfumo utakaoondo watu kujazana mahabusu na magereza kwa sababu hili linasababisha mateso na rushwa.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama nchini. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kutoa tamko kwamba watu wawe mbele ya matokeo kabla hayajatokea kwamba yaweza kudhibitiwa, kauli hii ilikuwa ni wimbo tu kwa sababu Mhariri Mchambuzi wa Gazeti la Mwananchi alitoa taarifa kwamba, maisha yake yako hatarini anatafutwa na watu wasiojulikana. Leo Msemaji Mkuu wa Serikali anasema ni usanii na upuuzi mtupu, matokeo yake Mtanzania huyu amekimbilla nchi ya Finland kuomba hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anasema, miili ya watu inayookotwa inaelea majini ni ya wahamiaji haramu, leo mwili wa tajiri wa mabasi anayemiliki Kampuni ya Mabasi ya *Super Sami* umeokotwa kwenye Kiroba na wavuvi unaelea kwenye Mto Ndabaka, Wilayani. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa kauli yake haina mashiko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya chaguzi nchini; wakati Mheshimiwa Waziri anasema Serikali haiwezi kuvumilia kuona wananchi wake wanaumizana kutokana na matokeo ya uchaguzi kisha Serikali ikae kimya bila kuchukua maamuzi yoyote, leo wanachama kadhaa wa upinzani wamepigwa, wameumizwa na wengine kuuawa. Je, mbona Serikali imeshindwa kuchukua hatua yoyote juu ya wahalifu waliohusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anaposema kuwa ni aibu kwa nchi yenye vyama vingi vya siasa wananchi wake kufanyiana fujo, lakini kwa upande mwingine Serikali ya CCM, vyombo vya dola na taasisi za

Serikali bila aibu zinashiriki kikamilifu katika kukivuruga Chama cha *CUF*. Je, kwa nini Jeshi la Polisi haliheshimu sheria na taratibu za vyama nya siasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alitoa tamko la kuwa, watu waache tabia ya kuunganisha matukio na imani ya dini, siasa au chama. Matokeo yanayotokea Zanzibar kabla, wakati na baada ya chaguzi mbalimbali huwa Serikali na vyombo nya dola vinayahuishisha matokeo hayo kuwa, yametekelezwa na wafuasi wa Chama cha *CUF*, bila kufanyiwa uchunguzi, jambo ambalo husababisha wafuasi wa *CUF* kupigwa na kuumizwa bila hatia yoyote. Mheshimiwa Waziri tunaomba tabia hii ikomeshwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Makamanda Wakuu wa Vyombo nya Ulinzi na Usalama kwa kuandaa hotuba nzuri na Waziri kuwasilisha vizuri. Nampongeza Waziri na Watendaji wote kwa kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao unaimarika siku hadi siku, kudhibiti dawa za kulevyta, kudhibiti uhamiaji haramu na kukabiliana na majanga ya moto nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na kuipongeza Serikali kwa kupeleka fedha kwa ajili ya shughuli za kawaida na shughuli za maendeleo na kufikia kiwango cha asilimia 78 bado tatizo la upelekaji wa fedha za kutosha katika sekta ya Mambo ya Ndani jambo ambalo linasababisha kushindwa kutekeleza kikamilifu wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuingalia Wizara hii nyeti ya Mambo ya Ndani kwa jicho la pekee na kuwapelekea fedha kama zinavyopitishwa na Bunge kwa sababu kutofanya hivyo wanashindwa kutengeneza magari, kununua vipuri nya magari, kununua mafuta ya magari na kununua vitendea kazi muhimu kama magari na hasa magari ya zimamoto. Mfano, Makao Makuu hapa Dodoma magari ya zimamoto yapo mawili ambapo moja lipo uwanja wa ndege na lingine ndilo linalotegemewa katika Mkoa mzima wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi wa nyumba za Askari na vituo nya Polisi; pamoja na kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa makazi na vituo nya Polisi na pia kumpongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, tarehe 7 Aprili, 2018 wakati akizindua nyumba za Askari Mkoani Arusha alitoa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Askari ngazi ya chini, ambapo fedha hiyo itasaidia kujenga nyumba 400 katika mikoa yote nchini, tunamshukuru Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni Jeshi la Polisi na Magereza wafufue Kitengo cha Ujenzi ambacho kipo na kilikuwa kikifanya vizuri sana kwa sababu, kinao wataalam ambao kwa sasa wamepangwi kazi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo kutasaidia kujenga nyumba nyingi za Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto, tena kwa wakati na kwa haraka na kuokoa fedha nyingi, kwa sababu Jeshi letu la Magereza litatoa nguvu kazi. Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyumba za Askari zilizojengwa katika Mkoa wa Mara na Mwanza hazitumiki, ningependa kujua ni lini zitatumika? Pia, ningependa kujua kuna majengo na ofisi zimejengwa, lakini hazijakamilika,

ningependa kujua mkakati wa kukamilisha majengo hayo na katika bajeti hii ni fedha ngapi zimetengwa kwa ajili ya kuyakamilisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya Askari wetu, utaratibu wa upandishaji wa vyeo; pamoja na kupongeza majeshi yetu ya vyombo vya ulinzi na usalama na kuwa na utaratibu wa kanuni ya ajira na upandishaji wa madaraja, bado yapo malalamiko kwa baadhi ya Askari wetu na hasa waliokaa kwa muda mrefu ambaao wamefanya kazi kwa uaminifu na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upandishaji wa vyeo haukuzingatia muda wa mtu alivyokaa kazini, bali unazingatia elimu aliyonayo. Nashauri kauni hii itazamwe upya ili kuwapa askari waliofanya kazi kwa muda mrefu, kwa weledi, uaminifu na uadilifu mkubwa ili na wao wapewe kipaumbele katika kuwaongezea madaraka na hasa kwa kuzingatia kwamba majeshi haya yanawategemea watumishi wa kada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandishwa vyeo bila kurekebishiwa mishahara; lipo tatizo la askari kuongezewa madaraka bila kurekebishiwa mishahara, jambo linaloathiri ufanisi. Vilevile Askari anapostaafu anajikuta amepata fedha ambayo hailingani na madaraka aliyonayo, ningependa kujua hapa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo pia la baadhi ya Askari wanaostaafu kucheleweshewa malipo yao ya nauli na mizigo na fedha za kustaaafu kupitia mifuko ya jamii. ningependa kujua hapa tatizo ni nini? Lipo pia tatizo la baadhi ya askari kukatwa madeni zikiwemo fedha za mikopo ya elimu ya juu, wakati mwagine askari hana elimu ya juu na wala hakuchukua mkopo. Swali, ningependa kujua hapa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu posho ya chakula ya askari na posho ya vinywaji. Naipongeza Serikali kwa kuwapa posho ya chakula na posho ya vinywaji. Pia ningependa

kuju posho ya nyumba kwa Askari wanaoishi uraiani kwa nini hazilipwi na lini zitalipwa? Ningependa kuju ni lini Serikali itawapa Askari Zimamoto posho ya nyumba na kuwajengea nyumba za kuishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya askari. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa askari wetu ili wawe na weledi na uelewa wa pamoja katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuju askari wanaokwenda kuchukua kozi mbalimbali za usalama barabarani, upelelezi na kozi nyingine gharama za mafunzo hayo nani analipa kwa sababu zipo taarifa kwamba, baadhi ya askari wanaokwenda kila askari atakatwa 7,000/= kwa siku, fedha ambayo hana uwezo wa kuilipa na pia, kuendesha familia yake. Ningependa kuju utaratibu huu umeanza lini na kwa nini Askari akatwe fedha yake ya chakula kwenda masomoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki ya kuishi; kama Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyoeleza kwa kila binadamu, Mtanzania ana haki ya kuishi. Nasikitika kuona Jeshi la Polisi Tanzania limekuwa linakiuka Katiba ya nchi ambayo ni Katiba Mama au mwongozo ambao umewekwa na Bunge letu Tukufu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa haki na bila kuvunja sheria za nchi yetu ya Tanzania. Polisi wamekuwa wakivunja sheria za nchi mara nyingi sana kwa kukatiza maisha ya watu kwa kutumia silaha za moto, vitu vyenye ncha kali na mambo mengine kama vipigo kwa kutumia nguvu za ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa matukio haya ni Ndugu Aquilina Aquiline wa Chuo cha Usafirishaji yaliyotokea

mwezi Februari, 2018 Jijini Dar es Salaam. Pia mauaji yaliyotokea kwa mdogo wa Mheshimiwa John Heche, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, lakini nashukuru kuwa Polisi aliyehusika Tarime ameshafikishwa Mahakamani na naamini haki itatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Polisi wafuate sheria zitokanazo na Katiba ya nchi ambayo ndiyo mwongozo wetu na Polisi wenyewe wamekuwa wakikamata raia yejote anayekiuka sheria ya nchi, lakini wao wenyewe ndio wamekuwa mstari wa mbele kutotii sheria za nchi kuititia Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya usalama wa mtu na faragha; Jeshi la Polisi pia limekuwa na tabia mbaya sana ya kuingilia haki ya faragha na usalama wa mtu. Ni sawa Askari Polisi anaweza kukagua simu ya rala mara anapomtilia mashaka, lakini kwa siku za hivi karibuni imezidi, kwani Polisi baada ya kukagua simu au *laptop* ya mtu anabaki nayo kwa muda mrefu sana huku akiwa anafahamu *password* ya kifaa hicho. Hii ni hatari sana kwani simu au *laptop* inakuwa haina usalama tena kwa maana ya mambo yaliyopo ndani ya simu na kama inavyofahamika simu na mawasiliano yaliyopo kwenye simu ni siri ya mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Jeshi la Polisi likague simu hizi na *laptop* na kuzikabidhi kwa mhusika mara tu wanapomaliza ukaguzi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya usalama nchini; kwa sasa hali ya usalama wa nchi yetu siyo salama sana, kumekuwa na matukio ambayo hatukuyazoea nchini kwetu, ambayo ni watu kupotea, watu kutekwa na kuuawa. Wananchi wameingia tataruki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhoji uraia wa watu wanapoipinga Serikali, jambo hili linaleta sintofahamu kabisa hajjawahi kutokea toka tawala mbalimbali zilizopita, jambo hili halikubaliki kwani linajenga hofu miiongoni mwa

Watanzania ambao wanatumia haki yao ya Kikatiba kutoa maoni yao kulingana na mwenendo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wasiojulikana jambo hili limekuwa kama kichaka cha wahalifu kujificha kwani kuna matukio yamejitokeza hivi karibuni ambayo wahusika hawajatambulika na ndiyo wanapewa majina hayo ya watu wasiojulikana, ni vema Wizara ya Mambo ya Ndani wakatueleza hawa ni watu gani, wako wapi na wanafadhiliwa na nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya Polisi katika Mkoa wa Rukwa; kuna ujenzi wa vituo vya Polisi katika Jimbo la Kwela, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. Kama Mbunge nimetembelea vituo hivyo, Serikali nayo itimize wajibu wake kwani wananchi wamechanga mpaka lenta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Polisi kubambikizia watu kesi ni jambo ambalo linaondoa weledi kwa Jeshi la Polisi na mambo hayo yanafanywa na baadhi ya askari wasio waaminifu; ni wajibu wa Wizara kulitazama jambo hili kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondolewa kwa kanuni ambazo ni kandamizi kwa Polisi hasa wadogo wasiokuwa na nafasi zozote katika Jeshi kwani wanafukuzwa hovyo jambo ambalo linaweza kuongeza wahalifu mitaani, kwani watu hawa wanakuwa hawana kazi mtaani.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Askari Polisi; Serikali ichukue hatua stahiki za kukarabati na kuendeleza nyumba za Askari Polisi hususani Wilaya ya Ludewa. Kuna nyumba za Polisi zilianza kujengwa toka mwaka 2012, lakini mpaka sasa hazijakwisha wakati askari wanaishi uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Ludewa; Serikali ione sasa kuna haja ya kujenga kituo cha Polisi cha Wilaya kwani Wilaya hii ni ya siku nyingi toka tarehe Mosi Julai, 1975. Tuiombe sasa Serikali kufikiria

kujenga kituo cha Polisi kwani ongezeko la watu na uhalifu unaongezeka kadri muda unavyokwenda. Ni tumaini la wana Ludewa kuwa suala hili litapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majengo ya Magereza; Majengo mengi ya Gereza la Ibihi lilitopo Ludewa yamechakaa mno kiasi ambacho yanahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa sana, naomba Serikali kuliona hilo. Pia gereza hili la Ibihi ni gereza la kilimo ambalo lina ekari nyingi sana lakini lina changamoto kubwa ya kutopata trekta kwa ajili ya kulimia na kuleta ufanisi. Tayari gereza hili lilitishaomba kupewa mkopo wa trekta jambo ambalo mpaka sasa hawajafanikiwa. Niiombe Serikali kuliona hilo na wapewe trekta ili ifanye kazi kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uchakavu wa sare za Askari Magereza na wafungwa. Sare zao zimechaka mno, tunaomba Jeshi la Magereza kuliona hili kwani linaaibisha taasisi hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji; Serikali ijaribu kuiangalia Idara hii hasa katika upande wa ofisi na watumishi. Wilaya ya Ludewa haina ofisi ya Uhamiaji na pia watumishi ni wachache mno. Ludewa ipo mpakani mwa nchi hivyo kuwa na watumishi wa kutosha ni jambo muhimu kwani zipo dalili za kuwa na wahamiaji haramu. Pia idara hii ipewe vitendea kazi kwani Ludewa ina eneo kubwa la mpaka kuliko Wilaya ya Nyasa na Kyela. Wapewe magari, maboti, pikipiki na kadhalika kwani miundombinu ya eneo hili ni migumu mno.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Zimamoto; katika Jiji letu la Dar es Salaam panakuwepo na ongezeko kubwa la majengo na yaliyojengwa karibu sana na majengo mengine ni mrefu sana. Pindi linapotokea janga la moto tumeshuhudia sehemu nyingi nchini magari hayo huwa yanaishiwa maji. Pili, kwa majengo mrefu yaliyopo Dar es Salaam ni magari mangapi yanayoweza kutoa huduma ya kuzima moto mfano ghorofa ya mwisho kabisa ni ya ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma kwa sasa hivi ni Jiji na patakuwepo na ongezeko kubwa la watu na majengo je, Serikali imejipangaje kuongeza magari ya zimamoto Dodoma na nchi nzima na yawe ya kisasa na yenye vifaa vyote vya kuokolea maji, ngazi ndefu, chopa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makazi ya kuishi Askari Polisi; Askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Mfano Askari wa Barabaran unawakuta wapo barabaran siku nzima wengine kujificha vichakani kuvizia madereva wanaoendesha magari kwa mwendo unaopita *limit* kupelekeea kuhatarisha maisha yao. Hivyo, wakirudi nyumbani wanatakiwa wakute makazi mazuri waweze kupumzika na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha hata hapa katika Jiji la Dodoma bado zile nyumba za bati kuanzia juu mpaka chini (*full suit*) bado zipo Dodoma na Askari wetu wanaishi kule. Tukumbuke hali ya hewa hapa Dodoma ilivyo na joto halafu watu waishi kule. Bado vyoo ni vya kuchangia, kichumba kidogo na wana familia, huu si utu kabisa. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwajengea makazi yenye hadhi kwa Askari wetu kwa kuanzia na hapa Dodoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Askari wa barabaran (*Traffic*) watumie muda mwingi zaidi kutoa elimu kwa madereva na watumiaji wa barabara, madereva wa bodaboda, baiskeli hata watembea kwa miguu; ajali nyingi zinatokea tu kwa sababu wengi hawajui sheria za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona Askari wetu wakitumika kama wakusanya mapato badala ya kufanya kazi zao za msingi. Kazi za ukusanyaji mapato zifanywe na idara husika na hatuwezi kuendesha nchi kwa faini za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya amani nchini; pamekuwepo na matukio ya uhalifu unaofanywa na watu wasiojulikana mfano watu wanauawa, kuokotwa katika

fukwe za bahari *Coco beach* Dar es Salaam, watu kutekwa na kuteswa na tukio la hivi karibuni lilitotokea huko Tarime kwa kijana Chacha kupigwa kisu na Askari Polisi hadi kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitendo cha kulaani sababu raia hata wahalifu hukimbia Polisi wakijua ndiko wanakwenda kwenye mikono salama lakini haikuwa hivyo. Ni hatua gani Jeshi la Polisi imemchukulia Askari huyo ili lisitokee sehemu nyine? Je, ni lini Jeshi litatoa *report* hizo maiti zinazookotwa zinatokea wapi na uchunguzi unaonesha maiti hizo zilifanyiwa nini hadi kufariki (*cause of death*). Ni vizuri wananchi wakafahamishwa kinachoendelea ili utulivu uliopo usije ukaharibu amani tunayoiimba ambayo kwa sasa haipo.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, kwa kuniamsha salama siku ya leo na kuweza kutoa mchango wangu wa maandishi, vilevile nimtakie rehema kipenzi cha *Allah Mtume Muhammad (S.A.W)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *E.T.D Passport*; kwa muda mrefu Serikali ilikuwa ikiwawezesha Watanzania kusafiri kuititia Idara ya Uhamiaji kusafiri nchi jirani na zisizokuwa jirani kwa kutumia *ETD- Passport* kwa muda wa mwaka mmoja, lakini kwa bahati mbaya sana sasa hivi Serikali kuititia Idara ya Uhamiaji imebadilisha utaratibu huo na sasa *passport* ya *ETD* imekuwa ni *Single journey*, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa na manung'uniko makubwa kwa Watanzania ambao hawana uwezo wa kumiliki *E-Passport* ambayo kwa sasa gharama yake ni 150,000/= tofauti na ile ya zamani ambayo ilikuwa ni 50,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi usumbufu ambao unapatikana ni pale Mtanzania anapotaka kwenda nchi jirani kwa kutumia *ETD- Passport* na ikawa katika shughuli zake au matembezi yake anahitaji kuyafanya zaidi ya mwezi inakuwa vigumu kupata muda huo haiwezekani

na kwa sababu *passport* yake imeonesha *single journey* inakuwa vigumu kupata muda huo na badala yake hupatiwa muda wa wiki moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu juu ya hili ni kwamba, ni vema Serikali ikarudisha utaratibu ule wa zamani ili na Watanzania wanyonge waweze kuitumia fursa ya soko la Afrika Mashariki, hasa ukizingatia *ETD-Passport* kabla ya utaratibu huo ilikuwa inapatikana kwa gharama ya shilingi 10,000 tu lakini kwa utaratibu huu mpya ni Sh.20,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *passport* ya Afrika Mashariki; Serikali kupertia Idara ya Uhamiaji ilisimamisha kwa ghafla utoaji wa *passport* ya Afrika Mashariki bila maeleo yoyote kwa Watanzania, jambo ambalo wapo ambao walikamilisha utaratibu wote wa kupata *passport* hizo, pamoja na kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kulipia ili kupata *passport* hizo ili ziweze kuwarahisishia shughuli zao katika nchi za Afrika Mashariki hawakuzipata. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa kufanya majumuisho aniambie; je, kuna utaratibu gani kwa Watanzania ambao walikamilisha utaratibu na kulipia na hawakupata *passport* hizo. Je, kuna utaratibu gani wa kupatiwa huduma ambayo waliilipia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Police Marine*; kumekuwa na *operation* ambayo inaendelea baharini inayosimamiwa na vyombo vyta ulinzi wakiwemo *Police Marine*. *Operation* hiyo inahusu uvuvi haramu na ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni wavuvi wapatao 54 walikamatwa na meli inayofanya *operation* hiyo wakitokea bandari ya Shimoni nchini Kenya. Wavuvi hao baada ya kushikwa na meli hiyo walilizwa ninyi ni nani na mnatoka wapi? Wavuvi walijitambulisha wao ni Watanzania na wanatoka Dago Kenya na walithibitisha kwa kuonesha *passport* zao. Hata hivyo, pamoja na kuonesha *passport* waliambiwa watoke kwenye boti ambayo walikuwepo na walipelekwa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, pamoja na kushikwa wavuvi hao katika eneo ambalo ilikuwa ni karibu sana na Pemba waliomba ikiwa wana hatia basi wakabidhiwe kwenye Vyombo vya Ulinzi vya Pemba ili kama nisheria kuchukua mkondo wake na hasa ukizingatia vyombo vya ulinzi ni Muungano basi wakabidhiwe huko Pemba, lakini walikataliwa na kupelekwa Tanga, ambapo kutoka Tanga na maeneo ya Pemba waliokamatwa ilikuwa ni mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tena Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha aniambie je, kulikuwa na ulazima gani wa wavuvi hao kupelekwa Tanga badala ya Pemba? Mambo kama haya ndiyo ambayo yanaleta manung'uniko yasiyo na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kutumia nafasi hii kuainisha upungufu unaofanywa na baadhi ya Jeshi la Polisi. Polisi kazi yao ni kulinda wananchi na mali zao, mipaka ya nchi na pia kuhakikisha amani inapatikana. Pia kudhibiti uhalifu wowote unaoweza kutokea ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa imekuwa ni kinyume na hayo, Jeshi letu la Polisi limepoteza uaminifu kwa wananchi wake kutokana na vitendo wanavyofanya. Kwa mfano, wananchi kubambikiwa kesi awapo kituoni. Unakuta mtu ana kesi ya kupiga mwenzake anaambiwa ameiba na kuvunja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia mikutano ya vyama vya siasa kinyume na taratibu ya Katiba ya nchi. Hivyo ningeomba Waziri mwenye dhamana aelekeze Jeshi la Polisi majukumu yao halisi na siyo vitendo vya uonevu wanavyovifanya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wanapenda rushwa na kuchelewesha kesi Mahakamani sababu wanachopewa

hakiendani na kazi wanazofanya. Hivyo naomba waongezewe mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na makazi ya baadhi ya askari nchini hayaridhishi na yanaenda kinyume na mila na desturi ya nchi yetu. Unakuta mtu anaishi kwenye chumba kimoja na ana familia, chumba kinatenganishwa na pazia au ma-box. Je, hayo ni maadili gani? Hao askari wanatembelewa na ndugu zao, uhuru hawaupati kabisa. Namwomba Waziri, Mheshimiwa Mwigulu jambo hili litazamwe kwa makini japo wakirudi majumbani kwao kupumzika wapumzike vizuri ili wakirudi kazini warudi na nguvu nzuri.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa na nzuri ya kulinda na kudumisha amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Waandamizi wake kwa hotuba nzuri ya kiwango na kwa kazi nzuri wanayoifanya. Baada ya pongezi, naomba sasa nichangie hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuhoji yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hati za dharura za safari, naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie kwa nini hati za dharura za safari kwa sasa zinatolewa kwa *single journey* badala ya *multiple trips* kwa muda wa mwaka mmoja kama zamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wengi wa wasafiri wanaokwenda nchi za jirani hususani Kenya kwa upande wa mpaka wa Namanga Wilayani Longido ni Watanzania maskini na wajasiliamali. Je, Serikali haioni inawakandamiza na kuwasababishia usumbufu usio wa lazima wananchi ambao watahitaji kufanya safari kadhaa kwenda na kurudi nchi ya jirani ndani ya muda mfupi au mara

kwa mara, kwa mfano wanaokwenda kwenye masoko ya *County* ya Kajiado na Nairobi kila wiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa hivi kwa wananchi wenyehaja ya kwenda Kenya angalau mara moja kila wiki na ambao ni maskini tu wasio na pesa kubwa wanalazimika kuomba mpya kila wiki na wanalazimika kuwasilisha upya viambatisho lukuki (Vyeti vya kuzaliwa vya Mwombaji na wazazi, vitambulisho na kadhalika) ambavyo mara nydingi hawana na hasa kwa jamii yetu ya Kimasai ambao wengi hawana vyeti vya kuzaliwa. Utaratibu wa sasa unaleta adha kubwa kwa wasafiri maskini na hivyo naomba Serikali irejeshe *Multiple Trips Travel Documents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa kutoa hati za dharura za safari mpakani. Naomba kuishauri Serikali iboreshe mazingira ya wananchi wanaohitaji kusafiri nchi za jirani kwa kutumia hati za dharura waweze kupewa pale mpakani tofauti na sasa ambapo wanalazimika kusafiri kwenda Makao Makuu ya Wilaya kupata Hati hizo ambazo uhai wake ni kwa safari moja hata kama atahitajika kurudi mara kadhaa ndani ya wiki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurahisisha upatikanaji wa Pasi za Afrika Mashariki; kwa kuwa hati za dharura za safari ina adha kubwa na gharama kwa wasafiri wanaohitaji kusafiri na kurudi ndani ya muda mfupi, watengenezewe mazingira ya kuweza kupata pasi za Afrika Mashariki zenyewe uhai wa muda mrefu palepale mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo kwa sasa upatikanaji wa pasi Afrika Mashariki ni mgumu kwani ni mpaka upeleke maombi Makao Makuu ya nchi na inachukua muda mrefu kabla ya kutoka. Kwa kuwa, Wilaya ya Longido ni ya mpakani na kuna haja ya kuiwekea ulinzi wa kutosha, naomba Serikali itujengee angalau kituo kimoja cha Polisi katika kila Tarafa hasa zile zinazopatikana Kenya ikiwemo Tarafa ya Katumbeine na Engarenaibor.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wilaya ya Longido ina vituo vitatu vya Polisi kimoja mpakani Namanga, kimoja Mjini Longido na Kata ya Kamwanga. Kwa uhaba uliopo wa vituo vya usalama wa raia, katika Tarafa ya Ketumbeine, karibu kila mwaka majambazi huteka watu na kuwapora mali. Hivyo, kuna haja kubwa ya kujenga kituo cha Polisi katika Tarafa hiyo hasa Kata ya Mairugoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. IKUPA S. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Magufuli kwa miongozo yake ambayo imepelekea nchi yetu kuendelea kuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchomba na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Masauni kwa kazi kubwa wanazozifanya na jinsi wanavyojitoa kwa ajili ya Taifa letu. Baada ya pongezi hizo nina maombi au ushauri ufuatao kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; zoezi la ukamataji mtu mwenye ulemavu unapotenda kosa sambamba na uwekwaji ndani (mahabusu). Mikataba ya Kimataifa tuliyosaini kama nchi sambamba na sheria na sera ya watu wenye ulemavu inataka kuwe na utofauti wa ukamataji wa nguvu inayotumika kati ya mtu mwenye ulemavu na asiye na ulemavu. Pia mtu mwenye ulemavu awekwe kwenye mahabusu au magereza inayoendana na ulemavu wake, miundombinu iwe rafiki kwa watu wenye ulemavu, mahabusu na magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; vibali vya mikutano ya hadhara vizingatie kundi la watu wenye ulemavu. Utollewaji wa vibali vya mikutano ya hadhara uzingatie uwepo wa ama matumizi ya lugha ya alama. Mwombaji kibali aoneshe kama kunakuwa na mkalimali ama wakalimali kwenye mkutano wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na utaratibu pia wa kutenga maeneo maalum ambayo yatatumika ama yatakaliwa na watu wenye ulemavu kwenye mikutano hii, hii itawafanya watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu kwenye mikutano hii tofauti na ilivyo sasa ambapo ushiriki wao ni mdogo kwa kuhofia usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; vitambulisho vya Taifa viwe na kipengele kinachoonesha ama kumtambua mtu mwenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia upande wa Mawaziri na tunaanza na Mheshimiwa Waziri Jafo dakika 10. Jiandae Profesa Kabudi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu wake, lakini kwa Wizara yote kwa ujumla wake kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya. Nami nasema hivyo nikijua wazi kwamba suala la kulinda amani ni jambo lenye changamoto kubwa. Ni Wizara ambayo kwa kweli niwapongeze wamefanya kazi kubwa sana na wanaendelea kufanya kazi kubwa. Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu ya kutosha kuhakikisha kwamba suala la amani ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika nafahamu kwamba hakuna mbadala wa amani. Kwa hiyo, suala la usalama wa watu ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwigulu na timu yake nawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nita-reserve muda kwa wenzangu wengine, nitaongea kwa ufupi sana. Kulikuwa na hoja ambayo ilikuwa ikijitokeza hapa kuhusu suala zima la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa utaratibu

ambao imeonekana kuna kesi mbalimbali zimejitokeza kuwaweka watu katika ule utaratibu wa masaa 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 1997, Wakuu wa Mikoa wamepewa mamlaka mbalimbali katika kifungu cha (7) na Wakuu wa Wilaya ni kifungu cha 15, kwamba pale ambapo saa nyingine wanaenda katika tukio, au kuna jambo limeonekana kwamba kuna uvunjifu wa amani na suala la kijinai, basi Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya inawapa nafasi. Lengo kubwa ni kumweka yule mtu chini ya usimamizi fulani kwa ajili ya kuepusha madhara hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali hapa, inaonekana sheria ile inatumika visivyo. Hata hivyo, jambo hili limejitokeza katika maeneo mbalimbali ndiyo maana ofisi yetu illamua kuchukua jukumu maalum kwa ajili ya kutoa maelekezo maalum hasa kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwamba sheria ile iendelee kutumika kwa kadri maudhui yake yalivyokusudiwaa, lakini tusi-over *do kinyume* cha taratibu. Tuliweza kutoa maelekezo hayo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, lakini hata hivyo tumeamua kuanzisha zile *session* maalum kwa ajili ya mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hata humu Bungeni, sote sisi ni Wabunge, lakini wote hatu-*act* kwa kufanana. Kuna style mbalimbali za utendaji wetu wa kazi, ndiyo maana kati ya Wabunge tuliokuwepo humu kila mtu ana sarakasi zake za utendaji wake wa kazi. Kwa hiyo, katika njia moja au nyingine, wakati mwingine kuna upungufu wa kibinadamu kwa baadhi ya viongozi inawezekana, lakini siyo kwamba ndiyo jambo la kila kiongozi afanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jambo hili najua sheria ipo, lakini tumeendelea kutoa maelekezo mbalimbali hasa pale tunapoona kwamba kuna taratibu kidogo za kisheria zinakiukwa tunatoa maelekezo haya. Kwa kuwa sasa hivi tuko katika mchakato wa kumaliza mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa ambapo tumemaliza kwa Wakuu wa Wilaya hapa

katikati na tunaenda katika *session* kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa, ni imani yangu kwamba utafika muda katika haya mambo ambayo tunaona kipindi kirefu wakati mwingine kuna utaratibu kidogo umekiukwa, naamini wote tutakuwa katika mstari mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kuwasih i hasa Watanzania wote kwa ujumla wetu kwamba mara nyingi sana tutii utaratibu wa sheria ambapo naamini haya yote tukiya fanya kwa umoja wetu, tutaweza kuepuka migogoro mingi sana ambayo inatokea katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo tu, kuweza kutoa ufanuzi katika maeneo hayo. Kubwa kama nilivyosema mwanzo ni kwamba niwasih sana hasa Wabunge wenzangu na viongozi wengine, kwamba mara nyingi sana katika utendaji wetu wa uongozi na maisha yetu tuweke suala zima la ustaarabu na maisha ya kawaida na kuheshimiana. Naamini kama viongozi wa Kitaifa na watu wa aina mbalimbali kila mtu akijua mipaka ya kanuni ile ambayo nasema siku zote STK - Sheria, Taratibu na Kanuni itakuwa imetuwezesha sana kuishi katika Taifa letu tukiwa katika hali ya usalama na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Niseme kwamba naunga mkono hoja hii asilimia zote mia moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Iko hoja nyingine kwanza Mheshimiwa Waziri Jafo, hii *fire* ilikuwa chini ya Jiji la Dar es Salaam na kulikuwa na mkataba kati ya Jiji la Dar es Salaam na *JICA* kwa masharti ya kujenga Kituo cha *Fire* na Japan wataleta vifaa vyote bure. Ndiyo Serikali wakajenga pale Mchicha. Sasa badala ya Waziri hapa kununua magari wakati huku yako magari ya bure, masharti yao ni jengo.

Pili, Wajerumani, *Hamburg* wako tayari kuanzisha Chuo cha *Fire Academy*. Sharti lao ni ardhi tu. Naomba wasiliana na Jiji la Dar es Salaam, mshirikishe Waziri tutapata

Chuo *Southern Sahara* hakuna, ambacho kitafundisha na kitaleta vifaa kusaidia *Fire Brigade*. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, nafikiri nawe unaskia. (*Makof*)

Mheshimiwa Kabudi, jiandae Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani, *Engineer Masauni*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni ngumu na nzito kama ilivyo Wizara ya Ulinzi. Unapozungumzia Polisi na unapozungumzia Jeshi unazungumzia *coercive instruments of the State*. Hiyo *fact*, ni lazima tufahamu, *we are dealing with coercive instruments of the State and which are indispensable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukiisoma Biblia hasa Agano la Kale na hasa Zaburi, Wanajeshi na Walinzi wamependelewa sana na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa uliza wataalamu wa maandiko, kwa nini inazungumzia Mungu wa Majeshi, Majeshi, Majeshi? Wakasema hata huko kulikuwa na vurugu na ndiyo maana ulinzi uliwekwa ndani na nje na ibilisi alipoasi akatupwa huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, daima watu ambao kazi yao ni ulinzi wa milki iwe ni ulinzi wa ndani wa milki au ulinzi wa nje wa milki, lazima watumie nguvu wakati mwingine inapolazimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni lazima wafanye hayo ndani ya mujibu wa sheria. Pia ni lazima wote tufahamu *these are coercive instruments of the State*. Wengi hapa mmesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine, mmesoma *Development Studies (DS 100)*, hayo ndiyo mliyofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vyombo ambavyo ni *coercive instruments of the State* ni lazima uviendee kwa namna inayostahili. Ukienda kinyume, vitachukua hatua kwa sababu ya kulinda Katiba. Zaidi hivyo ndiyo vyombo pekee vinavyoapa hata kufa ili kulinda nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeapa kuiheshimu Katiba, lakini wao pamoja na kuapa kuiheshimu Katiba, wamekwenda mbali zaidi, ndiyo peke yao wanaoapa katika viapo vyao, kuna kufa kwa niaba ya nchi. Ila hiyo haina maana wafanye mambo kiholela, lakini daima tujue, nasi tumepata bahati, tumepita katika kipindi kigumu mwaka jana. Watanzania tunasahau haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nytingine za Ulaya nami nimekuwa na bahati, nimekaa miaka michache Ulaya, miaka 10 michache sana, lakini katika vipindi vigumu. Walifika zile nchi zilitangaza hata *state of emergency*. Mamlaka hayo Rais anayo ya kutangaza hali ya hatari chini ya Ibara ya 32 kwa eneo lenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuchukua hatua ya kudhibiti hali ya Kibiti na Rufiji, hatukufika mahali Rais wa Jamhuri ya Muungano kutangaza hali ya hatari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Italia, Ujerumani na Uingereza, walipopitia katika hali hii na sitaki kuitaja nchi, Askari wao walipewa haki ya *ku-shoot on site*, sisi hatukufika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tuvipongeze vyombo hivi kwa *ku-contain* hali ngumu lakini bila kulifikisha Taifa ama Rais kutumia mamlaka yake ya Ibara ya 32 ya kutangaza hali ya hatari kwa eneo la Rufiji, Ikwiriri au kufika kutoa amri ambayo ingekuwa na madhara. Tuwapongeze, tuwape nguvu. Kwa kufanya hivyo, wamekufa. Polisi wamekufa; *cold blood on behalf of the United Republic of Tanzania*. Mimi na ninyi hatukuapa kufa.

Wao wameapa kufa. Watu walioapa kufa kwa niaba yenu muwastahi, lakini zaidi muwaombee Mwenyezi Mungu kwa sababu ndio peke yao wamechukua dhamana hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio watu wa kuwabagaza, kuwazoza, kuwakejeli, kuwadharau na kuwadhihaki. Mtakatifu Agustino wa Hippo aliaonya watu wa *Carthage* walipoanza kuwa na majivuno, akasema siku wanaosafisha mitaro watakapoacha kusafisha mitaro ndipo watu mtakapoja umuhimu wao. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesimama ili kutoa maelezo ya mambo mawili ambayo yameelekezwa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo nadhani yanaangukia katika Sekta ya Sheria. Haya ni yale yanayohusu kesi ya Mashehe wa Uamusho wa Zanzibar na suala la Akwilini. Mambo haya yote mawili hayaihusu Wizara ya Mambo ya Ndani. Mambo yote haya mawili yanamhusu Mkurugenzi wa Mashtaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Watanzania wote tuelewe, Mkurugenzi wa Mashtaka ameanzishwa kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 59B ambayo inaeleza wazi kabisa kwamba:

*"kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atateuliwa na Rais kutoka mionganini mwa watu wenye sifa zilizoainishwa katika Ibara ndogo ya (2) na Ibara ya 59 na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka 10. Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasomee Ibara ya (4):-

*"Katika kutekeleza mamlaka yake Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote na atazingatia mambo yafuatayo:-*

(a) *Nia ya kutenda haki;*  
(b) *Kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki;*  
na  
(c) *maslahi ya Umma.*"

Ibara hiyo hiyo unaikuta katika Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 56A ambayo inaeleza wazi kabisa, hakuna anayeruhusiwa kumwingilia *DPP* hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata Zanzibar Ibara ya 56A inatamka wazi na niende kifungu cha nane (8) na chenyewe kiko *very clear*, "Hakuna mtu anayeruhusiwa kumwingilia Mkurugenzi wa Mashtaka."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Bunge hili hili llipitisha Sheria Na. 27 ya mwaka 2008, *The National Prosecution Services Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 19 ya kifungu hicho iko wazi kabisa. Mkurugenzi wa Mashtaka ana-*enjoy security of tenure* kama anavyo-*enjoy* Jaji wa *High Court* na ndiyo maana Rais hawezi kumwondoa *DPP* akishamteua. Ili amwondoe *DPP* na akidhani amefanya makosa au amekwenda kinyume, ni lazima amuundie *Tribunal* na *tribunal* hiyo ni lazima iwe na Majaji watatu na mmoja awe wa *Court of Appeal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, aliondolewa na kupandishwa cheo kile kile cha *Security of Tenure*, huwezi kumshusha chini. Sifa yake ni kama ya *High Court Judge*, ndiyo maana huwezi kumtoa *DPP* kumpeleka chini. Ndiyo, hawezi na pale hakuondolewa, amepandishwa.

Mheshimiwa Lema, uwe na adabu! (*Makofii*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwonye Waziri asi...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nakuheshimu sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema kaa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nakuheshimu, *you know / respect you.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri zungumza na kitii.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Haya, tuheshimiane.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa *order.*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Mashtaka ana uhuru kamili wa kufungua mashtaka na kuyafuta, ndiyo maana katika haya mambo mawili ambayo nataka kuyazungumza na kwa sababu Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuingia Bungeni nimemwomba leo anipe maelezo ili nilieleze Bunge hatua anazozichukua kuhusu suala la Mashehe wa Uamsho na suala la Akwilini, yeye hawezi kuja hapa. Alikuwa Singida nimemwomba aje leo Dodoma ili atoe maelezo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kipindi hiki hakuna taarifa, kaa Mheshimiwa Salome.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mashehe wa Uamsho wa Zanzibar ni suala nyeti sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ni suala ambalo linahusu tuhuma za Mashitaka ya Ugaidi, mashitaka ambayo ni mazito na adhabu yake ikiwa watathibi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabudi, subiri dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge, toka jana mnataka majibu ya Serikali. Mmejaza maswali, mnajazwa majibu, mnaleta fujo sababu yanawaingia. (*Makofii*)

Sitaruhusu Mwongozo wala Taarifa mpaka Serikali wamalize. Sababu mliuliza na Serikali imekuwa *very fair*, sasa wanajibu mnaanza ku-*react*, nje na utaratibu. *Issue* ya muda wake anachozungumza haiingiliani na nyie. Wengine mmechangia mliviyotaka, wengine mambo mnayoyajua, naye ana nafasi ya kuchangia, kujibu yale anayotaka kuyajibu. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nategemea *order* ndani ya Bunge. Mheshimiwa Waziri endelea na muda wako dakika zako mbili nimekutunzia. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Unajua upya wangu unanisaidia kujua nani ni wajuvi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, *please!* Mheshimiwa Waziri, *address* kitii.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Kwa hiyo, jambo hili nataka niwaambie Watanzania kwamba Serikali inatambua uwepo wa kesi hii na kuwa imechukua muda mrefu Mahakamani. Kwa hiyo, ni nia ya dhati ya Serikali kuona kuwa kesi hii inafikia mwisho. Hata hivyo ucheleweshwaji wake unasababishwa na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme ni bahati mbaya sana watu tunaowajadili sasa wana heshima na hadhi ya Mashehe, lakini hawakuingizwa kwa sababu ya heshima ya hadhi ya Ushehe, ni kwa sababu kuna tuhuma za ugaidi. Tuhuma hizi ni lazima zipelelezwe. Kesho na keshokutwa akitokea mwanasiasa au nani

ameshetumiwa, lazima yafanyiwe uchunguzi. Kwa sababu mwisho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungala, hebu kuwa na heshima ya Bunge.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu adhabu yake ni kubwa na ndiyo maana Mashtaka ya Mauaji na mashtaka ya aina hii upelelezi wake unachukua muda mrefu ili mjiridhishe kabisa, mnapotapeleka Mahakmani kweli uko ushahidi unaotosha. Kwa sababu baada ya hapo wakitiwa hatiani adhabu yake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kesi hii upelelezi pia umefanya nje ya nchi ambapo tumeomba baadhi ya taarifa na vielelezo ili viletwe visaidie katika kesi hiyo. Ndiyo maana Mwendesha Mashtaka kupitia ofisi yangu ambayo ndiyo ina mamlaka ya kusaini hizo *documents* za kuomba nchi nyininge zitusaidie kuleta ushahidi, kazi hiyo imekuwa inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inachukua hatua za kuharakisha upelelezi huo ili ukamilike mapema iwezekanavyo. Ndiyo maana nimesema hivi leo *DPP* alikuwa Singida nimemwita ili nipate maelezo haya ya kiliarifu Bunge lako. Naamini mambo haya yakikamilika, basi hatua za kisheria zitachukuliwa. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA,  
BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri, ndugu yangu

Mheshimiwa Lameck Mwigulu, *Doctor* kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. *Doctor* nakupongeza sana. Pia nampongeza sana Naibu Waziri Mheshimiwa *EngineerMasauni*.

Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi jambo ama kiatu usichokivaa huwezi kujua maumivu yake. Nasema hivi kwa sababu gani? Kuongoza Wizara ya Mambo ya Ndani na kuhakikisha kwamba misingi ile ya usalama wa raia inasimamiwa mahali ambapo unawasimamia binadamu wenyewe hulka na tabia tofauti, kwa kweli ni kazi ngumu na ndio maana nasema ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu na Naibu wake wanapaswa kupongezwa kwa kazi hii wanayoifanya katika Taifa letu; na sio wao tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwa dhati ya moyo wangu, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Kamanda Sirro na timu yake ya Jeshi la Polisi katika nchi yetu ya Tanzania. Ninaposema hivyo, sitaki kumaanisha kwamba askari wetu wote labda ni wazuri, hapana. Ni lazima Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, naomba niseme na wala ninaposema haya sitaki kumaanisha kwamba Serikali yetu eti inafurahia askari labda mmoja kwa kutokufuata utaratibu na sheria, akasababisha matatizo makubwa kwenye nchi yetu, hapana. Serikali haisemi hivyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka wote tukubaliane, kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi kwa namna yoyote ile ni lazima tuwapongeze, tuwaunge mkono na tuhakikishe kwamba tunawatia moyo katika kazi hii ngumu walijonayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi amesema hapa, wameapa kuilinda nchi na wawe tayari hata kufa kwa ajili yetu. Jambo hili siyo dogo, ni jambo zito sana. Kwa hiyo, hata sisi kama Wawakilishi wa Wananchi, tuna kila namna na sababu ya kuwapongeza askari wetu kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa raia katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema maneno kidogo tu, labda huko mbele nitaomba mwongozo wako baadaye kidogo kwa sababu Mheshimiwa dada yangu Mheshimiwa Mary Muro wakati anachangia amesisitiza sana kwamba kila jambo bayo linalotokea kwa Jeshi la Polisi, kila akifuatilia anaambiwa kwamba ni maagizo kutoka juu. Hatupendi kuwe na watu wanaharibu halafu wanasingizia ni maagizo kutoka juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ili tuweze kushughulika na hao watu wanaoharibu taswira ya Taifa letu, tutaomba angalau tuambiwe tu mmoja ama wawili wanaosema hayo maagizo kutoka juu ili watupe tu ushahidi wa mtu mmoja au wawili kusudi tusichafue taswira ya Jeshi letu la Polisi katika nchi yetu ya Tanzania. Nadhani huko mbele kwa kweli tuondoe jambo hili. Tukiliondoa nadhani tutaweza kulifanya jeshi letu libaki katika misingi ya heshima yake. Hivyo, baadaye tutaomba tu mwongozo Mheshimiwa Dada Mary atusaidie tu ili tuweze kuwa kwenye nafasi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza sana hapa masuala ya Vyama vya Siasa na nampongeza sana mdogo wangu Mheshimiwa Upendo Peneza, alizungumza Ibara ya tati (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alitusomea kwamba Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini yenye kufuata Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Ni kweli kabisa Ibara ya tatu (3) inasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda Ibara ya 3(2) inasema:-

*"Mambo yote yanayohusu uandikishaji na uendeshaji wa Vyama vya Siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajilli hiyo."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sheria iliyotungwa na Bunge *Cap 258* ambayo ndiyo inasimamia uhuru huo wa

Vyama vya Siasa vyote vilivyosajiliwa katika nchi yetu ya Tanzania. Ukienda kwenye kifungu cha 11 cha hiyo Sheria ya Vyama vya Siasa kwenye suala la mikutano ya hadhara, limetolewa maelezo mazuri sana tu. Maelezo haya kama vyama vyote vya siasa vingekuwa vinayafuata, tusingefika katika hii migogoro na kuwasababishia Polisi kama ndio vyanzo vya kuharibu amani katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na ushauri wako uliousema asubuhi, Waheshimiwa Wabunge tukiweza kuisoma katiba kwa ujumla wake, lakini tukaweza kusoma na sheria zilizotungwa kwa mujibu wa Katiba, ninaamini kabisa hakuna mtu ambaye ataingia kwenye mgogoro na Jeshi la Polisi kwenye nchi yetu ya Tanzania. Kwa mfano, kifungu cha (5) cha Katiba, kinaeleza kabisa haki ya kupiga kura na uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu wa kisheria wa uchaguzi uliowekwa, baada ya uchaguzi Jenista anakuwa amechaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na mwagine, kila mtu anakuwa tayari ni mwakilishi kwenye Jimbo lake husika. Inapendeza; na kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea na hasa kwenye sheria hii, nimesema kifungu cha 11 ukisoma, kila Mbunge awajibike kwenye Jimbo lake kwa wananchi waliomchagua. Ukishachaguliwa kwenye Jimbo husika, yapo mambo mengi ambayo wananchi wako wanatarajia utawawakilisha inavyopasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukisoma kifungu hicho cha 11 nenda kwenye kifungu kidogo cha (2) utapata maelekezo kabisa hapa, wajibu wa Polisi kutumia sheria walizonazo katika kusimamia masuala yote ya mikutano ya hadhara; iko wazi kabisa na wala haihitaji ugomvi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwetu sisi Wanasiasa wote kutambua haki za Kikatiba lakini kwenda kwenye wajibu wa Kikatiba kama Ibara ya 25 ya Katiba inavyosema, kila mtu ana haki lakini ana wajibu katika nchi

yetu kuhakikisha anazingatia sheria za nchi zilizowekwa kwa misingi ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba sana Vyama vya Siasa vifanyayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, vijielimishe zaidi kuhusu katiba tuliyonayo katika nchi yetu ya Tanzania; pili, vijielimishe kuhusu maana na muktadha wa sheria ambazo zimetungwa kwa kuzingatia Katiba tuliyonayo; na tatu, Vyama vya Siasa vijifunze utii wa sheria bila kushurutishwa. Tukifanya hivi nadhani tutaweza kuwa tunaenda vizuri na hatutakuwa na migongano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Siasa vikubali kuwa sheria kwa kweli ni msumeno na itakata kila chama; iwe ni Chama cha Mapinduzi, CHADEMA, CUF, ni kila mahali. Ni lazima tunapofika kwenye suala la kuheshimu sheria, kila kiongozi na kila chama kijue kwamba kina wajibu wa kuheshimu sheria kwa mujibu wa Ibara ya 25 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitafakari sisi kama viongozi, tumepewa dhamana, tuna kila namna ya kuheshimu dhamana tulizopewa na wananchi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeaminiwa, lakin tunategemewa na Watanzania. Tunapokiuka miiko ya kisheria na dhamana tulizopewa, hatutendei haki dhamana tulizopewa wala hatutendei haki Katiba wala sheria ambazo tumezitunga wenyewe Wabunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, navipongeza vyama vile ambavyo kwa kweli vimeonyesha ukomavu wa kisiasa. Ukiangalia kama kaka yangu Mheshimiwa Mbatia na chama chake huwezi kukuta kwamba kimekuwa na migogoro; na vyama vingine vingi. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba viko vyama unavipima tu na unaona kwamba vimetambua hii

mipaka ya demokrasia ilivyo, sheria tulizonazo na Katiba ya nchi yetu ya Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuvihimiza vyama kwa mujibu wa sheria tulizonazo na kwa mujibu wa Katiba, hakika tunapaswa kuheshimu sheria, tunapaswa kuheshimu Katiba tuliyonayo. Tukifanya hivyo, tutawawakilisha wananchi wetu vizuri sana na hakutakuwa na haja ya kugongana na vyombo vyovyote vinavyosimamia usalama wa raia katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, /GP na timu nzima ambayo inasimamia usalama katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Mheshimiwa Engineer Masauni, dakika 25.

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa na imani nami kwa nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa miongozo ambayo wanaendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Namshukuru vilevile Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Watendaji, Makamanda na Maofisa wote waliopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi nikianzia na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Vikosi na Taasisi mbalimbali kwa ushirikiano wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishukuru sana familia yangu kwa ujumla pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni kwa kuendelea kuniunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze moja kwa moja kuchangia mada ama maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yaliwasilishwa kwa njia ya maandishi na kwa njia ya kuzungumza. Ili kuokoa muda, naomba niwatambue Waheshimiwa hawa Wabunge ambao wamechangia baada ya kutoa ufanuzi wa hizi hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pamoja natarajia kuzungumzia mambo kama manne kama muda utaruhusu. Kwanza kabisa naomba nizungumzie suala la usalama barabarani. Hii ni moja katika hoja ambazo zimeibuka kwa kiwango kikubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Nachukua fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wanaonekana wanaunga mkono jitihada za Serikali za kupunguza ajali nchini ambazo zimekuwa zikipoteza maisha ya Watanzania wenzetu na wengine kuwaacha vilema kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inadhihirisha sasa hivi katika Bunge letu Tukufu kuna Chama cha Mabalozi wa Usalama Barabarani chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Adadi. Nawapongeza sana kwa jitihada hizo. Kuungwa mkono kwao, kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge kumechangia leo hii kusimama mbele yenu tukijivunia mafanikio makubwa sana ambayo tumefikia kwa kupunguza ajali hizi chini kwa wastani wa asilimia 35.7 toka mwezi Julai, 2017 mpaka Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi, katika miaka ya nyuma hapa tulikuwa tunashuhudia ajali nyingi zimetokea hasa mwisho wa mwaka, watu wengi walikuwa wanafariki lakini sasa hali hiyo imepungua kwa kiwango kikubwa. Mafanikio hayo yametokana na kazi kubwa ambayo tunaifanya kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupertia Baraza la Usalama Barabarani na Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi tuliandaa mikakati kabambe ya kupunguza ajali hizo ambapo leo hii tunazungumzia utekelezaji wa mkakati wa awamu ya tatu, tunaenda nao. Katika kila mkakati, tunaangalia upungufu wa mkakati wa kwanza kurekebisha tunapoingia katika mkakati unafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge leo hapa yatasaidia sana katika kurekebisha upungufu uliojikoteza ili mkakati wetu wa awamu ya tatu tunaoenda nao uweze kuwa na mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujazungumza suala la ajali barabarani lazima tujue vyanzo vya ajali barabarani ni nin? Vyanzo vikubwa vya ajali barabarani ni vitatu. Cha kwanza ni upungufu wa kibinadamu ambao mara nyingi unatokana na uzembe na hiki ndio chanzo ambacho kinachangia kwa wastani wa asilimia 76 na vyanzo vingine viwili ikiwemo ubovu wa magari na ubovu wa miundombinu vinifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia chanzo cha binadamu maana yake mikakati yake ni lazima ilenge katika kushughulikia na changamoto ambazo wanadamu hawa wanasababisha ajali. Ukifanya hivyo maana yake utawagusa hawa binadamu ambao ni wananchi na raia wa nchi hii ambao sisi Waheshimiwa Wabunge ndio tunawawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa hapa, kwa mfano wapo Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba Askari wetu wa Usalama Barabarani hawana muda wa kutoa elimu, wamekuwa wakitoa *fine* kwenda mbele tu. Wako ambao walizungumzia kuhusiana na utaratibu mzima wa namna ya utoaji *fine*, hawajaridhika nao. Yote haya yanalenga katika madereva ambao hao binadamu wanasababisha matatizo ya ajali kwa makosa ya kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mifano miwili, mitatu kuthibitisha hili. Nikichukua ajali za mwisho kubwa zilizotokea, maana bahati mbaya sana ajali za barabarani zikitokea zinavuta hisia nyingi sana kwa jamii kiasi kwamba yale mafanikio makubwa ambayo tunayazungumzia yanafichika. Ikitokea ajali moja inaweza ikaua watu hata 20 kwa mpigo na Taifa linapata tataruki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mifano miwili ya karibuni hii ya mwisho. Kuna ajali ambayo ilioke tarehe 9 Aprili, kule Mbeya ambapo Lori la *Scania* lilihamza njia na kuifuata *Noah*. Hao wananchi wasiokuwa na hatia waliokuwa kwenye *Noah* walikuwa wanaelekeea msibani takriban familia nzima. Basi lile likaenda kuivaa ile *Noah* na kuua takriban watu wanane na kusababisha majeruhi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi tuloufanya, chanzo cha ajali hii ni kwamba basi hili liliacha njia na dereva yule sijui alikuwa ameleta au amelala, lakini aliifuata *Noah* ile na kusababisha ajali ya watu wengi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali nyingine ambayo ilioke tarehe 24 mwezi wa Tatu maeneo ya Mkuranga, Lori la *Scania* vilevile liliacha njia na kuivaa *Hiace*. Katika ajali hii walikufa watu 24 na majeruhi takriban 10. Tatizo lilikuwa ni mwendokasi. Hizo hizo changamoto za kibinadamu tunazozizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hali kama hii na uzembe huu ambao unasababishwa na baadhi ya madereva, mbali na jitihada kubwa za utoaji elimu ambao tunafanya, leo hii mkifungua vipindi vyta radio na TVmtakuta Askari wetu wakitoa elimu kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna utaratibu wa kutoa elimu kwa jamii na makundi mbalimbali, utaratibu hata wa kutoa elimu kabla dereva hajapata leseni ndio aingie barabarani. Juu ya jitihada hizi bado kuna changamoto za

madereva ambao wamekuwa hawafuati sheria za barabarani na wamesababisha vifo vyta watu wengi wasiokwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hiyo, elimu ambayo inabakia, elimu hiyo itatolewe katika Gereza. Maana Gerezani moja ya kazi yake ni kurekebisha tabia za watu waliofungwa, lakini hata kufungiwa leseni na ndiyo maana sasa hivi tunaelekea katika mpango wa kuanzisha utaratibu wa nukta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakopofanikiwa kuoanisha mifumo yetu hii wa Polisi na *TRA* tuweze sasa kufungia leseni mifumo hii ikisomana, lakini itakwenda sambamba na malengo yetu kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amezungumza katika hotuba kwamba sasa suala la leseni tunataka libakie katika Polisi ili kuepusha urasimu usiokuwa na faida. Lingine ni elimu kwa utaratibu wa kutoa *fine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaomba sana mwendelee kuunga mkono Serikali yenu inapopambana kuhakikisha kwamba inaokoa uhai wa wananchi wanaokufa na wengine kupata vilema bila hatia. Vile vile tunaendelea kutoa elimu. Kwa sauti hizi za Wabunge hatuwezi tukazidharau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowenza kusema ni kwamba, nitoe wito kwa baadhi ya Maafisa wetu wa *Traffic* ambao wanatumia fursa hii vibaya, wachache, kama wapo kuacha tabia hii. Maana makosa mengine ni madogo madogo. Unaweza kukuta mtu pengine kwenye foleni kubwa katika Jiji la Dar es Salaam, halafu hajafunga mkanda unamtoza faini badala ya kumwelekeza. Mambo kama hayo, nadhani wanatusikia, waweze kuzingatia. Tunazungumzia yale makosa hatarishi, lakini yapo makosa madogo madogo ambayo tunadhani wanaweza wakaanza kusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hatutaki baadhi ya Maafisa wetu wa Serikali ama wa vyombo

hivi waitie madoa Serikali yetu. Waendelee kusimamia sheria lakini waendelee vilevile kuangalia mazingira na uzito wa makosa yenyewe kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo suala la masuala ya *notification*. Wapo Waheshimiwa Wabunge walilalamika wakasema kwamba kuna wakati mwingine wanapewa *notification* lakini hawapewi risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwa ufupi. Ni kwamba bahati mbaya sana hizi mashine tulikuwa nazo katika Mikoa miwili ya Dar es Salaam na Pwani, lakini nataka nichukue fursa hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari tumeshapata mashine takriban 3,000, tunatarajia kuzisambaza mikoani kwa awamu. Zitakapokamilika kutawanya kote, ambapo sasa hivi tunaanza Arusha na mikoa mingine saba ambayo imeanza kupewa elimu, nadhani changamoto hii itaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwe na hofu, *notification* ile ina kumbukumbu zote, hakuna mwananchi ambaye atapewa *notification*, halafu fedha ile isiende kwenye mamlaka husika na iingie mfukoni kwa mtu binafsi. Kwa hilo, tumejiridhisha kwamba kwa mfumo uliopo vilevile fedha hizi ziko salama. Hata hivyo jambo hili tunatarajia kulikamilisha hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika eneo la pili. Jambo la pili ambalo nataka nilichangie ambalo nimekuwa nikilijibu kwa muda mrefu sana katika Bunge letu hili Tukufu ni kutokana na Waheshimiwa Wabunge wengi wa Bunge hili kuguswa na hali ya mazingira ambayo askari wetu wanafanya kazi. Kama tunavyoja, askari wetu hawa wanafanya kazi ngumu sana katika mazingira magumu. Moja katika mazingira magumu ambayo wanafanya kazi ni maeneo ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge leo tukitoka hapa Bungeni baada ya kazi ngumu ya

kuwawakilisha wananchi, halafu turudi nyumbani mazingira yakiwa siyo mazuri, nadhani hata *concentration* ya kazi siku ya pili haiwezi kuwa nzuri. Askari wetu wamekuwa wakifanya kazi hii kwa mafanikio makubwa kwa miaka yote na ndiyo maana nchi yetu iko salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha miaka ya mwanzo hapa wakati tunaingia, suala hili nilikuwa nikilijibu na nilikuwa nikisema, jamani tuna mpango wa kujenga nyumba 4,136 kuitia mkopo wa *Exim Bank*. Baadaye Waheshimiwa Wabunge wengine katika michango yao wakadiriki kusema kwamba tunawapiga danadana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie tu kwamba wakati mwingine danadana nyingine zinakuwa ni kwa maslahi yetu sisi wenyewe na maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Nadhani sasa hivi wananchi takriban wote wa Tanzania wameshamfahamu, labda wale wasiotaka tu kwa sababu ya ajenda zisizokuwa za msingi. Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mara zote akipigania matumizi sahihi ya rasilimali zetu, kwamba fedha ambazo zinatoka za wananchi zitumike kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano mmojawapo. Kwamba mradi huu ambaeo tulikuwa tunatarajia kupata mkopo wa takriban shilingi bilioni 500 kuitia *Exim Bank* ambaeo ungejenga nyumba kama 4,136 ukiachia gharama nyingine za Bima, *Consultation Fee* na kadhalika, unakuta ungeweza kugharimu wastani wa kama dola milioni mia nne na kitu ambapo kwa hesabu ya harakaharaka ukigawa kwa nyumba 4,136 unaweza ukapata dola takriban 98,000, unazungumzia shilingi milioni 220 mpaka 240, nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais juzi ametoa shilingi bilioni 10 baada ya kujiridhisha juu ya ujenzi wa nyumba ambazo tunajenga kwa kutumia rasilimali zetu za ndani kwa nyumba moja ya Polisi kugharimu shilingi milioni 25. Unaona tofauti hiyo kubwa! Takriban mara kumi au mara tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekubali kwenda haraka na mradi ule ambao tumeukuta, tungeweza kupoteza fedha za wananchi ambazo zingeweza kutumika kwa kazi nyingine, lakini tungeweza vilevile kupata nyumba za ziada kwa askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba Serikali yenu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ni Serikali makini na inayotoa maamuzi yake kwa maslahi ya Taifa na wananchi wa nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia hatua ambayo tunakwenda nayo katika kupunguza changamoto ya ujenzi wa nyumba za Askari wa aina zote tukianzia Magereza, Polisi, Uhamiaji na kwingineko, mpaka *Fire* na kwingine tutafika huko. Nataka nitoe mfano mmoja. Katika mradi wa Arusha ambapo Mheshimiwa Rais aliuzindua juzi, tulijenga takriban nyumba 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais baada ya kuungua zile nyumba alitoa shilingi milioni 250. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, *Comrade Gambo* kwa kuhamasisha wadau mbalimbali tukaweza kujikuta tunatumia fedha hizo kujenga nyumba 31. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano huo huo, tumefanya Pemba. Kuna ujenzi wa nyumba unaendelea Pemba tunavyozungumza sasa hivi. Nachukua fursa hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wote wawili; wa Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Kusini na wadau mbalimbali walioshiriki. Kuna programu ya ujenzi wa nyumba 36 Pemba. 12 Unguja, 24 Pemba na tayari nyumba 12 tunatarajia zitakamilika kabla ya kumalizika kwa mwaka huu kwa sababu vifaa vyote vya ujenzi wa nyumba zile vipo, vimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kutoa wito na kusisitiza Jeshi la Polisi kuzingatia maagizo ya

Mheshimiwa Rais pamoja na Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa kutumia fedha hizi zilizotolewa, shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Polisi zitumike kama zillivyokusudiwa. Wahamasishe wadau katika mikoa yao ili tuweze kupata nyumba nyingi zaidi. Lengo letu ni tunatarajia katika pesa hizi tutapata nyumba takriban 400 kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbe vyetu kwanza ni Mkoa wa Dodoma ambapo ni Makao Makuu ya Serikali, yameshahamia. Maeneo mengine ni mikoa yote mipy ya Kipolisi; Simiyu, Njombe, Katavi, Geita, Songwe, Rufiji, Pwani pamoja na Zanzibar. Haina maana kwamba tutaacha maeneo mengine. Ninachozungumza ni kwamba mgawanyo unaangalia ukubwa wa changamoto katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba kwa utaratibu huu wa kutumia rasilimali zetu vizuri na leo hii tunazungumzia kuimarisha kikosi chetu cha ujenzi katika Jeshi la Polisi (*Police Building Brigade*) ambayo tumeiwezesha kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi na kuwapatia mafunzo mbalimbali, hali kadhalika kwa upande wa Magereza, tunafanya hivyo hivyo. Ndiyo maana nyumba ambazo tunajenga Ukonga kwa fedha ambazo Mheshimiwa Rais ametoa kwa utaratibu huo huo, takriban 320, mchango wa Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza, wafungwa na rasilimali zilizopo kwa kweli unafanikisha sana kufanya tujenge kwa fedha hizi kwa unafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji ni mashahidi, juzi Mheshimiwa Rais amezindua nyumba 103 pale Dodoma. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini katika miaka michache inayokuja, masuala yenu kuhusiana na changamoto ya makazi kwa askari wetu itakuwa inapungua, haitakuwa tena ni swali la kila siku katika Bunge hili kwa kasi hii. Kwa hiyo, hayo ni moja ya maelezo yangu katika eneo la nyumba za Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kwa haraka haraka suala la Uhamiaji haramu. Kwanza nataka nirudishe kumbukumbu nyuma. Wakati Serikali hii inaingia madarakani, tulikuwa tuna tatizo kubwa la wahamiaji haramu katika nchi hii. Mtakumbuka miaka miwili iliyopita tulifanya operesheni kabambe na tukafanikiwa kuwaondoa wengi sana katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa operesheni hiyo kwa kushirikiana na Wizara yenye mamlaka ya Kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tuliweza kukagua makampuni 429 na watuhumiwa takriban 2,199 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ya Uhamiaji. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani, wengine waliondolewa nchini, wengine walihalalishwa ukazi wao na vilevile tukafanikiwa kuweza kukusanya maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumetengeneza nidhamu katika nchi yetu kwamba sasa nchi yetu siyo sehemu ambayo unaweza ukaja tu ukaishi kiholela bila kufuata utaratibu; kwamba unaweza ukaja hapa ukafanya kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya, kwamba unaweza ukaja hapa ukajifanya ndio una nguvu zaidi ya kunyanyasa wananchi wa nchi hii. Kuna vijana wetu ambao wangeweza kutumia fursa hizi wakatumia watu wengine wa nje ya nchi bila sababu ya msingi. Nidhamu hiyo imerudi katika nchi yetu kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya na tunaendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, operesheni hizi zilikuwa zimetengeneza misingi, maana nchi yetu haiwezi kuendeshwa kwa operesheni. Tumeleta operesheni kutengeneza misingi na mifumo ambayo sasa hivi tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka mmoja huu uliopita, tunazungumzia wahamiaji haramu takriban 13,000 waliokamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali na wengine kushtakiwa, lakini idadi hii kubwa inahusisha pia wale wapitaji haramu. Nataka niseme kwamba wote ni wahamiaji haramu lakini najaribu kutofautisha ili nieleweke

vizuri na hasa wale raia wa Ethiopia. Wako Waheshimiwa Wabunge ambao walisema kwa nini tusiwarudishe kwao? Kwa nini tusiwasindikize tu wakaenda wanapoenda midhali hawakai hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo siyo tu kukiuka Sheria za Uhamiaji, lakini vilevile ni kukiuka Sheria za Kimataifa kuhusiana na biashara haramu ya kusafirisha binadamu. Kwa hiyo, kama nchi yetu ambayo tunaheshimu misingi ya utawala bora, hatuwezi kufanya hivyo. Tunachokifanya ni kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba jambo hili linakoma na ni endelevu, badala ya kukimbizana nao kila siku, ili rasilimali zetu chache tulizonazo katika vyombo hivi likiwemo Jeshi la Uhamiaji, ziweze kutumika kwa mambo ambayo yana faida zaidi, sisemi kwamba hili halina faida, lakini tuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mkakati kabambe ambao tumeuandaa wa kudhibiti mipaka yetu ambao utahitaji fedha nyingi sana ikihusisha ujenzi wa *Mobile Immigrations Posts* katika mipaka yetu na kwenye vipenyo vyote tulivyovihesabu katika nchi hii. Kwa kuanzia tunaweza kuanza na vipenyo takriban 107 ambavyo ni vipenyo sugu pamoja na vifaa vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hayo yanaendelea, tunaomba ushirikiano kwa wananchi katika kupambana na tatizo hili, maana wahamiaji haramu hawa wengine tunaishi nao, wengine wanatoa majumba yao kuwahifadhi hawa. Moja katika mikakati yetu, tunasema kwamba tunataka tufumue mtandao wote wa wasafirishaji wa biashara hii haramu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri katika hilo tumeshaanza kufanikiwa. Japo najua jambo hili halitachukua muda mfupi, lakini tayari tumekamata watuhumiwa kadhaa ambao mionganoni mwao wanahuksika na bishara hizi kwamba ni wenyeji, wengine ni wananchi wa nchi hii, maana haiwezi kuwa mtu ambaye anatoka nchi nyingine akafahamu mazingira ya nchi yetu ya kupitisha hawa watu. Kwa hiyo,

wapo watu ambao tayari tumeshawashikilia na sheria inafuata mkondo wake. Katika hili naomba sana wananchi ushirikiano na msaada wenu kulifanikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna mikoa ambayo ina changamoto nyingi, hasa Mkoa wa Kigoma. Wapo Wabunge wa Kigoma walizungumza hapa kwa masikitiko na wengine wameandika. Nataka niwakumbushe tu kwamba hata takwimu zetu zinaonesha kwa mazingira ya jiografia ya Kigoma ambayo inapakanana nchijirani zetu tatu, Mheshimiwa Nsanzugwanko ananikumbusha, ambazo zimepita katika changamoto mbalimbali za kiusalama, siyo jambo la ajabu kuona, mimi nipo zaidi kwa watu ambao wanaitwa wahamiaji haramu. Nanyi ni mashahidi, leo tuna Kambi tatu kubwa za Wakimbizi; Nyarugusu, Mtendeni na Nduta, zote zipo Mkoa wa Kigoma. Wakimbizi wengine badala ya kukaa makambini wanatoroka kuja kukaa uraiani, wengine wanaingiza silaha kutoka katika nchi zao ambazo zinatumika kufanya ujambazi hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hali kama hiyo Serikali lazima ipeleke nguvu zaidi katika mkoa ule ili kuhakikisha usalama siyo tu wa wananchi wa Kigoma lakini wananchi wa Tanzania nzima. Ikiwa kuna upungufu katika utekelezaji wa majukumu hayo, tunayachukua na tunafuutilia. Ila lengo siyo hilo, lengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Kigoma wanaendelea kuishi vizuri na kwa kufuata sheria. Tunatambua juu ya ujirani mwema uliopo katika ya mikoa yetu iliyopo mipakani yote, siyo Kigoma peke yake, lakini kuna utaratibu wa mahusiano na uingiaji na utokaji kati ya wananchi wanaotoka katika nchi moja na nchi nyingine. Utaratibu huu tutaendelea kuufuata na tunaomba wananchi wa maeneo yote waendelee kuhakikisha kwamba wanatuunga mkono katika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa masikitiko makubwa, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia na bahati mbaya michango yao wakaielekeza katika misingi ya dini, mingine mwelekeo wa kikabila. Sisi ni watu ambao tumepewa dhamana kubwa

sana na wananchi wa nchi hii. Moja katika dhamana kubwa tuliyopewa ni kuhakikisha kwamba kauli zetu tunazozitoa katika Bunge hili zinaendelea kuhakikisha umoja na mshikamano uliodumu katika nchi yetu kwa miaka tokea nchi yetu hii imeungana na imepata uhuru na mapinduzi, unaendelea kuimarika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nashangaa kwamba sisi tunakuwa ni wepesi sana kusahau juu ya matatizo mbalimbali yaliyojitekeza. Leo tunajivunia juu ya mafanikio makubwa ambayo tumefikia katika kupungua kwa uhalifu nchini. Hata ukiangalia takwimu za uhalifu, labda nitoe mfano wa nchi ambayo inaongoza kwa uhalifu duniani au Afrika; *South Africa* au Honduras ambayo wanasema katika watu 100,000 watu 98 wanauawa kwa njia mbalimbali, wengine wanapotea, wengine wanatekwa. Nani anajua kama pengine wakati anafanya uhalifu ule alivaa nguo yenye mwelekeo wa dini fulani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linapofanya kazi yake katika kudhibiti uhalifu halishughuliki na dini ya mtu, halishughuliki na kabila la mtu, halishughuliki na sehemu mtu anapotoka. Wakati mwengine ni matumizi mabaya tu ya hivi vitu. Wapo watu wanatumia dini kwa manufaa ya kisiasa, kitu ambacho siyo sahihi kwa dini zote. Hakuna dini ambayo inaruhusu hilo. Wako watu kwa kukubalika tu anatumia ukanda, siyo sawa. Wapo wahalifu vilevile katika kutimiza uhalifu wao wanaweza wakatumia dini, ukanda au ukabila. Nasi hao tunawa-*treat* kama wahalifu wengine wowote. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge katika hili tuwe makini sana. Serikali hii ya CCM ni Serikali ya Watanzania wote ambapo Serikali hii imechaguliwa na Watanzania wa dini zote, makabila yote, maeneo yote na rangi zote na iko kwa maslahi ya watu wa aina hiyo mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo mkimwona Mheshimiwa Rais wetu anahangaika usiku na mchana halali kwa sababu ya kuinua uchumi wa nchi hii ili faida hii ipatikane. Mkiona barabara imezinduliwa, viwanda vinajengwa, ni kwa maslahi ya watu wote wa nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali au Jeshi la Polisi nasi ambao tumepewa dhamana ya kusimamia, hatuwezi kukubali. Kama kuna Mbunge yeoyote ana uthibitisho wa hilo basi waje watuletee, tutafuatilia. Kama kuna mtu ambaye amechukuliwa hatua kwa sababu ya misingi ya imani yake au anakotoka, Waheshimiwa Wabunge, sisi ndio wenzeni, leteni tutafuatilia na kama kuna ukweli hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani kuna Maaskari wangapi ambao hili suala la usalama barabarani ambalo mmelizungumza sana mwanzo, nikiwapa takwimu za askari ambao tumewashughulikia kwa kukiuka maadili yao katika kusimamia usalama barabani mtashangaa ninyi. Kwa sababu siyo malaika! Ila haiwezekani kosa la mtu mmoja lijumuise taswira nzima ya Jeshi la Polisi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kutokana na umuhimu wa hayo unayoelezea, nakuongezea dakika tano. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hata hivyo nilikuwa naelekeea mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge na kuwaomba sana wawe na imani na Serikali yao na Jeshi lao la Polisi ambalo lipo kwa ajili yao. Hawa mnaowaona, wengine wako kule, wengine hapo, wengine hawapo hapa; hawapati usingizi, hawalali ili Watanzania tulale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwe *fair* Waheshimiwa Wabunge, kwamba wao hawaruhusiwi kuingia humu ndani wakajitea, isiwe sababu ya sisi kuwazungumza vibaya. Hii ni nchi yetu sote, vyama hivi visitugawe wala siasa zisitugawe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisichukue muda wa Mheshimiwa Waziri wangu, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri dakika 35.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja kwa kusemea hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walizitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme kwamba hatutaweza kuzijibu hoja zote kwa muda huu, lakini Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wao wametoa hoja nzuri, hoja nzito na sisi kama Wizara zile ambazo zimekaa kwa muundo wa ushauri tumezichukua tutazifanya kazi na zile ambazo zipo kwa maandishi tutaweza kujibu kwa maandishi. Nia yetu sote ni ya kujenga na tunakubali sana hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la hoja zilizotolewa kwenye upande wa Jeshi la Zimamoto, kimsingi zilikuwa linaongelea kuhusu vitendea kazi na umuhimu wa Jeshi letu hili la Zimamoto. Tumepokea jambo hili na bahati nzuri umelikazia sana jambo hili tungali kwenye Kamati na tumelipokea ndani ya Serikali na tunaendelea kufanya mawasiliano kuweza kuhakikisha kwamba tunakamilisha viporo vile ambavyo ni vya ununuzi wa magari lakini pamoja na maeneo mahsusи yakiwemo ya majengo na kama ambavyo umetoka kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yanayohusu sare za Askari wetu Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa hisia tumepokea na tunaendelea kuyafanya kazi na hatua za mwanzo zimeshaanza zinazohusisha sare ili Askari wetu waweze kupata sare na waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yanayohusu kuweka miundombinu ya kisasa ili Jeshi la Zimamoto liweze kufanya kazi hizo na yenyewe tumeendelea kufanya mawasiliano ndani ya Serikali na kuwezesha mazingira yaye rafiki ili Jeshi la Zimamoto liweze kufanya kazi vizuri. Mambo haya yanahusiasha masuala ya ujenzi, masuala ya ujenzi wa miundombinu kama maji pamoja na vitendea kazi vingine

ambavyo vinatumika katika masuala mazima ya kazi kuhusu Jeshi letu la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kutoa elimu na wananchi waweze kutambua kwamba pana mambo ambayo ni ya msingi ya kuzingatia kabla moto haujatokea ama kabla janga halijatokea ambayo yanafanya ufanisi uwe mkubwa punde janga linapotokea tofauti na ilivyo sasa ambapo mambo hayo yasipozingatiwa huwa yanakuja kuleta upungufu katika utekelezaji wake punde janga linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si tu la Wizara wala si tu Jeshi la Zimamoto na wala siyo tu la Wabunge ni jambo la nchi nzima, kuzingatia masuala ya tahadhari kwenye masuala ya moto kabla moto haujatokea ama kabla janga hilo halijatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa upande uhamiaji jambo hili limesemewa sana na Waheshimiwa Wabunge, tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua kwamba kwanza kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu la Uhamiaji, lakini na kazi nzuri ambazo zinafanywa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma na kila mmoja amekiri kwamba kazi hizo zinafanyika vizuri na niendelee kusisitiza hata Wabunge tusiondoke hapa Dodoma kabla hatujapata *passport* zetu za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao tayari wameshapata *passport* zao, zoezi hili ni jepesi tu ukichukua zile alama asubuhi baada ya nusu saa ama dakika 40 taarifa zote zinakuwa zimeshaingia kwenye mfumo na *order* ya *ku-print* inafanyika na kwa mazingira maalum tumeshalionelea kwa wale ambao watahitaji mazingira maalumu tutayafanya kwa umaalum huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo niliona nillisisite sana na nilifanue na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuelewane vizuri kwa sababu sisi

ndiyoi tunakaa na wananchi ni hili suala la uraia na watu kuhojiwa panapotokea masuala ya *passport*, licha ya kwamba wapo ambao walishapata *passport* zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imepita katika hatua tofauti kuhusu utambuzi wa uraia, jambo hili la uraia ni jambo la kisheria siyo jambo la jiografia wala siyo jambo la hisia ni jambo la kisheria. Hata hivyo, kwa wananchi wetu wengi wengi bado tunaenda na jambo la historia pamoja na jambo la jiografia. Hata wengine wapo ambao nimeongea nao mimi mwenyewe wakisema wazazi wangu walizaliwa Tanzania ama wazazi wangu walikuja wakati wa uhuru na wengine wa rika letu wakisema mimi nimezaliwa Tanzania nitakuwaje siyo Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili wala siyo la ugomvi na nitoe rai kwa Watanzania tuelewane kwamba, ni jambo la kisheria na panapotokea mambo yanayohusu sheria ni vema tukafanya marekebisho yake. Jambo hili liko namna hii, mwanzoni tulikuwa na sheria iliyokuwa inatambua mtu aliyezaliwa ndani ya Tanzania kuwa raia wa Tanzania na nadhani kuna nchi ambazo zina utaratibu huo kwamba raia ye yeyote aliyezaliwa ndani ya jiografia ya eneo husika la nchi hiyo anakuwa raia wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye nchi yetu tulienda hatua zaidi za kisheria ambazo zinamtambua raia wa Tanzania si tu kwa kuwa alizaliwa ndani ya eneo la Tanzania bali awe amezaliwa na mzazi mmoja aliye raia wa Tanzania. Yule aliyezaliwa na mzazi mmoja aliye raia wa Tanzania analazimika na ye ye atapofika miaka 18 aweke wazi kama anataka kuwa raia wa Tanzania ama anaafuata uraia mwingine ambao ni wa mzazi asiye Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tuna idadi ya Watanzania ambao katika kipindi fulani waliwahi kuwa na *passport* za Tanzania. Hata hivyo, sheria ilipokuja kutambua kwamba raia wa Tanzania lazima awe amezaliwa ama na mzazi mmoja wa Tanzania ama wazazi wote wote wa Tanzania wale ambao walishapata hata hizo *passport*

wanalazimika kurekebisha uraia wao ili waweze kuendana na masharti ya kisheria. Ni masharti ya kisheria na sheria tumetunga wenyewe wala Idara ya Uhamiaji siyo iliyotunga na masharti ya sheria ambazo zimetungwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wale ambao ama wazazi wake walikuja Tanzania na ye ye akazaliwa na wazazi wakiwa bado hawajawa Watanzania ana wajibu wa kurekebisha *status* yake ya uraia ili aweze kuwa raia wa Tanzania wa kisheria. Watu wa aina hii hawana masharti magumu kwa sababu tunatambua kwamba hawana nchi nyine, nchi yao ni hii kwa maana ya kwamba wamezaliwa hapa hawana nchi nyine. Tunachofanya ni kuweza kurebisha *status* za kisheria na hata gharama zao ni tofauti na wale watu wanaokuja kuomba uraia wa Tanzania kwa kutokea Mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe rai watu wanapoona kwamba kuna jambo la kosoro kwa upande wa masharti haya ya kiuraia wasichukulie kama ni jambo la ugomvi, wachukulie ni jambo la kisheria na wanachotakiwa kufanya ni kupewa ushauri, kupewa mwongozo na wao wafuate mwongozo huo ili kuweza kurekebisha matatizo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo liliongelewa amelisema sana Mheshimiwa Mwilima na ameliongea kwa hisia sana kuhusu masuala ya watu kuhojiwa masuala ya uraia na akasemea sana kuhusu watu wa mipakani. Serikali kwa sasa inafanya zoezi kubwa sana ambalo litaenda kumaliza matatizo hayo ambayo yamekuwa yakiwapata wananchi wa mipakani kwa kutokutambulika ama kwa kupata kashikashi za kutiliwa mashaka. Zoezi la vitambulisho vya Taifa linaloendelea litakapokuwa limemalizika na kila Watanzania wakatambulika tutakuwa tumeshapata jawabu la nani si Mtanzania na nani ni Mtanzania, kwa hiyo na hiyo itaenda kuondoa bughudha hizo ambazo zimekuwa zikijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ameileta hoja kwa uzito mkubwa na alishailleta hata Ofisi tumeipokea na tutayafanyia kazini hasa haya ambayo aliyoysesemea ambayo yanahusu utendaji kazi hasa aliposemea kuwa kuna watu wanadaiwa fedha ili waweze kuandikishwa vitambulisho hivyo vya Taifa. Jambo hilo ambalo halijatolewa maelekezo kwamba wafanye hivyo tunachukulia kama masuala ya kimaadili na tutafuatia nimeshaelekeza timu ya Wataalam, nimeshaelekeza idara inayohusika waweze kufuatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili alililetu Mheshimiwa Mbogo pia kutoa Mkoa wa Katavi pamoja na Wabunge wengine ambao jambo hili lilito keza katika mazingira ya aina hii. Ikitokea mmoja mmoja akafanya hivyo siyo maelekezo ya Wizara na wala siyo mpango wa Wizara kufanya hivyo, atakuwa ametokea mtu mmoja akapotoka na sisi wakitokea watu wa aina hiyo tutachukua hatua zinazostahili. Kwa hiyo, tuendelee kuwasiliana, kupeana maendeleo ya jinsi zoezi hili linavyoendelea ili tuweze kulifanya zoezi la ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilito keza linalohusiana na masuala ya uraia pamoja masuala ya vitambulisho vya Taifa alilisemea ndugu yangu Mattar Ali Salum, aliposemea kuhusu kitambulisho cha Mzanzibari *vis-a-vis* kitambulisho cha *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kitambulisho cha Mzanzibari kinatambulika ni kitambulisho halali kimetumia ghamra za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kutengenezwa. Wizara idara hizi ambazo ziko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinafanya kazi kwa pamoja, lakini maelekezo tuliyoyatoa ilikuwa tu ni kwamba maadam kwa Zanzibar uandikishaji wa kitambulisho cha *NIDA* umeshafanyika kwa zaidi ya asilimia 90 na kwa kuwa taarifa hizo zinasoma upande *NIDA* pamoja na Idara yetu ya Uhamiaji tuliona tuwapunguzie Watanzania usumbufu wa kutoa taarifa kama tayari walishatoa taarifa, waweze kutumia taarifa hizo ambazo tayari

zimeshapatikana ili kuweza kuwapunguzia mlolongo wa kuendelea kuulizwa taarifa zilezile ambazo wameshatoka kuzifanya huku *database* zetu zikiwa zinasomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haikuwa nia mbaya ya kutaka kutokutambua kitambulisho cha mkazi ama kutokutambua juhudhi ambazo zimefanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini ilikuwa ni kuweza kutumia *data* ambazo zimeshafanyika. Kwa Zanzibar zoezi la utambuzi na uandikishaji wa vitambulisho vya Taifa limeshafanyika kwa kiwango kikubwa mno na ndiyo maana tuliona tuanze zoezi hilo la kuanza kuoanisha *data* ambazo tumeshazipata kwa ajili ya Watanzania wetu, kuliko kila wakati kuwa tunatumia utaratibu wa kuanza kumhoji Mtanzania upya ilihali akiwa ameshatoa taarifa hizo katika ofisi ya Serikali ile iliyo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Magereza zilijitokeza hoja nyingi, moja zinazohusu mambo ya sare, tayari zabuni ya upatikanaji wa sare imeshafikia hatua za mwisho na inafanyika ndani ya nchi hapa kwenye viwanda vinavyotengeneza majora hapa na hatua zitakazofuata sasa itakuwa ni ushonaji, vijana wetu wataenda kupata sare na baada ya vijana wetu kupata sare tutazingatia pia na suala la wafungwa ambalo na lenyewe lilisemewa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo niliona niliweke sawa, Mheshimiwa Mbunge nadhani Mheshimiwa Mary Deo Muro wakati anachangia alisemea masuala ya watoto. Ni kweli kuna watoto ambao wazazi wao wanatumikia vifungo mbalimbali, kwa sasa watoto ambao walishachukuliwa na ndugu zao kwa takwimu zilizopo sasa ni sita, watoto walioko magerezani ni kama 45 na wafungwa wajawazito ni 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu naomba Bunge lako Tukufu lipate kumbukumbu zilizo sawa, hakuna mimba zinazopatikana gerezani. Narejea tena hakuna mimba zinazopatikana magerezani, kuna akinamama wajawazito ambao wamepata ujauzito kabla hawaajaanza

kutumikia vifungo, kwa maana hiyo zinafuata taratibu za kisheria, kwanza mtoto akiwa bado mdogo kwa umri ambaao akina mama mnajua, analazimika kuwa na mama yake. Akiwa katika umri ambaao unamruhusu mtoto kutenganishwa na mama inafuata tu utaratibu kama ndugu atawepo atakayejitokeza kumpokea mtoto yule wanampokea, lakini kama ni upande wa Ustawi wa Jamii na yenyewe anaenda kupokelewa kufuatana na makubaliano yanayokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilijitokeza, ilikuwa la masuala ya kulifanya Jeshi la Magereza kujitegemea. Jambo hili Wizara tumepokea ushauri huu na jambo hili tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu alishalitolea maelekezo, tulishakaa tutaanza kwa mfano, kwa Magereza yaliyo na maeneo makubwa kuweza kufanya utaratibu wa kulima kwa kisasa na tayari Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaelekeza utaratibu wa kuyaunganisha matreka utakapokamilika tutaanza na 50 kwa upande wa Jeshi la Magereza ili kuweza kuhakikisha kwamba tunalima kwa kisasa na tunalifanya Jeshi la Magereza liweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo haya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyaelekeza kwa uzito mkubwa na mara kadhaa Mheshimiwa Rais ameelekeza kuhakikisha kwamba hatuchukui fedha ambazo zingetumika katika maeneo mengine kwenda kulisha wafungwa na badala yake Jeshi la Magereza lijitegemee na ikiwezekana hata likatoa huduma zinazotokana na uzalishaji wake katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara tumezingatia na tumeshaanza miundombinu kama hii niliyoisemea, tukianza na tunalenga Gereza la Songwe, Kitengule, upande wa Ludewa, Isapilo pamoja na maeneo mengine ambayo ipo miundombinu ya asili ama miundombinu ya awali ambayo italiwezesha Jeshi la Magereza kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazingatia ushauri ambaao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwenye upande wa kuboresha masuala mazima yanayohusu magereza ili tuweze

kuhakikisha kwamba tunavuka hatua hii tuliyonayo tuweze kwenda ngazi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazingatia masuala ambayo yamesemewa ya kiutumishi ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema masuala yanayohusu masuala ya kiutumishi, masuala ya maslahi kwa vijana wetu, tunaendelea kuyafanya kazi na hii kwa sababu tuna mambo tunaendelea kuyafanya kazi yatakopokuwa yamekamilika, tutafanya utaratibu rasmi wa kuweza kuliarifu Bunge lako ama kupitia Kamati ili tuweze kuwa na uwelewa wa pamoja kwa jinsi ambavyo tutakuwa tumeshafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jambo ambalo lina umuhimu mkubwa sana ukizingatia kazi wanazofanya vijana wetu na tunaheshimu kazi wanazofanya, tunaheshimu mchango wanaoufanya na tunaheshimu moyo wao wa kujitoa kwa uadilifu na kwa uaminifu mkubwa katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyoongeleta yanahuusu maslahi ya askari wetu haya ni mengi, tutakapokuwa tumeyashughulikia tutaendelea kupeana taarifa ili tuweze kuhakikisha kwamba Waheshimiwa Wabunge hoja zao wanaona kuwa tumezifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilijitekeza Mheshimiwa Maige alisemea kuhusu Muswada wa Ulinzi wa Sekta Binafsi. Jambo hili tumeshalipokea na Serikali imeshafanya nalo kazi kubwa, tayari Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kushirikiana na wadau ilishaandaa rasimu ya mapendekezo ya kutunga sheria na hatua kubwa zilishafanywa kuhusu utaratibu wa rasimu wa kutunga sheria, kwa Tanzania Bara tayari yalishakamilika na maoni ya kutoka Zanzibar yalishakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia mpaka ifikapo mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumeshafika hatua nyingine ambayo inaelekea kwenye utungwaji wa sheria hiyo ikiwepo kupitia *Cabinets Secretariat* pamoja na Baraza la

Mawaziri ili jambo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amekuwa mdau mkubwa na amekuwa akitoa maoni mazuri liweze kutimia na hatimaye liweze kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka michango mizuri iliyotolewa na Wabunge kuhusu masuala ya magereza Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Deogratius Ngalawa, Mheshimiwa Maige mwenyewe, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko pamoja na wengine wote ambao wameongelea masuala haya yanayohusu masuala ya magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ninayo ndefu sana ikiwemo Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Zacharia Issaay ndugu yangu wa kutoka Mbulu na Mheshimiwa Zuberi pamoja na wengine, tumepokea hoja zenu zote tutazifanyia kazi, tutachambua moja baada ya nyingine, yale ya kiushauri tutayafanya kazi na yale ambayo ni maelekezo tutapokea tuweze kuyafanya kazi kwa sababu ni maoni mazuri na tunaamini yatatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walilizungumzia sana ni hili la vijana wa bodaboda. Kwanza kuna mambo ambayo sote tunakubaliana. Moja ni kweli, matumizi haya ya bodaboda ama usafiri huu wa bodaboda umetengeneza ajira nyingi sana kwa vijana wetu, hakuna Jimbo hata moja ambalo hawana bodaboda. Katika kuzunguka kwangu kila eneo kuna bodaboda. Kwa maana hiyo ni kweli jambo hili limetengeneza ajira kwa vijana wetu wengi sana hili hatubishani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kwamba jambo hili la usafiri wa bodaboda linaajiri vijana wengi sana na wengine wanafanya shughuli hizi za bodaboda wakiwa wamepata uelewa mdogo sana kuhusu matumizi ya vyombo vyta moto. Hili wala hatubishani nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumeelekeza maeneo yote, mikoa yote kuwapa elimu vijana hawa wanaofanya shughuli hizi za bodaboda, lakini changamoto tunayokutana nayo kwa sababu ni wengi na wanaoingia kwenye sekta hiyo wanaingia karibu kila siku, kwa hiyo hakuna mkoa ambao unaweza ukasema umefanya mafundisho hayo na kuyamaliza kwa sababu wanaingia kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine ambao wanaazimana pipipiki ndani ya muda mfupi Wizara tunaendelea kulikazia kwamba jambo hili ni la kijamii wala siyo jambo tu la Wizara na hata Waheshimiwa Wabunge ni vema tukawaambia wananchi wetu kwamba hili ni jambo la kijamii na tukaliongea kama mambo mengine ambayo huwa yana athari kubwa katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema yanaathari kubwa kwa sababu ukienda kwenye takwimu ni kweli kwamba vijana hawa wengi wanaumia, wengi wanapata ulemavu wa kudumu, wengi wanapoteza maisha, wengi wanapoteza maisha ya abiria waliokuwa wamewabeba kwa sababu ya haya niliyoyasema ya kujifunza muda mdogo, kutokuwa na uelewa wa matumizi ya vyombo vyya moto, kutokuwa na matumizi ya barabara ambapo kuna vyombo vingine vyya moto na mambo haya yanababisha hasara kubwa kwa Taifa letu kwa sababu yanapunguza nguvu kazi za vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, kwa yale ambayo yanafanyika kwa utaratibu wa ukamataji ambao unasababisha ajali zingine au unaleta madhara hiyo tutaelekezana ndani ya Ofisi kuweza kuzingatia utaratibu bora wa ukamataji ili kuweza kuwalinda vijana wetu hawa wakati tukiendelea kuwfundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa maelekezo hata nilipokuwa Tanga naendelea kusisitiza pia kwamba vijana hawa wengine wamepata mikopo, lakini pia

wanatengeneza ajira. Tumesema kwa wale ambao tunafahamu walipo tusichukue njia ya kuona ni vema pikipiki hiyo ikaozea kituoni kwetu badala ya kuwapa na kuwataka walipe gharama zile ambazo wanatakiwa walipe. Huu ni utaratibu ambao unatumika hata katika nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea mtu akifanya kosa kama ana gari halazimiki ku-park gari ile mpaka alipe gharama ile anayodaiwa. Anapewa kwamba unatakiwa ulipe gharama hii na anapewa muda kwa hiyo hata upande wa bodaboda nimeelekeza wakishamtambua na kituo chake kinatambulika na kosa ameshaelezwa alilokosea apewe pikipiki yake, aendelee na kazi lakini aelekezwe kwamba unatakiwa ulipe, pia unatakiwa usifanye makosa ya aina hiyo ili kuepuka kugeuza ofisi zetu kuwa ni karakana ama kuona ni vema pikipiki yake ikaozea pale kwa sababu hajaleta Sh.60,000 pikipiki ambayo ilinunuliwa kwa zaidi ya milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunaendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha kutofautisha faini kwa pikipiki hizi ukilinganisha na magari, kwa sababu kwa kweli kuweka faini ile ile kwa Basi ama *Coasterilyobeba* watu 20 ama 30 inavyopita kwenye kosa moja la barabarani utoze faini sawa sawa na pikipiki iliyobeba mtu mmoja ndiyo tunawafanya wale vijana wanashindwa kuzikomboa pikipiki zao na kuzifanya ziendelee kubaki katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo ni vema tu likawa wazi, kuna makosa ambayo pikipiki zile zimebakia kama ushahidi. Kwa mfano, kama pikipiki mtu alibeba watu wa madawa ya kulevyia ama watu waliofanya uhalifu wa matumizi ya silaha, ama watu waliofanya ubakaji na makosa mengine makubwa makubwa, ambapo pikipiki hizo zinatakiwa ziende kama ushahidi kwenye taratibu zingine za kisheria, hayo yanatakiwa yaendelee kubaki hivyo hivyo ya ukubwa wa makosa na uhitaji wa pikipiki hizo katika kesi ambazo zinatakiwa zisonge mbele. Kwa yale ambayo tunaweza tukayamaliza kwa kuonyana na masuala ambayo

hayakuwa na athari ndio hayo ninayosemea, akishajulikana na kituo chake kinajulikana waruhusiwe kuendelea na kazi huku wakiwa wamepewa lini wanatakiwa wamalize kufanya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda upande wa Jeshi la Polisi. Moja ya mambo ambayo yamejitokeza kwa kiwango kikubwa, nikianza na suala la watu kupotea, suala la mauaji, Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa hisia kubwa sana. Nikianza na matatizo haya yaliyojitokeza kwa siku za hivi karibuni, nianze kwa kumpa pole sana Mheshimiwa Heche kwa kuondokewa na Ndugu yake na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wametolea mfano, hatua zimeshachukuliwa kwenye jambo hilo na taratibu za kisheria zitafuata mkondo wake. Nitoe pole pia kwa familia na jamaa wengine ambao wamepatwa ama wameguswa na matatizo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie tu Bunge lako Tukufu kwamba panapotokea matatizo ya kiutendaji ya aina hiyo, hayo siyo maagizo na wala siyo maadili ya Jeshi la Polisi, inakuwa imetokea mtu mmoja katika upungufu wake wa kibinadamu anafanya hivyo na akishafanya mmoja siyo maelekezo ya Wizara wala siyo maelekezo ya Jeshi la Polisi na kwa maana hiyo yanapofanyika hiyo ambayo yanakiuka maadili, mara zote sisi kama Wizara na kama Jeshi la Polisi tunachukua hatua kwa wale wanaofanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za aina hiyo kwa watu wanaofanya makosa hilo ni kosa kubwa lililopitiliza, lakini yapo na mengine yanayofanyika ambayo yanatambulika kwamba yanakiuka maadili namiko ya utendaji wa kazi kila wakati taratibu za kisheria na taratibu za kijeshi zimekuwa zikichukuliwa ili kuweza kauhakikisa kwamba wananchi wananzaika na uwepo wa Jeshi la Polisi na wanafurahia uwepo wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mambo mengine yaliyoongeleva, tulitaka kuingia kwenye mtego wa kuona kama vile tuna madaraja ya Watanzania. Ni vema sana

Bunge lako Tukufu likaelewa vizuri sana kwamba hapa Tanzania wananchi wote walioko ndani ya mipaka ya Tanzania, kwanza ambalo ni kubwa kuliko yote, tulipozaliwa tulizaliwa wanadamu hilo ni la kwanza. La pili ikafuatia kwamba atakuwa amezaliwa mwanadamu amezaliwa Mtanzania baadae anatambulika anatokea eneo (a), baadae anatambulika anatokea imani (a), baadaye anatokea anatambulika imani ya Chama (a), lakini la kwanza ambalo ni kubwa kuliko yote tumezaliwa wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishazaliwa mwanadamu, damu ya mwanadamu haiwezi ikalinganishwa na gharama ama na thamani ya Chama chochote cha Siasa, haiwezi ikalinganishwa na thamani ya imani yoyote wala haiwezi ikalinganishwa na thamani ya kabilia lolote. Kwa maana hiyo, hii dhana ya kwamba labda kuna utaratibu wa watu kutokupewa uzito ulio sawa kutokana na ama vyama vyaa siasa, ama kabilia, ama dini, hiyo dhana siyo njema ikawepo katika nchi yetu. Ni dhana potofu na Serikali tunalinda usalama wa raia wote wa nchi yetu na hivyo ndivyo ambavyo tumekuwa tukifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea haya masuala na huku tukiwa tunaongelea katika kipindi ambacho kuna watu wengine wameguswa na matatizo kama hili tulilosema, ni vema sana tukahifadhi utu ambao unawahuusu watu ambao wamepatwa na matatizo ya aina hiyo. Tukijumuisha tu kwamba kuna watu wamepotea, wameuawa, moja siyo dhana sahihi nitawapa sababu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika kipindi hiki kuna mambo mengi ya kimaadili ambayo tumeyafanya msako. Kuna watu wengine hawako kwenye familia zao kwa kukimbia misako ya ushiriki kwenye madawa ya kulevyaa, wapo ambao tunaendelea kuwatafuta mpaka sasa ambao wapo kwenye orodha ya watu wanaojihusisha na madawa ya kulevyaa na wengine tumeambiwa hata wameshavuka mipaka ya nchi yetu. Sasa mtu wa aina hiyo ambaye ameshiriki kwenye madawa ya kulevyaa, tunamtafuta,

amekimbia familia yake, akitokea mtu akisema mtu huyu haonekani kwamba ameuawa na mtu huyu kwamba haonekani kwamba anatafutwa, ukituuliza yuko wapi nasi tunakuuliza yuko wapi tunamtafuta, kwa sababu tunaendelea kufanya msako wa watu wote wanaofanya vitu vya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tumefanya msako ya watu ambao wamefanya uhalifu kwa kutumia silaha maeneo tofauti tofauti, tumefanya mapambano hayo. Kuna wengine ambao tuliwakamata wanaendelea kuwataja wenzao waliokuwa wanafanyakazi hizo pamoja wakiwa wanatumia silaha, tumewasaka watu wa aina hiyo na watu wa aina hiyo wengine tunaambiwa wameshavuka hata mipaka ya nchi yetu, wapo watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama watu wanatumia silaha na wenzao tumeshawakamata na wamekimbia, wametorokea mipaka ya mbali ama wako nje ya mipaka ama popote pale walikojificha, kama tunaendelea kuwatafuta kwa uhalifu huo, ukituuliza kwamba kwenye familia hii huyu mtu yuko wapi nasi tutakuuliza yuko wapi tunamtafuta, kwa sababu wale wote wanaofanya uhalifu nasi tunaendelea kuwatafuta watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ukijumuisha tu watu wote wambao hawako kwenye familia zao ukasema wamekufa *that is totally wrong over generalization*. Kwa sababu hata sasa hivi, Watanzania ambao wako wanashikiliwa nchi zingine kwa kushiriki kwa madawa ya kulevyo wako kwenye magereza ni zaidi ya 1,000. Hivi sasa watu wa aina hiyo, familia za aina hiyo, hao watu wao hawapo, wewe ukisema tu kwamba watu wa aina hiyo wameuawa, *that is wrong* kwa sababu kuna watu wako na makosa mbalimbali, lakin hata ondoka zao wanaondoka kwa njia ambazo ziko tofauti tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, kuna kijana mmoja siku moja nilitembelea gerezani nikaenda kuongea

naye akakiri kufanya matukio ya uhalifu, alitaja zaidi ya matukio matano ya uhalifu. Walipochukua silaha Bukombe akasema na mimi nilikuwepo, walipoua Askari pale Sitakishari akasema na mimi nilikuwepo, waliposhiriki matukio ya Mbagala pale akasema na mimi nilikuwepo, akasema lakini naomba kama utanihakikishia niendelee kukwambia, nikamwambia nimekuhakikishia sema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema Mheshimiwa mimi nimeshiriki sana haya matukio hata kwenye utekaji wa basi kutoka Itigi kuelekea Makongorosi hadi Mbeya mimi nilikuwepo. Akasema tuliteka Sekenke nilikuwepo lakini akasema Mheshimiwa Waziri jambo moja tu, katika hizi kazi tulizofanya, ilikuwa kila tukifanya shughuli hiszo, katika mapambano wengine wanauawa. Akasema mimi mnihakikishie kwamba mtanisamehe, nimeshaacha kufanya hivyo, yuko gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama watu wengine ambaao wako gerezani wanasema mwengine huyu tumefanya naye tukio hapa akauawa, mkija mkauliza tu kwamba kuna watu hawa hawapo, mmeshachukua takwimu za wahalifu? Mmeshachukua takwimu za madawa ya kulevy? Mmeshachukua takwimu za wale ambaao tunawatafuta mpaka sasa ambaao wameshiriki kwenye uhalifu wa silaha? Mmeshachukua takwimu za wale wengine ambaao wamekimbia tu wako kwenye mafunzo ya mambo ya uhalifu katika maeneo mengine? Waheshimiwa Wabunge, ni vema sana jambo ambalo linahusu masuala ya usalama tukayabeba kwa umakini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IGP*, kama tunasema kuna watu tunawatafuta, tunasema kuna watu wamekimbia na tunasema kuna watu wameshiriki kwenye uhalifu na tunasema hakuna mtu ambaye ameuawa, kama kuna mtu anayesema kuna mtu ameuawa ni vema sana akajitokeza akaenda akasaidia jambo hilo kwa sababu mambo ambayo yanatokea ya kiuhalifu tunahitaji kuyashughulikia, kwa sababu kuua mtu asiye na hatia ni uhalifu na kama kuna mtu amefanya hivyo ili tuweze kufanya kazi mambo ambayo

yanahusu uhalifu wa aina hiyo, kuliko kuwa watu wana majonzi halafu sisi tunafanya ni jambo ambalo tunaweza tukajibizana. Hii haiwezi ikajenga jamii yetu, inaweza ikatengeneza uhasama ambao hautalifaa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine tukiongelea hawa watu ambao wamekuwa wakitupwa na hawa watu wanaosafirisha watu kwa njia haramu, kuna wengine wana-*challenge*. Ndugu zangu mnapo-*challenge* basi muwe na takwimu rasmi. Tumekamata kule watu wakiwa wamebebwa pamoja na mkaa, wame-*faint*, wakapoteza maisha kule Lituhi na Kitahi, tumekamata watu huku Handeni wakiwa wamechanganywa na *cement* wame-*faint* wakapoteza maisha. Tumekamata watu 80 wakiwa wametupwa, *actually* tumewaokota wakiwa wametupwa kwenye hifadhi kule mpakani mwa Tanga na Bagamoyo. Polisi na Magereza wamelazimika kuwatengenezea uji mwepesi ili wapate fahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu kwa sababu wakichoka wengine wanawatupa ili safari iendelee. Kama wanaweza kutupa watu 80, hivi mpaka watu 80 wa-*faint* kwa nini huwezi ku-*suspect* kwamba inawezekana walishatupa wengine ambao walipoteza maisha? Kwa nini sisi tunafurahia sana kujengea taswira nchi yetu kwamba kuna mambo mabaya yanafanyika kuliko kuona na tunabisha ambayo yanaonekana, *interest* yetu ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani haya yote yanayotokea Waheshimiwa Wabunge hatuoni kwamba inaweza ikawa moja ya jambo na tuhamasishe ama tuhimize jambo hili udhibiti ufanyike kwa kiwango kikubwa zaidi kwa sababu unachafua taswira ya nchi yetu, sisi tunatamani yale ambayo yana taswira kwamba yanaweza yakawa yana *reason* kwamba siyo hayo, tunatamani yale yanayochafua nchi yetu, tunanufaika na nini ikiwa hivyo? Hivi nani ananufaika ama nani anafurahia ikioneckana kuna Watanzania wanaauawa, Watanzania wauawe ili tunufaika na nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo,

Waheshimiwa Wabunge ni vema sana na ni afya sana kwa Taifa letu tunapoongelea mambo haya makubwa tuwe na *vivid evidence* na kama tuna *vivid evidence* tu-report kwenye chombo kilicho rasmi ili taratibu ziweze kufanyika. Sasa mtu akikataa akasema wale walookotwa walikuwa ndugu wa hawa watu, tunawaambia basi kama kuna ndugu wanahisi wale walikuwa ndugu zao kila mwili uliokotwa tunachukua *DNA* ili kama kuna mtu atajitokeza afananishwe na yule mtu aende kwenye *DNA* ili afananishwe hivyo ndivyo tunavyofanya. Sasa wewe kama watu wanaelekeea kuharibika unataka tufanyeje? Tuwahifadhi Ofisini? Tunachukua *DNA* halafu ndiyo tunawazika hivyo ndivyo duniani kote wanavyofanya ili ikitokea mtu akafanya *claim* iweze kufananishwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, niwaamble tu jambo moja, siyo jambo zuri sana kujadiliana ama kutolea mfano watu ambao wako kwenye majonzi lakini ilishatokea mifano ya watu ambao wametaka kufananisha *DNA* na jambo hilo likafanyika na vipimo vikaonesha, sasa kwa nini tunang'anga'na tu kutaka kulazimisha yale ambayo kuna Mataifa wangetamani *anyway* iwe hivyo nasi tunatamani yawe yale, tuna *interest* gani kwenye hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwanza tunapojadili jambo la aina hii twende kwa tahadhari lakini kama tuna mtu ambaye ana taarifa za mambo haya *specific issues* tusaidiane ili tuweze kuisaidia jamii yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa sababu kengele ilishagongwa, lilijitokeza suala la maagizo. Kama kuna mtu ana maelekezo yaliyo tofauti atayafikisha kama Waziri wa Nchi alivyosema, lakini mambo yanayohusu Wizara ya Mambo ya Ndani kama kuna Mbunge hajapata kibali, alitoa taarifa ya kufanya jambo lake hakupata kibali, taratibu zinasema *ana-appeal* kwa Waziri. Kama kuna jambo linahusu uraia wa mtu yejote ama jambo lolote linalohusiana na uraia anayetoa uraia ni Waziri. Kama kuna

jambo la mtu kuondoshwa nchini anayeondosha watu hao ni Waziri, sasa mnatafuta juu ipi? Juu yenyewe ndiyo hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna jambo unakutana nalo ukiona *OCD* akasema limetoka juu na yuko Wizara ya Mambo ya Ndani, *RPC* akasema limetoka juu na yuko Wizara ya Mambo ya Ndani wewe tuko wote hapa mara zote, Mbunge mwenzangu na mimi ndiyo niko juu sasa si useme kuna jambo liko hapa. Nimeshafanya mambo ya aina hiyo ambayo yalijitokeza katika maeneo husika nimeshafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja nitoe mfano tu, kuna siku moja Mbunge wa Viti Maalum, Njombe, Diwani wake alikuwa na mukutano pale yeye wakamwambia hatakiwi kuhutubia, akaja... (*Makofii*)

(*Hapa Mhe. Pascal Y. Haonga alizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga hebu jiheshimu. Kama una jambo simama, fuata taratibu, huwezi kanywe chai, ondoka. Kaa chini. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anayetambua juu akaniambia Mheshimiwa Waziri, mimi ni Diwani katika Manispaa hii kuna mukutano wa Diwani mwenzangu hapa na niko Mkutanoni nimezuiwa kuongea. Nikawaambia mukutano ule ni wa nani? wa Diwani wa CHADEMA na yule Mbunge ni wa Chama gani? Ni Mbunge wa CHADEMA, kuna jambo lolote la kiusalama hakuna! Nikawaambia basi mwachenii aongee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine lilitokea la *misinterpretation* mkoaa mmoja, Maaskofu waliandaa kongamano lao, wanafanya kongamano lao wameshaweka vyombo pale wameshaweka maturubai, wameshaita wahubiri wao kikatoka kibali wasifanye mikutano, nauliza kwa nini, yule mmojawao pale akaja juu kwangu, nilivyouliza kwa nini mmewazuia, wakasema unajua Mheshimiwa Rais

4 MEI, 2018

amezuia mikutano, nikawauliza amezuia lini? Kwa hiyo nikawaambia waruhusuni waendelee na mikutano yao. Sasa wewe ukishapata jambo hilo ukatulia tu na huku tuko wote siku zote hapa, unatafuta kutengeneza taswira ya juu yako unayoilewa, huo siyo utaratibu wa Kiserikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twendeni kama tuna hoja tusaidiane, wala msitafute juu wala msitafute taswira, hapa tuliko hapa juu zote ziko hapa, mbona mambo mengine mkiyapata hapa mkitoka kwa Waziri mnaenda juu nyingine iko hapa hapa? Kwa nini tunataka kutengeneza na yenyewe iwe story. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hoja nyingine mlizosema za ufanyaji wa kazi za Kibunge Wabunge wote ni daraja moja, kazi za kibunge Wabunge mnatakiwa kufanya kazi za Kibunge, tusichanganye taratibu, tufanye kazi za Kibunge kwa taratibu na wala tusitengeneze ajenda ambazo zinatugawanya badala ya kutuunganisha kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Hebu kaeni chini tumalize kazi.

4 MEI, 2018

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu akidi ya Wabunge hajatimia.

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Katibu

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuko kwenye mshahara wa Waziri

Kif.1001 *Administration & HR Mngnt.....Sh. 14,138,386,221/=*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majina nimeshapokea ya vyama vyote tunaanza na Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anajibu hoja za Wabunge mbalimbali alizungumzia jambo la Mashekhe wale wa UAMSHO. Jambo hili ni jambo ambalo limegusa sana hisia nadhani unaweza ukaona hata michango ya Waheshimiwa Wabunge ilivyokuwa, sasa wakati anaendelea kutoa ufanuzi kulitokea kidogo sintofahamu upande wa pili kiasi kwamba hatukuweza kupata muafaka wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa tupate ufanuzi wa kutosha katika jambo hili ili hii sintofahamu iliyoko Bungeni pia iliyoko nje ya Bunge iweze kuondoka na kama majibu ya Serikali yatakuwa hayaridhishi, nakusudia kuondoka na shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kueleza niliyokuwa nimeyaanza

kuyaeleza kwamba kesi hii ni kesi ambayo inahusu makosa ya ugaidi. Ni jambo lisilopendeza kwamba tumekuwa tunaangalia sana hadhi na heshima ya wale watu ambaao ni lazima iheshimiwe kwa sababu ni Mashehe lakini kikubwa hapa ni suala la ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya Kupambana na Ugaidi uko utaratibu wa kukusanya ushahidi. Ushahidi wa maandishi, ushahidi wa mawasiliano na ushahidi ambaao unahusisha makundi mengine ambayo yako nje ya nchi, ushahidi wa ndani kwa kiasi kikubwa umekamilika na ambacho kimekuwa kinasubiriwa kukamilika ni ushahidi kutoka nje ambaao ni mawasiliano yawe ni ya simu au ya *email*. Kwenye matatizo haya ya ugaidi mara nyingi pia inakuwa na mitandao ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Kupambana na Ugaidi ni jukumu la Serikali pia kuomba msaada kutoka nje, msaada huo umeombwa na tunachofanya ni kuhimiza kwa sababu na huko nje tulikoomba ushahidi na wenywewe wanao utaratibu wao kama sisi tulivyo na utaratibu, kwamba moja hawawezi kutoa ushahidi huo mpaka wawe wamejiridhisha baadhi ya mambo ya msingi kwa sababu ushahidi huo kama nilivyosema mwisho wa siku kosa hili adhabu yake ni kubwa, ni adhabu ambayo ikidhihirika na kama maisha ya watu yamedhurika maana yake watu hao kwa mujibu wa sheria yetu adhabu yao ni kubwa ambayo inaweza kuwa ni kifungo cha muda mrefu au hata wao kuhukumiwa kuwaondoa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jitihada zote zinafanyika ili kukamilisha ushahidi wa ndani na wa nje. Niseme kwamba ushahidi huu ni lazima ufanyike kwa makini kwa sababu mambo haya hayafanyiki kwa njia ya uwazi na kwa namna ambayo kila mtu anaifahamu. Kwa hiyo nipende kuwahakikishia Watanzania wote kwamba ushahidi kwa kiasi kikubwa wa ndani umekamilika kwa maelezo ya anayehusika ushahidi wa nje nao unakuja, mara baada ya kuwa umekamilika watu hawa watafikishwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yetu kwamba kipindi hicho haki itatendeka, lakini kama hawaridhiki bado wana nafasi ya Wanasheria wao kwenda Mahakamani kuomba afua nyingine yaani afua kiingereza chake ni *intervention*. Kwa hiyo wanaweza wakafuata afua nyingine za kisheria kuwasaidia kuhakikisha wanapata haki yao, kwa sababu mpaka sasa ni watuhumiwa na hawajahukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama watuhumiwa bado wanazo haki nyingine na Wanasheria wao wamefanya hivyo na wameshakwenda Mahakama Kuu na wanakwenda Mahakama ya Rufaa, ni imani yetu kwamba kwa yale ambayo yako ndani ya uwezo wa Mahakama katika hatua za mwanzo Mahakama itafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina hii ya makosa yananyimwa dhamana siyo kwa sababu tunapenda kuwaweka ndani lakini ni makosa ambayo wakiwa nje wao wenyewe wanaweza kuhatarika pia ni makosa ambayo ni rahisi mtu kutoweka au kupotea. Kwa hiyo, nawasihi watu wote pamoja na kwamba jambo hili liko hivyo, tutambue kwamba tunapambana na matatizo ambayo ni makubwa siyo tu Tanzania, Afrika ya Mashariki na duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona yalitokea nchi ya jirani jinsi vijana wa Chuo Kikuu walivyoshambuliwa na watu walivyouawa, tumeona yaliyotokea Uganda, lakini sisi pia tuisahau yaliyotukuta wakati Ubalozi wa Marekani uliposhambuliwa. Kwa hiyo ni jambo ambalo linahitaji umakini na ushahidi wa ndani umekamilika, ushahidi wa nje utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri ambayo kiasi fulani yanaleta nafuu, yanaonekana yana maana lakini

tunachozungumza hapa kuna suala ambalo ni haki ya kiraia ya hawa watu, pia hawa ni viongozi wa dini ambao wanagusa imani za watu, sasa sina haja ya kufika huko kwenye kushika shilingi, lakinii nataka sasa tupate *commitment* kwamba baada ya hayo mambo kwamba tumetafuta ushahidi wa nje na kadhalika umekamilika, ni lini sasa watu hawa watapelekwa Mahakani na kesi ianze kusikilizwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama niliyoyeleza kwa mujibu wa Ibara ya 59(b) na sheria ya *National Prosecution Services Act*, mtu pekee mwenye mamlaka ya mwisho ya kuamua lini hawa washtakiwa wapelekwe Mahakamani ni Mkurugenzi wa Mashtaka, wote haturuhusiwi kumshinikiza. Kama wapo watu ambao wanaona Mkurugenzi wa Mashtaka anachelewa kama nilivyo sema, chombo pekee kinachowezwa kumuita Mkurugenzi wa Mashtaka na kujua amefikia hatua gani ni Mahakama peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu Mkurugenzi wa Mashtaka atakapokuwa ameridhika na ushahidi atalipeleka suala hili Mahakamani. Tumetunga wenyewe Katiba kumlinda Mkurugenzi wa Mashtaka, Ibara ya 59 tumetunga wenyewe Sheria ya *National Prosecution Services Act* ya kumlinda na kumlinda huko ni kumzuia kumpa mashinikizo na ndiyo maana yametokea mabadiliko makubwa katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hana *security of tenure* amebadilishwa, DAG hana *security of tenure* amebadilishwa, DPP amebaki kwa sababu Sheria na Katiba inamlinda na huyu Rais ameheshimu hilo. Kwa hiyo, mara baada ya kuwa imekamilika na mimi nitaendelea kumshauri kwa sababu siwezi kumwamuru, kumshauri kwamba kwa haraka inavyowezekana suala hili lipelekwe Mahakamani ili likamilike. (*Makof*)

4 MEI, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesikiliza kwa makini sana hitimisho la Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuhusiana na jambo la watu kupotea, watu kutekwa, watu kuuawa na wakati mwingine kutishiwa na mambo kama hayo. Nataka kuelewa jambo hili limekuwa likijirudia sana na jambo la namna hii linapojirudia na ni jambo bayo linaitia doa nchi yetu siyo jambo ambalo unaweza ukalitolea maelezo tu halafu ikaishia hapa, nadhani linahitaji mkakati unaotosheleza kuhakikisha kwamba jambo hili haliendelei kusemwa au kutokea na kuitia doa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mkakati wa kihalsia wa Serikali juu ya mambo haya, Serikali ina mkakati gani, mambo haya yasiendelee kutokea na kuendelea kuitia doa nchi yetu. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jambo hili lina *dimensions* nyangi. Kwanza jambo lenyewe kama liliyvo kwa maeneo ambayo ni *evident* kwamba kuna utekaji umefanyika ni jambo la uhalifu kama uhalifu mwingine. Utaona kwamba katika kipindi ambacho matukio yamejitokeza kama nilivyosema siyo nzuri sana kutaja masuala haya kwa sababu yameacha makovu kwenye familia, ilitokea watoto wadogo ambao hawana vyama vya siasa wala hawana madeni tukiona waktekwa na wengine hata kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo Serikali imejidhatiti kukabiliana nalo kama ambavyo uhalifu mwingine ambavyo tunakabiliana nao. Utaona kwenye jambo kama hilo tuliweza kumuokoa mtoto mwingine akiwa mikononi mwa watekaji pia kuwapata wale waliokuwa wanafanya matukio ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halijaishia hapo tu, kuna masuala mengine ambayo yameendelea kujitokeza kama ya akinamama tumeona katika upande wa Kanda ya Ziwa ilijitokeza katika kipindi fulani kilichopita upande wa watu wenyewe ulemavu, ilijitokeza kwa vikongwe, kwa hiyo haya ni mambo ya matukio ya uhalifu kama uhalifu mwingine na tunaendelea kujizatiti kwa upande wa idara yetu ya intelijensia kujizatiti upande wa doria, kujizatiti upande wa kukabiliana na matukio hayo kwa sababu ni uhalifu. Hatuna *negotiation* na uhalifu kuwaambia kwamba sasa msifanye uhalifu, bali tuna njia moja ya kukabailiana nao kuweza kuhakikisha kwamba tunakomesha uhalifu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba haya ni mambo ambayo tunajizatiti nayo kuweza kuhakikisha kwamba tunakabiliana nayo ni uhalifu kama ambavyo umetokea maeneo mengine hata yale ya Kibiti, watu walikuwa wanavamiwa tu na wenyewe ni uhalifu kama huu anaousemea, lakini tumeendelea kukabiliana nao. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa dira hiyo, hakutokuwepo kitongoji kimoja ama mtaa mmoja ambao wao wataweza kusema kwamba kwa uhalifu wamekithiri na Serikali haiwezi ikashughulika nao, tutashughulika na uhalifu wowote ule na tutakomesha mambo ya aina hiyo ambayo yanajitokeza na kugharimu maisha ya watu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimemkiliza Mheshimiwa Waziri vizuri wakati anahitimisha taarifa yake kuhusiana na suala la uhamiaji. Suala hili limekuwa na shida sana katika Mkoa wa Kigoma. Mfano, wanapoita vijana kuwahoji kwamba wao ni raia au siyo raia, vijana wale wanakuwa mfano mzuri ni mimi, babu yangu ame-*paralyse* ana miaka 20 ndani, juzi wakamkamata mdogo wangu wanasema ili wamuachie na wahakikishe kwamba ni raia lazima wakambebe yule mzee wa miaka 20 yuko ndani ame-*paralyse* akatoe ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha tu hivyo sisi hatukatazi Uhamiaji kufanya kazi yao. Tunatambua kwamba uhamiaji wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria, lakini tunachoomba, kazi hizi za kutaka utambuzi nani ni raia nani wanamtilia mashaka wazifanye kwa uweledi, wakifanya kwa weledi hata wanasiasa hatuwezi kuwapigia kelele kwa sababu tunajua kwamba mionganoni mwa baaadhi ya ambao siyo raia ndio wanaotumia uhalifu wa silaha kama alivyosema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka *commitment* hapa kwa Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwa wale wananchi wa Mkoa wa Kigoma wanaokuwa *harassed* na uhamiaji wa Mkoa pamoja na Maafisa Uhamiaji wa Wilaya, kama nisipopata *commitment* inayoeleweka nitatoa shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* yake. Tunamjua Mheshimiwa Mbunge huyu ni mwanamke shupavu kweli na hasa yanapokuja masuala ya wananchi wake hana mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jambo moja kwamba, moja tuwatoe hofu Watanzania, kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja pale kwamba mambo haya siyo ya ugomvi, lakini hulka ya Watanzania si tu wengine hata mimi sikuzoea masuala ya kuhojiwa. Nakumbuka nimekuja kuingia kwenye vituo vya Polisi baada ya kuwa Kiongozi wa Idara hii. Kwa hiyo Watanzania hawajazoea haya mambo ya kuhojiwa, ndiyo hayo wanayoona kama *harassment*, lakini kwa manufaa ya mazoezi tunayoendelea ni lazima watu tuhujiane, ni lazima watu tuwe na vitambulisho ambavyo vitatutambulisha, pia lazima tutambue mwuingiliano wa jamii zetu ambazo tunazo, kwa hiyo kwa taasisi yetu hii ili iweze kujiridhisha kwa kweli ni lazima ifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie siku ambayo mtataka taasisi hii isijiridhishe tutakuwa tumefungua mlango vibaya sana kwa wale walio wahalifu kuweza kutumia fursa hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge pamoja na sisi kupokea hoja yake ili tushughulikie yale yaliyo ya kimaadili ikitokea ukiukwaji wa kimaadili, hayo tutayafanya kazi, lakini yale yanayohusu utendaji wa kazi ambaao kwa kweli msingi wa hiyo kuwa ni udhibiti tuwaruhusu waendelee kudhibiti ili watu ambaao watapata vitambulisho vyta uraia wawe kweli ambaao walio raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambaao hawana nchi nyingine ni Watanzania wa hapa tumesema tu waelezee *status zao* wala watu wasione haya kusema wazazi wao walikuja siyo raia na wao walipozaliwa hawakuwa raia, lakini wamezaliwa na nchi yao ni hii, tumesemeari hiyo kwamba sheria inatambua watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi njema sana tuna hata watu ambaao walikuja siku nyingi chungu nzima wapo ambaao walishaloweaa wako hapa, wala hakuna siku Tanzania ambaao imeenda kuwaswaga kuwaondoa. Kwa hiyo Watanzania wasiwe na hofu sana yanapotokea masuala haya, tunafanya hivyo ili kuweza kuwabaini wale walio wahalifu ama wale wasio Watanzania, wale ambaao hawastahili kupata haki hizo ambazo wanatakiwa wapate Watanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Waziri anashindwa kunielewa vizuri. Mheshimiwa Waziri hatukatazi Uhamiaji kufanya kazi yao, tunachokataa ni watu kuvamiwa usiku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwilima hukutoa hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ili nishike shilingi ili watu waweze kulijadili hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa someni Kanuni vizuri, hakuna hoja ya kuungwa mkono watu 10 akishasimama akisema anaweza kuendelea peke yake tu pale. Someni Kanuni hizi vizuri mzielewe. Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Rashid A. Shangazi, mtoho hoja wewe kaa, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Hussein Bashe. Tunaanza na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na kwamba suala hili ni la kisera lakini maeleo aliyotoa jirani yangu Mheshimiwa Hasna Mwilima imenibidi na mimi nisimame niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na Jeshi la *Immigration*. Nilidhani Wabunge tungejadili au mtoho hoja angetoa hoja ya kuomba bajeti ya Jeshi la *Immigration* iongezwe ili iweze kukabiliana na wimbi la ongezeko la wakimbizi, badala yake analituhumu Jeshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu natoa mfano, tunalima sana na wafanyakazi wengi wa kulima ni Warundi ambaao ni wakimbizi, lakini Warundi wanaongea kama Waha wa Kigoma na kule wale wakimbizi wanakaa kule mashambani. Tunavamiwa na kikundi cha watu zaidi ya 20.

**MHE. KABWE. Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Jeshi letu tunapoenda kulalamika, linaenda kufanya operesheni, wanakamata watu na *SMG*, vitendo ambavyo sisi....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma muda wako umekwisha. Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hasna kwanza nimwombe ili tusonge mbele amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi, lakini nimuunge mkono

katika muktadha ufuatao kwamba, kwanza nchi yetu imezungukwa na nchi zaidi ya sita, saba hadi nane na kwa jiografia yake na mengine wanaendelea katika nchi nyingine hata ambazo hazina mapigano ni nchi inayovutia watu kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa ni nchi ambayo inavutia watu kuja huwezi ukaacha mambo yaende holela holela. Hata hivyo, ni vizuri katika kule kudhibiti, kuendane na taratibu na mila na staha ya Kitanzania, kwa hiyo namwomba amrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi lakini na Serikali iendelee kufanya kazi kwa weledi kama ambavyo mwenyewe amesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofj*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mwilima ni kwamba Maafisa Uhamiaji kwenda kufanya shughuli zao usiku, anasema ni kuwavamia wananchi, lakini akumbuke kwamba Majeshi haya yanapongezwa humu ndani kwamba wanafanya kazi kubwa ikiwemo na kufanya kazi usiku. Wanapofanya kazi usiku, usiku ndipo wahalifu huwa wanafanya uhalifu zaidi ya mchana. Pia wakumbuke kwamba mikoa ambayo ipo pembezoni lazima itapata misukosuko...

(*Hapa Mheshimiwa Zitto Z. R. Kabwe alizungumza bila utaratibu*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto tupo Bungeni hapa, kaa chini, *No! No!* kaa chini. Mheshimiwa Zitto kaa chini. Mheshimiwa Zitto nitakutoa nje, Mheshimiwa Zitto kaa chini. Tafuta utaratibu wa kusema, siyo hivyo unasimama, hapa siyo sokoni wala siyo Ujiji. Kaa chini! Mheshimiwa kaa chini.

(*Hapa Mhe. Kabwe Z. R. Zitto aliendelea kuongea bila utaratibu*)

4 MEI, 2018

Waheshimiwa Wabunge, *no!* hata wewe unafanya kosa kubwa sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kosa gani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kaa chini! Hatuzungumzi ukabila wala mikoa hapa, tunazungumzia *issues*, unaendela bado kusema? Mheshimiwa Zitto kaa chini. Mheshimiwa Lugola muda umekwisha, kaa chini. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewane tu. Hoja anayozungumza Mama Hasna ni kwamba, tunachokikataa watu wa Kigoma ni *harassment* ambazo ni *unnecessary* ndiyo hoja iko hapo. Hatukatai Uhamiaji kufanya shughuli zao, lakini haiwezekani uhamiaji wawe wanafuata watu usiku wa manane, uhamiaji hao wanaweka siku za soko, wanafunga njia Manyovu pale, ndiyo tunachokikataa, *harassment* ambazo ni *unnecessary* ndiyo tunachokikataa, wala Waha hawajawahi kuwa Warundi hata siku moja! Tuelewane vizuri humu ndani.

**MHE. KABWE. Z. R. ZITTO:** *Yes!* actually huyu anaonekana Mrundi zaidi kuliko Waha. (*Kicheko*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji tunawahitaji wafanye kazi zao, watu wa mipakani tunajua kazi zao. Hoja ya msingi ni kwamba wafanye kazi kwa weledi na kwa staha na kwa mila za Watanzania. Ndiyo hoja iliyoko mezani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaombe Wabunge kama nilivyosema tangu mwanzo tunapokea hoja na lengo letu ni kujenga. Tunapokea hoja, wala wasigombane. Jambo moja la msingi ambalo hoja imeletwa na mtoa hoja, tumeshamhakikishia kwamba pale panapotokea matatizo ya kimaadili kama Wizara tunafanya kazi, kwa sababu tunesema yale ambayo

siyo ya kikazi wala sio ya kimisingi ya kazi, tunayafanyia kazi. Nilizungumzia yale yaliyo ya kazi ndiyo hayo ambayo tunatakiwa tulachie Idara iweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hatuwezi tukawabagua wananchi kwa misingi ya mikoa yao na mazoezi ya aina hii yanafanyika katika kila mikoa lakini pale ambapo watu wameenda kufanya msako tena huwa siyo kila familia ni pale ambapo wana dondoor kwamba panaweza pakawepo na jambo (a), (b), (c), (d).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na hasa Wabunge wanaotokea Mkoa wa Kigoma niwahakikishie kwamba hoja tunazipokea na yale ambayo hayaendi kwenye miiko ya kiutendaji tutayafanyia kazi, lakini yale yaliyo ya kazi hata ninyi tunawaomba watuunge mkono na wao wanatambua. Mheshimiwa mtoa hoja, anajua kwamba Wizara tunatambua kazi yako na tunatambua jinsi ambavyo anatetea haki za wananchi wako, basi aridhie kwamba yale kama kuna yalitokea kiukwiukaji basi tutayafanyia kazi, lakini yale ambayo yanajenga ustawi wa nchi yetu kwa maana ya kuhakikisha kwamba wahalifu hawapenyi, aturuhusu hayo tuweze kuendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe arudishe shilingi yangu na tuweze kuendelea na tuwaruhusu wenzetu wa Uhamiaji waweze kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Kabwe Zitto, tunawapenda watu wa Kigoma na tunapenda mpaka migebunga yao, kwa hiyo hatuwezi tukawatenga wakati tunatarajia na tunapenda Kigoma ni moja ya *potential* ya uzalishaji wetu. Tunachosema tu ni kwamba, ni ukweli usiopingika kwamba Kigoma pia ukienda kwenye historia, ndiyo mkoa uliowahi kupokea wageni wengi kuliko mikoa yote. Kigoma ndiyo Mkoa ambaa umepokea kambi za wakimbizi nyingi sana. Kwa maana hiyo, tunapofanya shughuli hizi tuna maana ya kuwasaidia wananchi wa Kigoma. Kwa hiyo, waridhie tu tutarekebisha yale yaliyo na kasoro lakini hatuna maana ya kubagua wananchi wa

Kigoma na pale yalipotokea matatizo ya kiutendaji yale tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe dada yangu arudishe tu shilingi. Tumeyapokea na tutaendelea kuwasiliana *case by case* kama kuna jambo litakuwa linajitokeza katika Jimbo lake na maeneo mengine ya Mkoa wa Kigoma. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, tulipitisha sheria na sheria was very specific, maeneo ambayo uhamiaji wana access ya kuvamia na kuingia popote ilibidi Afisa wa Cheo Maalum Kilichotajwa ndiyo anaruhusiwa kufanya hiyo kazi, siyo mtu ye yote tu wa uhamiaji anakwenda kufanya hizi kazi. Kwa hiyo, walivyosema mnafuata utaratibu, mfuate na sheria kuwa mnapofanya kazi ni Afisa wa cheo maalum ana access ya kuingia popote na akafanya kazi yake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme siyo kwamba tunasema Mkoa wa Kigoma tunabaguliwa, lakini tunaona ni mikoa mingi ambayo ipo mpakani, *harassment* tunayoipata Kigoma hakuna mkoaa wowote wa Tanzania ambaa unapata *harassment* na uhamiaji kama Kigoma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tunaomba hili alielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikairejesha hiyo shilingi lakini kwa *commitment* moja ya Waziri. Hii ni mara ya pili naongea hapa Bungeni, kulalamikia abiria kushushwa kwenye mabasi kuanza kupekuliwa, mmoja baada ya mwingine, nani raia na nani siyo raia. Hivi kwa nini hili jambo lisitolewe leo *commitment* hapa kwamba llnasimamishwa? Wananchi hawasafiri na amani, tunavyoongea hamtuelewi lakini watu wa Kigoma tunaongea kitu ambacho ni *reality*, kinafanyika ndani ya mkoa. Naomba hiyo *commitment* ya Waziri.

4 MEI, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwilima.  
Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuna mambo mawili hapa ambayo umetoa. Moja hilo ulilolitoa ambalo ni la kisheria tumelipokea na tutalifanya kazi, lakini hili la Mheshimiwa Mbunge tukubaliane tu kwamba hatutafanya kuwa ni utaratibu kama ambavyo umeshatolea ambavyo siyo utaratibu kwamba kila siku watu usiku wawe wanapekuliwa mpaka ambapo pana jambo mahsus. Hata hivyo, hatutaweza kusema kwamba kuanzia sasa hatutafanya misako hiyo kwa sababu tukitangaza hilo tutakuwa tumeruhusu wahalifu nao kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, tutakachofanya kama ambavyo umesema, tutafanya mambo haya kwa umahsus, hatutaweza kuacha kama tuna taarifa kwamba kuna jambo la tatizo halafu tukaacha. Kwa hiyo, tutazingatia hicho ulichokisema, kufanya jambo hilo kwa utaratibu na kuweza kuhakikisha kwamba kazi za Wizara zinaendelea na kazi za idara zinaenda.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwilima maliza hoja yako.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, unajua wenzangu wanapopiga makofi hapa ni kwa sababu hawajapata adha tunayoipata Kigoma. Kama mngepata adha tunayoipata Kigoma...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, narudisha shilingi, lakini Waziri nitaongea naye pembeni kuhusiana na Uhamiaji wa Wilaya yetu.

**MWENYEKITI:** Jambo la muhimu! Ahsante. Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa napitia kabrasha hapa la Wizara nimeona kuna *vision* ya *Ministry of Home Affairs and Police Service* na ninaomna ninukuu. *Vision* inasema kwamba; *to be professional Police Force that ensure security of people and property of the United Republic of Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia kwenye *mission* ya Wizara hii inasema: *to provide high level Police Services for the purpose of education, preventing and combating crime in the United Republic of Tanzania.* Hiyo ndio *vision* na *mission* ya Jeshi la Polisi Tanzania ikiwa na kazi ya kutoa huduma badala ya kutumia *force*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja amejaribu kuzungumza kwa mapana sana suala la bodaboda Tanzania. Kumekuwa na tatizo hili la muda mrefu sana na mimi kama Mbunge nimeweza kuchangia kimaandishi kwamba, vijana wetu wengi ambao walikuwa wahalifu baada ya kuingia pikipiki hizi Tanzania, wengi wameacha uhalifu na wanajishughulisha na kazi hizi za bodaboda na wanajipatia riziki, lakini Jeshi la Polisi limekuwa linawakamata na pikipiki zinashikwa sana, zinawekwa sana kwenye vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelekezo ya Serikali kwamba wamejipangaje ili kuondoa hili tatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama kuna eneo ambalo lina changamoto sana kwenye ajali za barabarani ni bodaboda. Bado waendesha bodaboda wamekuwa wagumu sana kufuata sheria, hata hivyo, moja ya jitihada ambazo tunafanya ni kutoa elimu. Tumekuwa na utaratibu mzuri tu wa kuwaelimisha makundi mbalimbali ya bodaboda kupitia kwenye vijiwe vyao ili waweze kufuata Sheria za Usalama Barabarani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipatiwe maelezo ya kina. Naomba nipatiwe maelezo ya kina juu ya nyumba na makazi ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wana makazi duni sana ambayo yanababisha kushindwa kufanya kazi zao vizuri, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu, nimemsikiliza kwa makini sijaona kama kuna mkakati gani wa Serikali au Wizara wa kuhakikisha Askari wetu wanapata nyumba zilizo bora mno. Kwa hiyo naomba *commitment* ya Serikali, naomba mkakati wa Serikali, wana mkakati gani wa kuwajengea nyumba askari wetu ili waishi mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika na maelezo, naomba kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilifafanua wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nilisema kwamba, tumeshaanza ujenzi wa nyumba kwa baadhi ya vyombo ambavyo viko chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi na katika hili lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka yangu naongeza nusu saa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Polisi kama Mheshimiwa Mattar Ali alivyozungumza, nimeeleza kwamba hivi sasa tunavyozungumza tuna ujenzi wa nyumba 12 ambaao unaendelea Pemba ikiwa ni mkakati wa ujenzi wa nyumba kwa kuanzia na nyumba 36, ukiacha hivyo hii ni nje ya *program* ile ya fedha hizi bilioni 10 ambapo pia zitagawiwa kwa ujenzi wa nyumba upande wa Unguja na upande wa Pemba. Kwa hiyo, swali lake kwa nilivyoolewa ni kwamba kimsingi tumeanza vizuri katika hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona majibu hayakuniridhisha, naomba kutoa hoja Wabunge wenzangu wanisaidie ili tuweze kulijadili hili suala kwa makini. Naomba kutoa hoja.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kutajwa jina haina maana utapata nafasi, natazama na muda unavyokwenda na Wajumbe wengine ambao wana hoja zao katika mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Askari wetu wana maisha magumu na mazingira magumu sana wanapoishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa mengine duniani ambayo yamefanikiwa kwenye kila jambo yalihakikisha wale wanaosimamia *rule of law* wamepewa mazingira mazuri ndio maana yameendelea. Hata hivyo, Tanzania, askari wetu ninyi Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi, wanakaa *line Police*, wengine hata nyumba hawana tunakaa nao mitaani, hii ni kuwaweka kwenye mazingira ambayo yanaweza kuwafanya wakapata madhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tumekuja hapa, tangu niwe Bungeni hapa Wabunge tunasema sana juu ya maisha ya askari wetu na Serikali hajjawahi kuleta mkakati unaoonekana kweli kwamba wanaondoa hili jambo, wanahakikisha hawa askari wetu wanakaa kwenye nyumba nzuri. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa hapa nikiomba pia kwamba Serikali kwa kweli itoe *commitment*. Watakuwa na mradi maalum wa mkakati maalum kuhakikisha Askari wetu wanaondoka kwenye mazingira haya.

4 MEI, 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano kule Nzega, Wilaya ambayo ilikuwa ndiyo...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Namwomba tu Mheshimiwa Mattar arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu kuu mbili. Moja, Serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba inajenga nyumba za askari. Tunafahamu ni kweli kabisa usiopingika kwamba askari wetu wana shida na makazi na kutokana na hili ndiyo maana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua nyumba za askari Mkoani Arusha hivi karibuni aliliona hilo na akasema kwamba anatoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba nyumba za askari zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia akatolea mfano na kusema kwamba njukumu letu pia hata Waheshimiwa Wabunge katika pesa za Majimbo wanazopewa kuhakikisha kwamba wana-*contribute* kuhakikisha tunajenga makazi ya askari wetu. Kwa kufanya hivyo tutakuwa pia tumesaidia Serikali na tumehakikisha kwamba pia tunaboresha makazi ya nyumba za Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali bado tuna kazi ya kuhakikisha kwamba askari wanapatiwa makazi bora ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Hata hivyo, mimi ambaye nilikuwa Askari Polisi nikiangaja hali tulyokuwa nayo zamani ambapo mimi nilipanga uraiani kwa kukosa nyumba lakini baadaye nikaishi kwenye makazi duni ya Polisi. Ukiangalia kwa sasa hivi kwa kweli Serikali imefanya kazi kubwa sana kiasi ambacho askari wengi mikoa ya Tanzania mpaka na Zanzibar makazi yanaendelea kuboreshwa na ghorofa

zinaendelea kujengwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba urudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Serikali ina dhamira njema na ndiyo maana Mheshimiwa Rais aliwapongeza askari akasema katika kipindi cha Awamu ya Tano atahakikisha askari wanapata makazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri una jambo la kuongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama nilivyozungumza mwanzo kwamba tumeimarisha kikosi chetu cha ujenzi kwenye Jeshi la Polisi na tumeweza kusajihisha wadau kushirikiana na Serikali katika kukwamua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi mbali ya hizo fedha ambazo zimetolewa na ujenzi unaanza wakati wowote pia katika siku za karibuni tumepokea takribani bilioni 1.3 ambazo tutazitumia kwa ajili ya kumaliza yale majego ambayo yamefikia katika hatua za mwisho Musoma na Mwanza. Kwa hiyo, niendelee tu kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mattar Ali kusaidia kuhamasisha wadau waweze kuongeza jitihada ya nguvu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya makazi ya Polisi haiwezi kutatuliwa kwa mara moja, lakini hapa tulipoanza tumeanza vizuri kwamba nyumba 400 ambazo zinatarajiwa kujengwa hivi karibuni ukiachilia mbali nyumba zingine ambazo nimezungumza zimejengwa kwa nguvu za wadau ni hatua ya kupongezwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Wakati anatoa majibu Mheshimiwa Waziri amesema askari hawa hawalali kwa kutulinda na kiukweli askari wetu wanafanya kazi nzuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar katika hatua hii ni

mawili unarudisha shilingi au unakwenda kwenye kupiga kura.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarejesha shilingi lakini nina maoni kidogo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwonekano wa Jeshi letu la Polisi kwa wananchi hauwavutii, hauwavutii kwa maana matendo mengi ambayo wanayafanya yanaonesha kama wamegeuka kuwa watesaji, waonevu na wanaokinzana na taratibu ambazo tumejiwekea. Kwenye vituo vyetu vya Polisi leo hii vimegeuka kuwa ni vituo vya kutesea watu, vituo vya uvunjivu wa sheria vya kuwatoza watu fedha bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaoaminika kuwa watuhumiwa wanawekwa vituoni kwa muda mrefu bila kufikishwa Mahakamani. Mtu anakamatwa hana leseni labda ya bodaboda, anawekwa kituoni siku tano hadi siku kumi. Wanapita Polisi mitaani jioni wanakamata watu wanaowaita wazururaji, wanawapeleka vituoni, wakifika vituoni ndugu kama una fedha unaenda unamlipia unamtoa, wale ambao ndugu hawajaenda kuwalipia au ndugu hawana fedha ya kuwalipia, wanaendelea kushikiliwa vituoni kwa siku zisizokuwa na idadi na hawapelekwi Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yamekuwa mengi sana kwenye maeneo yetu ya mijini ukienda huko vituoni unawakuta watu wamejazana, hawapelekwi Mahakamani wanateswa, wanapigwa huku wameendelea kurundikana Polisi na wengine wanaumwa hali zao ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua nini utaratibu, Serikali imejipangaje kuhakikisha inakuja na njia mbadala ya kukomesha vitendo hivi ili ile taswira nzuri ya Jeshi la Polisi iendelee kuwepo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mambo mawili; moja tunahitaji sana Polisi na tunahitaji sana vituo vya polisi, hata kwenye maswali na michango utaona hata Wabunge tunakubaliana kwenye hili kila Mbunge anaomba vituo vya polisi na vitendeakazi Jimboni kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba pale panapotokea vitu ambavyo haviridhishi na vinaudhi tumepokea kesi za aina hiyo, kama nilivyosema mwanzo Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vya dola ni vyombo vinavyoongoza sana kuchukua hatua pale maadili ya kazi yanapokuwa yamekiukwa ambayo yanababisha kupaka matope taasisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama tuna maeneo ambayo kuna *case by case* umelisemea kwa hisia sana jambo hili na hata Mheshimiwa Goodluck Mlinga wakati anachangia alilisemea kwa hisia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki kubishana na Wabunge pale wanapotuletea jambo ambalo linahusu ukiukwaji wa maadili ya kazi. Sisi kama Wizara yale yanayohusu ukiukwaji wa maadili ya kazi tunapokea na tunaahidi kwamba tunafanya kazi, hata Mheshimiwa Rais alipomteua Inspeksa Jeneral alielekeza kufanya *reform* kwenye Jeshi la Polisi na hata alipoteua Kamishna wa Uhamiaji alielekeza hivyo hivyo kufanya *reform*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi tulipokuwa Arusha na wewe ulikuwepo Mheshimiwa Rais alielekeza kuondoa makondokando, zile kero kwa wananchi ambazo zinasababishwa na taasisi zetu hizi. Vitu vya aina hii wala hatubishani na Mheshimiwa Mbunge tumelipokea na kwa sababu hata *Inspector General*yupo na Wakuu wengine wa vyombo ambavyo viko ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani wapo, yale yanayokwaza wananchi wetu hata kuona hasira na taasisi zetu ni mambo ambayo hata sisi hatukubaliani nayo, tutayaafanya kazi ili kuweza kuhakikisha tunachukua

4 MEI, 2018

hatua kwa wale ambao wanafanya hivyo na kusababisha taswira ya taasisi zetu ziweze kubadilika ili taasisi zetu zifanye kazi zilitokusudiwa na ziweze kuungwa mkono na wananchi taasisi zetu zinapofanya kazi hizo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru natoa shillingi kabisa ili nisije nikafanyiwa *trick* kama iliyofanywa huku. Kwa hiyo, shillingi nimeitoa kwa sababu nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri majibu yake alipokuwa anatoa ufanuzi wa suala la watu kupotea. Kwanza ielewewe hakuna Mbunge anayepigania *dignity* na uhai wa mtu ambaye ana lengo la kuchafua taswira ya nchi ila wanaotaka kuzuia mijadala ya aina hii ndiyo wanaotaka kuchafua taswira ya nchi. Mtu mmoja thamani yake ni kubwa sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema kaa kwanza, kwa mujibu wa kanuni zetu jambo ambalo limeshafanyiwa maamuzi ndani ya Bunge na limepitishwa hapa limezungumzwa nafikiri na Mashimba halirudiwi tena.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizumnguza bila kufuata utaratibu*)

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza kuongea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwa Kanuni, nimeshaisikia hoja yake, unabishana na mimi sasa? Ameshazungumza hoja yake na ameshasema amem-quote Waziri na Waziri aliyetoa majibu, haya Mheshimiwa Lema *benefit of doubt*.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri unataka kuwa Spika kwa sababu *style* yako siyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema endelea .

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni

4 MEI, 2018

kwamba mimi hapa nina jina nitampa *IGP* la mtu ambaye inasadikika ndiye aliyemuua Daniel John, nina jina na namba ya simu. Sasa tunaposema watu wanaendelea kupotea hatujaridhika kama Kambi. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba Inspeka Jenerali wa Polisi katika Gazeti la Mtanzania la Novemba 30, 2017 alikiri kwamba Kibiti kuna watu 1,300 wamepotea alinukuliwa na gazeti. Kwa sababu jambo hili ni kubwa naomba...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Haya mwenye hoja Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke sawa hili jambo alilosema Mheshimiwa Lema. Inspeka Jenerali hakusema watoto wamepotea, alisema hawako mashulenii. Hii *absconding* kwenye mashule hata Tabora, hata Iramba ipo, aliongelea watoto ambao hawako mashulenii na Serikali tulisema tu tuhamasishe ufuutiliaji ndiyo maana mnaona Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wanafuutilia watoto ambao hawako mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *doubt* yetu ilikuwa kama watoto wanaweza wakakosekana mashulenii *equally* wanaweza wakawa wametoka kwenda kufanya mafunzo. Kwa hiyo, siyo kwamba alikuwa anamaanisha wamepotea, hawakupotea ni watoto ambao hawako mashulenii kwenye orodha. Hata Arusha wapo wanaokosekana ambao hawaendi mashulenii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema ngoja, Kiti kimejiridhisha hoja hii imeshajadiliwa.

*(Hapa Mhe. Godbless Lema alizungumza bila kufuata  
utararibu)*

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa Lema unao ushahidi wa kutosha na mimi nakushauri Mheshimiwa Lema unaye mtu ambaye una usahihi naye amefanya kitendo

4 MEI, 2018

hicho. Kwa mujibu wa sheria ukiendelea kukaa na jina hilo unakuwa ni *accessory to that process*.

Mheshimiwa Lema ngoja nikusaidie, kwa kuwa una jina hilo tayari na Vyombo vyta Ulinzi hujavikabidhi mpaka sasa hivi, umengoja kuja ndani ya Bunge ndiyo ukabidhi kwa *technic* uliyotumia, bado nakushauri hoja hiyo imeshajadiliwa na Waziri. Kwa mujibu wa Kanuni zetu na nakupongeza kwa jina hilo nakushauri kabla ya saa mbili kasoro robo leo mkabidhi jina hilo Waziri waanze kulifanyia kazi kisheria. Baada ya hapo utajikuta unaingia kwenye mashtaka ya *accessory*...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Bungeni hawezi kuingia, acheni vitisho bwana!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, ndiyo nasema akitoka nje na ushahidi huo. Mheshimiwa Lema hoja yako imeshakuwa *redundant*.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijamaliza hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kama ulikuwa na haja ya kutoka unaweza ukatoka tu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaendeshaje Bunge bwana!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kama ulikuwa una haja ya kutoka wewe unaweza ukatoka tu. Mheshimiwa Lema mnaweza mkaamua kutoka tu, naona mmeshikwa pabaya leo.

**MBUNGE FULANI:** Umeshikwa pabaya mwenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*..... Sh. 436,299,000/=

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Wenye akili hawatoki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ryoba hata kama unatoka unaweza ukachukuliwa hatua, Mheshimiwa Ryoba! Mmekaa kimya eeh. (*Kicheko/Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumzi bila mabadiiliko yoyote*)

Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..... Sh. 586,067,000/=  
Kif. 1004 – *Probation and Community Service Division*.....Sh. 2, 710, 848,379/=  
Kif. 1005 – *Government Comm. Unit* ..... Sh. 187,411,000/=  
Kif. 1006 – *Mgt. Information System Unit* ..... Sh. 364,137,000/=  
Kif. 1007 – *Internal Audit Unit*..... Sh. 202, 928,900/=  
Kif. 1008 – *Procurement Mgt. Unit* .....Sh. 357,162,000/=  
Kif. 1009 – *Complaints Division* .....Sh. 146,341,000/=  
Kif. 1010 – *Legal Services Division* ..... Sh. 533,762,000/=  
Kif. 4001 – *Refugees Unit* ..... Sh. 904,335, 500/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote*)

#### **Fungu 14 - Jeshi La Zimamoto na Uokoaji**

Kif. 3001 – *Fire and Rescue Service* .....Sh. 19,241,632,000/=  
Kif. 3002 – *Fire and Rescue Services Training Inst.* .....Sh. 544,420,000/=  
Kif. 3003 – *Fire Safety* .....Sh. 208,500,000/=  
Kif. 3004 – *Operations* .....Sh. 1,004,000,000/=  
Kif. 3005 – *Dar es Salaam Regional Office* ..... Sh. 816,300,000/=  
Kif. 3006 – *Arusha Regional Office* ..... Sh. 524,100,000/=  
Kif. 3007 – *Dodoma Regional Office* .....Sh. 401, 550,000/=  
Kif. 3008 – *Mwanza Regional Office* ..... Sh. 685, 050,000/=  
Kif. 3009 – *Mbeya Regional Office* ..... Sh. 303,300,000/=  
Kif. 3010 – *Kinondoni Regional Office* ..... Sh. 624,909,000/=  
Kif. 3011 – *Mara Regional Office* ..... Sh. 322, 500,000/=  
Kif. 3012 – *Kigoma Regional Office* .....Sh. 284,100,000/=  
Kif. 3013 – *Pwani Regional Office* ..... Sh. 519,300,000/=

Kif. 3014 – *Manyara Regional Office* ..... Sh. 288,600,000/=  
Kif. 3015 – *Geita Regional Office* ..... Sh. 216,600,000/=  
Kif. 3016 – *Temeke Regional Office* ..... Sh. 694,500,000/=  
Kif. 3017 – *Singida Regional Office* ..... Sh. 269,400,000/=  
Kif. 3018 – *Tabora Regional Office* ..... Sh. 401,550,000/=  
Kif. 3019 – *Iringa Regional Office* ..... Sh. 384,600,000/=  
Kif. 3020 – *Rukwa Regional Office* ..... Sh. 220,400,000/=  
Kif. 3021 – *Ruvuma Regional Office* ..... Sh. 351,300,000/=  
Kif. 3022 – *Kagera Regional Office* ..... Sh. 339,450,000/=  
Kif. 3023 – *Mtwara Regional Office* ..... Sh. 341,700,000/=  
Kif. 3024 – *Lindi Regional Office* ..... Sh. 274,200,000/=  
Kif. 3025 – *Njombe Regional Office* ..... Sh. 245,700,000/=  
Kif. 3026 – *Shinyanga Regional Office* ..... Sh. 411,450,000/=  
Kif. 3027 – *Ilala Regional Office* ..... Sh. 659,509,000/=  
Kif. 3028 – *Kilimanjaro Regional Office* ..... Sh. 454,350,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sisikii sauti  
huku.

Kif. 3029 – *Morogoro Regional Office* ..... Sh. 458,250,000/=  
Kif. 3030 – *Katavi Regional Office* ..... Sh. 212,150,000/=  
Kif. 3031 – *Tanga Regional Office* ..... Sh. 459,450,000/=  
Kif. 3032 – *Simiyu Regional Office* ..... Sh. 196,200,000/=  
Kif. 3033 – *Songwe Regional Office* ..... Sh. 156,789,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ..... Sh. 377,313,000/=  
Kif. 2001 – *Police Main Force* ..... Sh. 260,557,336,500/=  
Kif. 2002 – *Police Marine* ..... Sh. 2,228,177,000/=  
Kif. 2003 – *Railway Police Division* ..... Sh. 1,844,943,000/=  
Kif. 2004 – *Police Signals Branch* ..... Sh. 2,177,246,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya

4 MEI, 2018

*Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 – *Police Zanzibar* .....Sh. 7,662,954,000/=

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kupata maelezo hapa Polisi Zanzibar, kifungu namba 22003, suala la mafuta, nataka maelezo kwa nini imepungua wakati bado tuna tatizo la mafuta kwa sababu, kasoro milioni 10 hapa imepungua na bado tuna matatizo ya mafuta kwa Polisi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la kibajeti.

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2006 – *Police Air Wing* .....Sh. 2,487,200,000/=

Kif. 2007 – *TAZARA Police* .....Sh. 2,128,749,000/=

Kif. 2008 – *Field Force Unit* .....Sh. 1,684,325,000/=

Kif. 2009 – *Traffic Police* .....Sh. 1,675,239,000/=

Kif. 2010 – *Police Airport* .....Sh. 2,173,295,000/=

Kif. 2011 – *Police Dog and Horses* .....Sh. 1,145,259,000/=

Kif. 2012 – *DSM Special Zone* .....Sh. 4,853,320,000/=

Kif. 2013 – *Police Ilala* .....Sh. 10,504,204,000/=

Kif. 2014 – *Police Kinondoni* .....Sh. 11,156,619,000/=

Kif. 2015 – *Police Temeke* .....Sh. 8,465,952,000/=

Kif. 2016 – *Police Arusha* .....Sh. 13,432,475,000/=

Kif. 2017 – *Police Iringa* .....Sh. 8,343,130,000/=

Kif. 2018 – *Police Kilimanjaro* .....Sh. 10,685,192,000/=

Kif. 2019 – *Police Kigoma* .....Sh. 9,377,044,000/=

Kif. 2020 – *Police Kagera* .....Sh. 12,083,552,000/=

Kif. 2021 – *Police Lindi* .....Sh. 6,052,053,000/=

Kif. 2022 – *Police Mwanza* .....Sh. 12,713,309,000/=

Kif. 2023 – *Police Mara* .....Sh. 7,986,061,000/=

Kif. 2024 – *Police Tarime, Roraya* .....Sh. 6,126,017,000/=

4 MEI, 2018

Kif. 2025 – Police Mbeya .....Sh.11,957,908,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2026 – Police Mtwara .....Sh. 7,253,097,000/=

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipaye ufanuzi kwenye kifungu hicho, maeneo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza *Sub-Vote 22019, Routine, maintenance and repair of buildings and routine maintenance and repair of vehicles.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ndicho ambacho kinaenda kukarabati majengo ya Polisi Tanzania na hasa katika Mkoa wangu wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Mtwara kinakaribia kubomoka kabisa, kinakaribia kudondoka pale Mtwara, lakini pesa zilizotengwa hapa ni pesa ndogo sana. Ni pesa shilingi 7,500,000 jengo hili ni kubwa sana jengo moja tu, lakini yapo majengo Newala, Tandahimba, Mtwara Vijijiini kule. Kwa hiyo, naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante umeelewaka. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hapa utaona kwamba hata miaka miwili iliyopita kifungu hicho hakikuwa na hela kabisa. Safari hii angalau tumeweza kupata hizi fedha kwa ajili ya kusogea kidogo, lakini kutoptana na ufinyu wa bajeti hatukweza kutenga fedha nyingi zaidi. (*Makofii*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu.

Kif. 2027 – *Police Morogoro* .....Sh.13,389,589,000/=  
Kif. 2028 – *Police Manyara* .....Sh. 8,050,406,000/=  
Kif. 2029 – *Police Singida* .....Sh. 8,174,274,000/=  
Kif. 2030 – *Police Pwani* .....Sh.10,210,004,000/=  
Kif. 2031 – *Police Ruvuma* .....Sh. 7,042,184,000/=  
Kif. 2032 – *Police Rukwa* .....Sh. 5,804,935,000/=  
Kif. 2033 – *Police Shinyanga* .....Sh. 6,362,775,000/=  
Kif. 2034 – *Police Tabora* .....Sh. 7,393,496,000/=  
Kif. 2035 – *Police Tanga* .....Sh. 9,562,716,000/=  
Kif. 2036 – *Police Mjini Magharibi* .....Sh.12,266,258,000/=  
Kif. 2037 – *Police Kusini Unguja* .....Sh. 5,787,660,000/=  
Kif. 2038 – *Police Kaskazini Unguja* .....Sh. 4,641,317,000/=  
Kif. 2039 – *Police Kusini Pemba* .....Sh. 4,218,628,000/=  
Kif. 2040 – *Police Kaskazini Pemba* .....Sh. 4,195,823,000/=  
Kif. 2041 – *Police Dodoma* .....Sh.10,325,628,000/=  
Kif. 2042 – *Police Geita* .....Sh. 6,840,352,000/=  
Kif. 2043 – *Police Katavi* .....Sh. 3,921,703,000/=  
Kif. 2044 – *Police Njombe* .....Sh. 4,225,876,000/=  
Kif. 2045 – *Police Simiyu* .....Sh. 4,490,894,000/=  
Kif. 3001 – *Police College Moshi* .....Sh. 5,218,496,000/=  
Kif. 3002 – *Police College* .....Sh. 2,242,358,000/=  
Kif. 4001 – *Police Vehicles*  
    *Maintenance Unit*.....Sh. 3,293,558,000/=  
Kif. 5001 – *Police Medical Unit* .....Sh. 2,216,893,000/=  
Kif. 6001 – *Police Building Brigade* .....Sh. 6,108,290,000/=  
Kif. 7001 – *Criminal Investigation Division*...Sh. 8,661,561,500/=  
Kif. 7002 – *Stock Theft Prevention Unit* .....Sh. 1,010,773,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### Fungu 29 - Jeshi la Magereza

Kif. 1001 – *Prisons Headquaters* .....Sh. 7,874,441,000/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* .....Sh. 235,750,000/=  
Kif. 2001 – *Parole Department* .....Sh. 1,021,654,000/=  
Kif. 2002 – *Prisons Welfare and  
Rehabilitation* .....Sh.165,395,323,000/=  
Kif. 2003 – *Resettlement of Offenders* .....Sh. 4,572,538,000/=

Kif. 2004 – <i>Prisons Arusha</i> .....	Sh. 855,901,000/=
Kif. 2005 – <i>Prisons Dar-es-Salaam</i> .....	Sh. 2,045,174,000/=
Kif. 2006 – <i>Prisons Dodoma</i> .....	Sh. 849,265,000/=
Kif. 2007 – <i>Prisons Kigoma</i> .....	Sh. 465,571,000/=
Kif. 2008 – <i>Prisons Tanga</i> .....	Sh. 780,654,000/=
Kif. 2009 – <i>Prisons Kagera</i> .....	Sh. 726,832,000/=
Kif. 2010 – <i>Prisons Mwanza</i> .....	Sh. 1,063,303,000/=
Kif. 2011 – <i>Prisons Tabora</i> .....	Sh. 697,110,000/=
Kif. 2012 – <i>Prisons Mbeya</i> .....	Sh. 895,169,000/=
Kif. 2013 – <i>Prisons Singida</i> .....	Sh. 553,188,000/=
Kif. 2014 – <i>Prisons Coast</i> .....	Sh. 835,018,000/=
Kif. 2015 – <i>Prisons Lindi</i> .....	Sh. 620,932,000/=
Kif. 2016 – <i>Prisons Manyara</i> .....	Sh. 470,204,000/=
Kif. 2017 – <i>Prisons Mtwara</i> .....	Sh. 693,050,000/=
Kif. 2018 – <i>Prisons Ruvuma</i> .....	Sh. 544,147,000/=
Kif. 2019 – <i>Prisons Rukwa</i> .....	Sh. 630,850,000/=
Kif. 2020 – <i>Prisons Mara</i> .....	Sh. 633,810,000/=
Kif. 2021 – <i>Prisons Iringa</i> .....	Sh. 626,840,000/=
Kif. 2022 – <i>Prisons Kilimanjaro</i> .....	Sh. 726,025,000/=
Kif. 2023 – <i>Prisons Morogoro</i> .....	Sh. 1,582,757,000/=
Kif. 2024 – <i>Prisons Geita</i> .....	Sh. 27,400,000/=
Kif. 2025 – <i>Prisons Katavi</i> .....	Sh. 0
Kif. 2026 – <i>Prisons Njombe</i> .....	Sh. 27,400,000/=
Kif. 2027 – <i>Prisons Simiyu</i> .....	Sh. 0
Kif. 2028 – <i>Prisons Shinyanga</i> .....	Sh. 574,212,000/=
Kif. 3001 – <i>Ukonga Prisons Staff College</i> ...	Sh. 3,373,636,000/=
Kif. 3002 – <i>Kingolwila Prisons Driving School</i> ..	Sh. 516,456,000/=
Kif. 3003 – <i>Ruanda Prisons Trade School</i> .....	Sh. 985,664,000/=
Kif. 3004 – <i>Prisons College Kiwira</i> .....	Shs. 1,788,648,000/=
Kif. 4001 – <i>Prison Building Brigade</i> .....	Sh. 1,257,412,000/=
Kif. 4002 – <i>Prison Industries</i> .....	Sh. 585,364,000/=
Kif. 4003 – <i>Prison Farms</i> .....	Sh. 1,132,698,000/=

(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji

Kif. 2001 – <i>Immigration Zanzibar</i> .....	Sh. 6,961,098,000/=
Kif. 2002 – <i>Immigration Head Quarter</i> ....	Sh. 47,102,253,000/=

Kif. 2003 – <i>Immigration Ilala</i> .....	Sh. 30,000,000/=
Kif. 2004 – <i>Tanzania Regional Immigration Training Academy</i> .....	Sh. 97,132,000/=
Kif. 2005 – <i>Immigration Kinondoni</i> .....	Sh. 29,600,000/=
Kif. 2006 – <i>Immigration Temeke</i> .....	Sh. 30,000,000/=
Kif. 2007 – <i>Immigration Arusha</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2008 – <i>Immigration Dar-es-Salaam</i> .....	Sh. 78,146,000/=
Kif. 2009 – <i>Immigration Dodoma</i> .....	Sh. 45,000,000/=
Kif. 2010 – <i>Immigration Geita</i> .....	Sh. 45,000,000/=
Kif. 2011 – <i>Immigration Iringa</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2012 – <i>Immigration Kilimanjaro</i> .....	Sh. 48,000,000/=
Kif. 2013 – <i>Immigration Kigoma</i> .....	Sh. 65,000,000/=
Kif. 2014 – <i>Immigration Katavi</i> .....	Sh. 56,000,000/=
Kif. 2015 – <i>Immigration Kagera</i> .....	Sh. 65,000,000/=
Kif. 2016 – <i>Immigration Lindi</i> .....	Sh. 46,000,000/=
Kif. 2017 – <i>Immigration Mwanza</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2018 – <i>Immigration Manyara</i> .....	Sh. 56,000,000/=
Kif. 2019 – <i>Immigration Mbeya</i> .....	Sh. 71,000,000/=
Kif. 2020 – <i>Immigration Morogoro</i> .....	Sh. 58,000,000/=
Kif. 2021 – <i>Immigration Mtwara</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2022 – <i>Immigration Mara</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2023 – <i>Immigration Njombe</i> .....	Sh. 40,000,000/=
Kif. 2024 – <i>Immigration Pwani</i> .....	Sh. 47,000,000/=
Kif. 2025 – <i>Immigration Ruvuma</i> .....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2026 – <i>Immigration Rukwa</i> .....	Sh. 52,000,000/=
Kif. 2027 – <i>Immigration Simiyu</i> .....	Sh. 47,000,000/=
Kif. 2028 – <i>Immigration Singida</i> .....	Sh. 40,000,000/=
Kif. 2029 – <i>Immigration Shinyanga</i> .....	Sh. 45,000,000/=
Kif. 2030 – <i>Immigration Tanga</i> .....	Sh. 64,000,000/=
Kif. 2031 – <i>Immigration Tabora</i> .....	Sh. 55,000,000/=
Kif. 2032 – <i>Immigration Songwe</i> .....	Sh. 60,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

## KITABU CHA NNE

### MIPANGO YA MAENDELEO

#### Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

4 MEI, 2018

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i> .....	Sh. 15,000,000,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kif. 3001 – <i>Fire and Rescue Services</i> .....	Sh. 4,500,000,000/=
( <i>Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote</i> )	

#### **Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

Kif. 2001 – <i>Police Main Force</i> .....	Sh. 1,777,851,000/=
Kif. 2005 – <i>Police Zanzibar</i> .....	Sh. 0
Kif. 2020 – <i>Police Kagera</i> .....	Sh. 1,256,000,000/=
Kif. 2022 – <i>Police Mwanza</i> .....	Sh. 0
Kif. 2023 – <i>Police Mara</i> .....	Sh. 0
Kif. 2026 – <i>Police Mtwara</i> .....	Sh. 0
Kif. 2041 – <i>Police Dodoma</i> .....	Sh. 1,000,000/=
Kif. 2044 – <i>Police Njombe</i> .....	Sh. 715,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 29 - Jeshi la Magereza**

Kif. 2002 – <i>Prisons Welfare and Rehabilitation</i> ..	Sh. 35,831,000/=
Kif. 4001 – <i>Prison Building Brigade</i> .....	Sh. 0
Kif. 4002 – <i>Prison Industries</i> .....	Sh. 2,000,000,000/=
Kif. 4003 – <i>Prison Farms</i> .....	Sh. 3,000,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

4 MEI, 2018

### Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji

Kif. 2002 – *Immigration Head Quarter* .....Sh.10,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3),(a) na (b), vya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono, Waheshimiwa Wabunge bajeti hajapita bado, subirini niwahoji, ipite, ndiyo mpige makofi. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalipitishwa na Bunge)*

4 MEI, 2018

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, natangaza sasa na ninakupongeza Waziri na timu yako, makamanda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ulinzi wa nchi hii ni wa wananchi wote siyo polisi peke yao. Unapooda polisi wanapata changamoto mnaingia na ninyi mnasaidia, masuala haya ya uvamizi, masuala ya uhalifu kwenye nchi yatatuathiri wote, kwa hiyo vyombo vya ulinzi vinahitaji msaada wetu wote. Tushirikiane kusaidia vyombo hivi na wao waweze kufanya kazi zao vizuri. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, timu yako ambayo imekuja hapa Katibu Mkuu na Makamanda wote kwa kazi nzuri mnazofanya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kurudia tangazo la asubuhi kuwa, kesho kuna mashindano ya mpira kati ya timu ya *Bunge Sports (Ndugai Boys)* na Benki ya BOA na Mgeni Rasmi atakuwa ni Mheshimiwa Zungu niliyesimama hapa. Baada ya hapo saa 1.30 usiku kutakuwa na mchapalo katika Hoteli ya *Royal Village*, Wabunge wote mnaalikwa na mgeni rasmi ni Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia, tarehe 6 Mei, siku ya Jumapili kutakuwa na mashindano kati ya *Ndugai Boys* na *Ilala Veterans (Zungu Boys)* katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 10.00 alasiri. Mgeni rasmi ni Mheshimiwa Spika tena. Mechi zote zitakuwa mubashara na zitaoneshwa na Kituo cha Azam Televisheni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 13 Mei, klabu ya Simba itakapotoka katika viwanja vya Singida itawasili katika Bunge letu kuja kutambulishwa na jioni kutakuwa na hafla ambayo mgeni rasmi atakuwa ni Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 2.14 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 7 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi*)